**7 FEBRUARI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

___

## MAJADILIANO YA BUNGE

___

## MKUTANO WA KUMI

### Kikao cha Sita – Tarehe 7 Februari 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na.44 la Tarehe 04 Novemba, 2022;
2. Toleo Na.45 la Tarehe 11 Novemba, 2022;

3. Toleo Na.46 la Tarehe 18 Novemba, 2022;
4. Toleo Na.47 la Tarehe 25 Novemba, 2022;
5. Toleo Na.48 la Tarehe 02 Desemba, 2022;
6. Toleo Na.49 la Tarehe 09 Desemba, 2022;
7. Toleo Na.50 la Tarehe 16 Desemba, 2022;
8. Toleo Na.51 la Tarehe 23 Desemba, 2022;
9. Toleo Na.52 la Tarehe 30 Desemba, 2022;
10. Toleo Na.01 la Tarehe 06 Januari, 2023;
11. Toleo Na.02 la Tarehe 13 Januari, 2023;
12. Toleo Na.03 la Tarehe 20 Januari, 2023; na
13. Toleo Na.04 la Tarehe 27 Januari, 2023.

**MHE. GEORGE N. MALIMA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MITAJI NA UWEKEZAJI WA UMMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**7 FEBRUARI, 2023**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kakoso.

Na. 86

**Hitaji la wahudumu wa afya na madaktari Wilaya ya Tanganyika**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itapeleka wahudumu wa afya na madaktari kwenye Vituo vya Afya na Hospitali ya Wilaya ya Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuboresha huduma za afya kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 na 2021/2022, Serikali imeajiri watumishi wa kada za afya 10,462 na kuwapanga kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia uhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya ajira 7,612 za kada ya afya zilizotolewa na Serikali mwezi Julai, 2022 Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika ilipangiwa watumishi 62 wa kada mbalimbali ikiwemo Wauguzi na Madaktari kwa ajili ya hospitali, vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa Sekta ya Afya na kuwapeleka katika vituo vya huduma kote nchini ikiwemo Halmashauri ya Tanganyika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwanza niipongeze Serikali kwa kujenga vituo vya afya na hospitali ya Wilaya. Kwa bahati mbaya sana idadi ya watumishi ambao ndio wanaokuja kufanya kazi kwenye maeneo husika kwenye vituo vya afya na hospitali ya wilaya bado ni wachache, Halmashauri yangu ya Wilaya kwenye hospitali ya wilaya mahitaji ya watumishi ni 608 waliopo ni 40 tu, kitu ambacho wanashindwa kufanya kazi na wanashindwa kutoa huduma ile iliyokusudiwa.

Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itapeleka wahudumu hasa kada ya wauguzi ili waweze kufanya kazi na hospitali ya wilaya ianze kufanya kazi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Serikali imeleta *X-ray* kwenye eneo la Wilaya ya Tanganyika, kinachokwamisha sasa hivi ni Bodi ile ya Mionzi kutokwenda kuthibitisha. Je, ni lini watawapeleka wataalam hao na hiyo *X-ray* ilishafungwa kama miezi minne iliyopita? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imejenga Hospitali ya Halmashauri ya Tanganyika na hospitali ile imeanza kutoa huduma za afya kwa awamu ya kwanza na watumishi waliopo 40 kwa sasa ni wale ambao wanatoa huduma za awali. Serikali imeweka utaratibu mzuri kuhakikisha kwamba majengo mengine yanapoanza kutoa huduma, watumishi pia wanapelekwa, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hawa watumishi 608 wanahitajika pale hospitali itakapoanza kutoa huduma katika majengo yote, lakini kwa sasa watumishi 40 wanatoa huduma zile za awali na Serikali itaendelea kupeleka watumishi ili waweze kutoa huduma zote katika wodi ambazo zinaendelea na ukamilishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la *x-ray* ni kweli Serikali imepeleka *digital x-ray* katika Halmashauri ya Tanganyika kama ambavyo imepeleka katika Hospitali za Halmashauri nyingi kote nchini na wataalam wa mionzi kutoka Arusha tutawasiliana nao wafike Tanganyika ili waweze kufanya ukaguzi na kutupa kibali cha kuendelea na huduma za *x-ray*, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa Serikali imejenga vituo vingi ikiwepo katika Jimbo la Makambako, Kituo cha Ikelu, Kitangililo na Lyamkena.

Je, ni lini sasa Serikali itatupelekea waganga ili kusudi wananchi waendelee kupata matibabu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Deo Kasinyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali imejenga Vituo vya Afya vya Ikelu, Kitandililo na Lyamkena na nimpongeze sana Mheshimimiwa Deo Sanga, kwa namna ambavyo anawapigania wananchi wa Jimbo la Makambako na huduma za afya zimeendelea kuboreshwa. Nimhakikishie kwamba Waganga watapelekwa katika vituo hivi ili waanze kutoa huduma za awali za msingi wakati Serikali inaendelea kuajiri watumishi wengine kwa ajili ya kuwapeleka katika vituo hivi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kata ya Sunya katika Kituo cha Afya tulipata ajali mbaya sana mwezi Novemba na tulipoteza watumishi karibu sita, sasa kituo kinataka kufungwa. Je, ni nini *commitment* ya Serikali kuweza kutuletea watumishi hao kwa haraka sana ili kituo kisifungwe? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali

la nyongeza ya Mheshimiwa Olelekaita, Mbunge wa Jimbo la Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ilitokea ajali na kupoteza watumishi wetu takribani sita katika Kituo cha Afya hiki cha Sunya. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, lakini shughuli za Serikali lazima ziendelee katika kituo kile cha afya na tulikubaliana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, kuhakikisha anafanya mgawanyo wa ndani wa watumishi waende kwenye kile kituo cha afya waanze kutoa huduma. Kwa hiyo, naomba nitumie fursa hii kumkumbusha Katibu Tawala wa Mkoa haraka iwezekanavyo apeleke watumishi kwenye kituo hiki cha afya ili wananchi waendelee kupata huduma za afya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kiswaga, kwa niaba yake Mheshimiwa Kisangi.

Na. 87

**Hitaji la Maabara katika Zahanati za Kalenga**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga Maabara kwenye Zahanati zote za Jimbo la Kalenga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya afya kwa kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi ya afya ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali ilipeleka fedha shilingi bilioni 27.8 kukamilisha maboma ya zahanati 555. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma ya zahanati 300.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Kalenga lina jumla ya zahanati 36 na kati ya hizo, zahanati 11 zinatoa huduma za maabara na zahanati 25 zinatoa huduma za maabara za msingi. Ili kuboresha huduma, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za maabara katika zahanati zote nchini zikiwepo zahanati za Jimbo la Kalenga, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kisangi.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninalo swali la nyongeza.

Kwa kuwa mgonjwa anapofika hospitalini hawezi kupata matibabu sahihi bila kupata vipimo; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha zahanati zote nchini zinapata maabara ili kutoa huduma sahihi kwa wagonjwa wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mariam Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ili upate huduma bora za afya lazima vipimo vya maabara vifanyike na Serikali kwanza imechukua hatua ya kuboresha ramani za majengo ya zahanati kwa kuongeza vyumba kutoka sita hadi vyumba 15, ambavyo vitawezesha kuwa na jengo zuri ambalo linakidhi huduma za maabara katika zahanati zetu.

Mheshimiwa Naibu Sspika, pili, zahanati zetu ambazo zilijengwa miaka ya nyuma ambazo hazikuwa na nafasi nzuri kwa ajili ya huduma za maabara, tumetenga maeneo ambayo huduma za maabara za msingi, kwa mfano vipimo vya *malaria*, vipimo vya wingi wa damu vinafanyika katika vyumba ambavyo vimekuwa *improvised* na huduma hizi zinaendelea kutolewa katika maeneo haya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. David Mathayo.

Na. 88

**Benki Kuu Kushusha Riba Inapokopa kupitia Hati Fungani**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza: -

Je, ni lini *BOT* itashusha riba inapokopa kupitia Hati Fungani kufikia asilimia 10 ili wananchi waweke fedha kwenye Benki za Biashara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo David, Mbunge wa Same Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya riba za hati fungani vilifanyiwa marekebisho mwezi Aprili 2022 ambapo hati fungani ya miaka 25 ilishuka kutoka asilimia 15.95 hadi 12.56; Miaka 20 kutoka asilimia 15.49 hadi 12.10; Miaka 15 kutoka asimilia 13.5 hadi 11.15; Miaka 10 kutoka asilimia 11.44 hadi 10.25; Miaka saba kutoka asilimia 10.08 hadi 9.48; Miaka mitano kutoka asilimia 9.18 hadi 8.6; na miaka miwili kutoka asilimia 7.82 hadi 7.6. Riba za hati fungani zilishushwa ili kuendana na riba za soko na pia wananchi waweze kuweka fedha zao kwenye benki za biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, wastani wa riba za hati fungani za Tanzania zipo chini ikilinganishwa na Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afika Mashariki. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa riba za hati fungani za Serikali na kuchukua hatua stahiki ili kutoathiri akiba za fedha katika benki za biashara, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mathayo.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Pia niipongeze sana Serikali kwa kupunguza riba katika hati fungani kwenye *level* tofauti. Ningependa kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika swali la kwanza; kwa sababu sasa hivi Serikali inafungua uchumi, inafungua nchi na kila mtu anatakiwa ashiriki katika suala zima la uchumi. Je, Serikali inaonaje kwamba ipunguze idadi ya minada ya hati fungani

kusudi mabenki ya biashara yaweze kufanya biashara yaweze kupata wawekezaji, ili tuweze kuongeza mzunguko wa fedha nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; ningependa kuiomba Serikali miaka saba iliyopita Serikali ilikuwa inapitisha fedha zake kwenye mabenki ya biashara na zile fedha zilikuwa zinakaa pale muda mrefu, kwa hiyo kulikuwa na mzunguko mkubwa wa fedha na wananchi walikuwa wanaweza kukopa na hata riba zilikuwa zimepungua kwa sababu kulikuwa na fedha nyingi kwenye mabenki ya biashara. Je, Serikali haioni muda umefika sasa wa kufungua tena kwamba fedha zake ziwe zinakaa kwenye mabenki ya biashara kusudi wananchi waweze kukopa, mzunguko wa fedha uongezeke lakini pia na riba ziweze kushuka?

**NAIBU SPIKA:** Swali lingine Mheshimiwa Waziri, je, Serikali ina mpango wowote sasa wa kushusha riba kwa mabenki ya biashara? Riba ishuke mpaka asilimia nne ili wananchi wakope nao kwa riba ndogo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kupunguza idadi ya riba katika hati fungani ni swali la kisheria, lakini Serikali imelichukua na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Dkt. Mathayo alileta ombi kwamba minada iwe inapungua mwenendo wake wa riba, basi nalo Serikali imelichukua na tutalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Kamonga.

Na. 89

**Kurasimisha kupanga na kupima ardhi - Ludewa**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kurasimisha, kupanga na kupima ardhi katika Miji Midogo ya Mawengi, Lugarawa, Luilo na Manda – Ludewa?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali Na. 89 lililoulizwa na Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara kupitia Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi iliikopesha Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kiasi cha shilingi milioni 405 kwa lengo la kupanga na kupima na kurasimisha miji midogo ya Mlangali, Mavanga, Ludewa na Mudindi ambapo jumla ya viwanja 7,911 vimepangwa na viwanja vingine 2,120 vimekamilika katika utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa maelekezo wataalamu wa ardhi Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa kuanza kukusanya takwimu muhimu kwa ajili ya kupanga na kupima katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, ila napenda kufahamu kwamba: Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa ni muda muafaka wa kufanya ziara Ludewa kwenda kutembelea hizo kazi na kugawa hati zile za mwanzo kwa wananchi ili kuongeza hamasa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kamonga, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mbunge kwamba umuhimu huo tunauona ndani ya Wizara na niko tayari sasa kuongozana naye baada ya Bunge kwenda kukabidhi ardhi zilizogaiwa ili kutengeneza hamasa kwa wengine waweze kujitokeza kwa wingi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Justin Lazaro, hayupo!

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Kwa niaba.

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba.

Na. 90

**Utata wa mauziano shamba kati ya mwekezaji EFATHA na Kijiji cha Ng'ang'ange – Kilolo**

**MHE. NANCY H. NYALUSI K.n.y. MHE. JUSTIN L. NYAMOGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itarudisha Shamba la Kijiji cha Ng'ang'ange kwa wananchi kufuatia mauziano kati ya EFATHA na Kijiji kutofuata sheria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2003 Taasisi ya *Efatha Ministry* iliomba eneo lenye ukubwa wa ekari 200 katika Kijiji cha Ng'anga'nge kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi, Kilimo na Mifugo. Taratibu zote za utoaji eneo husika zilifuatwa ikiwemo Kikao cha Halmashauri ya Kijiji, Mkutano Mkuu wa Kijiji na Kamati ya kugawa ardhi ya Wilaya pamoja na fidia za mali zililipwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nancy.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Kwa kuwa mgogoro huu umekuwa ni wa muda mrefu na ni kero kubwa kwa wananchi wa Ng'ang'ange; je, Mheshimiwa Waziri upo tayari kufanya ziara katika kijiji hicho ili kuweza kutatua hiyo kero kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri, ziara lakini na Mheshimiwa Nyamoga, sio huyu. Uko tayari? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza linaloulizwa kwa niaba ya Mheshimiwa Justin Nyamoga, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumhakikishia Mbunge kwamba kwa kuwa tumepanga ziara ya Mkoa wa Iringa, ambayo tutataka tutembelee majimbo yote na Halmashauri zote za Iringa, niko tayari pia kufika Halmashauri ya Kilolo ili kwenda kukutana na wananchi tuzungumze na kumaliza mgogoro huu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Bupe.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Serikali ina mpango gani wa kuwarudishia mashamba wananchi waliodhulimiwa na taasisi ya EFATHA Kijiji cha Moro, Msandamungano na Mpwapwa, vilivyopo Wilaya ya Sumbawanga Vijijini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua mgogoro uliopo baina ya vijiji hivo vilivyotajwa na Shirika la *Efatha Ministry* ambapo katika kuhangaika nalo, tunatambua kwamba zipo kesi zinazoendelea na nyingine ambazo zimeshaamuliwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakapokuwa tunafanya ziara ya Nyanda za Juu Kusini, tutafika na eneo la Rukwa ili kuzungumza na wananchi na kutatua mgogoro uliopo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Tunza.

Na. 91

**Kukamilisha ujenzi wa chujio la maji Manispaa ya Mtwara Mikindani**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni lini chujio la maji linalojengwa katika Manispaa ya Mtwara Mikindani litakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilika ujenzi wa chujio la kuchujia maji mwezi Aprili, 2022. Kukamilika kwa ujenzi wa chujio hilo kumeweza kuboresha upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu hayo, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kama chujio limekamilika kujengwa, kwanini maji yanatoka machafu na wakati mwingine wananchi wanashindwa kuyatumia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Mkataba wa uboreshaji wa miiundombinu ya maji katika Manispaa ya Mtwara Mikindani wenye thamani ya Shilingi bilioni 19 ulisainiwa mbele ya Mheshimiwa Waziri. Nataka kujua utekelezaji wake umefikia hatua gani? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maji kutoka machafu baada ya ukamilishaji wa chujio ni suala la kiufundi. Ni sehemu chache ambapo mabomba ni chakavu wakati fulani bado yanaleta udongo kwa ndani lakini tayari watendaji wetu wanalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mkataba kusainiwa mbele ya Mheshimiwa Waziri uko sahihi, tayari Shilingi bilioni 19 zimetengwa, Mkandarasi ameshapatikana, yuko kwenye *mobilization,* anafanya uandaaji wa *site* na hivi punde atalipwa *advance payment* ili kazi zianze.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Cherahani.

Na. 92

**Hitaji la Chuo cha VETA-Ushetu**

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kujenga Chuo cha *VETA* Ushetu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, Mbunge wa Jimbo la Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni azma ya Serikali kujenga Chuo cha Ufundi Stadi *(VETA)* katika kila Mkoa na Wilaya nchini. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyuo vya *VETA* katika Wilaya 63 ambazo hazina vyuo hivyo. Kiasi hiki pia kitatumika katika ujenzi wa chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kahama ni miongoni mwa Wilaya zitakazojengewa Vyuo vya *VETA* ambapo kwa sasa Serikali ipo katika hatua za maandalizi ya ujenzi. Hivyo wananchi wa Jimbo la Ushetu watanufaika na Chuo cha *VETA* cha Wilaya ya Kahama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza niwapongeze Wizara niwapongeze Wizara ya Elimu kwa kazi nzuri wanazofanya. Kwa kuwa Manispaa ya Kahama ina chuo cha *FDC* ambacho kinafanya kazi kama ile ile ya Chuo cha *VETA*: Kwa nini sasa chuo hiki cha *VETA* kisijengwe katika Halmashauri ya Ushetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili: Kwa kuwa uhitaji wa Chuo cha *VETA* kwa wananchi wa Ushetu mkubwa sana kulingana na ongezeko kubwa la vijana ambao wanamaliza vyuo vikuu lakini hawaendelei na masomo ya

juu: Kwa nini sasa Serikali isione hili kwa umuhimu kulingana na umbali wa kilometea zaidi ya 113 kutoka Ushetu kuja Manispaa ya Kahama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara haipangi maeneo ya kujenga vyuo hivi vya *VETA*, ni jukumu la Serikali za Mikoa pamoja na Wilaya kupanga maeneo kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivi vya *VETA*. Naomba nitoe wito kwa Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakuu wa Mikoa washirikishe Waheshimiwa Wabunge wa maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba wanakwenda kupanga maeneo sahihi ya kuweza kufanya ujenzi wa vyuo hivi vya *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lakwe la pili, tunajua umuhimu wa vyuo hivi na hivi sasa tumeanza katika ngazi ya Wilaya pamoja na Mikoa; baada ya kukamilika zoezi hili katika ngazi za wilaya pamoja na mikoa, tutafanya tathmini ya kina ili kuweza kuona namna gani tunaweza kuzifikia zile Halmashauri ambazo labda ziko mbali na maeneo ambayo yamejengwa katika *VETA* zile za Wilaya pamoja na Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Noah.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je,

ni lini Serikali itakwenda kujenga *VETA* katika Jimbo la Arumeru Magharibi katika Wilaya ya Arumeru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Arumeru, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyozungumza katika majibu ya msingi, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba inajenga vyuo vya *VETA* katika kila Mkoa na Wilaya nchini na tumeweza kufikia Mikoa yote na hivi sasa tunakamilisha Mkoa wa mwisho ule Mkoa wa Songwe. Katika mwaka huu wa fedha tunakwenda kujenga katika Wilaya 63 ambazo zilikuwa hazina vyuo hivi. Iwapo kama Arumeru ni miongoni mwa Wilaya zile 63 bila shaka tutaifikia wilaya hii na kuhakikisha kwamba tunakwenda kujenga katika Wilaya ya Arumeru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Butondo, jiandae Mheshimiwa Ng'wasi.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Wilaya ya Kishapu ni moja kati ya wilaya ambazo zinatekeleza ujenzi wa miradi hii ya *VETA;* na mpaka sasa hivi mradi huu una zaidi ya miaka mitatu uko katika ujenzi, lakini bado kuna upungufu wa ukamilishaji wa umeme, *furniture*, maji, na baadhi ya miundombinu katika maeneo hayo. Ni zaidi ya Shilingi milioni 400 zinahitajika kwa ajili ya kukamilisha mradi huu. Ni lini Serikali itakamilisha suala la kuleta fedha kwa ajili ya kukamlisha mradi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge wa Kishapu na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao maeneo yao tayari tumeweza kujenga vile vyuo 25. Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mwaka huu tayari ameshatoa jumla ya Shilingi bilioni 10.3 kwa ajili ya kukamilisha maeneo yale katika vile vyuo vyote 25. Katika zile kazi ambazo bado hatujakamilisha, na tayari tumeshaanza kuzipeleka kwenye maeneo yale kwa lengo la kukamilisha kazi hizo. Kwa hiyo, muda mfupi ujao tutakuwa tumekamilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Ng'wasi.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilitenga eneo la ekari 50 kuipa Wizara ya Elimu bure kabisa kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha *VETA:* Sasa ni lini chuo hiki kitaanza kujengwa rasmi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Ng'wasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ilemela ni miongoni mwa Wilaya 63 ambazo tunaanza ujenzi katika mwaka huu wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Mkundi.

Na. 93

**Kuanza kazi Chuo cha VETA Ukerewe**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza: -

Je, ni lini Chuo cha *VETA* Ukerewe kitaanza kufanya kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kukamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA Ukerewe ili kiweze kutoa mafunzo yatakayowezesha vijana kujiajiri na kuajiriwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa chuo hiki upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji ambapo ujenzi umefikia asilimia 97. Aidha, tayari Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa chuo hiki ili kianze kutoa mafunzo ya muda mfupi ifikapo mwezi Aprili, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa hatua kubwa iliyofikiwa ya ujenzi wa chuo hiki cha *VETA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa dhamira ya Serikali kujenga vyuo vya *VETA* ni kusaidia vijana wetu kupata taaluma itakayowasaidia kujiajiri au kuajiriwa kulingana na mazingira yao, nataka kujua, ni kozi zipi au aina ipi ya mafunzo itakayotolewa kwenye chuo hiki cha *VETA* ukerewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyozungumza kwenye majibu ya msingi kwamba mafunzo tutaanza mwezi wa Nne na tutaanza kwa kozi fupi; na tuliwaelekeza Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, katika Mabaraza yetu ya Madiwani waweze kuamua au ku-*detect* na aina ya kozi ambazo tunatarajia kuanza nazo; ziko zile kozi za jumla ambazo tunatarajia kuanza nazo kama za ufundi umeme wa majumbani, uchomeleaji na ufundi wa mabomba; hizo ni kozi muhimu ambazo tunatarajia kuanza nazo katika kipindi hicho kifupi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei, halafu jiandae Mheshimiwa Matiko.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi. Serikali imeahidi kujenga Chuo cha *VETA* Jimbo la Mbulu Vijijini na tumeandaa ekari 50, na umetuma wawakilishi wako; je, lini mnaanza kujenga Chuo cha *VETA* Mbulu Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, lini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Flatei, Mbunge wa Mbulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika swali la mwanzo kwamba ujenzi wa vyuo 63 unatarajia kuanza hivi karibuni, kwa hivi sasa tunaandaa michoro pamoja na kufanya *geotechnical survey*, *topographical survey,* pamoja na kufanya *estimate* kwa ajili ya kuanza ujenzi kwenye maeneo mbalimbali, ikiwemo na Wilaya ya Mbulu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Wilaya ya Tarime haina Chuo cha *VETA*. Mwaka 2022 niliuliza swali hili hili kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na akaahidi kwamba wataiweka kwa upande wa Rorya na Tarime. Nataka nijue, katika hivyo vyuo 63 ambavyo mnatarajia kujenga, Wilaya ya Tarime nayo imo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Matiko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika kipindi kilichopita Mheshimiwa Mbunge aliuliza hoja hii. Naomba tu Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi hiki cha maswali uje kuangalia orodha iwapo kama Wilaya walioiyoitaja ipo au haipo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Maendeleo ya Jamiii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu.

Na. 94

**Kukomesha ukatili wa kijinsia nchini**

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha ukatili wa kijinsia nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamiii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernadeta Kasabago Mushashu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili wa Kijinsia unaozingatia kuimarisha uchumi wa kaya, kutokomeza mila na desturi zinachochea ukatili, kuimarisha malezi na makuzi na kusimamia sheria na kuwezesha huduma kwa waathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto zimeundwa kuanzia ngazi ya Taifa hadi Kijiji. Zinafanya kazi zake katika Halmashauri kuhusu kutokomeza ukatili. Vituo vya Jeshi la Polisi, Magereza na Madawati ya Jinsia, Vyuo na Sehemu za Umma wanaunda madawati ya jinsia, Shule za Msingi na Sekondari zinaunda Madawati ya Ulinzi wa Watoto. Vilevile, Kampeni za kupinga ukatili zinaendelea sambamba na hatua za kuboresha sheria mbalimbali, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mushashu.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Taarifa za Polisi na mambo tunayoyaona kila siku kwenye jamii yanaonesha kwamba ukatili wa kijinsia unaendelea kuongezeka; je, nini sababu ya ongezeko hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeweka mikakati mingi ya kudhibiti ukatili wa kijinsia ikiwemo Mabaraza ya Watoto, Madawati ya Jinsia, Kamati za Ulinzi, nani anaratibu afua hizi zote? Kwa nini basi tunapata taarifa tu kutoka kwenye Dawati la Polisi, lakini kwenye hizi afua mlizoweka hatupati taarifa zake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bernadeta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli taarifa za Jeshi la Polisi zinaonesha kwamba ukatili umeongezeka. Sababu ya kuongezeka vitendo vya ukatili ni mmomonyoko wa maadili wa malezi na makuzi kwa Watoto; wazazi na walezi kutowajibika kumlinda mtoto; matumizi mabaya ya kieletroniki, na pia kuiga maadili ambayo siyo utamaduni wa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wanapokuwa katika majukwaa yao kutoa elimu hii ya kutokomeza ukatili wa jinsia kwa wananchi wao. Vilevile tunaambiwa mtoto wa mwenzio ni wako, kwa hivyo tuwajibike sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Swali lake la pili, afua zote zinatekelezwa na Wizara tukishirikiana na wadau mbalimbali hasa Jeshi la Polisi ambalo lina mamlaka ya kutoa taarifa zote za ukatili wa kijinsia katika nchi yetu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimwa Waziri kwa majibu mazuri. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Taletale.

Na. 95

**Mkakati wa kukuza kilimo cha mazao ya viungo – Morogoro Vijijini**

**MHE. HAMISI S. TALETALE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukuza kilimo cha mazao ya viungo katika Wilaya ya Morogoro Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi Shabani Taletale, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeandaa mkakati wa kuendeleza mazao ya bustani *(National Horticulture Development Strategy 2021 - 2031)* yakiwemo mazao ya viungo. Ambapo mazao ya iliki, karafuu, vanilla, pilipili manga, tangawizi na mdalasini ni kati ya mazao ya bustani yaliyopewa kipaumbele katika mkakati huo unaolenga kuongeza uzalishaji wa mazao, kuboresha mazingira ya biashara na kuongeza Pato la Taifa linalotokana na mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Morogoro Vijijini Serikali kwa kushirikiana na *Sustainable Agricultural Tanzania (SAT)* inatekeleza mradi wa kuendeleza mazao ya viungo katika maeneo yanayozunguka Milima ya Uluguru *(Uluguru Spice Project)* kuanzia mwaka 2017. Mradi huu umenufaisha wakulima 1,668 katika vijiji 27 vilivyopo Kata za Tawa, Kibongwa, Konde, Kibungo, Mtombozi, Kisemu, Mkuyuni, Kinole. Vilevile, katika kuimarisha uendelezaji wa mazao ya viungo, Chama cha Msingi cha Ushirika wa Wakulima wa Viungo (CHAUWAVIMU) kimesajiliwa kwa lengo la kuimarisha uendelezaji wa mazao ya viungo (pilipili manga, mdalasini, karafuu, taangawizi, iliki na vanilla) katika Wilaya ya Morogoro Vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taletale.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza kabisa naitwa Dkt. Taletale. Moja ya changamoto kubwa ya……

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia tena.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwanza kabisa nimesema naitwa Dkt. Shabani Taletale. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Haya.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto kubwa ya wananchi wa Morogoro Kusini Mashariki na Morogoro Vijijini kwa ujumla ni ukosefu wa mitaji. Je, Serikali ina uratatibu gani wa kutuletea mitaji wana Morogoro Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Hamisi Shabani Taletale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mitaji kwa wakulima ni suala ambalo tunalipa kipaumbele Serikali, tupo tayari kukaa na Mheshimiwa Mbunge pamoja na ushirika wa wakulima hawa ili tuangalie fursa ambayo wanaweza kuipata kuimarisha mitaji yao.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Kasaka.

Na. 96

**Kupunguza Msitu wa Mbiwe kwa matumizi ya kiuchumi**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapunguza ukubwa wa Msitu wa Mbiwe na kurudisha kwa Wananchi?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Msitu wa Hifadhi wa Mbiwe una ukubwa kilomita za mraba 491 na umeanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 598 la mwaka 1995. Hifadhi ya Msitu wa Mbiwe ni muhimu kwa uhifadhi vyanzo vya maji, kuhifadhi mimea na wanyama, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, na kivutio cha utalii. Eneo hili pia ni ushoroba

unaounganisha mapori ya akiba ya Rukwa - Lukwati, Lwafi na Hifadhi ya Taifa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu huo, Serikali haioni haja ya kupunguza eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Msitu wa Mbiwe ilianza rasmi mwaka 1995, wakati shughuli za kibinadamu za kiuchumi katika mamlaka ya Mji Mdogo Makongolosi hasa kilimo zilikuwa zinafanyika;

Je, Serikali haioni haja sasa kwa kipindi hiki kuweza kuweka utaratibu maalum kama ilivyofanya kwenye uchimbaji wa madini ili na hawa wananchi wanaoshughulika na shughuli za kilimo waweze kufuata hizo taratibu waweze kufanya shughuli zao za kilimo kwenye maeneo yanayofaa kwa kilimo?

Swali la pili, Wilaya ya Chunya imekuwa muhanga wa kupokea wahamiaji wengi waliotoka maeneo mbalimbali walikofukuzwa huko hasa maeneo ya Usangu pamoja na Wilaya ya Songwe;

Je, Serikali haioni haja sasa kuweza kuona utaratibu maalum hawa wananchi ambao wametoka kwenye maeneo hayo, wanafika Wilaya ya Chunya na kuharibu mazingira hasa na mifugo yao kuweza kuingia kwenye maeneo ya mashamba kuweza kutoa tamko rasmi ili wananchi wetu wale wasiweze kuathirika na mifugo hiyo inayoingia ndani ya Wilaya ya Chunya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masanche Njeru Kasaka Mbunge wa Rupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu wa kuruhusu shughuli za kilimo ndani ya hifadhi, taratibu na kanuni zinaelekeza kwenye uapnde wa misitu ya *TFS* kwamba kunapokuwa na uchimbaji wa madini basi wale wachimbaji wanaruhusiwa kuchimba na wakati huohuo kurudishia miti ili kuendelea kuhifadhi maeneo hayo. Kwa hiyo, sheria na taratibu zinazoongozwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania ni kwamba hairuhusiwi kufanya shughuli za kilimo isipokuwa uchimbaji wa madini, ambalo ni eneo maalumu lililo ndani ya hifadhi ya misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wahamiaji, binadamu au wananchi kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haimzuii mwananchi yoyote kuishi eneo lolote analohitaji. Katiba inaruhusu mtu yoyote kuishi pale ambapo anaona panafaa, isipokuwa kwa wale ambao wanavamia maeneo ya hifadhi sheria na taratibu zitafuatwa ikiwemo kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nawaomba wananchi waheshimu maeneo ya hifadhi kwa mustakabali wa Taifa letu na kwa faida ya wananchi wenyewe.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Condester

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa vijiji vya Twentela, Mbalwa, Ntungwa, Mbawo, Moraviani na Itumbula wamezungukwa na hifadhi, hapo nyuma wananchi hao wenyewe kwa ridhaa yao walitoa maeneo hayo ya hifadhi ambayo yalikuwa ni ya kwao.

Je, Serikali haioni ipo haja ya kumega kipande kidogo tu cha hifadhi kuwasaidia wananchi hawa wapate eneo la kulima kwa sababu wamezaliana na hawana sehemu nyingine ya kwenda kwa ajili kuendesha shughuli zao, lakini kwa kufuata utaratibu na kutoa elimu bila kuathiri sheria zetu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Condester kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili pia aliwahi kuuliza Mheshimiwa Mbunge na taratibu nilimwelekeza kwamba, maombi yanatakiwa yaletwe na sisi tutaangalia tathmini, kama kuna umuhimu wa kumega eneo hilo basi tutapeleka mapendekezo kwa Mheshimiwa Rais, lakini pale ambapo tutaona kuna haja ya kutunza vyanzo vya maji basi wananchi wataelimishwa na maeneo haya tutayahifadhi kwa ajili ya kizazi hiki na kinachokuja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Pallangyo maswali mafupi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunatangaza Hifadhi ya Nyerere, National Park tayari kuna maeneo ya *WMA*, mfano kama Wma ya Magingo katika vijiji vya Mpigamiti, Barikiwa na Mlembwe tayari vimechukuliwa na *TANAPA*.

Je, ni lini Serikali itakuja kuhakiki hiyo mipaka ili yale maeneo yaliyokuwa yamehifadhiwa na vijiji yaendelee kuwa yanahifadhiwa na vijiji?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu wananchi wa Liwale niwaahidi kwamba kwa kuwa taratibu za kuainisha mipaka ni kazi inayoshirikisha Wizara ya Ardhi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, tutaenda kuhakiki hiyo mipaka ili kuruhusu wananchi watambue maeneo yao na kisha yaendelee kuhifadhiwa vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Palalngyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogogro wa mpaka kati ya *TANAPA* na wananchi wa Momela ambao unatokana na *TANAPA* kutwaa mashamba Namba 40 na Namba 41 bila kushirikisha Serikali ya Kijiji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuahidi Mbunge tutaenda kuzungumza na wananchi nikishirikiana na wataalamu tupate maelezo ya kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante majibu mazuri mkienda mtamalizia hukohuko. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu.

Na. 97

**Pori la Akiba Mabwepande kuwa chanzo cha mapato**

**MHE. ISSA J. MTEMVU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutumia Pori tengefu la Mabwepande kama chanzo cha mapato?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Jumanne Mtemvu, Mbunge wa Jimbo la Kibamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha Pori la Akiba Pande linaendelea kuwa kitovu cha utalii katika Jiji la Dar es Salaam na maeneo jirani kuwa chanzo cha mapato, Serikali imetumia kiasi cha shilingi 710,789,122 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya utalii zikiwemo *public camp site* Mbili katika eneo la Msakuzi na Jomeke na *Picnic Site* Mbili eneo la Bwawani na *Crater* pamoja na ujenzi wa uzio wa bustani ya wanyamapori.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hiyo imekamilika na imeanza kutumiwa na watalii ambapo kwa sasa shughuli

mbalimbali zikiwemo mbio za *Marathon*, nyama choma *festival*, utalii wa kutembea kwa miguu na kuendesha baiskeli, upigaji picha na matamasha mbalimbali vimeanza kutumika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa shughuli zote zilizotajwa ambazo zimeanza kufanyika ndani ya Pori la Akiba la Mabwepande, tayari wananchi wengi hawajui na hata wananchi wa Jimbo la Kibamba pia hawajui;

(a) Je, Serikali ipo tayari kufungua geti upande wa Jimbo la Kibamba ili wananchi wengi sana waweze kushiriki kwenye shughuli zilizotajwa kwenye jibu la msingi?

(b) Kwa kuwa katika kila uwekezaji tunategemea mapato na seerikali imejibu hapa imeshatumia shilingi 710,789,122. Je, ni yapi makadirio ya mapato katika mwaka 2022/2023?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Mtemvu Mbunge wa Kibamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pori hili la Mabwepande ni pori ambalo limepekena na Mikoa jirani ikiwemo Pwani na pori hili lipo katikati ya Dar es salaam, kwa sasa tumeshaanza kufanya hamasa mbalimbali na kwa kuwa mwanzoni

tulikuwa hatuna miundombinu tumeweza sasa kuwekeza na sasa hivi tuna miundombinu ya kutosha na hivyo watalii wameshaanza kuingia na matamasha mbalimbali yameshaanza kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaanza pia kutumia mitandao ya kijamii kuhamasisha wananchi, pia tunatumia televisioni matamasha mbalimbali kama ambavyo nimeyataja ikiwemo nyama choma *festival* hii yote ni kuwafanya wana Dar es salaam wawe na maeneo maalum ya kupumzika ikiwemo kulala ambapo tumeshaandaa maeneo ya *camp site* kwa ajili ya wananchi kulala.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuhamasisha Watanzania wote unapofika Dar es Salaam basi tembelea Pori la Pande utapata huduma zote za kiutalii na utaweza kuwa umepumzika kama vile upo *Serengeti National Park.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa mapato tangu tulipowekeza katika pori hili kwa sasa tumesha kusanya jumla ya shilingi milioni 4.9 na kwa kuwa uwekezaji ni endelevu tunaendelea kuwekeza ili kuhakikisha kwamba eneo hili linakuwa ni kivutio kikubwa katika mkoa wa Dar es Salaam.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Afya. Mheshimiwa Kilave

Na. 98

**Kupunguza gharama kwa akinamama wanaojifungua**

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama za malipo kwa Akinamama wanaojifungua kawaida na wale wa operesheni?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya inaendelea kutekeleza Sera ya Afya ya mwaka 2007 inayoelekeza kutoa huduma za matibabu bure kwa makundi maalum, ikiwemo akinamama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano. (Kipengere 5.3.4 chenye Tamko linalosema "Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inayotoa huduma bila faida na mashirika ya Kimataifa itaendelea kutoa huduma bila malipo kwa wanawake wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano").

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vituo vya binafsi visivyo na ubia na Serikali ukamilishaji wa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote utakapopitishwa utakuwa suluhisho la tatizo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini nilitaka kujua ni mpango upi wa kupunguza kabisa gharama hasa za mama mjamzito anapojifungua kwa operesheni, ambapo Temeke tunalipa laki mbili kwa operesheni na Vituo vya Afya ni shilingi laki moja; je, mpango huo ukoje wa kupunguza kabisa gharama hii?

Swali la pili; je, kuna mkakakti gani wa kufanya ili sasa Serikali itoe vifaa vile ambavyo akina mama tunapokwenda kujifungua tunaambiwa tununue pamba viwembe vile na kadhalika.

Je, Serikali ina mpango mkakati gani sasa wa kuweka vile vifaa ndani ya hospitali zote ili tusiweze kununua. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninampongeza kwa jinsi ambavyo anafuatilia masuala haya kwa ukaribu kwenye Jimbo lake. Niseme tu kwamba suala ni la kisera kwamba mama mjamzito na watoto chini ya miaka mitano hawatakiwi kulipishwa. Ninaomba Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa tuweze kushirikiana pamoja kusimamia hili takwa la kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dar es salaam kwa kweli nilitembea kwenye baadhi ya vituo vya afya na hospitali za Wilaya nilichogundua ni kwamba, unaweza ukakuta Kituo cha Afya kinapata wagonjwa wengi kuliko hata baadhi ya hospitali za Wilaya. Kwa hiyo, wakati mwingine mgao wanaoupata *MSD* unakuwa mdogo kiasi kwamba wanaishiwa mapema kulingana na idadi ya watu, hata kwa mwaka ni zaidi ya 160,000 watoto wanazaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni nini? Kwamba mgao wanaoupata *MSD* ni mdogo ukilinganisha na idadi ya watu, kwa hiyo tutakwenda sisi kama *MSD* kufanya kuhakikisha inatolewa mgao wa dawa na vifaa kulingana na idadi ya watu na siyo kuangalia kituo, aidha ni kituo cha afya au na ku-*generalize*. Hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwamba naomba kama Mheshimiwa anaweza akarudia swali lake la pili.

**NAIBU SPIKA:** Swali la pili rudia kwa kifupi na wewe jibu kwa kifupi.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mna mkakati gani wa kuweka vifaa kama *gloves*, pamba, viwembe katika hospitali hizi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie tu mkakati ndiyo huo, kwamba tukiweza kwa Dar es Salaam ambapo unakuta kituo cha afya kinapata wagonjwa kuliko hata baadhi ya Hospitali za Wilaya sehemu nyingine, tukienda kuwapa vifaa kulingana na idadi ya wagonjwa badala ya kuangalia ni *statu*s gani hospitali inayo, maana yake hawatakuwa tena na huo upungufu na pale *MSD* zimenunuliwa *kit* za kutosha kwa ajili ya akina mama kujifungua. Hivyo hilo tatizo litaenda kuisha, nafikiri shida kwako ni idadi ya watu kwa hiyo kinachopelekwa kinakuwa kidogo sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara hiyo Mheshimiwa Hokororo.

Na. 99

**Huduma za Afya kwa Watoto Njiti**

**MHE. AGNES E. HOKORORO** aliuliza:-

Je, kwa nini huduma za afya kwa Watoto Njiti zinatozwa fedha ilihali Sera ya Afya inaelekeza huduma bure kwa Watoto chini ya miaka mitano?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Elias Hokororo, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utoaji wa huduma za afya kwa watoto chini ya miaka Mitano wakiwepo Watoto Njiti kwa vituo vya Serikali na vile vya binafsi vilivyo na ubia na Serikali ni bure na ni takwa la kisera.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukamilishaji wa Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote utamaliza utata huu kwa wananchi wanaotibiwa katika vituo binafsi vya huduma za afya.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Hokororo

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mhesimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba niulize maswali madogo mawili. Kwa kuwa katika majibu ya msingi amesema matibabu ya wototo njiti hayatozwi, lakini kwa kuwa mpaka sasa huduma hizo zinatozwa;

Je, Serikali iko tayari kurejesha fedha ambazo wazazi waliojifungua watoto njiti walizitoa?

Kwa sababu ninayo madai ya mama anayedaiwa milioni moja na laki nane katika Hospitali ya Muhimbili.

Mhesimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watoto njiti wamekuwa na changamoto mbali mbali za kiafya zinazowakosesha pengine kuendelea kuishi vema sawa sawa na watoto wengine;

Je, Serikali iko tayari kufanya mapitio ya likizo ya uzazi kwa wazazi wanaojifungua watoto njiti?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mhesimiwa Naibu Spika, nijibu maswali yake mawili kama ifuatavyo: -

Mhesimiwa Naibu Spika, moja; nitoe agizo kwa hospitali zote lakini vile vile mfuko wetu wa bima ya afya, kwamba suala la watoto njiti kama ni mama amejifungua na mtoto njiti au wakati wowote bima ya afya iweze kumuhudimia kama ni mwenye bima ya afya. Kuhusu kwamba wakizaliwa kwenye hospitali zetu zote watibiwe bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Hokororo amesema je Serikali iko tayari kwa sababu ana ushahidi wa hospitali ambayo wanatoza. Ninakuomba Mheshimiwa Mbunge nikishakaa uje unionyeshe halafu tufuatilie nini kilichotokea. Siwezi kukuambia kwamba zitarudishwa lakini tutampata anayefanya hivyo na tuweze kumpa maelekezo mazuri, ili suala hilo lisijitokeze tena.

Mhesimiwa Naibu Spika, lakini la pili, suala la sheria ya likizo, hilo sasa ni la kisheria sio suala la Wizara ya Afya, lakini nimeshasikia kuna harakati hizo zinaendelea na kuna majadiliano ndani ya Serikali kuona hilo linafanyikaje. Tungojee hayo majadiliano ndani ya Serikali halafu yakifikia muafaka tunaweza tukajua ni nini kitakachofanyika. Kwa sababu hilo si suala la Wizara ya Afya pekee yake, hilo linahitaji masuala mengi kama vile utumishi, Wizara ya Katiba na mambo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

Na. 100

**Hitaji la Majosho – Msalala**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga majosho ya kuogesha mifugo katika Halmashauri ya Msalala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, (Mb), kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilifanya ukarabati wa majosho matano (5) katika kata za Burige, Lunguya, Mega, Ntobo na Ngaya zilizoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala. Aidha, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majosho katika halmashauri mbalimbali nchini; ikiwemo Halmashauri ya Msalala. Pia Serikali inaendelea kuhamasisha wafugaji kuchangia ujenzi wa miundombinu ya mifugo ikiwemo ujenzi wa majosho. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassim.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza niipongeze Serikali kwa kutenga fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya ukarabati wa majosho matano. Nilitaka kuuliza swali langu la kwanza, kama Serikali ilitenga fedha kukarabati majosho haya Matano;

Je, fedha zilizotengwa kwenda kukarabati majosho Kata ya Ngaya na Ntobo zilikwendwa wapi na kama zipo Wizarani, ni lini sasa fedha hizo zitakuja kukarabati majosho hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa tulipokea barua iliyotuonesha kwamba tutaletewa majosho Matano, na Mkeka uliotoka, kwa maana ya idadi ya majosho ya mwaka huu haijaonyesha Msalala kuwemo.

Je, ni lini sasa Wizara itatuletea majosho hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza; majosho mawili pesa zake hazifahamiki zilipo na kwa hivyo ninaomba nimueleze tu kwa mujibu wa utaratibu wa ujenzi wa majosho haya. Utaratibu wote wa manunuzi hufanywa na halmashauri ya wilaya. Baada ya kuwa wamekamilisha taratibu zote za manunuzi hutuletea Wizarani ambapo Katibu Mkuu wa Mifugo huenda kuziombea pesa zile Hazina. Ikiwa kama katika kata alizozitaja na hivyo vijiji alivyovitaja liko hilo tatizo, niko tayari mimi kumpa ushirikiano Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, kufanya uchunguzi kwa kutumia wataalam wetu ili tuweze kubaini wapi mkwamo huu ulikotokea na baadaye kuweza kuwanusuru wananchi wa pale Msalala.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ni hili la kata alizozitaja ambazo zilikuwepo lakini sasa anaona katika mkeka huu wa mwaka huu hazipo. Naomba nimuhakikishie, Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan imetenga pesa za

kutosha na mpaka sasa tumeshapeleka kiasi cha shilingi bilioni 5.4. Naomba nimuhakikishie tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi hivi vijiji vinavyohitaji na anavyosema vilikuwepo katika mkeka nivipate tena ili tuweze kufanya ufuatiliaji wa pamoja wa kuona wapi palikosewa tuparekebishe na hatimaye wananchi wale waweze kupata ile huduma ya josho na hatimaye kuhudumia mifugo ile. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwenye Tarafa yangu ya Ingo yenye kata kumi na Ichuku kata tano, Inano kata tano hakuna josho hata moja katika eneo hilo. Nini mpango wa Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waitara aainishe mahitaji yake, ashirikiane na Mkurugenzi wake Mtendaji alete Wizarani tutamhudumia kwa jambo hili katika Bajeti ya Mwaka 2023/2024 ambayo tunaielekea sasa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Regina.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri alipofanya ziara kule Wilayani Simanjiro aliahidi Serikali kuipatia Wilaya ya Simanjiro majosho 22 lakini mpaka sasa tumepokea majosho mawaili tu. J

e, Serikali ni lini itajenga majosho katika vijiji vyote ambavyo havina kabisa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Regina, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yalikuwa ni vijiji 22, hadi sasa wamepata majosho mawili. Mgawanyo wa majosho haya nchi nzima ni mkubwa kwa mahitaji na kwa hivyo huwa tunatenga kulingana na bajeti yetu. Haya waliyoyapata ni mwanzo na zoezi la kuendelea kupangiwa fedha linaendelea, tayari nimeshazungumza na Mheshimiwa Ole-Sendeka, alinisisitiza kuhakikisha kwamba yale yaliyosalia tuyapate. Ninataka nikuhakikishie Mheshimiwa Regina na Mheshimiwa Ole-Sendeka na Wanasimanjiro, mtapata; katika bajeti zinazoendelea kutengwa na ninyi Simanjiro mtaendelea kupata fedha hizo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi

Na. 101

**Adhabu kudhibiti vifo vya akina mama**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa adhabu kali kudhibiti vifo vya akina mama vinavyosabishwa na waume au watoto wao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Kanuni ya Adhabu imeweka adhabu ya kosa la mauaji ya kukusudia kuwa ni kunyongwa hadi kufa. Aidha, kwa makosa ya mauaji bila kukusudia Mahakama inaweza kutoa adhabu nyingine yoyote kulingana na mazingira na namna kosa lilivyotendeka. Hata hivyo kwa kosa la mauaji ya bila kukusudia sheria imeweka adhabu ya juu ya kifungo cha Maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Adhabu ya Kunyongwa hadi kufa ndiyo adhabu kali kuliko zote hapa nchini pamoja na ulimwenguni kote. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwinyi.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza;

Kwa kuwa watuhumiwa wa matukio haya wanaachiwa huru kwa kigezo kwamba ushahidi haujapatikana.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha kitengo cha ushahidi na uchunguzi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nini mpango wa Serikali wa kuzuia mauaji haya ili kuwanusuru wanawake hawa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza linaonesha kwamba kumekuwa na muda mrefu wa kesi hizi zikiwa na visingizo vya kupatikana kwa ushahidi wa haraka. Kesi za mauaji zina utaratibu wake katika upelelezi wake. Walio wengi wanafikiri ni jambo la mara moja katika kufikia maamuzi ya upelelezi unaohusisha mauaji, lakini kwa namna yeyote ile muda uliowekwa na mahakama na vyombo vya upelelezi umekuwa ukizingatiwa sana katika masuala ya kesi hizi za mauji na hivyo hatuna kumbukumbu sahihi za watu ambao wamekaa magerezani muda mrefu kuliko kile kipindi ambacho tumekiweka kama dhamirio la kuwapa nafasi wapelelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu namna ya kuzuia mauaji haya; hili ni jambo la kijamii. Mambo haya mengi yamekuwa yakitokea kwenye jamii zetu na sisi wanajamii ndio tunastahili kuyakemea maana ni maisha yetu ya kila siku ambayo yanasababisha mauaji haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kumpa maelezo muuliza swali; ni kwamba si mauaji tu kwa kina mama na watoto ukienda pale Njombe, nimetembelea Gereza la Njombe, asilimia 75 ya akina mama waliopo mle jela wakisubiri hizo kesi wanahusishwa na mauaji ya kuwaua waume zao. Kwa hiyo unaweza ukaona jinsi ambavyo mauaji haya yanajiografia zake; na mengine yote haya yanayojitokeza kweye jamii zetu wakemaji namba moja lazima tuwe sisi wenyewe wanachi katika maeneo yetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la matukio ya wanafunzi kupewa adhabu kali ya viboko shuleni inayosababisha majeraha,

kuzimia, kulazwa na hivyo kushindwa kuhudhuria shule ipasavyo.

Je, Serikali haioni ipo haja ya kuweka adhabu kali kwa waalimu wanaofanya vitendo hivi ili kuwalinda watoto wetu shuleni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ongezeko la adhabu zisizo na kiasi kwa wanafunzi kule shuleni, na kwamba anaomba adhabu kali zitolewe kwa waalimu wale ambao wanachukua sheria mkononi; kimsingi limekuwa ni tatizo. Kila siku naona kwenye mitandao hatua ambazo walimu wanachukua. Mimi niwasihi, hasa walimu, kwa sababu tunayo sheria ya elimu inayotoa utaratibu wa adhabu kwa watoto wetu. Pale mtu anapochukua sheria mkononi atashtakiwa kama mhalifu mwingine yeyote ambaye ametumia nguvu katika kutoa adhabu kwa watoto wetu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Kabati.

Na. 102

**Sheria ya Wamiliki wa Vyombo vya Usafirishaji**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza: -

Je, ni lini serikali italeta sheria ya wamiliki wa vyombo vya usafiri kuwa na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dokta Ritta Kabati, Mbunge wa viti maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2019, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilipitisha Sheria ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)* na kuweka kifungu katika Sheria hiyo kinachozingatia uwepo wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 6(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 413, kimeeleza kuwa moja ya Majukumu ya *LATRA* ni kuhakikisha uwepo wa huduma ya usafiri wa umma unaoweza kutumiwa na watu wote wakiwemo watu wenye vipato vya chini, waishio vijijini, na watu wenye mahitaji maalum ambayo inajumuisha watu wenye ulemavu. Aidha, Kifungu cha 5(c) (i) na (ii) kimeeleza kuwa moja ya Kazi za *LATRA* ni kuweka viwango vya bidhaa na huduma pamoja na vigezo na masharti ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2022, Kifungu cha 5(1) na (2) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura ya 415…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, *order please*, makelele yamekuwa mengi ndani ya Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):**... kilirekebishwa kwa kuiondolea *LATRA* jukumu la kuweka viwango vya bidhaa na huduma zinazodhibitiwa. Jukumu hilo kwa sasa linatekelezwa na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* ambalo ndilo lenye dhamana ya kuweka viwango vya bidhaa na huduma mbalimbali nchini. *LATRA* imebaki na jukumu la kusimamia utekelezaji wa viwango na kuweka masharti na vigezo vya bidhaa na huduma zinazodhibitiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naielekeza *LATRA* ishirikiane na *TBS* katika kuweka na kusimamia utekelezaji wa viwango vya vyombo vya usafiri wa umma ili viwe na miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza nishukuru sana majibu ya Serikali, lakini sisi humu sote ndani wote ni watu wenye ulemavu watarajiwa na lazima tukiri kwamba mtu mwenye ulemavu hawezi kutoka *point A* kwenda *point B* kwa kutumia vyombo vya usafiri kwa sababu miundombinu haikidhi haja kabisa na katika jibu la Waziri amesema kwamba kuna *TBS* kuna *LATRA* ambao wanatakiwa kuangalia hivyo viwango;

Je, ni ipi sasa kauli ya Serikali kutoka na hili jambo ili watu wenye ulemavu na wenyewe wapatiwe haki ya msingi ya kupanda haya mabasi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali langu la pili, watu wenye ulemavu wamekuwa wakinyanyapaliwa sana katika vituo vya mabasi na madaladala wakati wa kuingia katika hivi vyombo, kwa sababu kuna watu wasioona kuna watu

ambao hawawezi kutembea unaona kwamba wanapata manyanyaso makubwa sana.

Je, ni utaratibu gani mzuri sasa ambao umewekwa kuhakikisha kwamba hawanyanyaswi na wanawekewa mpango mzuri wa kupanda katika hivi vyombo vya usafiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa balozi mwema wa watu wenye ulemavu. Kwa swali la kwanza anataka asikie kauli ya Serikali, kauli ya Serikali ni hii; kwanza natoa wito kwa wamiliki wote wa vyombo vya usafiri, daladala pamoja na mabasi na kwa kushirikiana na *LATRA* pamoja na *TBS* wahakikishe ya kwamba wanaweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuwanyanyapaa watu wenye ulemavu hususan katika maeneo ya stendi ama mabasi, hili tunatoa onyo kali sana kwa sababu watu wenye ulemavu ni binadamu kama binadamu mwingine yeyote na ahaki zote za msingi. Kwa maana hiyo, kupitia vyombo vyetu vya sheria na kupitia Jeshi la Polisi pamoja na *TARURA* pamoja na *TANROADS* kuhakikisha kwamba miundombinu yote wezeshi hususan barabara pamoja na mabasi kwa maana ya vyombo vya usafiri kwa wale wamiliki tunaweza kuhakikisha hivyo vinawekwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nisisitize hapa suala la kisheria kwa mtu yeyote atakayeonewa, tutahakikisha

tunachukua sheria kali sana na itakuwa fundisho kwa watu wengine wote wanaonyanyapaa na kuwanyasa watu wenye ulemavu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa tunaendelea Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Ndugulile.

Na. 103

**Ujenzi wa Barabara za Kigamboni kwa kiwango cha lami**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itazijenga barabara za Kibada – Mwasonga – Tundwi – Songani na Ngomvi – Kimbiji hadi Pembamnazi kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa naiaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi ninapenda kujibu Swali la Mheshimiwa Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami kwa Barabara ya Kibada-Mwasonga, Tundwi-Songani hadi Kimbiji yenye urefu wa kilometa 41 zimetangazwa tarehe 6 Januari, 2023 na zitafunguliwa tarehe 17 Februari, 2023. Kwa upande wa Barabara ya Ngomvu – Kimbiji hadi Pemba Mnazi yenye urefu wa kilometa 27, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika na sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Wizara ya Ujenzi na majibu yenye faraja kwa wakazi wa Kigamboni hususan maeneo ya Mwasonga, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* ilifanya ujenzi wa kipande kidogo cha kilometa moja kutoka Kibada *junction* kwenda Mwasonga. Sasa hivi ni zaidi ya mwaka mmoja na nusu, kipande kile cha kilometa moja hakijakamilika.

Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa kile kipande cha kilometa moja ambao ujenzi wake umeanza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; barabara nyingi pale Kigamboni zimemeguka kutokana na kukosa kingo kutokana na magari mazito kuchepuka nje ya barabara na kwingine barabara zimekatwa kashata kutokana na ubovu lakini hazijakarabatiwa. Sasa ni lini barabara zile zitakarabatiwa lakini vile vile kuwekwa kingo ili barabara zile zisiendelee kumomonyoka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli mkandarasi ambaye alipewa kazi ya kukamilisha kipande cha kilometa moja amechelewa na tayari ameshaandikiwa barua na anatumikia adhabu ya *liquidated damage* na kama atakuwa hajakamilisha ndani ya siku 100, tunafunga

mkataba kumtafuta mkandarasi mwingine. Hivi tunavyoongea yupo anakamilisha hiyo kazi na yuko kwenye 75%-80%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mashimo na kingo za barabara, tayari tumesham-*engage* mkandarasi, *Mark Construction* na ameshaanza kazi na kuharibika kwa barabara hii ni kweli ni barabara ya zamani, *traffic* imeongezeka sana na magari mengi makubwa yanapita. Kwa hiyo tayari mkandarasi yupo kwa ajili ya kukarabati barabara hizo za lami. Pia hata hizo za changarawe tumeshamweka mkandarasi kuhakikisha kwamba anakarabati hizo barabara, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Teclas.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ni lini Barabara ya Masasi – Nachingwea - Liwale itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Teclas Ungele, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja sasa hivi zinafanyiwa *evaluation,* ndiyo moja ya barabara ambazo ziko kwenye *EPC+F*. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oran.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa Barabara ya Mbalizi - Shigamba ni

ahadi ya muda mrefu ya viongozi wetu na pia ni kiungo muhimu kwa Tanzania na Malawi. Je, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi, ajiandae Mheshimiwa Paresso.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyoongea sasa hivi, Mhandisi Mshauri yuko *site* akifanya usanifu wa kina na baada ya hapo, barabara hii itatafutiwa fedha kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Karatu – Njiapanda - Mang'ola - Lalago kwa kiwango cha lami. Je, ni lini ahadi hii itatekelezwa ili barabara hiyo ijengwe kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ahadi hiyo ipo ya kujenga hiyo barabara ya Karatu hadi Lalago kwa kiwango cha lami. Serikali bado haijaufuta mpango huo, inaendelea

kutafuta fedha na fedha zikipatikana basi barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nataka kujua ni lini Barabara ya Nyakanga kwenda Nyaishozi kuja mpaka Benako itajengwa kwa kiwango cha lami, kwa sababu ni barabara kuu inaunganisha Tanzania na Rwanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tumeshaanza kuijenga kwa kiwango cha lami kilometa 60 na barabara iliyobaki, *African Development Bank* wako kwenye majadiliano ili kuikamilisha yote kuunganisha Tanzania, Burundi na Rwanda.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.  Mheshimiwa Mama Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Barabara ya Dar es Salaam inaunganisha baina ya Dar es Salaam na Pwani. Vilevile barabara hizi ni kiunganishi kati ya Mkuranga na Ilala ambayo ni Kiguza – Hoyoyo – Mwanadilatu - Msongola. Sasa lini barabara hizi zitajengwa kwa kiwango cha lami?  *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi ni muhimu kama alivyozitaja na zinaunganisha barabara kuu na barabara hizi ambazo tunasema ni *feeder roads.* Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kufanya usanifu wa kina na baadaye ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ally. Ajiandae na jirani yako hapo Mheshimiwa Samwel.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Kiranjeranje - Makangaga – Nakiu - Nanjilinji na hatimaye Ruangwa imefikia hatua gani ili ijengwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii imeshafanyiwa usanifu na Serikali inatafuta fedha kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Kiranjeranje hadi Ruangwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Samweli.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itajenga Barabara ya Mogitu - Hydom kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, barabara aliyotaja Mheshimiwa Hhayuma, ni *link* kati ya Barabara ya Babati - Hydom kwenda Sibiti. Kwa hiyo itakavyoanza kujengwa, hicho kipande kitakuwa ni sehemu ya hiyo barabara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, halafu Mheshimiwa Mtenga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali, barabara ya kutoka Chimara kwa maana ya Mfumbi kuelekea Matamba-Kitulo, kilometa 51. Barabara ambayo inaelekea kwenye hifadhi ya utalii. Ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hii kwa sababu upembuzi yakinifu ulishaanza kufanyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuifungua barabara hii kwa ajili ya kuunganisha maeneo ya Chimara - Itamba hadi Makete, lakini pia tunajua tutakuwa tunafungua utalii eneo hilo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga, halafu Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa barabara ya kutoka Mtwara mpaka Msimbati, ambayo takribani sasa ina zaidi ya miaka 15, barabara hii inajengwa kwa vipande vipande? Sasa hivi wamejenga kilometa tano tu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamsikia vizuri kuhusu barabara aliyoitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtenga, rudia tena swali lako.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo inatoka Mtwara kwenda Msimbati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mtwara kwenda Msimbati.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wameshajenga kwa kiwango cha lami kilometa tano tu zaidi ya miaka 12.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtenga, Mbunge wa Mtwara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tunajenga kwa awamu kadiri fedha inavyopatikana. Azma ya Serikali ni

kujenga barabara yote. Kwa hiyo Serikali inatafuta fedha ili zikikamilika basi tuweze kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kufanya upembuzi yakinifu Barabara ya kutoka Nyoni hadi Mipotopoto-Mitomoni kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer* Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo kwenye ilani hii barabara kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami na tunategemea katika bajeti ijayo iweze kuingia ili iweze kufanyiwa usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na wewe.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha na maswali yamekwisha. Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni walioko Jukwaa la Spika, wageni wanane wa Bunge kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambao ni Ndugu Charles Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo pia Ndugu George Haule, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Ndugu Wendi Massoy, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Ndugu Benja Majura, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Ndugu Salhina Mkumba, Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Ndugu Patrick Bwelindo, Mkaguzi Mkuu wa Bunge; Ndugu Edwin Rweyemamu, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na Ndugu Gabriel Ntego, Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Jukwaa la Spika wanaendelea; wapo wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara ambao ni Maafisa kutoka Ubalozi wa Marekani wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Biashara ya Serikali ya Marekani, Bi. Marisa Lago; ameambatana na Maafisa wa Ubalozi ambao ni Ndugu Christina Killingworth, Mnadhimu; Ndugu Susannah Marshall, Mkurugenzi wa Afrika; Ndugu Fred Stewart, Afisa Dawati la Afrika Ubalozi wa Marekani; Ndugu Ken Walsh, Afisa Biashara Mwandamizi; Ndugu Andrew Mahiga, Mtaalam wa Biashara Ubalozi wa Marekani; Ndugu Talha Waziri, Afisa Mambo ya Nje Mkuu; na Ndugu Samwel Weber, Afisa Dawati Ofisi ya Afrika, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 50 wa Mheshimiwa Noah Lemburis Mollel ambao ni Wenyeviti na Makatibu wa Kata kutoka Arumeru Magharibi, Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Paschal Patrobass, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Wenye Ulemavu ambaye ni Katibu wake kutoka Jimboni Shinyanga, Ndugu Samwel Jackson. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhani ambao ni Madiwani kutoka Chake Chake, Mkoa wa Kusini Pemba. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Makoa ambao ni Mwenyekiti wa CCM, Ndugu Hija Suru na Katibu CCM, Ndugu Ibrahim Mpwapwa kutoka Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma, Kazi iendelee Kondoa huko. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Ally Kassinge ambao ni Watendaji wa *RUWASA* na Meneja *RUWASA* kutoka Wilaya zote za Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha St. John cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Simon Songe ambao ni Viongozi wa Kanisa la *Mennonite* Tanzania kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Vita Kawawa ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Namtumbo. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Martha Mariki ambao ni Wawakilishi wa UWT kutoka Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni jamaa zake kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Japhet Hasunga ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 40 wa Mheshimiwa Hasunga ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambao ni wanachama wa *UDOM*

*Health Club* wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Paschal Lucas. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 90 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi ya St. Monica ya Jijini Arusha. Karibuni. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma Kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022 na

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)*. *(Makofi)*

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli zinazotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma *(Public Investment Committee)* kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako

Tukufu na kupata fursa ya kuwasilisha Taarifa hii ya Kamati. Kutokana na ufinyu wa muda, naomba Taarifa hii yote kama ilinavyosomeka katika kitabu cha Kamati iingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023. Wasilisho hili ni kwa mujibu wa Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya taarifa hii ni kueleza yatokanayo na shughuli za Kamati kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma na kuliwezesha Bunge kujadili hali hiyo na kufikia uamuzi kwa mfumo wa hoja Bungeni. Ili kufanikisha azma hiyo, taarifa hii inaeleza kwa undani shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati kuanzia mwezi Februari, 2022 hadi mwezi Januari, 2023 kama ilivyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Tano. Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili inafafanua shughuli za Kamati; Sehemu ya Tatu inafanya majumuisho ya maoni yanayotokana na shughuli zilizotekelezwa; Sehemu ya Nne inahitimisha hoja kama ilivyoelekezwa na kanuni ya 61(3) ya Kanuni za Bunge ili kuliomba Bunge lifanye uamuzi; na Sehemu ya Tano na ya mwisho ni kiambatanisho kinachohusu orodha ya Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyokutana na Kamati kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa shughuli zote za Kamati hii ni utekelezaji wa madaraka ya Bunge yanayofafanuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo

la Juni 2020, Sheria ya Msajili wa Hazina ya Mamlaka na Majukumu, Sura ya 370.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria nyingine ambazo pia zilisaidia kuona vigezo vya uendeshaji na matumizi ya mitaji ya umma ni Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410, Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348, Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257 na Sheria ya Bajeti, Sura ya 439.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia mwongozo wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni mwaka 2020, kifungu cha 12 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu hicho kinaifunga kazi ya Kamati kwenye masuala makuu mawili ambayo ni kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma ina nafasi ya kuwa umezingatia taratibu, sheria, miongozo mujarabu ya biashara na kuchambua na kujadili taarifa zinazohusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache. Kwa utaratibu huo shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2022 mpaka Januari, 2023 zilipangwa kutokana na taarifa ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa hizo, Kamati ilipokea Taarifa ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kila shirika na taasisi kadri zilivyopangwa kulingana na matokeo ya mapitio ya taarifa kuu ya Msajili wa Hazina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi wa taarifa hizo umeiwezesha Kamati kufuatilia utekelezaji wa mitaji ya umma kama ilivyoripotiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa taarifa hii iliwasilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, naomba kubainisha njia na mbinu *(methodology)* zilizotumika kufanikisha majukumu ya Kamati kama inavyoelekeza Kanuni

ya 142 ya Kanuni za Bunge. Mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti *(Reliability)* na ustahiki…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu subiri kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, leo tuna mijadala Kamati tatu, na mijadala yote ni muhimu, lakini naona zogo na mazungumzo humu ndani yamezidi. Kila mtu arudi kwenye kiti chake. Kukaa kwenye kiti ambacho siyo chako ni kinyume na kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti endelea.

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kamati ilitumia njia nne kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya Kamati kuripoti Bungeni shughuli zilizotekelezwa, ni kuliwezesha Bunge kubaini mafanikio na changamoto zilizopo katika uwekezaji wa mitaji ya Umma. Madhumuni hayo yatatimia kwa kubainisha shughuli zilizotekelezwa pamoja na yatokanayo na shughuli hizo. Kwa ajili ya urahisi wa mtiririko, shughuli hizo zimegawayika katika makundi makuu manne kama yalivyoainishwa kwenye taarifa ya Kamati. Taarifa hii inatoa ufafanuzi wa kina wa shughuli hizo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kwa kupitia taarifa mbalimbali za uwekezaji. Vigezo vilivyozingatiwa vilitokana na masharti ya Kanuni za Bunge yanayoitaka Kamati kujiridhisha iwapo uwekezaji huo una tija na kama umezingatia sheria, taratibu na miongozo mbalimbali ya biashara. Katika kufanya

hivyo, Kamati ilipitia Taarifa za uwekezaji wa Mitaji ya Umma katika mashirika na taasisi za umma 47. Orodha ya taasisi na mashirika hayo yapo kwenye Kiambatisho Na. 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uchambuzi, dhima ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ilizingatiwa na kuangalia uwekezaji wa mitaji ya umma ndani na nje ya nchi. Kwa ujumla, Kamati ilizingatia thamani ya uwekezaji iliyofikia Shilingi trilioni 67.95 ambapo kiasi cha Shilingi trilioni 66.27 ni thamani ya uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma 237 na kiasi cha Shilingi bilioni 932.83 kikiwa ni mtaji wa umma katika kampuni 40 ambazo Serikali inamiliki hisa chache hadi kufikia mwaka 2020/2021. Kiasi hicho katika kampuni, Serikali inamiliki hisa chache, kilifikiwa kutokana na ongezeko la mali *(an increment in reserves)*, ongezeko la thamani ya hisa za Serikali *(Government's Shareholding)* na ongezeko la mtaji *(Capital Injection)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo hayo yanaonesha kuwa uwekezaji wa Serikali katika taasisi na mashirika ya umma, unachangia zaidi ya asilimia 95 ya uwekezaji wote wa mitaji ya umma. Kwa msingi huo, uchambuzi wa rejesho la mitaji ya umma *(Returns on Investment)* uliofanywa na Kamati, ulizingatia umuhimu wa kutofautisha uwekezaji wa uendeshaji *(Investment on Operating Capital)* na uwekezaji usio wa uendeshaji *(Investment on non-operating capital)*. Lengo la Kamati kujielekeza kwenye ainisho *(classification)* la uwekezaji huo, ni kuwezesha uchambuzi wa matokeo ya uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma kuwa na uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na shughuli hiyo, Kamati ilitoa Taarifa yake Bungeni wakati wa Mkutano wa Tisa wa Bunge, Mwezi Novemba, 2022. Taarifa hiyo ililiwezesha Bunge kupitisha maazimio yanayotarajiwa kufanyiwa kazi na mamlaka ya Utendaji nchini. Ni ahadi ya Kamati kwamba,

itaendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma. Aidha, kwa maeneo ambayo hayakuwa yamefanyiwa kazi wakati huo, Kamati inayaripoti Bungeni kupitia Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichambua utendaji wa taasisi na Mashirika ya Umma ili kujiridhisha kama uwekezaji katika mashirika na taasisi hizo unaweza kuwa na tija. Matokeo ya uchambuzi huo yalionesha mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto iliyojitokeza baada ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* kuongezewa Idadi ya Hifadhi. Shirika la Hifadhi za Taifa *(TANAPA)* linasimamia hifadhi za Taifa 22 zenye ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 104,578 kwa sasa, wakati za mwanzo zilikuwa hifadhi 16 ambazo zenye kilometa za mraba 57,107. Maeneo yaliyoongezeka yanajumuisha hifadhi sita zilizoanzishwa mwaka 2016 ambazo ni Burigi - Chato, Ibanda - Kyerwa, Rumanyika - aragwe, Mto Ugalla, Kigosi na Hifadhii ya Nyerere, zenye ukubwa wa kilometa za mraba 47,471 ambazo ni sawa na asilimia 45.4 ya eneo lote linalosimamiwa na Shirika kwa sasa. Kwa ujumla, eneo linalosimamiwa na shirika ni sawa na asilimia 11.6 ya eneo lote la nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuongeza hifadhi nchini ili kuvutia watalii wengi, hivyo nchi kupata mapato zaidi, kuna changamoto ya upungufu wa fedha za uendeshaji na za utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ambayo inachochea ukuaji wa sekta ya utalii, kwa kuwa bajeti iliyokuwa inatumika kwa hifadhi 16 ndiyo hiyo hiyo inayotumika sasa kwa hifadhi 22, pamoja na kanda nne, vituo vitano vya malikale na ofisi mbili kiunganishi zilizopo Dar es Salaam na Dodoma. Hali hii inapelekea *TANAPA* kushindwa kuitika kwa haraka kwenye shughuli za dharura,

ulinzi na usalama na kuzorota kwa utoaji wa huduma za kitalii na kuwa, uwekezaji unaofanywa kwenye hifadhi hizi haufanywi kwa ufanisi, hivyo kupelekea kukosa tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na changamoto ya upatikanaji wa mitaji ya uwekezaji kwa wakati kwenye Taasisi, Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali na Kampuni ambazo Serikali inamiliki hisa na Mfuko ambao unakuwa na fedha maalum wakati wote kwa ajili ya uwekezaji *(Investment fund)*. Hali hiyo ya kukosekana kwa rasilimali fedha kwa wakati sahihi ili kuendana na uhitaji wa wakati huo kwa lengo la kutumia fursa zinazojitokeza kunaathiri uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya taasisi ambazo Kamati ilikutananazo na kupitia na kuchambua taarifa za kiutendaji kipindi hiki ambazo zina changamoto za mtaji, ni Wakala wa Umeme na Ufundi *(TEMESA)* na Shirika la Viwango *(TBS)* ambapo yanakabiliwa na upungufu wa mtaji hivyo kupunguza ufanisi na tija katika utekelezaji wa shughuli zake, hali inayopelekea taasisi na mashirika haya kuwa na mchango mdogo au kutokuchangia kabisa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo Kamati ilikutana nayo ikiwemo *TRA, TPA* na *BoT,* moja ya changamoto kubwa ni mifumo duni na kuwa na mifumo mingi isiyosomana ya TEHAMA. Kutokana na changamoto hii ya mifumo, kunapunguza ufanisi kwenye ukusanyaji wa mapato, kwani mapato mengi yanapotea kutokana na kuwa na mifumo isiyosomana. Pia mifumo duni inakwamisha na kuzorotesha shughuli za kiutendaji, kibiashara na kiuwekezaji, hivyo kukosekana kwa ufanisi na tija ya mitaji ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msongamano wa shehena katika Bandari Dar es Saalam *(TPA),* Kamati inaipongeza Serikali kwa kuteua Bodi mpya ya Mamlaka ya Bandari na kufanya mabadiliko katika menejimenti yake. Hatua hii inaonesha nia njema ya Serikali ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Mamlaka ya hii ya Bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa inaendelea kupanuliwa kwa kuongeza gati na kina kwa ajili ya meli kutia nanga kwa ajili ya kushusha shehena za mizigo. Kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba, 2022, Bandari hii imepokea na kupitisha mizigo jumla ya tani milioni 10.4 ambayo ni rekodi ya juu tangu kuanzishwa kwake, hivyo kuisababishia Mamlaka ya Mapato Tanzania nayo kuvunja rekodi ya mapato kwa kukusanya Shilingi trilioni 11.6, ambapo katika makusanyo ya *TRA* asilimia 41 ya ushuru wa forodha yanatokana na huduma zinazotolewa na *TPA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio hayo, bado kumekuwa na changamoto ya msongamano wa shehena za mizigo, kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa bandari na kukosekana kwa mapato ya forodha kwani wanashindwa kushusha baadhi ya shehena za mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam. Changamoto hizi zinaisababishia Bandari ya Dar es Salaam kushindwa kushindana na Bandari za karibu ikiwemo Bandari ya Mombasa, Kenya na Bandari ya Beira iliyopo Msumbiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu tarehe 4 Novemba, 2022 ambapo pamoja na Maazimio mengine yaliyotolewa kwa Serikali, kulikuwa na azimio mahususi kuhusu deni la pamba kwa wanunuzi wa zao la pamba katika msimu wa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya azimio hilo, na kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta Ndogo ya Pamba nchini, Kamati katika pindi hiki kiliomba kukutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Kilimo na Bodi ya Pamba ili kupata hali halisi ya deni lenyewe, kiasi kinachodaiwa, kuwa kimelipwa na Serikali, hatua Serikali inazochukua ili kulipa deni hilo na mwisho kujua ni lini Serikali itakamilisha kulipa deni hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitaarifiwa kwamba hadi sasa deni lililopo ni jumla ya Shilingi bilioni 102.51 ambayo inajumuisha hasara ya Shilingi bilioni 21.879 kwa Kampuni zilizonunua pamba na kiasi cha Shilingi bilioni 80.63 ni madai ya watoa huduma za pembejeo ambao wangelipwa kwa fedha ambazo zingetokana na makato ambayo Serikali iliyafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Kamati imekutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Waziri wa Kilimo, na kutokana na taarifa na maelezo ya kina waliyotoa mbele ya Kamati, yanaonesha jitihada za makusudi za Serikali kulipa deni hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Februari, 2022, Bunge lako Tukufu lilipitisha maazimio14 yaliyotokana na Taarifa ya Kamati kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari 2022. Chimbuko la Maazimio hayo, ni nia ya kupata ufumbuzi wa changamoto zilizokwamisha kufikiwa kwa matarajio ya uwekezaji wa mitaji ya umma. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi lilitoa maazimio hayo yanayoonesha matarajio yake katika uwekezaji wa mitaji ya umma. Hivyo, ni jukumu la Kamati hii kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo na kulijulisha Bunge hatua iliyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matamanio ya Kamati yalikuwa ni kuona maazimio ya Bunge yanatekelezwa kwa

ukamilifu ili kufikia tija iliyolengwa. Hata hivyo, Kamati imepokea taarifa ya kushughulikiwa kwa maazimio hayo katika hatua mbalimbali, hali inayoonesha utayari na usikivu wa Serikali kwa Bunge. Pamoja na hilo, kasi ya utekelezaji wa baadhi ya maazimio kama vile azimio la miradi kutokamilika kwa wakati, uwiano usioridhisha wa gharama za uendeshaji kwa mapato, kupungua kwa mtaji wa uendeshaji na taasisi kutokuwa na mtazamo wa kibiashara, siyo ya kuridhisha sana. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa maazimio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo. kutokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati kuhusiana na uwekezaji wa mitaji ya umma, Kamati inamaoni ya jumla ambayo yatachochea ufanisi na kuongeza tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua dhima ya Serikali kuwekeza katika taasisi na mashirika ya umma ni kukuza uchumi wa nchi kwa madhumuni ya kupata mapato kwa njia ya faida (gawio), kutoa huduma za jamii kwa urahisi na kuchochea sekta mbalimbali za uchumi na kutengeneza ajira kwa wananchi. Hata hivyo, kama taasisi na mashirika ya umma yatashindwa kujiendesha kwa faida, hivyo kukosa ufanisi na tija itasababisha kushindwa kufikia dhima ya Serikali iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi zinazotolewa na Serikali kwa taasisi na mashirika ya umma ambapo Serikali imewekeza mitaji, zinapaswa kutekelezwa ili kuwepo na ufanisi wa mitaji inayotumika kwenye taasisi na mashirika hayo na tija ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kutoa mapendekezo kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko Maalum wa Uwekezaji *(Investment Fund):-*

Kwa kuwa, baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yana changamoto ya upatikanaji wa mitaji ambayo ingetumika kutekeleza shughuli za uwekezaji za taasisi na mashirika hayo;

Na kwa kuwa, pamoja na jitihada za Serikali za kuwapatia mitaji ya Uwekezaji taasisi na mashirika ya umma, bado kuna taasisi na mashirika ya umma hayana mtaji wa kutosha jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wa shughuli za uwekezaji;

Kwa hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, kuanzishwe Mfuko Maalum wa Uwekezaji *(Investment Fund)* ambao utasaidia taasisi na mashirika ya umma yenye uhitaji wa haraka na ukosefu wa mitaji kwa ajili ya kutoa huduma pindi inapohitajika. Vilevile, Mfuko huu Maalum wa Uwekezaji utasaidia kipindi kuna mwanguko wa kiuchumi *(economic shocks)* au jambo lolote lisiloweza kuzuilika *(unavoidable circumstances)* ambalo linaathiri mtaji wa taasisi au mashirika ya umma. Chanzo cha fedha cha Mfuko huu kinaweza kuwa fedha ambazo hazijadaiwa kutoka mabenki, taasisi za kifedha zisizo za kibenki, taasisi za bima, kampuni za mawasiliano na asilimia 20 ya mapato yasiyo ya kikodi yanayokusanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Viwanda vinavyomilikiwa na Taasisi za umma kuzalisha chini ya uwezo *(under capacity):-*

Kwa kuwa, kuna changamoto ya upungufu wa malighafi kwenye viwanda vinavyomilikiwa na taasisi mbalimbali za umma ikiwemo vile vinavyomilikiwa na Bodi ya mazao Mchanganyiko *(CPB)* na Kiwanda cha Bidhaa za

Ngozi cha Kimataifa cha *Kilimanjaro Leather International Company Limited (KLICL*) kinachomilikiwa kwa ubia kati ya Jeshi la Magereza na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma *(PSSSF)*;

Na Kwa Kuwa, upungufu huo wa malighafi unasababisha viwanda hivyo kuzalisha chini ya uwezo wake na mtaji wa uwekezaji wa Shilingi bilioni 143 kutotumika kwa ufanisi; hatua hii inaathiri upatikanaji wa tija iliyokusudiwa ya mtaji uliowekezwa kwenye viwanda hivi.

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali kuhakikisha wanaimarisha menejimenti zinazosimamia viwanda hivi kwa kuwa na menejimenti zenye mtazamo wa kibiashara na ushindani. Hatua hii itaongeza ufanisi na kulinda thamani ya mitaji iliyowekezwa kwenye viwanda hivi, hivyo kuleta tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya kifedha iliyojitokeza baada ya Shirika la Hifadhi la Taifa Tanzania *(TANAPA)* kuongezewa idadi ya hifadhi:-

Kwa kuwa, kuongezeka kwa idadi ya Hifadhi zinazoongozwa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)* kutoka hifadhi 16 hadi hifadhi 22, kumepelekea kuwa na changamoto ya fedha za uendeshaji na za kutekeleza miradi ya uwekezaji ya hifadhi;

Na kwa kuwa, kutokutekeleza miradi ya uwekezaji ya hifadhi kunaathiri upatikanaji wa mapato ya kutosha kutokana na kupungua kwa watalii, kwani mazingira ya hifadhi hayaridhishi, hivyo kukosekana ufanisi na tija ya uwekezaji katika hifadhi;

Kwa hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inalipatia Shirika la *TANAPA* fedha za kutosha ili

kuongeza ufanisi katika hifadhi zote 22 ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu na tija iweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Msongamano wa Shehena katika Bandari Dar es Saalam:-

Kwa kuwa, Bandari ya Dar es Salaam ndiyo lango la uchumi kwa nchi nyingi za Kusini na Mashariki mwa Afrika zikiwepo *Congo DRC*, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, Uganda, Zimbambwe na Sudan Kusini ambazo zinatumia Bandari ya Dar es Salaam kupitisha shehena ya mizigo, jambo linalopelekea bandari hii kuelemewa na shehena ya mzigo inayohudumiwa;

Na kwa kuwa, upanuzi wa bandari hiyo unaoendelea sasa hautaweza kumaliza changamoto iliyopo sasa ya wingi wa shehena zinazohudumiwa na nyingine kushindwa kushushwa kutokana na eneo kuwa dogo na kina kidogo;

Kwa hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(i) Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ihakikishe inamaliza kwa haraka changamoto zinazozuia kuanza kufanya kazi kwa Bandari Kavu ya Kwala, kwani hadi sasa Bandari hii imekamilika kwa asilimia 98. Kuanza kufanya kwa Bandari hii itaongeza ufanisi na kiasi cha shehena itakayohudumiwa na Bandari ya Dar es salaam na kupunguza msongamano wa shehena ya mzigo kwa asilimia 30; na

(ii) Kuharakisha mchakato wa Ujenzi wa Bandari ya Mbegani, Bagamoyo kwa kutumia mapato ya ndani ambayo inatarajiwa kuwa na vigezo vya Kimataifa, hivyo kuongeza ushindani wa Bandari

zetu katika soko na kupata tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukosefu wa Mfumo Mmoja unaosomana wa TEHAMA katika Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma:-

Kwa kuwa, Kamati imebaini changamoto ya kukosekana Mfumo mmoja na madhubuti wa TEHAMA katika Utendaji wa Taasisi, Mashirika ya Umma na Serikali kwa ujumla;

Na kwa kuwa, changamoto hiyo inapelekea kukosa ufanisi na tija kwenye utendaji wa Taasisi, Mashirika ya Umma na Serikalini kwa ujumla, hivyo Serikali kupoteza mapato, wafanyabiashara kupata hasara kutokana na kushindwa kupata huduma kwa wakati na wananchi kupata madhara hususan ya kukosa huduma za kijamii kwa wakati;

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali itengeneze mfumo mmoja na madhubuti wa TEHAMA *(Single Integrated Information Management System and Network)* ambao utasaidia kutatua changamoto zilizopo sasa ya kuwa na mifumo mingi, duni na isiyosomana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini kwa kuniongoza na kuniwezesha kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo ya kiti chako ikiwa ni pamoja na ushauri, miongozo na msaada uliotupatia kwa kipindi chote cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, napenda kumshukuru Msajili wa Hazina Ndugu Benedicto Mgonya kwa ushirikiano wake wa dhati alioutoa kwa Kamati kwa kushauri namna bora ya kuzifanya Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji na kuleta tija kwa Taifa ili kukamilisha dhima ya Serikali ya kufanya uwekezaji wa mitaji ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na Kamati katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti wa Taasisi na Mashirika ya Umma wakiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Uwekezaji katika Ofisi ya Msajili wa Hazina mwana mama Bi. Lightness Mauki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwatambua Wajumbe, lakini kutokana na changamoto ya muda nisiwataje lakini majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Pia natoa shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu vema shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athumani Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto *ndc,* na Makatibu wote wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo ulete tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuijadili na hatimaye kuridhia Maoni na Mapendekezo yake ili Serikali iweze kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**7 FEBRUARI, 2023**

# TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC) KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2022 HADI JANUARI, 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*(Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020)*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023. Wasilisho hili ni kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

### 1.2 Madhumuni ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Taarifa hii ni kueleza yatokanayo na shughuli za Kamati kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma na kuliwezesha Bunge kujadili hali hiyo na kufikia uamuzi kwa mfumo wa hoja Bungeni. Ili kufanikisha azma hiyo, Taarifa hii inaelezea kwa undani shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Kamati kuanzia mwezi Februari, 2022 hadi mwezi Januari, 2023 kama inavyoelekezwa na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.3 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya kwanza ni ya utangulizi ambayo inatoa maelezo ya jumla kuhusu maudhui na muundo wa taarifa hii ili kujenga msingi mzuri wa majadiliano;

(b) Sehemu ya pili inafafanua shughuli za Kamati kwa kipindi kinachohusika, pamoja na kuelezea shughuli hizo, msingi wake na mambo yaliyobainika;

(c) Sehemu ya Tatu inafanya majumuisho ya maoni kutokana na shughuli zilizotekelezwa. Lengo la sehemu hii ni kujenga msingi wa mapendekezo katika hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma inayojadiliwa Bungeni leo;

(d) Sehemu ya Nne inahitimisha hoja ili kuliomba Bunge lifanye uamuzi.

(e) Sehemu ya Tano na ya mwisho ni Kiambatisho kinachohusu Orodha ya Taasisi na Mashirika ya Umma yaliyokutana na Kamati hii kuanzia Februari, 2022 hadi Januari, 2023.

### 1.4 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa shughuli zote za Kamati hii, ni utekelezaji wa madaraka ya Bunge yaliyofafanuliwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 na Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 370.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria zingine ambazo pia zilisaidia kuona vigezo vya uendeshaji na matumizi ya mitaji ya umma ni: -

(a) Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410;
(b) Sheria ya Fedha za Umma, Sura ya 348;
(c) Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257; na
(d) Sheria ya Bajeti, Sura Na. 439.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mwongozo wa Kanuni za Kudumu za

Bunge, Toleo la Juni, 2020, Kifungu cha 12 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ambayo ni: -

(a) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma ina ufanisi na kuwa umezingatia taratibu, Sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na
(b) Kuchambua na kujadili Taarifa zinazohusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache.

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 12 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimeweka masharti kuhusu msingi wa kazi za Kamati. Kwa masharti hayo, kazi za Kamati zinatokana na Taarifa zinazohusu uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache. Kwa utaratibu huo, shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januari, 2023, zilipangwa kutokana na Taarifa za Msajili wa Hazina. Taarifa kuu zilizorejewa wakati huo ni: -

(a) Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2019/2020; na
(b) Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na Taarifa hizo, Kamati ilipokea Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kila Shirika na Taasisi kadiri zilivyopangwa kulingana na matokeo ya mapitio ya Taarifa Kuu za Msajili wa Hazina. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Uchambuzi wa Taarifa hizo umeiwezesha Kamati kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya Umma kama invyoripotiwa.

## 1.5 Njia zilizotumika (Methodology)

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Taarifa hii inawasilishwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, naomba kubainisha njia na mbinu zilizotumika kufanikisha majukumu ya Kamati kama inavyoelekeza Kanuni ya 142 ya Kanuni za Bunge. Mantiki ya kufanya hivyo ni kuliwezesha Bunge kuhakiki uthabiti (*Reliability*) na ustahiki (*Validity*) wa matokeo ya uchambuzi wa Kamati. Njia hizo ni:

(a) Vikao kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kwenye Kamati. Lengo ni kuiwezesha Kamati kufikia uamuzi wa pamoja na kuweka mwelekeo wa majadiliano;
(b) Mahojiano na Uongozi wa Taasisi zinazotumia mtaji wa umma katika uwekezaji. Lengo ni kupata ufafanuzi wa kina kuhusu masuala yaliyobainika kwa lengo la kutoa ushauri unaostahili; na
(c) Kutembelea na kukagua miradi mbalimbali inayotekelezwa kwa kutumia mitaji ya umma na kwa misingi ya kibiashara na uchumi. Lengo la njia na mbinu hii ni kuoanisha matokeo ya mahojiano na hali halisi ya miradi ya uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kwamba, njia hizo zilifanikisha utekelezaji wa majukumu ya Kamati kwa kipindi cha Februari, 2022 hadi Januri 2023. Naliomba Bunge lako tukufu liipokee Taarifa hii kwa kuzingatia uthabiti wa njia nilizozitaja.

# SURA YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

## 2.1 Maelezo ya awali

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya Kamati kuripoti Bungeni shughuli zilizotekelezwa, ni kuliwezesha Bunge

kubaini mafanikio na changamoto zilizopo katika uwekezaji wa mitaji ya Umma. Madhumuni hayo yatatimia kwa kubainisha Shughuli zilizotekelezwa pamoja na yatokanayo na shughuli hizo. Kwa ajili ya urahisi wa mtiririko, shughuli hizo zimegawayika katika makundi makuu nne ambayo ni: -

(a) Kupatiwa mafunzo/semina mbalimbali kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma yaliyotolewa na taasisi na mashirika mbalimbali ya umma. Mafunzo hayo yameiwezesha kamati kufanya uchambuzi wa taarifa mbalimbali za uwekezaji na kutoa ushauri wenye tija wa kuboresha utendaji wa taasisi hizo;

(b) Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Uwekezaji wa mitaji ya umma yaliyotolewa wakati wa Mkutano wa Tano wa Bunge, Mwezi Februari, 2022. Madhumuni ya Shughuli hii ni kulisaidia Bunge kujua hatua iliyofikiwa katika kutekeleza maazimio yake;

(c) Uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa lengo la kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kwamba, umezingatia taratibu, sheria na miongozo mingine mujarabu ya biashara; na

(d) Ziara za ufuatiliaji na ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji wa umma kwa lengo la kubaini iwapo utekelezaji wake unazingatia miongozo ya uwekezaji wa umma.

## 2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** katika Kipindi cha Februari 2022 hadi Januari 2023, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu

uwekezaji wa mitaji ya umma kwa kupitia taarifa mbalimbali za uwekezaji. Vigezo vilivyozingatiwa vilitokana na masharti ya Kanuni za Bunge yanayoitaka Kamati kujiridhisha iwapo uwekezaji huo una tija na kama umezingatia sheria, taratibu na miongozo mbalimbali ya biashara. Katika kufanya hivyo, Kamati ilipitia Taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma katika mashirika na taasisi za umma **47**. Orodha ya Taasisi na mashirika hayo yapo kwenye **Kiambatisho Na. 1**.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa uchambuzi, dhima ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ilizingatiwa na kuangalia uwekezaji wa mitaji ya umma ndani na nje ya nchi. Kwa ujumla Kamati ilizingatia thamani ya uwekezaji iliyofikia shilingi **trilioni 67.95** ambapo kiasi cha shilingi **trilioni 66.27** ikiwa ni thamani ya uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma 237 na kiasi cha shilingi **Bilioni 932.83** kikiwa ni mtaji wa umma katika kampuni 40 ambazo Serikali inamiliki hisa chache hadi kufikia mwaka 2020/21. Kiasi hicho katika kampuni serikali inamiliki hisa chache kilifikiwa kutokana na ongezeko la mali (*An increment in reserves*), Ongezeko la thamani ya Hisa za Serikali (*Government's Shareholiding*) na ongezeko la Mtaji (*Capital Injection*).[1]

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo hayo yanaonesha kuwa uwekezaji wa serikali katika taasisi na mashirika ya umma, unachangia zaidi ya asilimia 95 ya uwekezaji wote wa mitaji ya umma. Kwa msingi huo, uchambuzi wa rejesho la mitaji ya umma (*Returns on Investment*) uliofanywa na Kamati, ulizingatia umuhimu wa kutofautisha uwekezaji wa uendeshaji (*Investment on Operating capital*) na Uwekezaji usio wa uendeshaji

[1] Taz. Uk. wa 11 wa Taarifa ya Utendaji ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliyotolewa na Msajili wa Hazina mwezi Januari, 2022.

(*Investiment on non operating capital*). Lengo la Kamati kujielekeza kwenye ainisho (Classification) la uwekezaji huo ni kuwezesha uchambuzi wa matokeo ya uwekezaji katika taasisi na mashirika ya umma kuwa na uhalisia.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na shughuli hiyo, Kamati ilitoa Taarifa yake Bungeni wakati wa Mkutano wa Tisa wa Bunge, Mwezi Novemba, 2022. Taarifa hiyo iliiwezesha Bunge kupitisha maazimio yanayotarajiwa kufanyiwa kazi na Mamlaka ya Utendaji nchini. Ni ahadi ya Kamati kwamba, itaendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma. Aidha, kwa maeneo ambayo hayakuwa yamefanyiwa kazi wakati huo, Kamati inayaripoti bungeni kupitia Taarifa hii.

### 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Utendaji wa Mashirika na Taasisi za Umma zinazotumia Mitaji ya Umma

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilichambua utendaji wa taasisi na Mashirika ya Umma ili kujiridhisha kama uwekezaji katika mashirika na taasisi hizo unaweza kuwa na tija. Matokeo ya uchambuzi huo yalionesha mambo yafuatayo: -

#### 2.3.1 Changamoto iliyojitokeza baada ya Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kuongezewa Idadi ya Hifadhi

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) linasimamia hifadhi za Taifa 22 zenye ukubwa wa eneo la kilometa za mraba 104,578 kwa sasa, wakati za mwanzo zilikuwa 16 ambazo zilikuwa na kilometa za mraba 57,107. Maeneo yaliyoongezeka yanajumuisha hifadhi sita (6) zilizoanzishwa mwaka 2019 ambazo ni Burigi-Chato, Ibanda-Kyerwa, Rumanyika-Karagwe, Mto Ugalla, Kigosi na Nyerere zenye ukubwa wa kilometa za

mraba 47,471 ambazo ni sawa na 45.4% ya eneo lote linalosimamiwa na Shirika kwa sasa. Kwa ujumla, eneo linalosimamiwa na Shirika ni sawa na 11.6% ya eneo lote la nchi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na nia njema ya serikali ya kuongeza hifadhi nchini ili kuvutia watalii wengi zaidi hivyo nchi kupata mapato zaidi, kuna changamoto ya upungufu wa fedha za uendeshaji na za utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ambayo inachochea ukuaji wa sekta ya utalii kwa kuwa bajeti iliyokuwa inatumika kwa hifadhi 16 ndio hiyohiyo inayotumika sasa kwa Hifadhi 22, pamoja na kanda nne, vituo 5 vya Malikale na ofisi 2 Kiunganishi zilizopo Dar es Salaam na Dodoma. Hali hii inapelekea TANAPA kushindwa kuitika kwa haraka kwenye shughuli za dharura, ulinzi na usalama na kuzorota kwa utoaji wa huduma za kitalii kwa kuwa uwekezaji unaofanywa kwenye hifadhi hizi haufanywi kwa ufanisi, hivyo kupelekea kukosa tija iliyokusudiwa.

### 2.3.2 Mfuko Maalum wa Uwekezaji (Investment Fund)

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwepo na changamoto ya upatikanaji wa mitaji ya uwekezaji kwa wakati kwenye Taasisi, Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali na Kampuni ambazo Serikali inamiliki hisa na Mfuko ambao unakuwa na fedha maalum wakati wote kwa ajili ya uwekezaji (Investment fund). Hali hiyo ya kukosekana kwa rasilimali fedha kwa wakati sahihi ili kuendana na uhitaji wa wakati huo kwa lengo la kutumia fursa zinazojitokeza kunaathiri uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya taasisi ambazo kamati ilikutana nazo na kupitia na kuchambua taarifa za kiutendaji kipindi hiki ambazo zina changamoto za mtaji ni Wakala wa Umeme na Ufundi (TEMESA) na Shirika la

Viwango (TBS) ambapo yanakabiliwa na upungufu wa mtaji hivyo kupunguza ufanisi na tija katika utekelezaji wa shughuli zake, hali inayopelekea taasisi na mashirika haya kuwa na mchango mdogo au kutokuchangia kabisa katika mfuko mkuu wa Serikali.

### 2.3.3 Viwanda vinavyomilikiwa na Taasisi za umma kuzalisha chini ya uwezo (Under capacity)

**Mheshimiwa Spika**, Viwanda vinavyomilikiwa na baadhi ya taasisi na mashirika ambavyo vinaongeza thamani mazao ya kilimo na mifugo, vinazalisha chini ya uwezo wake kulingana na mpango wa kiwanda walioupanga (Under capacity).

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa taasisi na mashirika ambayo viwanda vyake vinazalishwa chini ya kiwango ni Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) ambapo viwanda vyake vilivyopo Kizota Industrial Area Dodoma vinavyosaga mahindi na kukamua mafuta ya alizeti. Kiwanda cha kusaga mahindi tangu kukamilika na kuanza kwake kazi mwezi Disemba 2019 kinazalisha 25% tu ya uwezo wake wa kuzalishaji na kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti kimeweza kukamua mbegu za alizeti kwa 7.12% tu ya uwezo uzalishaji wake tangu kilipokamilika mwaka 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imefanya mabadiliko makubwa CPB kwa kuteua Bodi ya wakurugenzi mpya na Bodi hiyo imeanza vizuri kwani imefanya maamuzi magumu ya kuisimamisha menejimenti ya zamani. Kamati inatambua juhudi za uongozi huo za kufanya mabadiliko katika menejimenti, hatua hii itasaidia kuboresha utendaji wa CPB hivyo kuongeza ufanisi na tija katika sekta ya mazao na kukidhi mahitaji ya soko.

**Mheshimiwa Spika,** Pia Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KLICL) kilichopo mjini Moshi kinamilikiwa kwa ubia kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Jeshi la Magereza Nchini. Wakati kamati inatembelea kiwanda hiki kilikuwa kinazalisha jozi za viatu takribani 146,000 kwa mwaka sawa na wastani wa jozi 400 kwa siku, ikiwa ni sawa na asilimia 12.2 tu ya uwezo wake wa kuzalisha viatu 1,200,000 kwa mwaka.

### 2.3.4 Ukosefu wa Mfumo Mmoja unaosomana wa TEHAMA katika Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma:

**Mheshimiwa Spika,** Katika Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo Kamati ilikutana nayo ikiwemo TRA, TPA na BOT, moja ya changamoto kubwa ni Mifumo duni na kuwa na mifumo mingi isiyosomana ya TEHAMA. Kutokana na changamoto hii ya mifumo kunapunguza ufanisi kwenye ukusanyaji wa mapato kwani mapato mengi yanapotea kutokana na kuwa na mifumo isiyosomana. Pia mifumo duni inakwamisha na kuzorotesha shughuli za kiutendaji, kibiashara na kiuwekezaji, hivyo kukosekana kwa ufanisi na tija ya mitaji ya umma.

### 2.3.5 Msongamano wa Shehena katika Bandari Dar es Saalam - (TPA)

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuteua Bodi mpya ya Mamlaka ya Bandari na kufanya mabadiliko katika Menejimenti yake kwani hatua hii inaonesha nia njema ya serikali ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Mamlaka ya hii ya Bandari.

**Mheshimiwa Spika,** Bandari ya Dar es Salaam kwa sasa inaendelea kupanuliwa kwa kuongeza gati na kina kwa ajili ya meli kutia nanga kwa ajili ya kushusha shehena za

mizigo, na Kwa kipindi cha Mwezi Julai hadi Disemba, 2022, Bandari hii imepokea na kupitisha mizigo jumla ya tani milioni 10.4 ambayo ni rekodi ya juu tangu kuanzishwa kwake hivyo, kusababisha Mamlaka ya Mapato Tanzania nayo kuvunja rekodi ya mapato kwa kukusanya shilingi trilioni 11.6, ambapo katika makusanyo ya TRA asilimia 41 ya ushuru wa forodha yanatokana na huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo, bado kumekuwa na changamoto ya msongamano wa shehena za mizigo, kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa Bandari na kukosekana kwa mapato ya forodha kwani wanashindwa kushusha baadhi ya shehena za mizigo katika Bandari ya Dar Es Salaam. Changamoto hizi zinaisababishia Bandari ya Dar es Salaam kushindwa kushindana na Bandari za karibu yake ikiwemo Bandari ya Mombasa, Kenya na bandari ya Beira iliyopo nchini Msumbiji.

### 2.3.6 Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi kwenye Miradi ya Utalii

**Mheshimiwa Spika,** Mashirika yetu ya Uhifadhi ikiwemo TANAPA, TAWA, NCCA na TFS ni moja ya taasisi zilizokumbwa na athari kubwa ya mlipuko wa Ugonjwa wa UVIKO-19 kwa sababu ya kuanguka kwa soko la Utalii nchini na duniani kwa ujumla. Hata hivyo, hali imeanza kuwa tofauti kwenye hifadhi zetu kwani juhudi za Serikali kupitia kwa uongozi wa Mheshimiwa Rais, Dkt Samia Suluhu Hassani za kuifungua na kuitangaza nchi kupitia Filamu ya **"The Royal Tour"** kumekuwa na ongezeko la watalii kwenye vivutio vyetu vya utalii. Hali hii imepelekea huduma muhimu zinazochagiza utalii kwenye hifadhi zetu kushindwa kuhimili ongezeko hilo.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto ya kushindwa kuhimili wingi wa watalii kunachangiwa na ufinyu wa mtaji wa uwekezaji katika kutekelezaji wa miradi inayochochea na kuwavutia watalii wengi zaidi, jambo ambalo linaondoa uwezekano kuongeza zaidi watalii na kurudi mara kwa mara kwa ajili ya kufanya utalii. Hivyo, kukosekana kwa ufanisi na tija ya uwekezaji iliyokusudiwa.

### 2.3.7 Deni la Bodi ya Pamba

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu tarehe 4 Novemba, 2022 ambapo pamoja na Maazimio mengine yaliyotolewa kwa Serikali, kulikuwa na azimio mahususi kuhusu deni la Pamba kwa Wanunuzi wa zao la pamba katika msimu wa mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Azimio hilo na kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ndogo ya Pamba nchini, kamati katika pindi hiki cha kiliomba kukutana na Waziri wa Fedha na Mipango, Waziri wa Kilimo na Bodi ya Pamba ili kupata hali halisi ya deni lenyewe, kiasi kinachodaiwa kuwa kimelipwa na Serikali, hatua Serikali inazochukua ili kulipa deni hilo na mwisho kujua ni lini Serikali itakamilisha kulipa deni hilo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kwamba hadi sasa deni lilipo sasa ni jumla ya shilingi Bilioni 102.51 ambayo inajumuisha hasara ya shilingi bilioni 21.879 kwa Kampuni zilizonunua pamba na kiasi cha shilingi bilioni 80.63 ni madai ya watoa huduma za pembejeo ambao wangelipwa kwa fedha ambazo zingetokana na makato ambayo serikali iliyafuta.

**Mheshimiwa Spika,** tayari kamati imekutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Waziri wa Kilimo, kutokana na taarifa na maelezo ya kina waliyotoa mbele ya kamati yanaonesha jitihada za makusudi za Serikali kulipa deni hili.

### 2.3.8 Mapungufu kwenye Sheria zinazoanzisha na kuendesha taasisi na mashirika ya umma

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilifanya uchambuzi na baini kuwa kuna udhaifu mkubwa katika sheria za baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma, ikiwemo Tume ya Ushindani Tanzania (FCC). Udhaifu huo unaathiri na kuzorotesha ufanyaji wa maamuzi ya kiutendaji na yale ya Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto inayoikabili Tume ya Ushindani (FCC) nchini ni mapungufu yaliyopo katika sheria ya ushindani na Sheria ya Alama za Bidhaa. Mapungufu hayo yanasababisha tume kutofanyakazi kwa ufanisi hivyo kukosekana kwa tija ya tume hii ya kuzuia bidhaa bandia zinazoingia nchini bila alama hivyo kupoteza mapato ya serikali.

### 2.3.9 Jukumu la kuweka Vinasaba kwenye Mafuta linalotekelezwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wa mafuta kuona wanalipia pesa nyingi kwa huduma ambayo haihitaji gharama kubwa ya kuwekewa vinasaba, Bunge lako Tukufu liliagiza Serikali kuhamisha jukumu hilo toka kwa mzabuni binafsi na kulipeka kwa Shirika la Viwango Tanzani (TBS) ambapo jukumu hilo lilianza kutekelezwa rasmi tarehe 28 April, 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika hadi sasa linaweka vinasaba kwenye maghala ishirini na moja (21) kwa lengo la kuendelea kudhibiti ubora wa mafuta na kulinda mapato ya Serikali ipasavyo. Pia, Kamati inaipongeza TBS kwa hatua iliyofikia katika utekelezaji wa jambo hili, ikiwa ni pamoja na kupunguza bei ya uwekaji wa vinasaba toka **shilingi 14** aliyokuwa anatoza mzabuni hadi **shilingi 8.0** wanayotoza TBS kwa sasa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio makubwa tangu TBS imepewa jukumu hilo, bado TBS inanunua vinasaba hivyo kutoka nje ya nchi hali ambayo inayoiongezea matumizi Shirika na kupunguza uwezo wao wa kutekeleza shughuli za uwekezaji kwa ufanisi na kushindwa kuchangia kwenye mfuko wa Serikali kama wanavyotakiwa.

### 2.3.10 Taasisi za umma kushindwa kukusanya Madeni (Receivables)

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za serikali za kupunguza mzito wa madeni kwa taasisi na mashirika ya umma, bado baadhi ya taasisi za umma zina mzigo mkubwa wa madeni (Receivables) ambayo bado hayajakusanywa huku mdaiwa mkubwa akiwa ni Serikali na taasisi zake. Hali hii inaathiri ukwasi na utendaji wa shughuli za taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa taasisi hizo ni Wakala wa Umeme na Ufundi Tanzania (TEMESA) inadai Serikali na Taasisi zake deni kubwa kutokana na utoaji wa huduma mbalimbali. Deni hilo linaongezeka kwa kasi kiasi cha kuathiri utendaji wa Wakala. Uchambuzi unaonyesha katika kipindi cha Mwaka 2020/21, madeni hayo yalikuwa yamefikia kiasi cha Shilingi **billion 45.39** ikiwa ni

ongezeko la 17% kutoka madai ya shilingi **billion 38.7** mwaka 2019/20.

**Mheshimiwa Spika,** Madeni haya yameathiri wakala na kupelekea wakati mwingine kukosa wazabuni au kuwekewa gharama kubwa zaidi ya zile za soko kwani imani ya wazabuni kwa Wakala kuwa atawalipa baada ya kukamilisha miradi ni ndogo.

### 2.3.11 Mfumo wa kutoa Fedha za Ruzuku kwa Mamlaka za Uhifadhi

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lilipitisha Sheria ya Fedha Na. 8 ya Mwaka Juni, 2020 ambapo mapato yote ya Mamlaka za Uhifadhi ikiwepo TANAPA, TAWA na NGORONGORO yakusanywe na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kupelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kutaka Mapato yote kukusanywa kwenye mfuko mkuu wa Serikali, kwa sasa ambapo kuna ongezeko kubwa la Watalii ambapo Mamlaka hizi za uhifadhi zinakabiliwa na changamoto ya kufanya ukarabati kwa wakati kwenye miundombinu inayotumiwa na Watalii ili kuendana na kasi ya ongezeko hili kwani kuna wakati wanachelewa kupata fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** mfumo huu kwa Mamlaka za Hifadhi kusubiri fedha kutoka hazina kunapunguza ufanisi kwa mamlaka hizi kuboresha mazingira ya hifadhi jambo ambalo linaathiri sekta hii ya utalii, kwani sekta hii kwa kiasi kikubwa inategemea ubora wa mazingira katika hifadhi hizo.

## 2.4 Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika**, Mwezi Februari, 2022, Bunge lako tukufu lilipitisha maazimio ya Bunge kumi nan ne (14) yaliyotokana na Taarifa ya Kamati kwa kipindi cha Februari, 2021 hadi Januari 2022. Chimbuko la Maazimio hayo, ni nia ya kupata ufumbuzi wa changamoto zilizokwamisha kufikiwa kwa matarajio ya uwekezaji wa mitaji ya umma. Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi lilitoa maazimio hayo yanayoonesha matarajio yake katika uwekezaji wa mitaji ya umma. Hivyo, ni jukumu la Kamati hii kufuatilia utekelezaji wa maazimio hayo na kulijulisha Bunge hatua iliyofikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** matamanio ya Kamati yalikuwa ni kuona maazimio ya Bunge yanatekelezwa kwa ukamilifu ili kufikia tija iliyolengwa. Hata hivyo, Kamati imepokea taarifa ya kushughulikiwa kwa maazimio hayo katika hatua mbalimbali, hali inayoonesha utayari na usikivu wa Serikali kwa Bunge. Pamoja na hilo, kasi ya utekelezaji wa baadhi ya maazimio kama vile azimio la Mradi kutokamilika kwa wakati, uwiano usioridhisha wa gharama za uendeshaji kwa mapato, kupungua kwa mtaji wa uendeshaji na taasisi kutokuwa na mtazamo wa kibiashara si ya kuridhisha sana, hivyo kamati inashauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa maazimio hayo. Ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itaona umuhimu wa kuongeza kasi ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge pamoja na ushauri wa wabunge ili kuongeza tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma nchini. Kamati itaendelea kufatilia utekelezaji wa maazimio yote ya Bunge ili yaweze kutekelezwa kwa wakati na ufanisi ili tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma iweze kupatikana.

## 2.5 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Uwekezaji iliyotembelewa na kamati

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa kutoa maelezo kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Kamati kuhusu Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji iliyowekewa Mitaji ya Umma. Miradi iliyotembelewa na kamati imegawanyika katika maeneo sita (6) kama ifuatavyo: -

i. Miradi ya Maji;
ii. Mradi ya kuongeza thamani mazao ya mifugo;
iii. Miradi ya Nishati;
iv. Miradi ya Afya na Ithibati;
v. Miradi ya Kutoa Huduma; na
vi. Miradi ya kuchochea Utalii.

### 2.5.1 Miradi ya Maji

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Arumeru (ASUWSDP) unaotekelezwa na Mamlaka Ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWSA). Mradi huu unafadhiliwa na serikali kuu pamoja na mkopo nafuu kutoka benki ya maendeleo ya Afrika (AfDB) na unakadiriwa kugharimu shilingi za kitanzania bilioni 520 (usd 233.9 mill).

**Mheshimiwa Spika**, Manufaa na tija ya mradi ni pamoja na kuongezeka wa uzalishaji maji kwa kiasi cha lita 17,400,000 kwa siku huku kukiwa na ongezeko la wateja wapya 3,300, kuweza kupima ufanisi wa dira za maji "Water Meter Testing Bench", upatikanaji wa ajira takribani 2,000 na matumizi ya zaidi ya billion 75.6 moja kwa moja kwenye manunuzi ya vifaa na malipo ya fidia ya eneo la mradi yameongeza mzunguko wa fedha ndani ya jiji na kusisimua uchumi kwa ujumla wake.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Maji Kisarawe – Pugu – Gongo la mboto unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA). Mradi huu ni miongoni mwa mradi wa kimkakati ambao unagharimu kiasi cha **TZS 7.5 Bilioni** ambazo ni fedha za ndani kutoka DAWASA. Mradi unatarajiwa kurudisha gharama zake (Return on Capital/Investment) kufikia mwaka 2023 huku wateja wapya waliofikia 5,700 mauzo ya maji yakiwa **lita 5,760,000** na mapato ya zaidi ya shilingi **9.5 Bilioni**, lengo likiwa ni kufikia wateja 50,000 mwaka 2025 na kukusanya mapato ya shilingi **bilioni 15.9**.

**Mheshimiwa Spika,** Pia kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazoikabili miradi hii ikiwemo kuchelewa kupata msamaha wa kodi (GN) kwa Wakandarasi na wataalam washauri vilevile msamaha huo kutokuzingatia kipindi cha maangalizi ya mradi (DLP), ukosefu wa mpango wa matumizi bora ya ardhi hali inayopelekea mradi kuwa na gharama kubwa kwa ajili ya fidia hasa maeneo ya upanuzi wa mradi hivyo kuongeza gharama ya uwekezaji.

### 2.5.2 Mradi ya kuongeza thamani mazao ya mifugo

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa ujenzi wa kiwanda cha Viatu na Bidhaa za ngozi cha kimataifa cha Kilimanjaro (KLICL) kinachomilikiwa kwa ubia kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Jeshi la Magereza, ambapo PSSSF inamiliki asilimia 86 ya hisa na Jeshi la Magereza linamiliki asilimia 14 ya kampuni. Mradi hadi ukikamilika utagharimu shilingi **bilioni 136** ikijumuisha gharama za uendeshaji na kununua mali ghafi uwekezaji huu uliofanywa na Serikali unatarajiwa kurudisha gharama (return on investment) ndani ya miaka kumi (10).

**Mheshimiwa Spika**, Manufaa na tija ya mradi ni kuongeza mnyororo wa thamani kwenye zao la ngozi nchini na kuongeza ajira toka 271 hadi 7000, kuongeza mapato yanayotokana na kodi, kupata fedha za kigeni kwa kuuza bidhaa za ngozi nje ya nchi na kupunguza kuagiza bidhaa za ngozi toka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini baadhi ya changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa mradi huu zikiwemo upungufu wa malighafi ya ngozi na ngozi bora hasa ukizingatia wafugaji wengi hawafuati hatua za uvunaji/uchunaji bora wa ngozi na kukosekana kwa soko la kutosha.

**2.5.3 Miradi ya Nishati**

**Mheshimiwa Spika,** Miradi ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi I na II Extension Megawati 185 na Megawati 240 inayotekelezwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Mradi wa Kinyerrezi I unatekelezwa kwa gharama ya dola za Marekani Milioni **188** na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100 na umefikia asilimia 87 ya utekelezaji, na Kinyerezi II unatekelezwa kwa gharama ya dola za Marekani Milioni **344.** Mradi wa Kinyerezi II uligharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 15 na asilimia 85 ikiwa ni Mkopo kutoka Serikali ya Japan na umekamilika asilimia 100 na tayari unachangia kiasi hicho cha Megawati **240** kwenye gridi ya Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kinyerezi I **(150MW)** unahusisha ujenzi wa mitambo mingine minne (4) inayotumia gesi asilia yenye uwezo wa **Megawati 185**. Mradi utakapokamilika utafanya mtambo wa Kinyerezi I uwe na uwezo wa jumla ya **Megawati 335**. Wakati huohuo mradi wa Kinyerezi II una mitambo minane sita

kati ya hiyo inatumia gesi asilia na miwili inatumia mvuke ikiwa na uwezo wa kuzalisha umeme **Megawati 240**. Kwa ujumla miradi hii inachangia nishati ya umeme kwenye mfumo wa gridi ya Taifa kwa asilimia 23.07 na hivyo kuboresha hali ya upatikanaji wa umeme nchini na kuchochea kwa utekelezaji wa shughuli za uwekezaji kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa miradi hii ya umeme TANESCO imeainisha changamoto ya gharama kubwa za uendeshaji wa kituo hasa kutokana na bei kubwa ya gesi asilia, mgogoro wa kikodi kati ya watengenezaji wa Japan na TRA na taratibu za manunuzi.

### 2.5.4 Miradi ya Afya na Ithibati

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ithibati za Maabara unaotekezwa na Mamlaka ya Afya za Mimea na Viuatilifu (TPHPA) wenye gharama ya shilingi bilioni 5.4 ambapo mwaka wa fedha 2020/21 ilipokea shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya ithibati ya maabara zake. Lengo la kufanya ithibati ni Kukidhi Matakwa ya masoko ya ndani na nje ya nchi, kuwa na Mazingira salama kwa Afya ya Binadamu, Wanyama na Mimea na kutoa huduma za uchambuzi wa sampuli viuatilifu, mazao, udongo na maji.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unakabiliwa na Changamoto ya urasimu katika usajili wa dawa na kupatikana kwa fedha pungufu za kutekeleza mradi ambapo inapelekea mradi kutekelezwa kwa awamu hivyo kuchelewesha manufaa na tija ya mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Keko Pharmaceutical Industries (1997) Limited ni kiwanda cha kuzalisha dawa kinachoendesha kwa ubia kati ya Serikali ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania (70%) na Kampuni ya Diocare inayomiliki asilimia 30. Wakati kamati imeenda kukagua kiwanda hiki kilikuwa kinazalisha dawa za vidonge aina kumi (10) ambazo zimeidhinishwa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ambazo ni Paracetamol, Diclofenac, Metronidazole, Erythromycin, Ampicillin, Pen V, Amoxicillin, Co-trimoxazole (Ciprofloxacin) na Griseofulvin.

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda kina uwezo wa kutengeza wastani wa vidonge **milioni 6** kwa saa **24** ambapo Uzalishaji unaofanyika kwa sasa unakidhi **asilimia 36** tu ya mahitaji ya nchi. Kutokana na maboresho mbalimbali yaliyofanywa kwenye kiwanda hicho ikiwemo kuwa na Menejiment mpya imepelekea kuongeza mapato ya kiwanda kutoka shilingi **Milioni 24,000,000** hadi kufikia shilingi bilioni 3.7 mwezi Machi, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio hayo, Kamati imebaini kuwa kunachangamoto ya ukosefu wa mtaji endelevu na kiwanda kina deni la shilingi bilioni 14 na ongezeko la Kodi kwa kifungashio cha dawa aina ya PVC (Poly vinyl Chloride).

### 2.5.5 Miradi ya kutoa Huduma

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Dar es Salaam Maritime Gateway project (DMGP) unaotekelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) unagharimu jumla ya dola za kimarekani 421 Millioni ambapo dola za kimarekani 345 Milioni toka Benki ya Dunia, dola za kimarekani 12 Milioni ni msaada toka FCDO na dola za kimarekani 64 Milioni toka Serikalini. Lengo la mradi ni kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya Mauzo ya nje (Exports) na uagizaji wa bidhaa kutoka nje (Imports) kwa kuboresha miundominu ikiwa ni kuongeza Gati 1-7, kuongeza kina na upana wa kugeuzia meli kutoka mita

9 hadi mita 15.5 na Kuongeza kina cha gati za sasa hadi kufikia mita 14.5.

**Mheshimiwa Spika,** Pia kuna Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Vingunguti – Baracuda kilometa 2.84 unaotekelezwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) unaogharimu shilingi bilioni 5.2, wakati kamati inatembelea mradi ulikuwa umefikia asilimia 98. Lengo la mradi ni kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa bidhaa ili kuongeza ukuaji wa uchumi kwa kuunganisha barabara ya Nyerere na Tabata Baracuda, pia inapita viwandani na machinjio mpya ya kisasa yaliyopo Vingunguti.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya changamoto zilizokuwepo kwenye mradi huu ni watu kugoma kulipwa fidia jambo lililopelekea baadhi ya kazi kutofanyika kama ilivyopangwa ikiwemo vituo vya daladala kulingana na barabara ilivyokuwa (existing road corridor) na kutopata ushirikiano wa kutosha kutoka Mamlaka nyingine za Serikali kama vile TANESCO (Nguzo za umeme), DAWASA (mabomba ya maji) wakati wa ujenzi wa barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Pia kuna Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Vingunguti – Baracuda kilometa 2.84 unaotekelezwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA) unaogharimu shilingi bilioni 5.2, wakati kamati inatembelea mradi ulikuwa umefikia asilimia 98. Lengo la mradi ni kurahisisha shughuli za usafiri na usafirishaji wa bidhaa ili kuongeza ukuaji wa uchumi kwa kuunganisha barabara ya Nyerere na Tabata Baracuda, pia inapita viwandani na machinjio mpya ya kisasa yaliyopo Vingunguti.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya changamoto zilizokuwepo kwenye mradi huu ni watu kugoma kulipwa fidia jambo

lililopelekea baadhi ya kazi kutofanyika kama ilivyopangwa ikiwemo vituo vya daladala kulingana na barabara ilivyokuwa (existing road corridor) na kutopata ushirikiano wa kutosha kutoka Mamlaka nyingine za Serikali kama vile TANESCO (Nguzo za umeme), DAWASA (mabomba ya maji) wakati wa ujenzi wa barabara.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Mfumo wa Tiketi Mtandao (e ticket) unaotekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), mfumo huu wa tiketi Mtandao unamuwezesha abiria kukata tiketi ya kielektroniki pasipo kulazimika kwenda kwenye vituo vya mabasi ikuhusisha matumizi ya programu tumizi (Mobile Application) katika simu janja (smart phone) na mawakala wa mabenki. Makapuni 60 yenye mabasi 155 yalijiunga na kutumia mfumo huu. Kipindi cha majaribio ya mfumo shilingi **4,840,264,570** zilipita kwenye mfupo kama mauzo ya tiketi.

**Mheshimiwa Spika,** faida za mfumo huu ni kusaidia mamlaka husika kupata takwimu sahihi za watumiaji wa huduma na kujua mapato halisi ya watoa huduma hivyo kupata mapato halisi na kuleta tija ya uwekezaji katika mfumo huo. Pamoja na faida zinazopatikana kutokana na mfumo, pia kuna changamoto za mfumo ikiwemo ulazima wa mfumo kutumia float na haijulikani anayepaswa kupelekewa taarifa pindi changamoto zinapotokea na Miamala kutofika kwa wakati kwenye akaunti za wasafirishaji.

**2.5.6 Miradi ya kuchochea Utalii**

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilikagua Miradi wezeshi ya maendeleo katika hifadhi za misitu na mazingira asilia Amani mkoani Tanga unaotekelezwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ambayo inagharimu jumla ya shilingi **1,206,400,440.35** ambazo ni fedha za

ndani toka TFS na zile za Miradi ya ustahimilivu wa UVIKO -19 katika hifadhi ya mazingira asilia Amani, wakati kamati inatembelea miradi hiyo ilikuwa imefikia asilimia 47 ya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Manufaa yatakayotokana na utekelezaji wa miradi hii ni pamoja na Kuvutia uwekezaji kwenye misitu ya hifadhi, Kuongeza mvuto kwa watalii na shughuli za utalii kupitia miundombinu itakayojengwa hivyo kuongeza mapato, Kuimarisha ulinzi wa rasilimali katika maeneo ya hifadhi na Lango kuu la mapokezi kuweza kuhudumia watalii wengi kwa wakati mmoja.

**Mheshimiwa Spika,** Majanga ya moto hasa ukanda wa chini na kuongezeka kwa kasi ya shughuli za binadamu nje na ndani ya hifadhi hususani uchimbaji wa madini, na kusimamishwa kwa biashara ya usafirishaji wa vipepeo nje ya nchi tangu mwaka 2019 kunakopelekea ukosefu wa mapato kwa kiwango cha asilimia 95% hali inayopelekea hasara na tija ndogo kwa uwepo wa hifadhi yenyewe.

**Mheshimiwa Spika,** Pia kamati ilikagua mradi wa Faru uliopo eneo la Mbula ndani ya hifadhi ya Mkomanzi unaotekelezwa na Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) ambao umeanza 2017/18 hadi 2021/22, lengo likiwa ni kupata zao jipya la faru weusi ambalo ni hitaji la watalii wengi. Mradi huu umegharimu Jumla ya Shilingi **2,256,036,944/=** hadi kukamilika na chanzo cha fedha hizo ni Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA).

**Mheshimiwa Spika,** Mafanikio ya mradi wa faru ni kuimarika kwa ulinzi wa faru kutokana na ujenzi wa uzio wa kilometa 18 na kuongezeka kwa faru kwa kutoka na kupungua kwa msongamano kwenye eneo la uzalishaji wa faru, hali hii imepelekea kuongezeka kwa watalii na

mapato yatokayo na utalii kufikia watalii takribani 5,937 na mapato ya Tsh **574,496,841.531**.

**Mheshimiwa Spika,** kwenye mradi huu wa faru bado kuna changamoto za uwepo wa tishio la ujangili na Uhaba wa maji ya kutosha katika eneo la Mradi kwa matumizi ya watumishi na wanyamapori.

## SEHEMU TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati kuhusiana na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kamati inamaoni ya jumla ambayo yatachochea ufanisi na kuongeza tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua Dhima ya Serikali kuwekeza katika taasisi na Mashirika ya umma ni kukuza uchumi wa nchi kwa madhumuni ya kupata mapato kwa njia ya faida/gawio, kutoa huduma za jamii kwa urahisi na kuchochea sekta mbalimbali za uchumi na kutengeneza ajira kwa wananchi. Hata hivyo, kama taasisi na mashirika ya umma yatashindwa kujiendesha kwa faida, hivyo kukosa ufanisi na tija jambo litakalopelekea kushindwa kufikia dhima ya Serikali iliyokusudia.

**Mheshimiwa Spika,** Ahadi zinazotolewa na serikali kwa taasisi na mashirika ya umma ambako serikali imewekeza mitaji zinapaswa kutekelezwa ili kuwepo na ufanisi wa mitaji inayotumika kwenye taasisi na mashirika hayo na tija ipatikane.

## 3.2 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo hayo sasa naomba kutoa mapendekezo kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kama ifuatavyo: -

### 3.2.1 Mfuko Maalum wa Uwekezaji (Investment Fund)

**KWA KUWA**, Baadhi ya taasisi na mashirika ya Umma yana changamoto ya upatikanaji wa mitaji ambayo ingetumika kutekeleza shughuli za uwekezaji za taasisi na Mashirika hayo,

**NA KWA KUWA**, pamoja na jitihada za Serikali za kuwapatia mitaji ya Uwekezaji taasisi na mashirika ya umma, bado kuna taasisi na mashirika ya umma hayana mtaji wa kutosha jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wa shughuli za uwekezaji,

**KWA HIVYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, kuanzishwe Mfuko Maalum wa Uwekezaji (Investment Fund) ambao utasaidia taasisi na mashirika ya umma yenye uhitaji wa haraka na ukosefu wa mitaji kwa ajili ya kutoa huduma pindi inapohitajika. Vilevile, mfuko huu maalum wa uwekezaji utasaidia kipindi kunamuanguko wa kiuchumi (economic shocks) au jambo lolote lisiloweza kuzuilika (unavoidable circumstances) ambalo linaathiri mtaji wa taasisi au mashirika ya umma. Chanzo cha fedha cha Mfuko huu kinaweza kuwa fedha ambazo hazijadaiwa kutoka mabenki, taasisi za kifedha zisizo za kibenki, taasisi za bima, kampuni za mawasiliano na asilimia 20 ya mapato yasiyo ya kikodi yanayokusanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**3.2.2 Viwanda vinavyomilikiwa na Taasisi za umma kuzalisha chini ya uwezo (under capacity)**

**KWA KUWA,** kuna changamoto ya upungufu wa malighafi kwenye viwanda vinavyomilikiwa na taasisi mbalimbali za umma ikiwamo vile vinavyomilikiwa na Bodi ya mazao Mchanganyiko (CPB) na Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KLICL) kinachomilikiwa kwa ubia kati ya Jeshi na Magereza na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Watumishi wa Umma (PSSSF),

**NA KWA KUWA,** upungufu huo wa malighafi unasababisha viwanda hivyo kuzalisha chini ya uwezo wake na mtaji wa uwekezaji wa shilingi Bilioni 143 kutotumika kwa ufanisi. Hatua hii inaathiri upatikanaji wa tija iliyokusudiwa ya mtaji uliowekezwa kwenye viwanda hivi.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali kuhakikisha wanaimarisha menejimenti zinazosimamia viwanda hivi kwa kuwa na menejimenti zenye mtizamo wa kibiashara na ushindani. Hatua hii itaongeza ufanisi na kulinda thamani ya mitaji iliyowekezwa kwenye viwanda hivi, hivyo kuleta tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

**3.2.3 Changamoto ya kifedha iliyojitokeza baada ya Shirika la Hifadhi la Taifa Tanzania kuongezewa idadi ya hifadhi (TANAPA)**

**KWA KUWA,** kuongezeka kwa idadi ya Hifadhi zinazoongozwa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kutoka hifadhi 16 hadi hifadhi 22, kumepelekea kuwa na changamoto ya fedha za

uendeshaji na za kutekeleza miradi ya uwekezaji ya hifadhi,

**NA KWA KUWA,** kutokutekeleza miradi ya uwekezaji ya hifadhi kunaathiri upatikanaji wa mapato ya kutosha kutokana na kupungua kwa watalii kwani mazingira ya hifadhi hayarithishi, hivyo kukosekana ufanisi na tija ya uwekezaji katika hifadhi,

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ihakikishe inaipatia Shirika la TANAPA fedha za kutosha ili kuongeza ufanisi katika hifadhi zote 22 hivyo, waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu na tija iweze kupatikana.

### 3.2.4 Msongamano wa Shehena katika Bandari Dar es Saalam - (TPA)

**KWA KUWA**, Bandari ya Dar Es Salaam ndio lango la uchumi kwa nchi nyingi za kusini na Mashariki mwa Afrika zikiwepo CONGO DRC, RWANDA, BURUNDI, MALAWI, ZAMBIA, UGANDA, ZIMBAMBWE na SUDAN KUSINI ambazo zinatumia Bandari ya Dar Es Salaam kupitisha shehena yao ya mizigo, jambo linalopelekea bandari hii kuelemewa na shehena ya mzigo inayohudumiwa,

**NA KWA KUWA**, upanuzi wa bandari hiyo unaoendelea sasa hautaweza kumaliza changamoto iliyokuwepo sasa ya wingi wa shehena zinazohudumiwa na nyingine kushindwa kushushwa kutokana na eneo kuwa dogo na kina kidogo.

**KWA HIVYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba,

(iii) Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ihakikishe inamaliza kwa haraka changamoto

zinazozuia kuanza kufanya kazi kwa Bandari Kavu ya KWALA kwani hadi sasa Bandari hii imekamilika kwa asilimia 98. Kwa kuanza kufanya kwa Bandari hii itaongeza ufanisi na kiasi cha shehena itakayohudumiwa na bandari ya Dar es salaam na kupunguza msongamano wa shehena ya mzigo kwa asilimia 30; na

(iv) Kuharakisha mchakato wa Ujenzi wa Bandari ya Mbegani -Bagamoyo kwa kutumia mapato ya ndani ambayo inatarajiwa kuwa na vigezo vya kimataifa, hivyo kuongeza ushindani wa Bandari zetu katika soko na kupata tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma.

**3.2.5 Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi kwenye Miradi ya Utalii**

**KWA KUWA,** Shirika la Hifadhi la Taifa (TANAPA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuwa na uwezo mdogo wa kifedha kuwekeza kwenye vituo na vivutio vyao vya utalii hasa kwenye ujenzi wa hoteli na hosteli za kulala watalii kama ilivyobainika kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi na ile ya hifadhi ya Mazingira Asilia ya Amani mkoani Tanga,

**NA KWA KUWA,** uwezo huo mdogo wa kifedha unapelekea taasisi kushindwa kuongeza thamani maeneo ya hifadhi hivyo, kukosekana kwa tija (optimum utilization) ya vivutio hivi na kudhoofisha mchango wake kwenye kuchangia Mfuko Mkuu wa Serikali,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali kupitia Bodi ya Utalii na Bodi za TANAPA na ile ya TFS, kushirikiana na wawekezaji kutoka sekta binafsi (PPP) kwenye ujenzi wa malazi na miundominu mingine ndani ya hifadhi za Taifa na zile za Misitu ya Mazingira Asili ili kuziwezesha hifadhi kutoa huduma bora kwa watalii

hatua itakayopelekea kuongeza ufanisi na mapato kwa hifadhi, hivyo kupatikana kwa tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma inayowekezwa kwenye hifadhi hizo.

### 3.2.6 Deni la Bodi ya Pamba

**KWA KUWA,** Agizo la Serikali la Mwaka 2019 lilitaka Pamba kununuliwa kwa bei ya juu zaidi ya bei ya soko la dunia limeathiri uwezo wa wanunuzi wa pamba kwa kiasi cha shilingi **Bilioni 21.8** kiasi ambacho Serikali iliahidi kufidia deni hilo,

**NA KWA KUWA,** maamuzi hayo yalisababisha watoa huduma za pembejeo za kilimo cha pamba walioingia mikataba na Bodi ya Pamba kutolipwa madai yao ya jumla ya shilingi **Bilioni 80.63**,

**NA KWA KUWA,** tangu azimio hili litolewe na Bunge katika Mkutano wa Tisa wa Bunge ambapo kamati iliwasilisha taarifa bungeni, hatua iliyochukuliwa na Serikali hadi sasa ya kutaka kufanya uhakiki wa deni hilo la jumla ya shilingi **bilioni 102.51** bado haijaweza kutatua changamoto iliyopo sasa katika sekta hii ndogo ya Pamba,

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali iongeze kasi na kuhakikisha hadi inapofika mwezi machi, 2023 iwe imekamilisha uhakiki na kuliweka deni hilo kwenye bajeti ya mwaka 2023/24 ili waweze kulilipa kikamilifu. Jambo litakalosaidia kukuza sekta ya pamba na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kutoka tani **350,000** hadi kufikia tani **1,000,000** ifikapo 2025.

**3.2.7 Ukosefu wa Mfumo Mmoja unaosomana wa TEHAMA katika Utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma:**

**KWA KUWA,** Kamati imebaini changamoto ya kukosekana Mfumo mmoja na madhubuti wa TEHAMA katika Utendaji wa Taasisi, Mashirika ya umma na Serikali kwa ujumla,

**NA KWA KUWA,** changamoto hiyo inapelekea kukosa ufanisi na tija kwenye utendaji wa Taasisi, Mashirika ya umma na Serikalini kwa ujumla, hivyo Serikali kupoteza Mapato, wafanyabiashara kupata hasara kutokana na kushindwa kupata huduma kwa wakati na wananchi kupata madhara hususani ya kukosa huduma za kijamii kwa wakati,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba Serikali itengeneze Mfumo mmoja na madhubuti wa TEHAMA (Single Intergrated Information Management System and Network) ambao usaidia kutatua changamoto zilizopo sasa za kuwa na mifumo mingi, duni na isiyosomana.

**3.2.8 Mapungufu kwenye Sheria zinazoanzisha na kuendesha taasisi na mashirika ya umma**

**KWA KUWA,** baadhi ya taasisi na mashirika ya umma yanakabiliwa na changamoto za kuwa na mapungufu ya sheria wanazozitumia, moja ya taasisi hizo ni Tume ya Ushindani (FCC) ambapo mapungufu yapo katika sheria ya ushindani (FCA) na Sheria ya Alama za Bidhaa (MMA).

**NA KWA KUWA,** upungufu huu wa kisheria unapelekea Tume ya Ushindani (FCC) kushindwa kutekeleza shughuli zao kikamilifu jambo ambalo linakwamisha juhudi za kushajiisha ushindani na kumlinda mlaji dhidi ya vitendo hadaifu na kandamizi na vita dhidi ya bidhaa bandia.

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ikamilishe kwa haraka mchakato wa mabadiliko ya sheria ya Tume ya Ushindani ili kutatua changamoto za kisheria zilizopo sasa ambazo zinakwamisha shughuli za taasisi hii na tija ya uwekezaji wa mitaji ya umma iweze kupatikana.

**3.2.9 Jukumu la kuweka Vinasaba kwenye Mafuta linalotekelezwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**

**KWA KUWA,** Shirika la Viwango Tanzania lilipewa jukumu la kuweka vinasaba kwenye mafuta mwaka 2021 kutokana na malalamiko ya wafanya biashara ya kulipa gharama kubwa kwa mzabuni kwa huduma hii ya kuwekewa vinasaba jambo ambalo si la kutozwa gharama kubwa.

**NA KWA KUWA,** vinasaba hivyo vinavyowekwa kwenye mafuta vilikuwa vinaagizwa kutoka nje wakati wa mzabuni na sasa Shirika la Viwango bado linaendelea kuagiza vinasaba hivyo kutoka nje na kuongeza gharama za uendeshaji.

**NA KWA KUWA,** kuongezeka kwa gharama hizo ni moja ya sababu zinazopelekea uhaba wa fedha za kutekeleza shughuli za TBS ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendeleo kikamilifu.

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, TBS wakamilishe kwa haraka tafiti wanayoifanya ya vinasaba vyao wenyewe na kuanza kutumika kwa vinasaba ili kuondokana na kadhia ya kuagiza vinasaba kutoka nje. Hatua hii itasaidia kuthibiti ubora wa mafuta zaidi na kulinda mapato ya Serikali ipasavyo.

**3.2.10 Taasisi za Umma kushindwa kukusanya Madeni (Receivables)**

**KWA KUWA,** Wakala wa Umeme na Ufundi Tanzania (TEMESA) inadai deni kubwa kwa Taasisi za Serikali na deni hilo limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka kutoka shilingi **billion 37.8** mwaka 2019/2020 hadi kufikia shilingi **billioni 45.38** mwaka 2020/2021,

**NA KWA KUWA,** deni hili linaathiri ukwasi wa TEMESA kama taasisi na utendaji wake kwani wanashindwa kufanya ukarabati wa karakana, kununua vipuli vipya na kukosa wa zabuni pale wanapotaka kutekeleza miradi kwa kuwa wazabuni wanaona TEMESA hawawezi kuwalipa kutokana na hali yao ya kifedha,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba,

i. Serikali ihakikishe inakamilisha kwa haraka uhakiki wa deni la shilingi **bilioni 45.38** unaofanywa na Mkaguzi wa ndani Mkuu na kulilipa deni hilo; na
ii. Serikali ihakikishe inatengeneza mfumo utakaosaidia TEMESA kulipwa fedha za matengenezo kwa wakati kama vile kutumia mfumo wa Pre paid ili kutozalisha madeni mapya na kuongeza ufanisi wa taasisi hii.

**3.2.11 Mfumo wa Kutoa Fedha za Ruzuku kwa Mamlaka za Uhifadhi**

**KWA KUWA,** Mapato yote ya Taasisi za Uhifadhi za TANAPA, TAWA na NCCA yanakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali,

**NA KWA KUWA,** hali hii inazipunguzia Mamlaka za TANAPA, TAWA na NCCA ukwasi na kuathiri uwezo wake wa kufanya maamuzi ya haraka na yenye tija ya

kuwekeza kwenye sekta ya utalii ambayo inapokea wageni wengi kila wakati.

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ianzishe mfumo maalumu (Revenue Disbursement automated system-ReDAS) ambao utahakikisha kuwa sehemu ya mapato ambayo yamekusanywa na Mamlaka ya Uhifadhi kutumia mfumo wa TRA inarudishwa kwenye taasisi kwa wakati. Sehemu ya mapato hayo yanayorudishwa ni kulingana na bajeti waliyopangiwa taasisi hiyo. Hatua hii itasaidia kuimarisha sekta hii ya utalii kwa kwa na uhakika wa fedha za uendeshaji lakini pia haitaathiri ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kutumia Consolidated Fund na hivyo itaongeza ufanisi kwenye uwekezaji wa mitaji ya umma inayofanywa na taasisi hizi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini wa kuniongoza ambao umeniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Utekelezaji wa majukumu ya Kamati umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutokana na maelekezo ya kiti chako ikiwa ni pamoja na ushauri, miongozo na msaada uliotupatia kwa kipindi chote cha mwaka mzima.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika uwekezaji wenye tija kwa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Vile vile, napenda kumshukuru Msajili wa Hazina Ndugu Benedicto Mgonya kwa ushirikiano wake wa dhati alioutoa kwa Kamati kwa kushauri namna bora ya kuzifanya Taasisi na Mashirika ya Umma, kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake na kuleta tija kwa Taifa ili kukamilisha dhima ya Serikali ya kufanya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na Kamati katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti wa Taasisi na Mashirika ya Umma wakiongozwa na Mkurugenzi Idara ya Uwekezaji katika Ofisi ya Msajili wa Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Jerry William Silaa, Mb _ Mwenyekiti
2. Mhe. George Natany Malima, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Daud Hassan, Mb _ Mjumbe
4. Mhe. Assa Nelson Makanika, Mb _ Mjumbe
5. Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb _ Mjumbe
6. Mhe. Charles Muguta Kajege, Mb _ Mjumbe
7. Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb _ Mjumbe
8. Mhe. Condester Michael Sichwale, Mb _ Mjumbe
9. Mhe. Dorothy George Kilave, Mb _ Mjumbe
10. Mhe. Ester Amos Bulaya, Mb _ Mjumbe
11. Mhe. Haji Amour Haji, Mb _ Mjumbe
12. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb _ Mjumbe
13. Mhe. Janeth Elias Mahawanga, Mb _ Mjumbe
14. Mhe. Dkt. John Danielson Pallangyo, Mb _ Mjumbe

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15. | Mhe. Josephine Thabita Chagula, Mb | | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Maryam Azan Mwinyi, Mb | _ | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Nora Waziri Mzeru, Mb | _ | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb | | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya, Mb | _ | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Sanya Jusa Jaffar, Mb | _ | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Silyvestry Francis Koka, Mb | | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Vuma Hole Augustine, Mb | | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Zuena Athumani Bushiri, Mb | | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, Pia napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa J. Mwihambi, *ndc*, kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Pia natoa shukrani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu vema shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athumani Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, *ndc,* na Makatibu wa Kamati Ndugu Zainabu Mkamba, Ndugu Mwajuma Ramadhan na Ndugu Charles Wanyancha na Msaidizi wa Kamati Ndugu Modesta Kipiko. Pia tunawashukuru Watumishi kutoka Idara ya Mshauri wa Masuala ya Sheria wa Bunge Ndugu Elizabeth Malongo na Ndugu Praisegod Lukio pamoja na Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo ulete tija kwa Taifa.

Naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuijadili na hatimaye kuridhia Maoni na Mapendekezo yake ili Serikali iweze kuyafanyia kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

Mhe. Jerry William Silaa, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**

7 Februari, 2023

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)*. *(Makofi)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha taarifa ya shughuli za Kamati ya *PAC* kwa kipindi cha Febuari 2022 hadi Febuari 2023. Taarifa hii inatolewa chini ya Kanuni ya 136(15) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi

Mungu kwa kutujalia zawadi ya uhai hivyo kuwa na fursa ya kukutana leo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 136 Kifungu Kidogo cha 15 cha Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya *PAC* ya mwaka kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Febuari 2022 hadi Febuari 2023 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili ilivyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za Kamati ya *PAC* zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Msingi wa majukumu hayo unatokana na taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali - *CAG* kama ilivyobainishwa katika katika Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipindi cha Febuari 2022 hadi Febuari 2023, Kamati ilijielekeza katika kubainisha namna taasisi za Serikali zinavyotumia Fedha za Umma katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali. Kwa kutumia taarifa za *CAG* kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30, Juni 2021, Kamati iliweza kutambua maeneo ambayo yana matumizi mabaya ya fedha za umma na kisha kutoa ushauri wa namna ya kushughulikia ubadhirifu uliobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo ya kina shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi kinachotolewa taarifa ni kama ifuatavyo:-

(i) Uchambuzi wa taarifa za hesabu zilizokagiliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na kaguzi

nyinginezo kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Tarehe 30 Juni 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Febuari 2022 hadi Februari 2023, Kamati ilipitia na kuchambua taarifa ya *CAG* kuhusu ukaguzi wa hesabu *(financial audit)* za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na baadhi ya kaguzi za ufanisi *(performance audit)* kwa mwaka wa fedha unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, *CAG* kwa kuzingatia masharti ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 alikamilisha kaguzi na kutoa Hati za Ukaguzi kwa jumla ya Taasisi 331 za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma 200. Vilevile *CAG* alikamilisha kaguzi za ufanisi 12, ambapo taarifa hizo ziliwasilishwa mbele ya Kamati na kujadiliwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Kamati. Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mafungu 12 ya Serikali Kuu, Mashirika ya Umma 21, Wakala za Serikali Mbili, kaguzi maalum Nne, Mabonde ya Maji mawili na kaguzi za ufanisi Nne. Shughuli hii ilifanyika kwa kupitia taarifa za ukaguzi za mafungu husika *(individual audit report)* pamoja na mahojiano na Maafisa Masuuli husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uchambuzi wa taarifa husika na mahojiano na Maafisa Masuuli kwa taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha uliyoishia tarehe 30 Juni, 2021, Kamati iliwasilisha taarifa yake Bungeni mnamo tarehe 02 Novemba, 2022, ambapo taarifa hiyo ilijadiliwa kwa siku tatu mfululizo na kisha kupata Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kuchukua nafasi hii kukupongeza sana na Spika Mwenyewe kwa kutoa muda wa kutosha wa kujadiliwa kwa taarifa ya Kamati mapema mwezi Novemba 2022 ni imani ya Kamati kuwa utaratibu huo utaongeza uwajibikaji wa Serikali katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Aidha, Kamati inategemea maazimio yote 14 yaliyotolewa na Bunge katika kipindi hicho yatatekelezwa kikamilifu na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 *CAG* alikamilisha kaguzi za kiufundi *(technical audit)*, kaguzi za ufanisi *performance audit* na kaguzi za kina - *comprehensive audit* kwa jumla sekta na miradi Tisa ya maendeleo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kaguzi zote hizo ziliwasilishwa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa taarifa za kaguzi hizo Tisa za kiufundi, ukaguzi wa kina na ukaguzi wa ufanisi. Aidha, kumefanyika mahojiano ya kina na Maafisa Masuuli wanaoshughulikia mafungu na sekta hizo. Naomba kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa uchambuzi yakinifu wa matokeo ya kaguzi hizo umejumuishwa katika aya ya 2.3 ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa za kaguzi za kiufundi, kaguzi za kina na kaguzi za ufanisi. Kaguzi za aina hii hulenga kuangalia kiwango cha uzingatiaji wa taratibu, sheria na kanuni *(compliance)* wakati wa utekelezaji wa miradi na iwapo thamani halisi ya fedha - *value for money* inakuwa imepatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa hizo kwa kila moja ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchaguzia wa ufanisi wa usimamizi wa Mifuko ya Uwezeshaji ya Wananchi Kiuchumi. Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mikopo chechefu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 50.4 kutoka kwenye mifuko Mitatu kama ifuatavyo:-

(i) Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ulikuwa na mikopo chechefu ya kiasi cha shilingi bilioni 20.1, kati ya shilingi bilioni 27.87 ya fedha zote zilizokopeshwa, kiwango ambacho ni sawa na asilimia 72 ya mikopo chechefu;

(ii) Mfuko wa Kilimo Kwanza ulikuwa na mikopo chechefu ya shilingi bilioni 27.6 kati ya shilingi bilioni 34.2 ya fedha zote zilizokopeshwa sawa na asilimia 80; na

(iii) Mfuko wa kutoa Mikopo kwa Wajisiriamali Wadogo *(SELF)* ulikuwa na mikopo chechefu ya shilingi bilioni 2.7 kati ya shilingi bilioni 36.9 zilizokopeshwa na sawa na asilimia Saba. Mikopo hii Chechefu ilichangiwa zaidi na utoaji wa mikopo kwa watu wasiyohusika, watu wasiyo na sifa. Vilevile ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa *SELF* uliwekeza kiasi kikubwa cha fedha sokoni kwenye dhamana na kutoa mikopo kwa Benki za Biashara ambayo hayaendani na shughuli za kimsingi zinazofanywa na mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa ufanisi katika usimamizi wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo. Ukaguzi ulibaini kuwa uandaaji wa mipango ya utekelezaji wa miradi, ulipaji wa fidia kwa waathirika wa miradi na upembuzi yakinifu umekuwa haufanyiki vya kutosha. Kwa mfano, kutokana na changamoto hizi ilisababisha kuchelewa kulipa fidia kwa waathirika wa mradi kwa siku zaidi ya 300 kwa miradi Miwili.

Kitendo hicho kilisababisha kuchelewa kwa miradi husika na kuongeza gharama za utekelezaji kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilihusu kutokuwepo kwa utaratibu madhubuti wa kuwezesha utoaji kwa wakati wa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)*. Changamoto hii ilibainika katika miradi mitatu kati ya miradi sita iliyokaguliwa. Mathalani ukaguzi ulibainisha kuwa uwepo wa makontena 233 yaliyokuwa na vifaa mbalimbali vya mradi wa umeme uliounganisha Tanzania na Kenya ambayo yalizuiliwa katika Bandari ya Dar es Salaam na kusababisha madai ya Wakandarasi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 3.55 kama gharama za kuhifadhi mizigo hiyo baada ya muda kupita, fedha hizi ni hasara kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa kiufundi kuhusu usanifu na usimamizi wa miradi teule ya usambazaji wa maji. Hadi kufikia Oktoba, 2021, kulikuwa na jumla ya miradi mikubwa 21 inayoendelea ya usambazaji maji nchini. Miradi hii ilikuwa na mikataba yenye jumla ya shilingi bilioni 110.7 dola za Marekani milioni 523.84 na Euro milioni 52.44.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muhtasari ukaguzi huu wa kiufundi ulibaini kukosekana kwa mpango kabambe wa Kitaifa kuwezesha Utekelezaji wa miradi ya maji *(National Water and Sanitation Master Planning)* haikuwepo. Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Maji haikuwa na mpango kabambe wa Kitaifa wa kuwezesha utekelezaji wa miradi ya usambazaji maji kinyume na Kifungu Na. 5(i) cha Sheria ya Usambazaji wa Maji na Usafi wa Usafi wa Mazingira ya 2019 *(Water Supply and Sanitation Act, 2019)*. Hali hii imesababisha utekelezaji wa miradi ya maji kufanyika bila kuzingatia mpango wa muda mrefu na endelevu, hivyo kuongeza gharama kwa Serikali na wakati mwingine kutopatikana thamani ya fedha, hali hii

ilipelekea gharama za miradi kuongezeka kwa dola za Marekani milioni 37.7, Euro 209176.74, shilingi trilioni moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kumekuwa na ucheleweshaji wa malipo kwa Wakandarasi ambapo Mkandarasi katika mradi mpya wa usambazaji maji wa Arusha na mradi wa maji wa Orkesumet aliomba kulipwa riba ya shilingi ya jumla milioni 728.6 na dola za Marekani 284,546.91.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa kiufundi katika usimamizi wa ujenzi wa mradi wa Daraja la Kigongo Busisi - Mwanza. Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi wa kiufundi wa mradi wa Kigongo Busisi umebainisha masuala ambayo Bunge linatakiwa kuyafahamu kama ifuatavyo:-

(i) Kuchelewa kumwajiri mshauri mwelekezi kwa hiyo Mkandarasi alitekeleza kazi ya ujenzi kwa Siku 54 bila ya usimamizi. Hali hii ingeweza kuathiri ubora wa shughuli za za ujenzi japo kwa sasa suala hili limefanyiwa kazi;

(ii) Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa malipo ya awali kwa Mshauri Mwelekezi wa mradi yalichelewa kulipwa kwa siku 154 yaani zaidi ya miezi mitano, jambo hili ni kinyume na mkataba hivyo kuisababishia Serikali gharama ya mradi ya takribani shilingi milioni 36.3 na riba ya shillingi milioni 58 kwa kuchelewesha kwa malipo.

(iii) Kuchelewa kwa malipo kwa Mshauri Mwelekezi kulichangiwa na kuchelewa kwa utoaji wa fedha kwa Wakala wa Barabara Nchini na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi - Sekta ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mahojiano na Afisa Masuuli wa Wakala wa Barabara Nchini, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ilichelewa kutoa fedha za Wakala wa Barabara Nchini kwa sababu ya kuchelewa kupokea fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa kina wa ujenzi wa ukarabati na uboreshaji wa viwanja 12 vya Ndege hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitumia jumla ya shilingi trilioni moja kwenye miradi ya ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa viwanja vya ndege 12, mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi huo ni pamoja na malipo ya fidia katika mradi wa Julius Nyerere kulipwa na kuongeza gharama za mradi hadi kufikia shilingi bilioni 29.7 kutoka shilingi bilioni 7.4 sawa na ongezeko la asilimia 302.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile *TAA* ilichelewa kufanya malipo kwa Mkandarasi kwa siku tano hadi 216 na kupelekea kuwepo kwa tozo ya riba kiasi shiling bilioni 11.4, kuchelewa huko ambako kumeingiza Serikali hasara ni kinyume na kifungu cha 5(b)(3) cha mkataba kati ya *TAA* na Mkandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi ulibaini pia kukosekana kwa mipaka ya wazi ya umiliki na majukumu baina ya *TAA* na *TANROADS* katika kufanya ununuzi, kusimamia mikataba usanifu, ujenzi na ukarabati wa viwanja 12 vya ndege vilivyojengwa hivyo kusababisha ongezeko la matumizi ya rasilimali za umma na kukosekana kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine ukaguzi ulifanywa katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma ulibaini matumizi ya ziada ya fedha za umma kutokana na *TAA* kuondoa taa zisizotumia nishati ya jua zenye thamani ya shilingi milioni 236 zilizowekwa na *TANROADS* wakati wa

upanuzi wa kiwanja hicho ili kuweka taa nyingine zinazotumia nishati ya umeme, hali hii inatokana na uwepo wa mwingiliano wa majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa kiufundi katika ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitenga Shilingi Bilioni 75.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali Mbili za Rufaa za Kanda za Mtwara na Mbeya na Hospitali Tatu za Rufaa za Mikoa ya Njombe, Katavi na Mara. Uchambuzi wa Kamati katika ukaguzi huu umebainisha dosari kadhaa ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi na Serikali ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha za umma iliyowekezwa inafikiwa, maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Dosari katika mipango ya usanifu wa majengo ya hospitali za Rufaa na Kanda;

(b) Mapungufu katika michakato ya taratibu za manunuzi na mapungufu katika uzingatiaji wa vipimo wakati wa ujenzi wa hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za usanifu zilisababisha majengo ya baadhi ya hospitali kutojengwa kwa viwango vinavyokubalika na Wizara ya Afya. Mathalani ilibanika vipimo vya majengo katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mara na Njombe vilikuwa na dosari.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa kiufundi katika ujenzi wa miradi ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari zilizobainika kupitia ukaguzi huu ni kama ifuatavyo:-

(i) Mapungufu katika uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake. Aidha, mikataba yote tisa iliyohakikiwa haikukamika ndani ya kipindi cha mkataba. Kulikuwa na kuchelewa kwa muda wa kukamilisha miradi ambapo muda wa kazi uliongezwa kwa vipindi kuanzia siku 80 hadi siku 450 sababu kubwa za ucheleweshwaji huo ni uwezo dhaifu wa Wakandarasi, kuchelewa kwa malipo kwa Wakandarasi, utendaji mbovu wa Wakandarasi na usimamizi dhaifu wa Mshauri Elekezi. Kwa mfano, ilibainika kuwa huduma za ushauri zilitakiwa kufanyiwa kwa gharama ambayo ni shilingi milioni 835.4 hata hivyo kiasi kilicholipwa kiliongezeka hadi kufikia shillingi bilioni 1.3 ongezeko hili ni sawa na asilimia 56 kiasi cha mkataba wa awali. Suala hili lilikuwa kinyume na Kanuni ya Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa kiufundi wa mradi wa umeme wa maporopmoko ya maji ya Mto Rusumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi wa ufanisi na kiufundi ya mradi wa umeme wa maporomoko ya Mto Rusumo imebainisha masuala yafuatayo:-

(a) Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi wakati wa mchakato wa kumpata mzabuni, dosari hii ilisababisha kufanyika kwa malipo zidifu yaliyosababishwa na kutunuku zabuni kwa mzabuni ambaye hakukidhi vigezo, ambapo kulingana na taarifa ya utekelezaji ya mradi gharama za mradi zitaongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 75.16 zilizopo katika mkataba hadi kufikia Dola za Marekani Milioni 119.6 sawa na asilimia 44.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatiliaji wa maazimio ya Bunge yatokanayo na taarifa ya mwaka ya Kamati Iliyowsilishwa Bungeni Februari, 2022; mnamo tarehe 26 Januari, 2023, Kamati ilikutana na Mlipaji Mkuu wa Serikali na *CAG* ili kupitia, kuchambua na kujadili Taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Yatokanayo na Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa katika Mkutano wa Sita wa Bunge wa Februari, 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baada ya kuchambua taarifa hiyo muhtasari wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge umechambuliwa katika Jedwali Na. 2.2 katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kutathmini thamani ya fedha iliyotumika; mapema mwezi Machi, 2022, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha na thamani halisi ya fedha iliyotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Ziara zilifanyika katika Mikoa ya Singida, Manyara, Arusha, Tanga, Dar es Salaam na Morogoro. Jumla ya miradi ya maendeleo 19 ilitembelewa na kukaguliwa kama ilivyofafanuliwa katika ukurasa wa 50 hadi wa 60 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mafunzo na Semina za Kuwajengea Uwezo Wajumbe. Naomba kumshukuru Spika na wewe mwenyewe binafsi kwa kutoa idhini kwa Kamati ya *PAC* kupatiwa mafunzo na semina mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uelewa, ufanisi na uwezo wa wajumbe katika kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapendekezo. Kuhusu dosari zilizobainika kwenye usimamizi wa mifuko ya uwezeshaji wanancbi kiuchumi, Bunge linaazimia kwamba: -

(a) Serikali ifanye tathmini ya kina na mapitio ya mifuko yote 52 ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuangalia iwapo kuna sababu za msingi za kuendelea kuwa na mifuko hiyo yote kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wa kila mfuko. Tathmini hii ikamilike kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha.

(b) Katika kipindi cha mpito, Serikali iimarishe udhibiti na usimamizi wa mifuko husika ili kuhakikisha utoaji wa fedha kwenye mifuko hiyo unafanyika baada ya uthibitisho wa mahitaji yote muhimu ya dhamana na nyaraka.
Aidha, fedha zinazotolewa zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa na urejeshaji wa mikopo ufanyike kwa wakati.

(c) *CAG* afanye ukaguzi wa kina *(comprehensive audit)* wa mifuko yote 52 ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kubainisha mapungufu yaliyopo katika mifuko hiyo. Baada ya Taarifa ya Ukaguzi huo, Serikali ichukue hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Riba Zinazotokana na Kuchelewesha Malipo ya Wakandarasi na Washauri wa Miradi Pamoja na Kuchelewa Kutoa Misamaha Stahiki wa Kodi ya *VAT*. Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali iwe na mfumo wa wazi, thabiti, uhakika na wa haraka wa kuhakiki, kutambua na kulipa malipo ya wakandarasi kwa wakati kwa kuzingatia masharti ya mikataba ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za umma.

(b) Serikali ipunguze mlolongo wa utoaji wa msamaha stahiki wa kodi ya *VAT* kwa vifaa vya miradi ya ujenzi toka nje. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe kwa Maafisa wa Serikali waliochelewesha suala hili kwa kutowajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Mapungufu Katika Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo Inayofadhiliwa Kupitia Fedha za Mikopo. Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali iboreshe eneo la uibuaji, usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwa ufadhili wa mikopo kwa kuhakikisha mapitio ya awali ya miradi yanakuwa toshelevu na uchambuzi wa kina unakuwa umefanyika.

(b) Serikali iboreshe utaratibu baina ya Wizara ya Fedha na Mipango na Watekelezaji wa Miradi katika Sekta na wadau wengine. Hii ifanyike sambamba na uboreshaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika miradi inayofadhiliwa kwa mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hasara zinazotokana na muingiliano wa kimajukumu kati ya *TAA* na *TANROADS* Bunge linaazimia kwamba;

Serikali irejeshe kikamilifu jukumu la ujenzi, ukarabati na usimamizi wa viwanja vyote vya ndege hapa nchini kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)* kabla ya mwaka huu wa fedha kukamilika ili kuokoa fedha za umma zinazopotea kwa muingiliano uliopo wa taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kutoanza ukarabati wa Kituo cha Umeme cha Hale tangu kusainiwa mkataba wa

mkopo tangu tarehe 11 Julai, 2013, hivyo kusababisha hasara ya shilingi 772,156,800 Bunge linaazimia kwamba;

Serikali itekeleze mradi huo mapema iwezekanavyo kabla ya kufikia ukomo wa mkataba wa fedha za mkopo na msaada ili kuokoa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mapungufu katika usimamizi wa mikataba na ongezeko la gharama za miradi, Bunge linaazimia;

(a) Serikali ihakikishe upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unafanyika ipasavyo kabla ya utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo,

(b) Serikali iwe na utaratibu wa kuchukua hatua stahiki kwa wakati kwa watendaji wote na wasimamizi wa miradi iliyobainika kuwa na dosari kutokana na kutokuwa na matumizi bora ya fedha za umma pamoja na kutowasimamia wakandarasi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya CAG katika kaguzi za kiufundi, kaguzi za kina na kaguzi za ufanisi, Bunge linaazimia kwamba; Serikali itekeleze ushauri na mapendekezo yaliyotolewa katika taarifa hizo tisa za miradi kwa ukamilifu. Aidha, katika kipindi cha kila robo mwaka, Sekta husika zilizokaguliwa ziwasilishe kwa CAG taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ambayo itafanyiwa uhakiki na kisha kuwasilishwa kwenye Kamati kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini hivyo kuliongoza Bunge letu kwa umakini na weledi mkubwa. Siku zote uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu

kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati kila mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. Tumefanya kazi wote kwa nusu ya uhai wa kwanza wa Bunge

letu la kumi na mbili kwa ushirikiano mkubwa. Naomba majina yao yote yaingie kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc*, kwa ushauri wake kwa Kamati. Natoa shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati kupitia kwa Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athuman Hussein, *ndc*, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, *ndc*, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Sosthenes Maseke, Ndugu Amina Salumu Namtema na Ndugu Joseph Munishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati inatambua na ka kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi yetu ya Taifa ya Ukaguzi *(NAOT)* na Wizara ya Fedha na Mipanmgo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**7 FEBRUARI, 2023**

## TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2022 HADI FEBRUARI 2023 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(*Inatolewa chini ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020)*

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kutujalia zawadi ya uhai hivyo kuwa na fursa ya kukutana hapa leo hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha kuanzia Februari 2022 hadi Februari 2023 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo ya kina na ufafanuzi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi chote hicho yamefafanuliwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

### 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Majukumu hayo ni: -

a) Kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika wizara za Serikali na mashirika ya umma yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yaliyobainika kwa mujibu wa kanuni hii; na

c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa wizara za Serikali na mashirika ya umma kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

### 1.3 Miongozo Iliyotumika na Namna Kamati Ilivyotekeleza Majukumu yake

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifanya rejea ya kina katika nyaraka zifuatazo: -

a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;
b) Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (2020/21);
c) Taarifa za kaguzi mahsusi *(individual audit report)* za mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma;
d) Barua za upungufu uliobanishwa na ukaguzi *(management letter)* za mafungu mahususi;
e) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008; Sura 418;
f) Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348;
g) Sheria ya Bajeti; Sura 439;
h) Sheria ya Msajili wa Hazina; Sura 370;
i) Sheria ya Manunuzi ya Umma; Sura 410;

j) Sheria ya Usajili wa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu, Sura 286;
k) Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura 296; na
l) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilitumia mbinu zifuatazo: -

a) Kupokea, kuchambua na kujadili maelezo mafupi *"briefs"* za CAG kuhusu hoja za ukaguzi za mafungu husika;
b) Mahojiano na Maafisa Masuuli kuhusu hoja za ukaguzi;
c) Uchambuzi wa kina wa taarifa za ukaguzi za mafungu mahususi;
d) Ziara za ukaguzi wa ufanisi katika miradi ya maendeleo;
e) Semina kuhusu majukumu ya Kamati;na
f) Tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya usimamizi wa fedha za umma.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### 2.1 Maelezo ya Jumla Kuhusu Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Februari 2022 hadi Februari 2023, Kamati ilijielekeza kutekeleza majukumu yake yaliyofafanuliwa katika Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020. Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilijielekeza katika kubainisha namna taasisi za Serikali zilivyotumia fedha za umma katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kutumia Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu na mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, Kamati

iliweza kutambua maeneo ambayo yana matumizi mabaya ya fedha za umma na kisha kutoa ushauri wa namna ya kushughulikia ubadhirifu uliobainika.

**Mheshimiwa Spika,** Maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma yalibainika kupitia uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kutathmini thamani halisi ya fedha iliyotumika na ufuatiliaji wa mapendekezo ya Kamati ambayo yalikuwa yakitolewa ili kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kutimiza majukumu yao kwa weledi na ufanisi, njia mbalimbali za kuwajengea uwezo zilifanyika ikiwa ni pamoja na semina na mafunzo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa maelezo ya kina, shughuli zilizotekelezwa na Kamati katika kipindi tunachokitolea taarifa ni kama ifuatavyo: -

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa za Hesabu Zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi Nyinginezo kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2021

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Februari 2022 hadi Februari 2023, Kamati ilipitia na kuchambua Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa hesabu (financial audit) za serikali kuu, mashirika ya umma na baadhi ya kaguzi za ufanisi (performance audit) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa

kuzingatia masharti ya Ibara ya 143[2] ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, alikamilisha kaguzi na kutoa hati za ukaguzi kwa jumla ya Taasisi 331 za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara na Idara zinazojitegemea, Wakala, Mifuko Maalum, Sekretarieti za Mikoa, Vyama vya Siasa na Bodi za Mabonde ya Maji. Aidha, ukaguzi ulifanyika kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa (consolidated accounts), ukaguzi wa Malipo Tarajali ya Pensheni, Hospitali za Rufaa na Kaguzi Maalumu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikagua na kutoa taarifa za jumla ya Mashirika ya Umma 200 ikilinganishwa na Mashirika ya Umma 165 yaliyokaguliwa kwa mwaka 2019/2020. Vilevile Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikamilisha Kaguzi za Ufanisi 12 ambapo taarifa hizo ziliwasilishwa mbele ya Kamati na kujadiliwa ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika ngazi ya Kamati, Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mafungu 12 ya serikali kuu, mashirika ya umma 21, wakala za serikali 2, kaguzi maalumu 4, mabonde ya maji 2 na kaguzi za ufanisi 4. Shughuli hii ilifanyika kwa kupitia taarifa za ukaguzi za mafungu husika (individual audit report) pamoja na mahojiano na Maafisa Masuuli husika.

**Mheshimiwa Spika,** Maafisa Masuuli wa mafungu husika walihojiwa na Kamati kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Fedha za Umma Sura 348 kama ilivyorekebishwa Mwaka 2020. Kifungu hicho kinampa jukumu la moja kwa moja (personal liability) Afisa Masuuli husika katika uwajibikaji na usimamizi wa matumizi ya fedha za umma kwenye fungu husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia uchambuzi wa taarifa husika na mahojiano na Maafisa Masuuli kwa taarifa ya hesabu

[2] Mamlaka na majukumu ya kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

zilizokaguliwa za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021, Kamati iliwasilisha taarifa yake Bungeni mnamo tarehe 02 Novemba, 2022 ambapo taarifa hiyo ilijadiliwa kwa siku tatu (3) mfululizo na kisha kupata maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii kukupongeza sana kwa kutoa muda wa kutosha wa kujadiliwa kwa taarifa ya Kamati mapema mwezi Novemba 2022. Ni imani ya Kamati kuwa utaratibu huo utaongeza uwajibikaji wa Serikali katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Aidha, Kamati inategemea maazimio yote kumi na nne (14) yaliyotolewa na Bunge katika kipindi hicho yatatekelezwa kikamilifu na Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwingine hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu alikamilisha kaguzi za kiufundi (technical audit), kaguzi za ufanisi (performance audit) na kaguzi za kina (comprehensive audit) kwa jumla ya sekta na miradi tisa (9) ya maendeleo. Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa kaguzi zote hizo ziliwasilishwa mbele ya Kamati. Kaguzi hizo ambazo zimepitiwa na kuchambuliwa na Kamati tarehe 16 hadi 27 Januari, 2023 ni kama ifuatavyo: -

a) Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kuhusu Usanifu na Usimamizi wa Miradi Teule ya Usambazaji wa Maji;
b) Taarifa ya Ukaguzi Maalum wa Ujenzi, Ukarabati na Uboreshaji wa Viwanja vya Ndege;
c) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo ya Ujenzi inayotekelezwa Kupitia Mikopo;
d) Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Usanifu na Utekelezaji wa Miradi ya Skimu za Umwagiliaji Nchini;
e) Taarifa ya Ukaguzi ya Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo (RRFHP);

f) Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi;
g) Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kuhusu Ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Kanda;
h) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mifuko ya Utoaji Mikopo na Uwezeshaji Kifedha; na
i) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Maendeleo na Ukuzaji wa Utalii;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa taarifa za kaguzi hizo tisa (9) za kiufundi, ukaguzi wa kina na ukaguzi wa ufanisi. Aidha, kumefanyika mahojiano ya kina na Maafisa Masuuli wanaoshughulikia mafungu na sekta husika. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi yakinifu wa matokeo ya kaguzi hizo umejumuishwa katika aya 2.3 ya taarifa hii.

## 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Kaguzi za Kiufundi, Kaguzi za Kina na Kaguzi za Ufanisi

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha kuanzia tarehe 16 Januari hadi tarehe 27 Januari, 2023, Kamati ilijielekeza kufanya uchambuzi wa kina wa taarifa za kaguzi za kiufundi (technical audit), kaguzi za ufanisi (performance audit) na kaguzi za kina (comprehensive audit) ambazo zinatokana na ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu za serikali kuu na mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muhtasari naomba kutoa maelezo mafupi kuhusu aina, malengo na tafsiri ya kaguzi hizi kama ifuatavyo: -

### a) Ukaguzi wa Ufanisi (Performance Audit)

Ni aina ya ukaguzi uliojikita kuangalia kama kuna *Uwekevu, Tija na Ufanisi* (economy, efficiency and effectiveness)

miongoni mwa taasisi za umma katika matumizi ya rasilimali ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Ukaguzi wa ufanisi huchunguza iwapo shughuli, mipango au miradi ya Serikali inayohusisha ukusanyaji au matumizi ya fedha za umma katika wizara, idara, mamlaka za serikali za mitaa na mashirika mengine ya umma inafanyakazi kwa kuzingatia kanuni tatu (3) yaani uwekevu, ufanisi na tija.

**b) Ukaguzi wa Kiufundi (Technical Audit)**

Ni ukaguzi unaojumuisha uchunguzi na tathmini huru juu ya upangaji, usanifu, ununuzi na utekelezaji wa miradi ya ujenzi, kwa lengo la kutoa matokeo ya usimamizi na utekelezaji wa miradi hiyo kwa wahusika juu ya masuala yote yanayo athiri utekelezaji na utendaji wa miradi hiyo.

Ukaguzi wa kiufundi ni ukaguzi katika mchakato mzima wa utekelezaji wa mradi kuanzia hatua ya *maandalizi ya awali*, *utekelezaji wa mradi*, *ukamilishaji na makabidhiano ya mradi*. Hujikita zaidi kutazama kama mradi umetekelezwa kwa wakati, ndani ya gharama iliyokusudiwa, kwa ubora uliokusudiwa na kama malengo ya uanzishwaji wa mradi yametimia.

**c) Comprehensive Audit**

Ni Mbinu ya Ukaguzi unaofanyika kwa kuzingatia misingi ya ukaguzi wa fedha na wa ufanisi. Mbinu hii huwezesha kuangalia kwa upana masuala ya fedha na yale ya uwekevu, ufanisi na tija iwapo shughuli, mipango au miradi ya Serikali inayohusisha ukusanyaji au matumizi ya fedha za umma katika wizara, idara, mamlaka za Serikali za mitaa na mashirika mengine ya umma inafanyika kikamilifu na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo ya ufafanuzi, naomba kusisitiza kuwa Taarifa hizi ni muhimu kwa kuwa zinahusu ukaguzi wa fedha zilizotumiwa na Serikali katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo katika maeneo tisa (9). Kaguzi za aina hii hulenga kuangalia kiwango cha uzingatiaji wa taratibu, sheria na kanuni (compliance) wakati wa utekelezaji wa miradi na iwapo thamani halisi ya fedha (value for money) inakuwa imepatikana.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya mahojiano ya kina na Maafisa Masuuli wanaosimamia sekta zilizofanyiwa ukaguzi nilioufafanua hapo juu, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa hoja zinazowasilishwa katika taarifa hii ni zile ambazo zinahitaji msisitizo wa Bunge ili kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Aidha, hoja hizo hazikuwa zimefungwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuwa hazikuwa na majibu ama vielelezo vya kujitosheleza.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uchambuzi wa taarifa hizo kwa kila moja ni kama ifuatavyo: -

### 2.3.1 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi wa Usimamizi wa Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ufanisi wa Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umebainisha kuwa, Tanzania imekuwa na historia ndefu kwenye sekta ya asasi ndogo ndogo za kifedha mijini na vijijini. Mnamo mwaka 1991, Serikali ilitambua umuhimu wa asasi ndogo ndogo za kifedha katika sekta ya fedha ambapo asasi ndogo za kifedha zilijumuishwa katika sera ya mageuzi ya kifedha ya mwaka 1991, (Sera ya Taifa ya Asasi Ndogo Ndogo za Kifedha ya mwaka 2000).

**Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kuongeza ushiriki wa Watanzania katika sekta ya fedha, Serikali iliamua kuweka mkazo kwenye kutanua huduma za kifedha hususani kwa watu wenye kipato cha chini. Miongoni mwa mikakati iliyochukuliwa na Serikali ilikuwa ni pamoja na; kuanzisha Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo ililenga kutoa huduma za kifedha kwa watanzania masikini na asasi ndogo ndogo; kutunga Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Namba 16 ya mwaka 2014; kuanzisha Sera ya Taifa ya Asasi Ndogo za Kifedha ya Mwaka 2000 na kupitishwa Mwaka 2017; na Kanuni za Asasi Ndogo za Kifedha ya Mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, pamoja na jitihada za Serikali, kiwango cha watanzania kutojumuishwa (financial exclusion) kwenye mfumo rasmi katika sekta ya fedha ni asilimia 28 ukilinganisha na nchi nyingine ndani ya Jumuia ya Afrika Mashariki ambapo Rwanda ni asilimia 11, Kenya asilimia 18 na Uganda asilimia 14 mtawalia. Kutokana na maelezo yaliyofafanuliwa hapo juu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliamua kufanya ukaguzi wa ufanisi katika eneo hili. Katika ukaguzi huu, CAG aliongozwa na sababu kuu tatu (3) zifuatazo: -

**a) Dosari Katika Usimamizi wa Mifuko ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi**

Mapitio ya Taarifa za Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ya mwaka 2019, yalibainisha uwepo wa mifuko takribani 13 kati ya 52 inayomilikiwa na Serikali ambayo inatoa huduma ndogo za kifedha nchini ingawa mifuko hiyo ilikuwa na changamoto ya uhaba wa mtaji, uwezo na ujuzi mdogo wa kiutendaji;

**b) Uwepo wa Mikopo Chechefu**

Taarifa ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha ulioishia mwezi Juni, 2017,

ilibainisha kuwa, mfuko wa wajasiliamali wadogo (SELF Microfinance) haukuweza kurejesha kiasi cha **Shilingi Milioni 27** kutoka katika mikopo iliyotolewa. Pia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alibaini kuwa kiasi cha **Shilingi Milioni 126.9** tu kati ya **Shilingi Bilioni 1.159** ya mikopo yote iliyotolewa sawa na asilimia 11 iliweza kurejeshwa; na

**c) Mikopo Inayotolewa Kutowafikia Walengwa**
Mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi haijawafikia walengwa na makundi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupitia na kuchambua sababu za ukaguzi huu wa ufanisi, Kamati imebaini kuwa ukaguzi huu ulilenga katika kuangalia mchakato mzima wa kutoa fedha, uratibu, usimamizi na tathmini zinazofanywa na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Wizara ya Fedha na Mipango; na namna mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinavyoendeshwa.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebainisha vilevile kuwa ukaguzi ulijikita kwenye mifuko na programu zinazotoa mikopo aidha moja kwa moja au kwa skimu za udhamini. Ukaguzi ulihusisha mikoa miwili (2) ya Dodoma na Dar es Salaam, hii ni kwa sababu makao makuu ya wakaguliwa yapo kwenye mikoa hii. Ukaguzi ulihusisha kipindi cha miaka minne (4) ya fedha kuanzia mwaka 2017/18 hadi mwaka 2020/21.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu matokeo ya ukaguzi huo wa ufanisi kama ifuatavyo: -

**a) Uwepo wa Mikopo Chechefu Kiasi cha Shilingi Bilioni 50.4 Kati ya Shilingi Bilioni 98.3 kwa Mifuko Mitatu (3)**
Ukaguzi ulibaini kuwa, kulikuwa na mikopo chechefu yenye

thamani ya **Shilingi Bilioni 50.04** toka kwenye mifuko mitatu. Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, ulikuwa na mikopo chechefu ya **Shilingi Bilioni 20.1** kati ya **Shilingi Bilioni 27.87** ya fedha zote zilizokopeshwa, kiwango ambacho ni sawa na **asilimia 72**; Mfuko wa Kilimo Kwanza ulikuwa na mikopo chechefu ya **Shilingi Bilioni 27.6** kati ya **Shilingi Bilioni 34.2** ya fedha zote zilizokopeshwa, sawa na **asilimia 80**; na Mfuko wa kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo wa SELF ulikuwa na mikopo chechefu ya **Shilingi Bilioni 2.7** kati ya **Shilingi Bilioni 36.9** zilizokopeshwa sawa na **asilimia 7**. Mikopo hii chechefu ilichangiwa zaidi na kutoa mikopo kwa watu wasiokuwa na sifa;

**b) Fedha Kutopelekwa Kwa Makundi Yaliyokusudiwa**

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF MF) uliwekeza kiasi kikubwa cha fedha sokoni kwenye dhamana na kutoa mikopo kwa benki za biashara ambayo haiendani na shughuli za kimsingi zinazofanywa na mfuko huo.

Mathalani, kwa kipindi cha mwaka wa fedha kuanzia Juni, 2017/18 hadi 2020/21, kiasi cha mkopo chenye thamani ya **Shilingi Bilioni 72.2** (sawa na asilimia 56) toka Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF MF) kilitolewa kwa benki za biashara badala ya kutoa mkopo kwa wajasiriamali waliopo kwenye maeneo ambayo huduma za fedha hazipatikani ipasavyo kadiri ya malengo ya kuanzishwa kwa mfuko huo;

**c) Kutofanyiwa Kazi kwa Maombi ya Dhamana ya Kiasi cha Shilingi Bilioni 227**

Ukaguzi ulibaini kuwa kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi 2020/21, maombi ya mikopo kutoka kwenye mabenki ya kibiashara yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 227** hayakupewa dhamana na Benki Kuu ya Tanzania.

Kushindwa kutoa dhamana kwa maombi ya mikopo hiyo kulisababishwa na kumalizika kwa muda wa Mkataba wa

Uwakala kati ya Wizara ya Fedha na Mipango na Benki Kuu ya Tanzania tangu tarehe 8 Julai, 2008. Kutokana na hali hii, lengo kuu la mfuko huu la kukuza uchumi kupitia kuuza bidhaa nje ya nchi kwa lengo la kuongeza fursa za ajira na kuongeza mapato kupitia fedha za kigeni linaweza lisifikiwe;

**d) Dhamana za Mikopo Kwenye Mfuko wa Dhamana ya Mikopo ya Kuuza Nje zilizotolewa Kinyume na Miongozo**

Kifungu Namba 8.1 cha Sera ya Mpango wa Dhamana ya Mikopo na Muongozo wa kazi ya mwaka 2003, kinaelezea kuwa kiwango cha juu cha dhamana kinatakiwa kuwa (i) dhamana ya kabla ya kusafirisha mzigo nje kuwa asilimia 80 (ii) dhamana ya kusafirisha mazao nje kuwa asilimia 85 (iii) dhamana baada ya kusafirisha mizigo nje kuwa asilimia 75 na (iv) dhamana ya ufanisi kuwa asilimia 75.

Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji ya mwaka 2020, yanaonesha kuwa, kiasi cha **Shilingi Bilioni 84** cha dhamana kilitolewa ikiwa ni kiwango cha juu kupita viwango elekezi;

**e) Shilingi Bilioni 7 za Mfuko wa Wakulima Wadogo Katika Benki ya Kilimo Kutotumika kwa Malengo Husika**

Muongozo wa Usimamizi wa Mfuko wa Dhamana wa Wakulima Wadogo unaelekeza fedha za mfuko kutumika kwa ajili ya kulipa madai kwa dhamana zilizotolewa na madhumuni mengine yoyote, kama inavyoweza kuwa imeidhinishwa na Serikali au Bodi ya Benki ilimradi inachangia malengo ya mfuko.

Mapitio ya Taarifa za Benki ya Akaunti ya Mfuko yalibainisha kuwa, **Shilingi 7,000,000,000** na **Shilingi 3,824,394,500** zilihamishwa kwenda kwenye akaunti ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) mtawalia. Benki ya Maendeleo ya Kilimo iliieleza Timu ya Ukaguzi kuwa **Shilingi 3,824,394,500** zilipelekwa Benki ya NMB kutoka TADB kwa ajili ya shughuli za Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo na **Shilingi 7,000,000,000** zilihamishiwa kwenye akaunti ya Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa dhumuni la usimamizi bora wa

ukwasi wa benki hiyo. Uamuzi wa kutumia fedha hizo kwa dhumuni la usimamizi bora wa ukwasi wa benki ni kinyume na kusudi la fedha hizo; na inaweza kuathiri utoaji wa dhamana kwa wakulima wadogo.

**f) Mapungufu Katika Uratibu wa Uanzishwaji na Uendeshaji wa Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Mapitio ya Ripoti ya Wizara ya Uwezeshaji, Viwanda na Biashara ilibainisha kuwa, kulikuwa na mifuko na programu za Serikali 52 ambayo inahusu uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Ukaguzi ulibaini kuwa, asilimia 88 (sawa na mifuko 46 kati ya 52) ya mifuko hiyo ilikuwa inatoa mikopo, dhamana, ruzuku, na programu zingine za uchumi. Asilimia 12 (sawa na mifuko 6 kati ya 52) ya mifuko hiyo ilijikita katika urejeshaji wa mikopo na haitoi mikopo mipya.

Ukaguzi ulibaini kuwa, uwepo wa mifuko mingi ambayo inalenga kutoa huduma zilezile umechangiwa na kutoanza kazi kwa Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji kwa miaka 17 sasa toka kuanzishwa kwake kwa mujibu wa Vifungu Namba 16 na 17 vya Sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004; na

**g) Dosari Katika Ufuatiliaji wa Mifuko ya Uwezeshaji Kiuchumi**

Ukaguzi ulibaini kuwa kwa kipindi chote cha ukaguzi huu kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2020/2021, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hawatekelezi ipasavyo jukumu lao la kutathmini utendaji wa mifuko na programu za Serikali za kuwezesha wananchi kiuchumi.

**2.3.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi Inayotekelezwa kwa Fedha za Mikopo**

**Mheshimiwa Spika,** Usimamizi wa miradi ya maendeleo

inayotekelezwa kwa kutumia fedha za mikopo ni muhimu ili kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa wakati na kupunguza tozo zinazotozwa kama amana za mkopo (commitment fee).

**Mheshimiwa Spika,** Usimamizi mzuri wa miradi utahakikisha kwamba urejeshaji wa mikopo unaanza pindi ambapo miradi inatoa huduma. Hivyo, ni muhimu kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba maswala yote yanayoweza kuathiri ukamilishaji wa ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa wakati yanapatiwa ufumbuzi.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Fedha na Mipango ndiyo msimamizi mkuu wa miradi yote inayotumia fedha za mikopo na ambayo inatekelezwa na taasisi mbalimbali za Serikali hapa nchini. Vilevile, Wizara ya Fedha na Mipango ina jukumu la kuidhinisha mapendekezo yote ya miradi, kusaini mikataba ya mikopo, kufanya ufuatiliaji na utathmini wa miradi na kuidhinisha malipo yote yanayowasilishwa na watekelezaji wa miradi inayotumia fedha za mikopo.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo kubwa lililochangia kufanyika kwa ukaguzi huu ni uwepo wa kiasi cha **Shilingi Trilioni 11.96** kilichopangwa kutumika katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (5) kuanzia 2016/17-2020/21. Kiasi hicho cha fedha kilipangwa kutumika ili kuweza kufikia malengo ya maendeleo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa msingi huo, ukaguzi huu wa ufanisi ulikusudia kuainisha maeneo ya kuboresha katika usimamizi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa kutumia fedha za mikopo ili kuifanya iwe yenye manufaa kwa nchi. Muhtasari wa matokeo ya ukaguzi huu wa ufanisi ni kama ifuatavyo: -


a) Ukaguzi ulibaini kuwa, uaandaji wa mipango ya

utekelezaji wa miradi, ulipaji wa fidia kwa waathirika wa miradi na upembuzi yakinifu umekuwa haufanyiki vya kutosha. Kwa mfano kutokana na changamoto hizi, ilisababisha kuchelewa kulipa fidia kwa waathirika wa mradi kwa siku zaidi ya 300 kwa miradi 2. Kuchelewa huko kulisababisha mradi kuchelewa kuanza na ongezeko la gharama za utekelezaji kwa Serikali. Miradi iliyochelewa kutokana na kuchelewesha fidia ni ule wa Kuwezesha Biashara na Uchukuzi Kusini mwa Afrika *(Southern Africa Trade and Transport Facilitation Project, SATTFP)* na mradi wa kuunganisha umeme Tanzania na Kenya;

b) Ilibainika kuwa baadhi ya vipengele vinavyohusu muda wa utekelezaji na gharama za mradi havikuchambuliwa ipasavyo kwa sababu ya uwepo wa wataalam wachache wenye uwezo wa kuchambua michoro na hesabu za usanifu wa miradi. Aidha, ilibainika kuwa Idara ya Mipango ya Taifa ina Wahandisi wawili (2) pekee na haina mkadiriaji majenzi hata mmoja (1) ambao ni wataalam muhimu kwa ajili ya kutathmini gharama za miradi hiyo kwa ufanisi;

c) Ukaguzi ulibaini pia kuwa kuchelewa kukamilika kwa miradi kwa wakati ilikuwa kinyume na masharti ya mikopo. Miradi yote sita (6) iliyokaguliwa ilichelewa kukamilika kwa wastani wa miezi kumi na mbili (12) hadi themanini (80). Aidha, kiasi cha **Dola za Marekani 1,180,578.42** zilitozwa kama tozo kwenye fedha za mikopo ambazo hazikuchukuliwa kwa miradi miwili (2) kutokana na kuchelewa kwa miradi husika. Mchanganuo wa kiwango cha kuchelewa kuanza miradi umefafanuliwa katika Kielelezo Na. 1 hapa chini: -

**Kielelezo Na. 1: Kiwango cha kuchelewa kukamilika kwa miradi 6 ya maendeleo**




**Chanzo:** ***Uchambuzi wa Kamati kutoka kwenye taarifa za ukaguzi za miradi inayofadhiliwa kwa mikopo.***

**Kielelezo Na.1** kinafafanua kwamba, miradi yote sita (6) ya maendeleo iliyokaguliwa, ilikamilika baada ya tarehe za kufungwa kwa mkataba wa mkopo, jambo ambalo lililazimu Wizara ya Fedha na Mipango kurekebisha tarehe za kufunga mkataba wa mkopo, hivyo thamani ya mradi inakuwa haijapatikana wakati mkopo umeanza kulipwa;

d) Kutokuwepo kwa utaratibu madhubuti wa kuwezesha utoaji kwa wakati wa Msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).[3] Changamoto hii ilibainika katika miradi mitatu (3) kati ya miradi sita (6) iliyokaguliwa. Mathalani ukaguzi ulibainisha uwepo wa makontena 233 yaliyokuwa na vifaa mbalimbali vya mradi wa umeme unaounganisha Tanzania na Kenya (KTPIP) ambayo yalizuiliwa katika bandari

[3] Rejea masharti ya Kifungu cha 6(2) b cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Toleo Lililorekebishwa, 2019, na masharti ya Kanuni ya 4 (2) ya Kanuni za Kodi ya Ongezeko la Thamani (Taratibu za Ufuatiliaji) za 2018.

ya Dar es Salaam na kusababisha madai ya wakandarasi yenye thamani ya **Dola za Marekani Milioni 3.55** kama gharama za kuhifadhi mizigo baada ya muda kupita. Fedha hizi ni hasara kwa Serikali;

e) Ukaguzi ulibaini kuwa malipo kwa baadhi ya wakandarasi huchelewa. Uchelewaji mkubwa zaidi wa malipo ulibainika katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20, ukilinganisha na mwaka uliofuata wa 2020/21 ambapo Serikali iliamua kubadili mfumo wa malipo. Kwa mfano hali hii ilileta athari za gharama za mradi zilizotokana na kuchelewa kwa malipo hususani kwenye mradi wa Mpango wa Kuimarisha Sekta ya Usafirishaji (TSSP) ambayo mkandarasi alidai riba ya kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.3** kwa vipande 4 vya mradi huo (lot1, lot2, lot 3 na Mbinga-Mbamba bay);

f) Mapungufu katika shughuli za uratibu kati ya wizara zinazotekeleza miradi na wizara ya fedha. Wizara ya Fedha na Mipango haikuwa na utaratibu madhubuti wa kuratibu shughuli za utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo. Ukaguzi ulibainisha kuwa kwa miaka ya nyuma wizara haikuwa imetayarisha na kutekeleza mipango kwa ajili ya kuratibu shughuli zinazofanywa na watekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa kutumia fedha za mikopo. Kutokuwepo kwa uratibu kunainyima wizara ya fedha na mipango fursa ya ufuatiliaji na tathmini ya matumizi ya fedha za umma japo yenyewe ndiyo inahusika na kuchukua mikopo; na

g) Dosari katika zoezi zima la ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa kwa mikopo. Ukaguzi ulibaini kuwa, Wizara ya Fedha na Mipango haikuwa na mpango madhubuti wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hili lilithibitishwa na kukosekana kwa mpango wa kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kipindi

chote cha kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2019/20 mfululizo. Jambo hili ni kinyume na Mwongozo wa Uendeshaji na Usimamizi wa Uwekezaji[4].

### 2.3.3 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Kuhusu Usanifu na Usimamizi wa Miradi Teule ya Usambazaji wa Maji

**Mheshimiwa Spika,** Sekta ya maji nchini ni mojawapo ya sekta muhimu kwa ustawi wa wananchi. Serikali ya Tanzania ilitenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya usambazaji wa maji ili kukidhi matakwa ya Lengo Na. 6 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) linalotaka kuwepo na uhakika wa upatikanaji wa huduma ya maji safi na utoaji wa maji taka kwa wananchi ifikapo mwaka 2030.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia mwezi Oktoba 2021, kulikuwa na jumla ya miradi mikubwa 21 inayoendelea ya usambazaji maji nchini. Miradi hii ilikuwa na mikataba yenye jumla ya **Shilingi Bilioni 110.7**, **Dola za Marekani Milioni 523.84** na **Euro Milioni 52.44**. Ukaguzi wa Kiufundi wa Utoaji wa huduma za usambazaji maji uliofanywa na CAG ulilenga kutathmini iwapo wizara ya maji inapanga, inasanifu na kutekeleza miradi ya maji ipasavyo ili kuhakikisha usimamizi na utoaji wa huduma za maji nchini unakuwa endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi ulihusisha miradi sita ya usambazaji maji ambayo ni hii ifuatayo: -

a) Mradi wa usambazaji maji wa Mugango–Kiabakari-Butiama;

b) Mradi wa upanuzi wa bomba la maji la ziwa victoria hadi Tabora- Nzega-Igunga;

[4] Rejea Kifungu cha 4.2 cha Mwongozo wa Kupanga Miradi na Majadiliano ya Kupata Mikopo, Kutoa Dhamana na Kupokea Msaada, 2020.

c) Mradi wa usambazaji maji wa Arusha mpya (New Arusha Water Supply Project);
d) Mradi wa usambazaji maji wa Orkesumet;
e) Mradi wa usambazaji maji wa Sumbawanga; na
f) Mradi wa usambazaji maji wa Chalinze.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muhtasari ukaguzi huu wa kiufundi ulibaini masuala yafuatayo: -
a) Kukosekana kwa mpango kabambe wa kitaifa wa kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maji (National Water and Sanitation Master Plan). Ukaguzi ulibaini kuwa Wizara ya Maji haikuwa na mpango kabambe wa kitaifa wa kuwezesha utekelezaji wa miradi ya usambazaji maji kinyume na Kifungu Na. 5(i) cha Sheria ya usambazaji maji na usafi wa mazingira, 2019 (Water Supply and Sanitation Act, 2019). Hali hii imesababisha utekelezaji wa miradi ya maji kufanyika bila ya kuzingatia mpango wa muda mrefu na endelevu hivyo kuongeza gharama kwa Serikali na wakati mwingine kutopatikana thamani ya fedha;

b) Usanifu wa miradi ya maji usiotosheleza kufanya miradi ya maji kuwa endelevu. Kifungu cha 1.1.4, 1.1.4.3 na 1.4.2 cha Mwongozo wa usanifu wa Wizara ya Maji, 2009 kinafafanua mambo ya kuzingatia wakati wa usanifu. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa, hakuna mradi wowote kati ya miradi sita (6) ya usambazaji maji uliokidhi kikamilifu mahitaji ya usanifu kulingana na Mwongozo wa usanifu wa Wizara ya Maji ambao ungewezesha kupatikana kwa takwimu za kutosha kwa ajili ya kuandaa usanifu mzuri na hivyo kupunguza gharama za miradi;

c) Kuchelewa kukamilika kwa miradi ya maji kwa miezi mitano (5) hadi kufikia miezi 32 ambapo, miradi minne (4) kati ya sita (6) iliyokaguliwa ilichelewa kukamilika kutokana na kuchelewa kwa misamaha ya kodi, kasi ndogo ya wakandarasi na kubadilika kwa usanifu;

d) Udhibiti usiojitosheleza wa gharama za miradi. Ukaguzi ulibaini uwepo wa udhibiti usiojitosheleza wa gharama za utekelezaji wa miradi kutokana na mikataba ya kazi kutoendana na uhalisia wa eneo la ujenzi, kubadilika kwa mawanda ya kazi ili kuendana na bajeti na kubadilika kwa viwango vya kazi. Hali hii ilipelekea gharama za mradi kuongezeka kwa **Dola za Marekani 33,707,003.72**, **Euro 209,176.74** na **Shilingi 1,025,700,014.00**. Aidha kumekuwa na uchelewaji wa malipo kwa wakandarasi ambapo, mkandarasi katika mradi mpya wa usambazaji maji wa Arusha na mradi wa usambazaji maji wa Orkesument aliomba kulipwa riba kutokana na kuchelewa kwa malipo jumla ya **Shilingi 728,670,742.1** na **Dola za Marekani 284,546.91**; na

e) Usimamizi wa Wizara ya Maji usiojitosheleza wa miradi ya maji hali iliyosababisha ubora wa miradi kutoweza kufikiwa kutokana na wataalamu wa Wizara kutokuwepo katika maeneo ya miradi (site) wakati wote wa ujenzi kuhakikisha viwango vinafuatwa.

### 2.3.4 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Usimamizi wa Ujenzi wa Mradi wa Daraja la Kigongo Busisi – Mwanza

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa nyingine iliyopitiwa na kuchambuliwa na Kamati inahusu Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi katika Usimamizi wa Ujenzi wa Mradi wa Daraja la Kigongo – Busisi Mkoani Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi imebainisha kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) inatekeleza Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi lenye urefu wa kilomita 3.0 na barabara zake za mkabala zenye urefu wa kilomita 1.66 kwa pande zote mbili za daraja. Ujenzi wa

daraja hilo ni miongoni mwa vipengele muhimu vya utekelezaji wa mpango wa maendeleo nchini kwani litakua kiungo muhimu kati ya mkoa wa Mwanza na nchi jirani za Rwanda, Burundi na Uganda.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi inaendelea kubainisha kuwa daraja la Kigongo – Busisi linatambulika kama daraja refu zaidi Afrika Mashariki na la sita (6) kwa urefu barani Afrika. Daraja hilo lina urefu wa kilomita 3.0 (maili 1.9) na upana wa mita 28.45 (futi 93.3). Ni daraja la kwanza kuvuka Ghuba ya Mwanza ya Ziwa Victoria. Ujenzi wa Daraja la Kigongo hadi Busisi unaogharamiwa na Serikali ya Tanzania ulianza kutekelezwa tarehe 25 Februari, 2020 na unatarajiwa kukamilika tarehe 24 Februari, 2024.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa lengo kuu la ukaguzi huu ilikuwa ni kutathmini mchakato mzima wa ujenzi kwa kuanzia na jinsi mradi ulivyopangwa, kubuniwa na kutekelezwa na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS). Aidha, ukaguzi ulilenga kutathmini ubora wa ujenzi na ufundi na hali halisi ya mradi ili kuhakikisha kuna thamani ya fedha za umma zinazotumika kutekeleza mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Mradi wa Kigongo - Busisi umebainisha masuala ambayo Bunge linatakiwa kuyafahamu kama ifuatavyo: -

**a) Kuchelewa Kumwajiri Mhandisi Mshauri Mwelekezi wa Mradi/ Msimamizi**

Mapitio ya mkataba wa ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi na Mkataba wa huduma ya ushauri wa mradi huo yalionesha kuwa mkataba wa ujenzi kati ya mwajiri na mkandarasi ulitiwa saini tarehe 29 Julai, 2019. Vilevile, Mkataba wa Usimamizi wa kazi ya ujenzi kati ya mwajiri na mshauri

mwelekezi msimamizi ulitiwa saini tarehe 27 Disemba, 2019. Hii ilikuwa ni kuchelewa kwa kipindi cha miezi mitano (5) katika kumwajiri mshauri mwelekezi/msimamizi wa mradi. Pia, ilibainika kuwa shughuli za ujenzi zilianza bila kuwepo kwa mshauri mwelekezi. Kwa mujibu wa nyaraka za makabidhiano ya eneo la mradi, kazi za ujenzi zilianza tarehe 3 Novemba, 2019, ambapo mshauri mwelekezi alianza kazi ya usimamizi baada ya kusaini mkataba tarehe 27 Disemba, 2019. Kwa hiyo, mkandarasi alitekeleza kazi za ujenzi kwa siku 54 bila usimamizi. Hali hii ingeweza kuathiri ubora wa shughuli za ujenzi japo kwa sasa suala hili limefanyiwa kazi;

**b) Kuchelewa Malipo ya Awali ya Huduma ya Mshauri Mwelekezi**

Kifungu cha 26 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC) kinahitaji malipo ya awali ya 15% ya bei ya mkataba katika Shilingi ya Kitanzania kufanywa ndani ya siku 30 baada ya tarehe ya kuanza kutumika. Malipo ya awali yalipaswa kulipwa baada ya kuwasilisha Dhamana ya Benki inayokubalika, isiyo na masharti na isiyoweza kubatilishwa ya kiasi sawa na kitakachotolewa na mteja kwa awamu sawa dhidi ya taarifa ya miezi 10 ya kwanza ya huduma hadi malipo ya awali yamekamilika.

Ukaguzi ulibaini kuwa Dhamana ya Malipo ya Awali Nambari 0374GAD200200001 kutoka Benki ya KEB HANA ya Korea Kusini, ikiwa ni mdhamini, ilikubaliwa na mwajiri tarehe 1 Juni, 2020. Malipo ya awali yalilipwa kwa mshauri tarehe 2 Disemba, 2020, ambayo iliashiria kuchelewa kwa siku 154, (yaani zaidi ya miezi mitano). Jambo hili ni kinyume na mkataba hivyo kuweza kuisababishia Serikali gharama ya takribani **Shilingi 36,323,278.91**;

**c) Kutokuwepo kwa Wafanyakazi Muhimu wa Mshauri Mwelekezi**

Ukaguzi ulibaini kuwa, mhandisi wa Jioteknolojia hakuwahi kuwepo tangu kuanza kwa utekelezaji wa mradi hadi wakati

wa ukaguzi huu. Ukaguzi ulibaini kuwa shughuli za kijioteknolojia zilikuwa zikiendelea pasipo uwepo wa mtaalamu huyo. Jambo hili linakiuka Kifungu cha 39.1 (i) ya masharti ya jumla ya mkataba;

**d) Malipo ya Riba ya Shilingi 58,048,892 Kutokana na Kuchelewesha Malipo kwa Mshauri Mwelekezi**

Kifungu cha 57.2 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba Namba TRD/HQ/1027/2019/20 kilimtaka mwajiri kulipa hati ya malipo ya Mshauri Mwelekezi ndani ya siku thelathini (30) baada ya kupokelewa kwa hati hizo na mwajiri.

Mapitio ya hati za malipo yamebaini kuwa hati za malipo ya awali na hati za malipo kwa kazi nyingine zilizoidhinishwa Na.1, 2, 3, 4 na 5 zilichelewa kulipwa kwa siku 154, siku 138, siku 82, siku 16 na siku 86 mtawalia. Hivyo malipo haya yote yalitokana na riba kutokana na kuchelewa kwa hati. Aidha, mapitio ya nyaraka za malipo kwa mhandisi mshauri yalibaini kuwa, mwajiri alilipa riba ya **Shilingi 58,048,892.00** kwa kucheleweshwa kwa malipo. Mchanganuo wa malipo hayo ya riba umefafanuliwa katika Jedwali Na. 2.1 liafuatalo: -

**Jedwali Na. 2.1: Riba Iliyolipwa kwenye Malipo Yaliyocheleweshwa ya Mshauri Mwelekezi**

| Vocha ya Malipo | Namba ya Hati ya Malipo | Kiasi Kilicholipwa (TSH) |
|---|---|---|
| PV00037715 | 3 | 14,237,589.00 |
| PV00038104 | 4 | 27,975,601.00 |
| PV00046307 | 6 | 15,835,702.00 |
| **Jumla** | | **58,048,892.00** |

**Chanzo:** ***Taarifa ya Hesabu za Mradi wa Kigongo – Busisi***

Kuchelewa kwa malipo kwa Mshauri Mwelekezi kulichangiwa na kuchelewa kutoa fedha kwa Wakala wa Barabara Nchini na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi). Kwa mujibu wa mahojiano na Afisa Masuuli wa Wakala wa Barabara

Nchini, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi haikupeleka kwa wakati fedha za Wakala wa Barabara Nchini kwa sababu ya kuchelewa kutolewa fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango;

**e) Riba Inayotokana na Kucheleweshwa Malipo kwa Mkandarasi Kiasi cha Sh. Bilioni 1.5**

Kifungu cha 51.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba kati ya Wakala wa Barabara Nchini na Mkandarasi uliosainiwa tarehe 29 Julai, 2019 kilimtaka mwajiri kumlipa mkandarasi kiasi kilichothibitishwa na Meneja wa mradi ndani ya siku 28 tangu tarehe ya kila hati ya malipo.

Mapitio ya hati za malipo yamebaini kuwa malipo ya awali 1 na 2, na hati za malipo ya Kazi zilizothibitishwa Na.1, 2, 3, 4 na 5 zilichelewa kulipwa kwa siku 32, siku 65, siku 77, siku 102, siku 65, Siku 27 na siku 14 kwa mtiririko huo. Hivyo malipo yalikuwa ya riba kutokana na kuchelewa kwa malipo kwa mujibu wa mkataba. Aidha, mapitio ya nyaraka za malipo ya mkandarasi yalibaini kuwa mwajiri alilipa riba ya **Shilingi 1,553,097,096.80** kwa kucheleweshwa malipo kwa wakandarasi. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa kuchelewa huku pia kulitokana na kuchelewa kupata fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

### 2.3.5 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kina wa Ujenzi, Ukarabati na Uboreshaji wa Viwanja 12 vya Ndege hapa Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kwa rejea ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi huu wa kina, ilibainika kuwa, sekta ya usafiri wa anga ina mchango mkubwa katika nyanja mbalimbali za kiuchumi kitaifa na kimataifa. Kwa kulitambua hilo Serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya ujenzi, uendelezaji na ukarabati wa viwanja vya ndege nchini ili kuongeza ufanisi wa viwanja hivyo.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 3.2 ya Jedwali lililowekwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (Agizo la Uanzishwaji la mwaka 1999 GN Na. 404) limeipa TAA majukumu ya uendeshaji, usimamiaji, utunzaji na uendelezaji wa viwanja vya ndege vinayomilikiwa na Serikali. Hata hivyo, Tangazo la Serikali Na. 232 la tarehe 27 Machi, 2020 liliipa TANROADS majukumu sawa katika kufanya ununuzi, na kusimamia mikataba ya usanifu, ujenzi na ukarabati wa viwanja 12 vya ndege vilivyojengwa hali iliyoleta mkanganyiko katika utekelezaji wa miradi kati ya TAA na TANROADS.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilitumia jumla ya **Shilingi 1,020,688,321,277.40** kwenye miradi ya ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa viwanja vya ndege. Kwa msingi huo, kwa lengo la kutathmini iwapo kuna mifumo imara ya usimamizi wa miradi ya viwanja vya ndege, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali alifanya ukaguzi wa kina katika viwanja vya ndege 12 vilivyopo Tanzania bara. Mawanda ya ukaguzi huu yalianzia mwaka wa fedha 2016/17 mpaka 2020/21.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini kama ujenzi, ukarabati na uboreshaji wa viwanja hivyo unafanyika kwa ufanisi na kuzingatia muda wa kutekelezwa mradi uliotengwa, gharama sahihi na ubora ili kutimiza lengo la kuboresha sekta ya usafiri wa anga.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi uliofanywa na Kamati katika kusimamia matumizi ya fedha za umma uliangalia zaidi mapungufu yaliyopo katika usanifu, kutofanyika kwa upembuzi yakinifu, mapungufu katika uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, usimamizi wenye dosari wa mikataba, malipo ya ziada pamoja na matumizi nje ya bajeti. Pamoja na mambo mengine, masuala ambayo yamebainishwa katika ukaguzi huo ni yafuatayo: -

**a) Malipo ya Fidia Katika Mradi wa JNIA[5] Kuchelewa Kulipwa na Kuongeza Gharama za Mradi Hadi Kufikia Sh. 29,768,029,951**

Ili kupisha mradi wa upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere, ilifanyika tathmini kwa kaya zilizoathiriwa na mradi ambazo ni zile zilizokuwa katika maeneo ya Kipawa, Kigilagila na Kipunguni. Katika mchakato wa ulipaji wa fidia, kaya 1,125 zilizopo Kipunguni A na kipunguni Mashariki zilisalia pasipo kulipwa madai yao yenye thamani ya **Shilingi 7,413,357,576** kwa zaidi ya miaka 23.

Ukaguzi uliofanywa na CAG katika kipindi cha mwezi Julai, 2021 umebaini kuwa, tathmini mbalimbali zimekuwa zikifanyika ili kuhakiki na kupata thamani halisi ya deni hilo kuendana na mabadiliko ya muda na thamani ya fedha. Aidha, marudio ya tathmini ya karibuni iliyofanyika mwezi Mei 2020 ilizalisha thamani mpya ya **shilingi 29,768,029,951** sawa na ongezeko la **Shilingi 22,354,671,575** ambayo ni sawa na 302%. Suala hili lisipofanyiwa kazi mapema linaongeza hasara kwa Serikali na pia kusababisha usumbufu kwa wananchi wa maeneo husika;

**b) Malipo ya Riba Kutokana na Kuchelewa kwa Malipo kwa Wakandarasi kwa Siku 5 hadi Siku 216**

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) iliingia mkataba na Mkandarasi M/s ARINC Information Management Services Tanzania Limited kwa ajili ya huduma ya ugavi, uwekaji, upimaji, uanzishaji na ukarabati wa Mifumo ya Taarifa katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA). TAA ilichelewa kufanya malipo kwa mkandarasi huyo kwa siku 5 hadi 216 na kupelekea kuwepo kwa tozo ya riba ya kiasi cha **Shilingi 11,393,464,629**. Kuchelewa huko ambako kumeiingiza Serikali katika hasara ni

[5] Julius Nyerere International Airport.

kinyume na kifungu cha 5(b) (3) cha mkataba kati ya TAA na mkandarasi.

Vile vile, Uchambuzi uliofanywa na Kamati kutokana na ukaguzi uliofanywa na CAG umebaini kuwa, Serikali imetakiwa kulipa kiasi cha **Shilingi 2,753,388,441.79** kama tozo ya riba kutokana na kuchelewa kufanya malipo ya madai ya mkandarasi aliyepewa kazi ya ujenzi na ukarabati katika kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Hadi ukaguzi huu ulipofanyika, Serikali imekwishamlipa mkandarsi huyo kiasi cha **Shilingi 2,069,098,269.36 na** kubaki na deni la **Shilingi 684,290,172.43;**

**c) Muingiliano wa Mamlaka kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) katika Uendelezaji na Udhibiti wa Viwanja vya Ndege Vinavyomilikiwa na Serikali**

Kama ambavyo nimefafanua hapo awali, mapitio ya nyaraka za utekelezaji katika taarifa ya ukaguzi yamebainisha kukosekana kwa mipaka ya wazi ya umiliki na majukumu baina ya TAA na TANROADS katika kufanya ununuzi, na kusimamia mikataba ya usanifu, ujenzi na ukarabati wa viwanja 12 vya ndege vilivyojengwa, kumesababisha kuongezeka kwa matumizi ya rasilimali za umma na kukosekana kwa tija.

TAA ilisaini mkataba namba AE-027/2016/2017/SHY/W/31 na mkandarasi mnamo tarehe 30 Juni 2017 kwa ajili ya kazi za ukarabati na uboreshaji kiwanja cha ndege Shinyanga. Aidha, mradi huo unafadhiliwa kati ya Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB)[6]. Uchambuzi umebainisha kuwa, utekelezaji wa mradi huo haujaanza kwa muda mrefu kutokana na kubadilishwa kwa mujukumu ya usimamizi wa shughuli za

[6] European Investment Bank.

ujenzi wa viwanja vya ndege kutoka TAA kwenda TANROADS hali iliyosababisha kuhamisha majukumu ya kimkataba.

Katika hatua nyingine, ukaguzi uliofanywa katika kiwanja cha ndege cha Dodoma ulibaini matumizi ya ziada ya fedha za umma kutokana na TAA kuondoa taa zinazotumia nishati ya jua zenye thamani ya **Shilingi 236,080,632** zilizowekwa na TANROADS wakati wa upanuzi wa kiwanja hiko ili kuweka taa nyingine zinazotumia nishati ya umeme. Hali hii inatokana na uwepo wa muingiliano wa majukumu;

Muingiliano huu wa kimajukumu kati ya TAA na TANROADS umechangia pia kupunguza uwezo wa TAA kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuwa uwezo wake wa mapato umepungua. Baada ya kuondolewa jukumu la kutengeneza na kukarabati viwanja vya ndege, mapato yanayokusanywa na TRA kwa niaba ya TAA kwenye tiketi za ndege hayarudishwi TAA hivyo kuathiri shughuli za ugharimiaji ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege; na

**d) Mapungufu katika ujenzi wa Jengo la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

Taarifa ya ukaguzi imebaini kuwa mradi wa ujenzi wa jengo la abiria katika kiwanja cha ndege cha Mwanza una mapungufu makubwa na haukukidhi viwango kutokana na kutofanyika kwa upembuzi yakinifu wa kina, pamoja na kutopata kibali cha Mamlaka ya Usimamizi wa Anga Tanzania (TCAA). Aidha TAA na TANROADS ambao ndio wenye jukumu la kujenga na kufanya ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege hawakushirikishwa katika usanifu na ujenzi wa jengo hilo.

Mapitio ya mradi yaliyofanywa na wataalamu yalibaini mifumo muhimu ya uendeshaji wa jengo kutojumuishwa hivyo

kutokuwepo kwa thamani ya fedha ambazo zimekwishatumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo.

### 2.3.6 Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Kanda

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa kiufundi katika ujenzi wa hospitali za Rufaa za Mikoa na Kanda umebainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali ilitenga **Shilingi Bilioni 75.533** kwa ajili ya ujenzi wa hospitali mbili (2) za rufaa za kanda za Mtwara na Mbeya na hospitali tatu (3) za Rufaa za Mikoa ya Njombe, Katavi na Mara.

**Mheshimiwa Spika,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliamua kufanya Ukaguzi wa Kiufundi katika miradi ya ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa na Kanda ili kubaini kama zimejengwa kwa viwango vinavyotakiwa na kuangalia kama malengo ya ujenzi wa hospitali hizo yamefikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi huu ulihusisha jumla ya miradi mitano (5) ya ujenzi wa hospitali za rufaa, mitatu kati yake ni hospitali za rufaa za mikoa na miwili ni hospitali za rufaa za kanda. Miradi hii ni pamoja na:

i. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara;
ii. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi;
iii. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Njombe;
iv. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya; na
v. Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mtwara.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika ukaguzi huu umebainisha dosari kadhaa ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi na Serikali ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha za umma iliyowekezwa inafikiwa. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo: -

**a) Dosari Katika Mipango na Usanifu wa Majengo ya Hospitali za Rufaa na Kanda**

Ukaguzi ulibaini mapungufu kadhaa katika eneo la mipango na usanifu wa majengo ya hospitali za rufaa. Mapungufu hayo katika eneo hili ni pamoja na haya yafuatayo: -

i. Kutofanyika ipasavyo kwa upembuzi yakinifu katika baadhi ya majengo ya hospitali za rufaa za Mikoa ya Njombe, Mbeya na Katavi. Hii ilichangiwa zaidi na sababu kuwa ujenzi wa hospitali hizi ulipoanza mwaka 2016 ulikuwa chini ya TAMISEMI badala ya Wizara ya Afya ambayo ndio ilikuwa na uwezo zaidi wa kuwezesha upembuzi yakinifu wa kina;

ii. Kutokuwepo na mipango toshelevu ya kibajeti ya utekelezaji wa ujenzi. Mathalani ujenzi wa hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Mara ulisimama kwa muda mrefu kwa ukosefu wa fedha; na

iii. Dosari katika usanifu wa majengo kwa kuzingatia TAMISEMI walianza kutekeleza miradi hii bila kuishirikisha Wizara ya Afya ipasavyo katika suala la usanifu wa majengo. Hivyo baadhi ya majengo yalianza kujengwa bila ya kuwa na sifa stahiki za matumizi ya hospitali hivyo kukosa thamani halisi ya matumizi ya fedha za umma;

**b) Mapungufu Katika Mchakato wa Taratibu za Manunuzi;**

Taarifa ya ukaguzi imebainisha dosari kadhaa katika mchakato wa manunuzi uliofanyika mwaka 2016 katika kuanza zoezi la ujenzi wa hospitali hizo za kanda na za rufaa. Mapungufu hayo ni pamoja na kutojumuishwa kwenye Mpango wa Manunuzi wa Mwaka (APP)[7] manunuzi ya huduma za Wahandisi washauri na wakandarasi, kutokuwepo

[7] Annual Procurement Plan.

kwa dhamana za utendaji, matumizi yasiofaa ya Waraka wa Bodi ya Zabuni (circular resolution) na utuzanzaji duni wa nyaraka za zabuni;

**c) Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Vipimo Wakati wa Ujenzi wa Hospitali**

Kama ilivyobainishwa hapo awali, changamoto za usanifu zilisababisha majengo ya baadhi ya hospitali kutojengwa kwa viwango vinavyokubalika na Wizara ya Afya. Changamoto za vipimo vya majengo vilibainika katika hospitali za rufaa za mikoa ya Mara na Njombe;

**d) Dosari Katika Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mikataba**

Katika eneo hili ukaguzi ulibaini mapungufu katika mfumo wa usimamizi wa ujenzi wa hospitali za rufaa na kanda hivyo kupunguza ufanisi katika zoezi hilo. Mfano katika ujenzi wa hospitali ya rufaa ya mkoa wa Mara, mkandarasi (M/s NHC) alindaaa BoQs ya kiasi cha **Shilingi 134,500,000** lakini kwenye hati ya malipo alilipwa **Shilingi 154,500,000.** Kwa upande wa hospitali ya mkoa wa Mtwara mkandarasi alilipwa fedha za ziada **Shilingi 200,544,000** kwa kutengeza dari wakati kazi hiyo ilikuwa sehemu ya mkataba wa awali.

**2.3.7 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji**

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 19 Januari, 2023, Kamati ilikutana na Afisa Masuuli Wizara ya Kilimo na Tume ya Umwagiliaji ili kupitia, kuchambua na kufanya mahojiano kuhusu Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi Katika Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inabainisha kuwa, Sekta ya Kilimo inategemewa na takribani asilimia **80** ya Watanzania kwenye shughuli zao za maisha ya kila siku. Kilimo kinachangia **asilimia**

**26** ya pato la Taifa na kiasi cha **asimiliia 30** ya mapato ya mauzo ya nje. Pamoja na mchango huo wa Sekta ya Kilimo, Kilimo cha Tanzania bado kimekuwa cha kutegemea mvua.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya ukaguzi inaendelea kufafanua kwamba, Tanzania ina kadiriwa kuwa na jumla ya eneo linaloweza kutumika kwa maendeleo ya umwagiliaji kuwa ni **hekta milioni 29.4**. Katika jumla ya eneo hilo, ni **hekta milioni 2.3** zilizo na uwezo mkubwa wa kufanyika shughuli za umwagiliaji, na **hekta milioni 4.8** kuwa na uwezo wa kati, wakati **hekta milioni 22.3** ni eneo lenye uwezo mdogo. Hata hivyo, pamoja na uwezo huo wote, ni **hekta 461,326** tu sawa na **asilimia 1.6** ya eneo lote ambalo hadi sasa limeendelezwa chini ya kilimo cha umwagiliaji.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa ukaguzi huu ulifanyika kwa sababu kuu moja ambayo ni kuwa, baadhi ya miradi ya umwagiliaji ilikuwa inatekelezwa bila kufuata taratibu bora za usimamizi wakati wa utekelezaji wake. Kwa mfano, ujenzi wa miradi ya umwagiliaji ilikuwa haitekelezwi kulingana na muda na bajeti iliyokubaliwa hivyo kuongeza gharama kwa Serikali na kutopatikana kwa thamani ya fedha za umma zinazotumika.

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi zilizokaguliwa ni Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Wizara ya Kilimo. Miradi iliyo kaguliwa ilitekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 na miradi ambayo ilikua inaendelea kujengwa wakati wa ukaguzi. Ukaguzi huu ulihusisha miradi iliyotekelezwa katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Mwanza, Kilimanjaro, Mara, Kagera na Manyara.

**Mheshimiwa Spika,** Dosari zilizobainika kupitia ukaguzi huu ni kama ifuatavyo: -

**a) Mapungufu Katika Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake**

Ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwa na mapungufu katika uzingatiaji wa Sheria ya manunuzi na kanuni zake wakati wa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya umwagiliaji kama ifuatavyo: -

i. Kwa baadhi ya skimu za umwagiliaji, uhakiki wa usanifu haukufanyika kabla ya kuanza kwa mradi. Kazi iliyosanifiwa na Mshauri elekezi ilitekelezwa bila kupitiwa na mteja na matokeo yake, mabadiliko yasiyo ya lazima yalijitokeza wakati wa hatua za ujenzi. Hii hatimaye ilisababisha gharama za ziada ya usimamizi na kupitiliza muda wa ujenzi wa mradi. Kwa mfano, kwa mradi wa Kilangali zilipita siku za ziada 240, wakati kwa mradi wa Msolwa Ujamaa, Morogoro zilipita siku za ziada 180; na

ii. Aidha, ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa uchunguzi wa kina kuhusiana na uwezo wa mkandarasi mshauri (due diligence) katika utekelezaji wa usimamizi wa ujenzi wa miradi ya umwagiliaji ya Kilangali, Moorogoro Wilaya ya Kilosa na Msolwa Ujamaa, Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilombero. Katika maombi ya kazi ya usimamizi kwenye miradi ya Msolwa- Ujamaa na shamba la Mbegu la Kilangali, mkandarasi mshauri aliwasilisha hati za wasifu wa wafanyakazi wake kutoka kampuni ya ushauri ya M/s Edge. Majina yaliyowasilishwa yalikuwa tofauti na majina yaliyopo kwenye nyaraka mbalimbali za Serikali. Aidha uchunguzi wa kina haukufanyika ili kujiridhisha iwapo kampuni husika ilikuwa inamiliki wafanyakazi hao kinyume na Kanuni za Manunuzi ya Umma[8] inayohusina na uchunguzi wa kina wa mkandarasi kabla ya kupewa zabuni;

[8] Kanuni ya 373 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma GN Na.446/2013

**b) Mapungufu Yaliyojitokeza Wakati wa Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji**

Wakati wa utekelezaji wa shughuli za ujenzi wa miradi ya umwagiliaji kulibainika mapungufu kadhaa kama yanavyofafanuliwa hapa chini: -

i. Mikataba yote tisa (9) iliyohakikiwa haikukamilika ndani ya kipindi cha mkataba. Kulikuwa na kuchelewa kwa muda wa kukamilisha mradi ambapo muda wa kazi uliongezwa kwa vipindi kuanzia siku 80 hadi siku 450. Sababu kubwa za kuongeza muda katika miradi iliyochaguliwa zilikuwa ni uwezo dhaifu wa wakandarasi, kuchelewa malipo kwa wakandarasi, utendaji mbovu wa wakandarasi; na usimamizi dhaifu wa mshauri elekezi; na

ii. Ukaguzi ulibaini kutokuwepo kwa udhibiti wa kuridhisha wa gharama zilizotokana na kubadilika kwa mawanda ya ujenzi. Mapitio ya nyaraka mbalimbali za hati za malipo yalibainisha mapungufu kuhusu gharama kwenye miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo. Kwa mfano ilibainika kuwa, huduma za ushauri zilitakiwa kufanyika kwa gharama ambayo ni **Shilingi 835,433,858**. Hata hivyo, mapitio ya nyongeza kwa ajili ya ushauri yalionesha kiasi kilicholipwa kimeongezeka hadi kufikia **Shilingi 1,301,119,529.29**. Ongezeko hili lilikuwa sawa na asilimia 56 ya kiasi cha mkataba wa awali. Suala hili lilikuwa kinyume na Kanuni za Ununuzi wa Umma[9];

**c) Mapungufu Katika Udhibiti wa Ubora wa Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji**

Katika eneo hili uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi ulibainisha mapungufu na dosari katika matumizi ya fedha za umma. Mapungufu hayo ni kama ifuatavyo: -

i. Kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji, 2013

[9] Kwa mujibu wa Kanuni ya 114 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma, GN. Na.446/2013

kinamtaka Mkaguzi wa umwagiliaji kuhakikisha viwango vya ubora wa miradi ya umwagiliaji vinafikiwa. Licha ya takwa hilo, ukaguzi ulibaini kuwa kulikuwepo na mapungufu kwenye vipimo na mawanda ya kazi. Aidha, ilibainika kuwa utofauti huo ulioonekana ulisababishwa na mapungufu yaliyotokana na usanifu. Kwa msingi huo eneo hili lina viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma;

ii. Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa Miradi miwili ya Ngage, Mkoa wa Manyara Wilaya ya Simajero na Katela Ntaba, Mkoa wa Mbeya Wilaya ya Busokelo ilikuwa na vigawa maji pungufu ambavyo vilipungua kutokana na kupunguza mawanda ya mradi ili uweze kukamilika sawa na kiasi cha pesa kilicho pangwa. Vilevile, miradi miwili (2) ya Msolwa Ujamaa na Shamba la Mbegu la Kilangali lilikuwa na vigawa maji pungufu hali ambayo ilisababishwa na usanifu usiojitosheleza; na

iii. Ukaguzi ulibaini kuwa miradi sita kati ya saba iliyotekelezwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji pamoja na Wizara ya Kilimo haikuweza kuleta kwa wakaguzi majibu ya vipimo vya uimara wa zege;

**d) Tathmini Katika Upangaji wa Miradi ya Umwagiliaji**

Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi wa usanifu na ujenzi wa miradi ya Umwagiliaji ulibaini mapungufu katika eneo la upangaji wa miradi ya Umwagiliaji. Mapungufu hayo ni kama ifuatavyo: -

i. Kupitia mapitio ya Ripoti ya Ukaguzi wa Ununuzi iliyofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), ilibainika kuwa, miradi ya umwagiliaji ya Msolwa-Ujamaa na Mradi wa shamba la Mbegu la Kilangali iliyokuwa ikitekelezwa na Wizara ya Kilimo mnamo Septemba, 2018, utekelezaji wa miradi hiyo haikuwa imejumuishwa ndani ya Mpango wa Manunuzi wa Mwaka.

Hata hivyo, Wizara ilihuisha mpango wake wa manunuzi wa mwaka mnamo tarehe 6 Machi, 2019 ikiwa ni miezi sita kupita baada ya maradi kuanza;

ii. Ukaguzi ulibaini kuwa manunuzi ya miradi mitatu (3) ya umwagiliaji kati ya miradi saba (7) yaliyofanywa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji yalifutwa kutokana na kutokuwa na fedha za kutosha. Taratibu za manunuzi yaliyofutwa yalizihusu zabuni namba PA.137/HQ/2017-18W/05 kwa Katela- Ntaba, PA/137/HQ/2017-18/SSIDP/W/05 kwa Mbaka na PA.137/HQ/2017- 18W/8 kwa Endagaw ingawa mikataba ilikuwa tayari imesainiwa;

iii. Ukaguzi pia ulibaini kuwa, katika shamba la mbegu la Kilangali mradi uliobuniwa haukujumuisha Mfereji mama (Parental canal), pia, haukusanifu vizuri mteremko wa Mfereji mkuu (Main canal) ili uwe kwenye ngazi za juu ili kuongeza ufanisi wa umwagiliaji na pia watumiaji waliopo mkondo wa chini wapate kufikiwa na maji ya kutosha. Ilibainika kuwa, hayo yote ni matokeo ya kwamba Mshauri Elekezi alibuni mradi huo bila kutembelea eneo husika.

Aidha, kwa mradi wa Msolwa Ujamaa mfereji mkuu uliobuniwa hapo awali ulikuwa ukipita katika maeneo ya makazi na uwanja wa michezo wa mpira wa miguu. Pamoja na hayo, miradi yote ya umwagiliaji ilikuwa na mapungufu kwenye usanifu wake hivyo kupunguza thamani ya fedha ambao ndio eneo la msisitizo la Kamati ya PAC kwa niaba ya Bunge.

### 2.3.8 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Kiufundi wa Mradi wa Umeme wa Maporomoko ya Maji ya Mto Rusumo

**Mheshimiwa Spika,** Nchi za Tanzania, Burundi na Randa ziliingia makubaliano ya ubia na ya utekelezaji wa mradi wa Umeme wa maporomoko ya maji ya mto Rusumo kupitia

kampuni ya nguvu za umeme ya Rusumo (Rusumo Power Company Limited). Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia wa jumla ya **Dola za Marekani Milioni 113.33.**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 11 Julai, 2014 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 31 Desemba, 2020. Hata hivyo, tarehe ya kukamilika kwa mradi ilibadilishwa na kuwa 31 Machi, 2023. Lengo la kutekeleza mradi huo ni kuondoa matatizo ya upatikanaji wa umeme katika nchi hizo tatu.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Tanzania inasimamia mradi huo kupitia wawakilishi wake waliopo katika Bodi ya wakurugenzi (The Board of Directors) pamoja na uwepo wa wajumbe katika Kamati tendaji (Steering Committee). Aidha, ukaguzi wa ufanisi na kiufundi uliofanywa katika mradi huu ulishirikisha Wadhibiti na Wakaguzi wakuu wa fedha za Serikali wa Nchi zote tatu (3) zinazoshiriki katika utekelezaji wa mradi ili kujiridhisha iwapo utekelezaji wa mradi ulizingatia sheria, kanuni, na miongozo. Pia, kujiridhisha kama thamani ya fedha imepatikana katika matumizi yaliyofanywa kwa kipindi cha kuanzia tarehe 24 Januari 2014 hadi 30 Juni 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa mradi huu ni kujiridhisha iwapo kuna matumizi sahihi ya fedha za umma kutokana na ukweli kwamba fedha zilizotumika kutekeleza mradi huu ni za mkopo na hivyo zitakuja kurejeshwa na wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya ukaguzi ya ufanisi na kiufundi ya mradi wa umeme wa maporomoko ya mto Rusumo imebainisha masuala yafuatayo: -

**a) Kutofuatwa kwa Taratibu za Manunuzi Wakati wa Mchakato wa Kumpata Mzabuni**

Ukaguzi wa CAG umebaini mapungufu wakati wa tathmini ya zabuni inayohusiana na kazi za ujenzi na usanifu, usambazaji na uwekaji wa vifaa vya injini ya maji (CP1) kutokana na Mzabuni kampuni ya CGCOC-JWHC ambaye hakutimiza vigezo vya awali (preliminary requirements) hivyo kuondolewa kwenye hatua za awali za mchakato wa ununuzi kupewa zabuni.

Hata hivyo, Benki ya Dunia ambayo ndio inatoa Mkopo wa mradi huo iliamua kuipa zabuni kampuni hiyo kwa gharama za **Dola za Marekani 75,134,641.16** na kuiacha Kampuni ya OZALTIN – MALTAURO – GV ambayo ilikuwa imeomba zabuni hiyo kwa gharama za **Dola za Marekani 93,960,447.99** na ambayo ilikuwa ilikuwa imependekezwa hapo awali na Timu ya Tathmini.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kufanyika kwa malipo zidifu yaliyosababishwa na kutunuku zabuni kwa mzabuni ambaye hakukidhi vigezo ambapo, kulingana na taarifa ya utekelezaji ya mradi, gharama za mradi zitaongezeka kutoka **Dola za Marekani 75,134,641.16** zilizopo katika mkataba hadi kufikia **Dola za Marekani 119,608,803.30;**

**b) Upembuzi Yakinifu Kutoonesha Uhalisi wa Eneo la Utekelezaji wa Mradi**

Pamoja na mapungufu mengine yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa mradi, kutojitosheleza kwa upembuzi yakinifu na usanifu kumesababisha ongezeko la gharama kwa kiasi cha **Dola za Marekani 15,263,167.5617** (ikijumuisha **Faranga za Rwanda 347,939,297.43** na **Dola za Marekeani 14,289,631.52**, **Dola za Kanada 137,726** na **Yuro 430,112**) kutokana na kukosekana kwa taarifa ya kina ya kihandisi pamoja na kutojitosheleza kwa taarifa za utafiti wa kiutaalamu wa ufanisi wa miamba.

Mapungufu hayo kwa kiasi kikubwa yamechangia kuongeza gharama za mradi pamoja na kuchelewa kwa muda wa utekelezaji wa mradi hali inayosababisha malengo ya mradi kutofikiwa kwa wakati uliopangwa;

**c) Masharti Katika Mkataba wa Mkopo**

Uchambuzi wa Kamati umebaini uwepo wa masharti hasi katika mkopo wa ujenzi wa mradi wa Bwawa la Rusumo. Ukaguzi umebaini kuwa Tanzania imepewa mkopo kwa asilimia 100 (CREDIT NUMBER 52/BI) wenye thamani ya **Dola za Marekani 113.33**, Rwanda wamepewa Ruzuku Kwa asilimia 50 na pia kupewa mkopo kwa asilimia 50 wenye thamani ya **Dola za Marekani 56.67**. Aidha Burundi wao wamepewa ruzuku kwa asilimia 100 wenye thamani ya **Dola za Marekani 113.33**; na

**d) Mapungufu Katika Masuala ya Usimamizi wa Mikataba**

Mapitio ya taarifa za mradi zimebainisha mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa mikataba ikiwemo kuchelewa kukamilika kwa mradi kwa muda wa mwaka mmoja na miezi sita (6) kutoka muda mradi ulipoanza kutekelezwa mwezi Februari, 2017 hadi muda wa ukaguzi ulipofanyika mwezi, Septemba, 2021.

Uchambuzi wa Kamati wa taarifa iliyowasilishwa na CAG ulibaini kuwa, tangu kuanza kwa utekelezaji wa mkataba huu hadi hati ya malipo 44 (IPC 45), mwajiri alilipa kiasi cha **Faranga za Rwanda 33,290,839** na **Dola za Marekani 315,375.66** kama kiasi cha fedha kwa kazi ambazo gharama zake hazikubainishwa kwenye mkataba (provisional sum) na ambazo hazikuwa na nyaraka zozote na uthibitisho wa malipo hayo.

### 2.3.9 Uchambuzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi Katika Uendelezaji na Utangazaji wa Sekta ya Utalii Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alifanya ukaguzi wa ufanisi katika eneo la Uendelezaji na Utangazaji wa Sekta ya Utalii Nchini kwa kuzingatia kwamba, Sekta ya Utalii ina mchango mkubwa katika pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Taarifa ya Umoja wa Mataifa (2020), mapato ya fedha za kigeni ya Tanzania yaliyotokana na utalii yalifikia **Dola za Marekani Bilioni 2.557**. Kwa mwaka 2017, mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa la Tanzania ulikuwa takribani **asilimia 17.5**.

**Mheshimiwa Spika,** Ukaguzi huu ulilenga kufanya tatahmini ya iwapo rasilimali zinazotumiwa na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Wizara ya Maliasili na Utalii zinasaidia kutangaza utalii ipasavyo ili kuliongezea Taifa fedha za kigeni na manufaa mtambuka. Aidha, hicho ni kipimo muhimu cha iwapo matumizi ya fedha za umma yamefanyika kwa ufasaha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa muhtasari ukaguzi huu ulibaini masuala makuu yafauatayo: -

a) Maendeleo yasiojitosheleza ya sekta ya utalii hapa nchini. Katika eneo hili ukaguzi ulibaini kuwa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (5) ulilenga kuongeza mapato yanayotokana na watalii wa nje hadi kufikia **Dola za Marekani Bilioni 3.6**, ambayo ni sawa na shilingi za Tanzania **Trilioni 8.374** ifikapo mwaka 2021. Uchambuzi wa wakaguzi ulibaini kuwa Wizara haikufikia lengo hilo kwani hadi mwaka 2020, ni **Shilingi za Tanzania Trilioni 1.6** pekee zilipatikana, sawa na asilimia 19 tu ya lengo lililowekwa ifikapo 2021;

b) Kutofikiwa kwa lengo la idadi ya watalii wanaotembelea


hapa nchini. Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (5) ulilenga kuongeza idadi ya watalii kutoka nchi za nje hadi kufikia **1,759,750** ifikapo mwaka 2020. Vilevile, Mpango Mkakati wa Bodi ya Utalii Tanzania, ulilenga kuongeza watalii wa kimataifa kutoka **1,284,279** Mwaka 2016, hadi **3,000,000** ifikapo Juni, 2022. Hata hivyo, uchambuzi wa takwimu kutoka katika Taarifa ya Takwimu ya Wizara ya Maliasili na Utalii ya Mwaka 2020, ulionesha kuwa, hadi mwaka 2020, lengo lilikuwa halijafikiwa, kwani idadi ya juu ilikuwa ni wageni **1,527,230**;

c) Bodi ya Utalii Tanzania kutowezeshwa ipasavyo kutangaza shughuli za utalii. Wizara ya Maliasili na Utalii ilitarajiwa kutoa/kupeleka asilimia 100 ya bajeti iliyotengwa na Bodi ya Utalii Tanzania kutoka katika Tozo ya Maendeleo ya Utalii 'TDL[10]'. Hata hivyo, uchambuzi wa Wakaguzi ulibaini kuwa, kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya fedha, Wizara iliipelekea Bodi ya Utalii jumla ya **Shilingi Milioni 5,875** kati ya **Shilingi Milioni 30,600** zilizokuwa zimepangwa. Kiasi hiki ni sawa na **asilimia 19** ya bajeti yote iliyopangwa na kupitishwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) ya fedha.

Vilevile, miongoni mwa nchi zenye ushindani katika sekta ya utalii ndani ya ukanda wetu wa Afrika, Tanzania ilibainika kutengewa kiasi kidogo zaidi cha bajeti. **Kielelezo Na. 2** kinaonesha bajeti iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya utalii kwa kipindi cha miaka mitatu (3) miongoni mwa nchi shindani katika ukanda wa Afrika.

[10] Tourism Development Levy

**Kielelezo Na. 2: Bajeti ya Tanzania kwa Ajili ya Utangazaji Utalii Ukilinganisha na Nchi Shindani katika Sekta ya Utalii (Dola za Marekani)**




*Chanzo: Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya Hesabu Zilizokaguliwa za Fedha za Bodi ya Utalii ya Taifa, 2021*

**Kielelezo Na 2** kinaonesha kuwa, bajeti ya utalii kwa Tanzania kwa ajili ya kukuza na kutangaza bidhaa za utalii ni ndogo ikilinganishwa na nchi nyingine katika ukanda wetu. Hii ni licha ya kuwa Tanzania ni nchi inayoongoza kwa kuwa na vivutio vingi vyenye kuvutia watalii miongoni mwa nchi washindani katika ukanda wetu;

d) Wizara ya Maliasili na Utalii kutofuatilia ipasavyo waendeshaji wa shughuli za utalii hali inayoweza sababisha upotevu wa mapato ya Serikali. Ukaguzi ulibaini kuwa kutoka mwaka 2016/17 hadi 2020/21, Wizara ya Maliasili na Utalii ilifanya ukaguzi wa waendeshaji wa shughuli za utalii katika Mikoa nane (8) kati ya 26 nchini. Mikoa iliyokaguliwa ni pamoja na Dar es Salaam, Manyara, Iringa, Arusha, Morogoro na Pwani. Hata hivyo, Mikoa ya Mbeya na Kigoma haikufikiwa licha ya kuwa ni mikoa yenye shughuli za utalii na inayojulikana kwa kuwa na waendeshaji wengi wa shughuli za utalii na maeneo ya utalii;

e) Bodi ya Utalii Tanzania kufikia asilimia 64 tu ya lengo la Utangazaji utalii na utafutaji wa masoko ya utalii kati ya mwaka 2016-2021. Kama ilivyobainishwa hapo awali, ukaguzi ulilenga kutathmini iwapo fedha za umma zinazotumika kutangaza utalii zinafikia malengo tarajiwa. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini TTB ilifikia malengo yake kwa asilimia 64; na

f) Kufanyika kampeni chache za uelimishaji wa masuala ya utalii. Ukaguzi uliofanyika kati ya mwaka 2016/17 – 2020/21, ulibaini kuwa Bodi ya Utalii ilifanya kampeni za uelimishaji 37 kati ya 240 zilizopangwa (sawa na asilimia 15.4). Hali hii ilitokana na ukosefu wa rasilimali fedha za kuwezesha utekelezaji wa utoaji wa elimu.

### 2.4 Ufuatiliaji wa Maazimio ya Bunge Yanayotokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati Iliyowasilishwa Bungeni Februari 2022

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 14 (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali imepewa jukumu la kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo yenye maeneo mabaya ya matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Pamoja na jukumu hilo la Kikanuni, Kamati ina dhima pia ya kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge yanayotokana na taarifa mbambali za Kamati zinazokuwa zimewasilishwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge uliofanyika tarehe 01 -18 Februari, 2022, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliwasilisha taarifa yake ya mwaka Bungeni. Taarifa hiyo ilikuwa na uchambuzi na mapendekezo. Baada ya majadiliano ya kina, maazimio makuu kumi na mbili

(12) ya Bunge yenye vipengele thelathini na moja (31) yalitolewa kwenda Serikalini kwaajili ya utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 26 Januari, 2023, Kamati ilikutana na Mlipaji Mkuu wa Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kupitia, kuchambua na kujadili Taarifa ya Wizara ya Fedha na Mipango ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge Yatokanayo na Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa katika Mkutano wa Sita wa Bunge wa Februari, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya uchambuzi wa taarifa hiyo muhtasari wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge umechambuliwa katika Jedwali Na. 2.2 hapa chini: -

**Jedwali Na. 2.2: Muhtasari wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**

| Na. | Maelezo | Idadi ya Maazimio | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Maazimio yaliyotekelezwa | 4 | 13% |
| 2. | Maazimio ambayo utekelezaji unaendelea | 22 | 71% |
| 3. | Maazimio ambayo hayajatekelezwa | 4 | 13% |
| 4. | Maazimio ambayo hayakuhakikiwa | 1 | 3% |
| 5. | Jumla | 31 | |

**Chanzo:** ***Uchambuzi wa Kamati kutoka kwenye taarifa ya MOFP kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, Januari, 2023.***

**Mheshimiwa Spika,** Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 2.2 utekelezaji wa maazimio ya Bunge kutokana na Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali

iliyowasilishwa wakati wa Mkutano wa Sita wa Bunge wa tarehe 01 hadi 18 Februari, 2022, umefanyika katika hatua mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Katika vipengele vidogo 31 vya Maazimio ya Bunge, Maazimio 4 sawa na 13% yalikuwa yametekelezwa kikamilifu, Maazimio 22 sawa 71% yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji, Maazimio 4 sawa na 13% hayajatekelezwa na Azimio 1 sawa 3% halikuhakikiwa na CAG kwa kuwa nyaraka zake ziliwasilishwa kwa kuchelewa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu Maazimio ya Bunge manne (4) ambayo hayajatekelezwa hadi sasa: -

**a) Hoja Kuhusu Kuiongezea Mtaji Benki ya Biashara ya Tanzania (TCB)**
Uhakiki wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika majibu ya Wizara ya Fedha na Mipango umebainisha kuwa hadi sasa Serikali haijatoa mkakati madhubuti wa kuiongezea mtaji benki ya TCB.

**b) Hoja Kuhusu Uwepo wa Mtaji Hasi kwa Benki ya Maendeleo (TIB)**
Uhakiki uliofanyika pia umebainisha kwamba Serikali haijabainisha mkakati yakinifu wa kushughulikia suala la mtaji wa benki ya TIB Maendeleo ambayo ina mtaji hasi kinyume na masharti ya Benki Kuu.

**c) Utekelezaji wa Mapendekezo ya CAG Kuhusu Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Shamba la Miwa Mbigiri**
Uhakiki wa utekelezaji wa agizo haukuweza kufanyika kutokana na Serikali kutowasilisha viambatisho.

**d) Deni la Benki ya BADEA linalotokana na Riba kwa Mkopo wa TIB**

Katika eneo hili Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hakupata majibu ya Serikali na nyaraka hivyo anasubiri majibu hayo ili kutoa maoni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya mahojiano ya kina na Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge hasa yale ambayo yapo katika hatua za utekelezaji. Maelezo ya Serikali yalibainisha hatua kadhaa ambazo zinaendelea kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na zile zinazohitaji utungwaji wa Sheria katika maeneo kadhaa. Hata hivyo kuna baadhi ya Maazimio utekelezaji wake unahitaji uamuzi tu wa Serikali bila kuhusisha mchakato wa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba Bunge lako Tukufu litoe msisitizo ili Serikali itekeleze Maazimio ya Bunge kwa wakati. Kwa msingi huo, vipengele 22 vya Maazimio ya Bunge ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ni muhimu vikakamilika mapema iwezekanavyo. Utekelezaji wa maazimio ya Bunge ni msingi muhimu wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

**2.5 Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo Ili Kutathmini Thamani ya Fedha Iliyotumika**

**Mheshimiwa Spika,** Mapema mwezi Machi, 2022, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujiridhisha na thamani halisi ya fedha iliyotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo. Ziara zilifanyika katika Mikoa ya Singida, Manyara, Arusha, Tanga, Dar es Salaam na Morogoro. Jumla ya miradi ya maendeleo kumi na nane (18) ilitembelewa.

**Mheshimiwa Spika,** Miradi iliyotembelewa ni pamoja na mradi wa "backbone transmission investment" unaohusu

ujenzi wa Kituo cha kupoza umeme uliopo Singida, mradi wa ujenzi wa jengo la RPC Singida, mradi wa njia ya usafirishaji umeme kati ya Tanzania na Kenya, mradi wa usambazaji maji katika Mji wa Babati na vijiji vya jirani, mradi wa usambazaji maji katika jiji la Arusha, miradi kadhaa katika Chuo cha Ufundi Arusha, miradi ya TARURA Moshi na upanuzi wa Bandari ya Tanga.

**Mheshiimiwa Spika,** Miradi mingine ilikuwa ni pamoja na ukarabati wa Kituo cha kuzalisha umeme Hale, ujenzi wa barabara ya Tanga – Pangani, miradi ya maji Dar es Salaam, upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam na miradi ya ukarabati wa barabara Dar es Salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia majukumu ya msingi ya Kamati hii, Kamati imetoa taarifa ya miradi iliyokaguliwa ambayo iligundulika kuwa na changamoto na dosari za kiutekelezaji hivyo kuwa na atahari katika matumizi ya fedha za umma. Maelezo ya miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

**a) Mradi wa “Backbone Transmission Investment” Awamu ya Pili (Substation ya Singida)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kukagua mradi huu unaotekelezwa na TANESCO katika mkoa wa Singida. Mradi huu unahusisha upanuzi wa kuviongezea uwezo vituo vya kupozea umeme vilivyopo katika miji ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga kutoka msongo wa kilovoti 220 kwenda msongo wa kilovoti 400. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka kwa wahisani wa maendeleo ya sekta ya nishati kwa jumla ya kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 120**.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mradi huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili (2) ambapo, sehemu ya kwanza ya mradi haijaanza kutekelezwa kutokana na benki ya uwekezaji ya ulaya kusitisha mkataba wa kufadhili sehemu hii ya mradi kutokana na changamoto mbalimbali. Sehemu ya pili ya

mradi huu ilianza kutekelezwa mnamo mwezi Machi, 2018 hadi Januari, 2020. Aidha, kulikuwa na nyongeza ya muda na mradi ulikamilika Mwezi Juni, 2021.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto zilizobainika wakati wa utekelezaji wa mradi ni pamoja mabadiliko ya Sheria za kodi kwa miradi ambayo imekwishaanza kutekelezwa, mabadiliko ya viwango vya malipo kwa TANROADS kwa kuzidisha uzito wa mizigo, kuchelewa kwa malipo kwa mkandarasi kwa miradi inayopokea malipo moja kwa moja kutoka kwa mfadhili na kushindwa kukamilika kwa wakati kwa vituo vya Iringa na Shinyanga. Hivyo thamani halisi ya fedha ya mradi huu haijafikiwa.

**b) Mradi wa Njia ya Usafirishaji Umeme kati ya Tanzania na Kenya "Interconnection investment project" Sehemu ya Singida, Manyara na Arusha**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu wa kuunganisha njia ya umeme kati ya Tanzania na Kenya una umuhimu mkubwa katika kuwezesha kuunganishwa kwa ukanda wa Kaskazini (EAPP) na kusini (SAPP) ili kuimarisha uwezo wa usambazaji wa umeme katika nchi zote mbili (2) na eneo la Afrika Mashariki kwa ujumla. Kamati imefanya ukaguzi wa mradi unaotekelezwa na TANESCO katika mkoa wa Manyara.

**Mheshimiwa Spika,** Fedha za utekelezaji wa mradi huu zimetokana na washirika wa maendeleo ya nishati na jumla ya gharama za mradi ni **Dola za Marekani Milioni 258.82** ambapo utekelezaji wa mradi kwa upande wa Tanzania umegawanyika katika sehemu kuu sita (6) na mradi ulitarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto zilizobainika katika mradi huo ni kuchelewa kwa zoezi la ulipwaji fidia kwa watu waliopitiwa na mradi, kuchelewa kwa tangazo la Serikali la

msamaha wa kodi kwa vifaa vya mradi hivyo kuongeza gharama za mradi, kucheleweshwa kwa malipo ya hati za madai za wakandarasi kupitia mfumo wa malipo (D-Fund system) na mabadiliko ya Sheria ya Kodi.

**c) Mradi wa Kuboresha Huduma ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Jijini Arusha na Baadhi ya Maeneo ya Wilaya ya Arumeru**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Jiji la Arusha (AUWASA) inatekeleza mradi mkubwa unaofadhiliwa na mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na mchango kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa gharama za jumla ya **Shilingi Bilioni 520 (233.9Mil USD)** ili kuongeza uzalishaji wa maji kutoka wastani wa lita 40,000,000 kwa siku hadi kufikia lita 200,000,000 kwa siku.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa mradi ulianza rasmi tarehe 18 Februari, 2016 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 30 Juni, 2022 na baade kusogezwa mbele hadi tarehe 30 Juni, 2023. Hadi kufanyika kwa ukaguzi wa mradi huu, kwa ujumla mradi umekamilika kwa asilimia 82 na kiasi kilicholipwa ni **Shilingi 26,367,433,124.43** na **Dola za Marekani 144,370,717.33** ambazo ni asilimia 67 ya jumla ya gharama yote ya mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika utekelezaji wa mradi huu, changamoto kadhaa zilibainika ikiwa ni pamoja na kuchelewa kupata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa wakandarasi kipindi cha kuanza mradi, ugumu wakati wa kuomba kuongezewa muda wa msamaha wa kodi na kutokuwepo kwa maeneo yaliyotengwa na mipango miji kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya huduma za majisafi na majitaka.

**d) Miradi ya Ujenzi wa Barabara Zinazohudumiwa na TARURA Mkoani Kilimanjaro**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania Mkoa wa Kilimanjaro unatekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na matengenezo ya barabara ili kuhakikisha barabara zote zinapitika wakati wote. Katika kipindi cha mwezi Machi, 2022, Kamati ilifanya ukaguzi katika miradi miwili inayotekelezwa na TARURA katika mkoa wa Kilimanjaro kama ifuatavyo; -

i. Mradi wa ujenzi wa Barabara ya TTCL-RC Church (0.15 km) pamoja na barabara ya Mt. Dorcas – Relini kwa kiwango cha lami ya tabaka mbili (0.34 km) pamoja na uzibaji wa viraka na kuongeza tabaka la lami katika barabara ya stendi ya basi Hai-Kingereka (0.10 km). Mradi huu wenye thamani ya **Shilingi 310,993,000** kwa ufadhili wa Mfuko wa barabara kupitia TARURA ulianza kutekelezwa tarehe 6 Disemba, 2021 na kukamilika tarehe 28 Mei, 2022. Hatua ya mradi hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2022 ilikuwa ni asilimia 90. Aidha changamoto ya mradi huu ni mitaro ya maji ya mvua katika barabara ya TTCL-RC Church kutokuwa na mwendelezo hivyo kuwa na hatari ya kuleta uharibifu katika barabara hiyo kwa upande wa mbele wa kuingilia Kanisa Katoliki;

ii. Mradi wa ujenzi wa barabara ya Soweto - Makaburini 1, Soweto – Makaburini 2 na barabara ya daladala (Hiace Road) kwa kiwango cha lami ngumu. Mradi huu umetekelezwa kwa ufadhili wa Mfuko wa Jimbo kupitia TAMISEMI na TARURA kwa thamani ya **Shilingi 490,489,000**. Ukaguzi ulibaini kukosekana kwa udhibiti wa magari na vyombo vingine vya moto wakati wa ujenzi na kupelekea uharibifu wa bainda iliyoandaliwa kupokea lami ngumu na kuishikiza pamoja na matabaka ya chini.

**e) Mradi wa Ukarabati wa Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Hale Tanga**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) inamiliki kituo cha kuzalisha umeme cha Hale kilichopo Tanga ambacho kina uwezo wa kuzalisha megawati 21. Tangu kuanzishwa kwa kituo hiko mwaka 1964, hitilafu mbalimbali zilitokea hali iliyosababisha kituo hicho kusimamisha uzalishaji mwaka 2004. Tarehe 11 Julai, 2013, Serikali iliingia makubaliano na Serikali ya Sweden kupita Shirika lake la misaada SIDA kwa ajili ya kufadhili matengenezo ya mitambo miwili (2) ya kufua umeme iliyopo katika kituo hicho ili kuongeza uzalishaji umeme.

**Mheshimiwa Spika,** kipindi cha utekelezaji wa mradi huo ulitakiwa kuwa ni wa miaka mitano kutoka mwezi Julai, 2013 hadi kufikia mwezi Machi, 2018 ambapo jumla ya **Kroner za Sweden Milioni 200** zilitakiwa kutolewa huku asilimia 60 sawa na **Kroner za Sweden Milioni 121** zitakuwa msaada na **Kroner za Sweden Milioni 79** zitakuwa na mkopo. Aidha, mabadiliko katika utekelezaji wa mradi ulisababisha kuongezwa kwa muda wa kukamilika kwa mradi hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati uliotokana na taarifa ya ukaguzi wa CAG katika mradi wa ukarabati wa kituo cha kuzalisha umeme cha Hale Tanga umebainisha changamoto mbalimbali zilizosababisha kuchelewa kukamilika kwa mradi huo kama ifuatavyo: -

i. Kuchelewa kupatikana na mkandarasi ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2022 mchakato huo ulikuwa haujakamilika na idhini ya kuendelea kusaini mkataba na mkandarasi ili kazi ya ukarabati iweze kuanza kutoka kwa mfadhili ilikuwa haijapatikana;

ii. Ongezeko la muda wa mkataba wa mkopo mara kwa mara kutokana na kuchelewa kupatikana kwa mkandarasi wa kutekeleza mradi;
iii. Ucheleweshwaji wa malipo ya Mhandisi mshauri mwelekezi (consultant) hali inayoweza kupelekea ongezeko la gharama za mradi;
iv. Kuchelewa kupata idhini ya kuendelea kwa mradi kutoka kwa mfadhili (No objection); na
v. Hasara kwenye kubadilisha fedha za kigeni (foreign exchange loss) zinazopokelewa na Serikali kutoka kwa mfadhili ya jumla ya **Kroner za Sweden 2,880,000** ambazo ni sawa na **Shilingi 772,156,800.** Hasara hii inatokana na utaratibu unaotumika ambapo, Serikali inapokea fedha kutoka kwa mfadhili zikiwa kwenye Kroner za Sweden, lakini fedha hizo zinapopelekwa TANESCO kwa ajili ya malipo kwa mhandisi mshauri zinatumwa katika fedha za Kitanzania wakati malipo kwa mhandisi mshauri yanafanyika kwa pesa za kigeni (Kroner za Sweden).

**f) Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Tanga Unaotekelezwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA)**

Bandari ya Tanga ilikuwa inafanya kazi umbali wa kilomita 1.7 kutoka gatini mpaka meli inapotia nanga hali hii inaongeza gharama za uendeshaji kutokana na mzigo mmoja kuhudumiwa mara mbili (double handling) pamoja na uhaba wa mitambo na vifaa vya kuhudumia meli na shehena. Ili kuboresha utendaji wa Bandari ya Tanga, TPA ilianza utekelezaji wa miradi mikubwa. Ufafanuzi wa utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

**i. Awamu ya Kwanza ya Mradi (phase 1)**

Katika awamu hii, TPA ilitekeleza mradi wa kuongeza upana wa lango la kuingilia na kugeuzia meli, kuongeza kina cha maji, ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuhudumia meli na shehena na ufanyaji wa upembuzi yakinifu wa mazingira

wenye thamani ya jumla ya **Shilingi Bilioni 172.36** ambapo **Shilingi Bilioni 111.4** zililipwa kwa Mkandarasi. Mradi huu ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 12 kuanzia tarehe 01 Oktoba, 2019. Hata hivyo, muda wa utekelezaji wa mradi umeongezeka hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2022 kutokana na kuchelewa kwa ununuzi wa mitambo 16 yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 27.39**.

**ii. Awamu ya Pili ya Mradi (phase 2)**

Awamu hii ilihusisha ujenzi wa gati mbili zenye urefu wa mita 450 wenye gharama za **Shilingi Bilioni 256.8** kwa fedha za ndani. Utekelezaji wa mradi ulitakiwa kuanza rasmi tarehe 16 Disemba, 2020 na kutarajiwa kukamilika ndani ya miezi 22 hadi tarehe 15 Oktoba, 2022. Hadi kufanyika kwa ukaguzi huu, utekelezaji wa mradi ulifanyika kwa asilimia 23 na jumla ya **Shilingi Bilioni 60.4** zilikuwa zimelipwa.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto za jumla zilizobainika katika utekelezaji wa miradi hiyo ni miradi kutokamilika kwa wakati kinyume na makubaliano ya mkataba hali ambayo inaashiria uwezekano wa kuongezeka kwa gharama za mradi. Pamoja na hilo, ukaguzi maalumu wa CAG ulibaini ubadhirifu katika utekelezaji wa miradi hiyo na Bunge lilishatoa azimio lake kwenye suala hilo.

**g) Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Tanga – Pangani (KM 50) kwa kiwango cha lami**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unaotekelezwa na Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS) ni sehemu ya utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Saadani – Pangani – Tanga (Km 256) pamoja na daraja la mto Pangani. Mkataba kati ya TANROADS na Kampuni ya M/s China Henan International Coorperation Group Co. Ltd (CHICO) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu ulitiwa saini tarehe 31 Julai, 2019 ambapo gharama za mradi ni **shilingi 66,853,268,467.70** na ujenzi ulipangwa kuanza tarehe 15 Novemba, 2019 na

kukamilika tarehe 14 Novemba, 2021. Hata hivyo, muda wa utekelezaji wa mradi uliongezwa hadi kufikia tarehe 05 Disemba, 2022.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi muda wa ziara ya Kamati, sehemu kubwa ya ujenzi ilikuwa katika hatua ya C1 (tabaka la mchanga uliochanganywa na simenti) na sehemu nyingine ya ujenzi upo katika tabaka mbalimbali la barabara na eneo la ujenzi la Kilomita 10 bado ujenzi haujaanza.

Katika ufuatiliaji wa maendeleo ya mradi huu, changamoto kadhaa zilibainika ikiwa ni pamoja na mkandarasi kuchelewa kupata malipo ya awali (advance payment), kuchelewa kutoka kwa toleo la Serikali la msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT), kuchelewa kulipa fidia kwa wananchi waliofuatwa na barabara ili kupisha mradi, kuchelewa kuhamisha miundombinu ya umeme, maji, simu na mkongo wa Taifa na kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi.

**h) Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia TPA inafanya maboresho makubwa ya bandari ya Dar es Salaam kupitia mradi wa Dar es Salaam Maritime Gateway Project (DMGP) ikiwa ni fedha za ufadhili wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kimataifa (IDA) na Serikali ya Tanzania kwa gharama ya kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 421**.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi uligawanyika katika vipengele viwili ambapo, kipengele cha kwanza kilihusisha uboreshaji wa miundombinu ya bandari kwa makisio ya gharama za **Dola za Marekani Milioni 400**.

**Mheshimiwa Spika,** mapungufu yaliyobainika katika ukaguzi wa miradi hii ni pamoja na kuchelewa katika utekelezaji wa kipengele cha mradi kihusianacho na uboreshaji wa

maunganisho ya reli na bandari, kuchelewa kwa malipo wa mkandarasi mshauri kutokana na utumiaji wa mfumo wa D-fund, kuchelewa kuboresha mfumo wa umeme kwenye gati, changamoto katika uendeshaji wa Gati 5-7 na viashiria vya mradi kutokamilika kwa wakati uliokusudiwa.

## 2.6 Mafunzo na Semina za Kuwajengea Uwezo Wajumbe

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kukushukuru wewe binafsi kwa kutoa idhini kwa Kamati ya PAC kupatiwa mafunzo na semina mbalimbali kwa ajili ya kuongeza uelewa, ufanisi na uwezo wa wajumbe katika kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma. Aidha, napenda kuishukuru Ofisi ya Katibu wa Bunge kwa kufanya uratibu na kuwezesha kufanyika kwa shughuli hizo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2022 hadi mwezi Februari, 2023, Kamati ilipata jumla ya mafunzo na semina kumi na Mmoja (11). Mafunzo na Semina hizo yalitolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na Asasi za Kiraia zinazoangalia matumizi ya fedha za umma. Mafunzo na Semina hizo ziliweka msisitizo katika maeneo yafuatayo; -

i. Uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;
ii. Uelewa kuhusu hati mbalimbali za ukaguzi zinazotolewa na CAG;
iii. Uelewa kuhusu kaguzi mbalimbali zinazofanywa na CAG;
iv. Uelewa kuhusu uwazi na uwajibikaji katika kusimamia matumizi ya fedha za umma;
v. Uelewa kuhusu wajibu wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani katika kuimarisha uwajibikaji, usimamizi wa fedha na utawala bora; na
vi. Uelewa kuhusu shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Taasisi na Mashirika ya Umma.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 3.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati yamezingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni ya jumla kwamba, katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo, Serikali imekuwa ikipata hasara kubwa kutokana na malipo ya riba kwa wakandarasi na washauri wa miradi kutokana na kucheleweshwa malipo ya kimikataba. Aidha, kuna changamoto kubwa katika suala la ufuatiliaji na tathmini wa miradi inayotekelezwa kupitia fedha za mikopo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Kamati ina maoni kuwa kumekuwa na kuchelewa kuunganisha Mifuko hiyo kwa muda mrefu licha ya baadhi ya mifuko kutokuwa na ufanisi. Kwa upande wa miradi ya maji, Kamati ina maoni kuwa fedha nyingi zinatumika kutekeleza miradi midogo midogo ya maji ambayo inakuwa haina matokeo makubwa badala ya kutekeleza miradi mikubwa yenye matokeo makubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hilo, Kamati ina maoni kwamba Taasisi za Serikali zinachelewa kutekeleza kwa wakati mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hivyo kuathiri mfumo mzima wa uwajibikaji wa matumizi ya fedha za umma hasa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati yamelenga katika kuboresha hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kaguzi za kiufundi, kaguzi za kina na kaguzi za ufanisi. Aidha, mapendekezo yamelenga kuboresha mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali. Mapendekezo ya Kamati ni kama ifuatavyo: -

#### 3.3.1 Ukaguzi wa Ufanisi Kwenye Usimamizi wa Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kuna jumla ya mifuko 52 ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na ambayo uendeshaji wake una mapungufu kutokana na uwepo wa mikopo chechefu na kunufaisha baadhi ya watu wasiostahiki;

**NA KWA KUWA,** Usimamizi wenye dosari wa mifuko hiyo unasababisha matumizi mabaya ya fedha za umma na hivyo kuathiri malengo ya uanzishwaji wake ikiwa ni pamoja na uwepo wa mikopo chechefu, mathalani kwa mifuko mitatu (3) mikopo chechefu ilikuwa takribani **Shilingi Bilioni 50.04**;

**KWA HIYO BASI,** Ili kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inavyostahili, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali ifanye tathmini ya kina na mapitio ya mifuko yote 52 ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuangalia iwapo kuna sababu za msingi za kuendelea kuwa na mifuko hiyo yote kwa kuzingatia malengo ya uanzishwaji wa kila mfuko. Tathmini hii ikamilike kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha;
b) Katika kipindi cha mpito, Serikali iimarishe udhibiti na usimamizi wa mifuko husika ili kuhakikisha utoaji wa fedha kwenye mifuko hiyo unafanyika baada ya uthibitisho wa mahitaji yote muhimu ya dhamana na nyaraka. Aidha, fedha zinazotolewa zitumike kwa madhumuni yaliyokusudiwa na urejeshaji wa mikopo ufanyike kwa wakati; na
c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi wa kina (comprehensive audit) wa mifuko yote 52 ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kubainisha mapungufu yaliyopo katika mifuko hiyo. Baada ya Taarifa ya Ukaguzi huo, Serikali ichukue hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya ukaguzi.

### 3.3.2 Riba Zinazotokana na Kuchelewesha Malipo ya Wakandarasi na Washauri wa Miradi Pamoja na Kuchelewa Kutoa Misamaha Stahiki wa Kodi ya VAT

**KWA KUWA,** Katika kaguzi nane (8) za kiufundi, kaguzi za kina na kaguzi za ufanisi changamoto ya riba inayotozwa kwa Serikali na wakandarasi kwenye miradi mbalimbali imekuwa ndio inayoongoza kuathiri utekelezaji wa miradi kwa wakati. Riba hii inatokana na kuchelewesha malipo halali kwa mujibu wa mikataba pamoja na uchkuchelewa kusiko kwa lazima kutoa *"Government Notes"* zinazohusu misamaha stahiki ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa vifaa vya ujenzi toka nje pale inapotakiwa kwa Mujibu wa Sheria;

**NA KWA KUWA,** Riba inayotozwa inaongeza gharama za miradi na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali kwani

inapunguza rasilimali ambazo zingeweza kutumika maeneo mengine na kuleta tija;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali iwe na mfumo wa wazi, thabiti, uhakika na wa haraka wa kuhakiki, kutambua na kulipa malipo ya wakandarasi kwa wakati kwa kuzingatia masharti ya mikataba ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha za umma; na
b) Serikali ipunguze mlolongo wa utoaji wa msamaha stahiki wa kodi ya VAT kwa vifaa vya miradi ya ujenzi toka nje vilivyokidhi matakwa ya kisheria. Aidha, hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati kwa Maafisa wa Serikali wanaochelewesha suala hili kwa uzembe na kutowajibika ipasavyo hivyo kusababisha Serikali kuingia gharama za ziada katika miradi.

### 3.3.3 Mapungufu Katika Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo Inayofadhiliwa Kupitia Fedha za Mikopo

**KWA KUWA,** Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi katika Miradi inayofadhiliwa kwa Fedha za Mikopo imebainisha dosari katika maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na maeneo ya upangaji wa miradi, usimamizi na tathmini na ufuatiliaji;

**NA KWA KUWA,** Dosari hizo zimesababisha ongezeko la gharama za miradi, kutokamilika kwa wakati kwa miradi, usumbufu mkubwa kwa wananchi kwa kuchelewa kulipwa fidia na ongezeko la tozo za riba kwa Serikali kwa kukiuka masharti ya mikopo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali iboreshe eneo la uibuaji, usanifu na usimamizi wa miradi ya ujenzi inayotekelezwa kwa ufadhili wa mikopo kwa kuhakikisha mapitio ya awali ya miradi yanakuwa

toshelevu na uchambuzi wa kina unakuwa umefanyika; na

b) Serikali iboreshe zoezi zima la uratibu baina ya Wizara ya Fedha na Mipango na Watekelezaji wa Miradi katika Sekta na wadau wengine. Hii ifanyike sambamba na uboreshaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini katika miradi inayofadhiliwa kwa mikopo.

**3.3.4 Hasara Zinazotokana na Muingiliano wa Kimajukumu Kati ya TAA na TANROADS**

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG kuhusu Ukaguzi wa Kina wa Uboreshaji, Ukarabati na Ujenzi wa Viwanja vya Ndege 12 hapa Nchini umebainisha changamoto ya muingiliano wa majukumu kwa Taasisi mbili za Serikali ambazo ni TANROADS na TAA;

**NA KWA KUWA,** Muingiliano huo umeisababishia Serikali hasara ikiwa ni pamoja na TAA kuondoa taa za mwanga wa jua zilizofungwa na TANROADS katika uwanja wa ndege Dodoma za thamani ya **Shilingi 236,080,632** ili kufunga taa mpya za umeme kwa kuwa zile za mwanga wa jua hazijakidhi mahitaji. Aidha, athari nyingine ni pamoja na kuchelewa kutekelezwa kwa mradi wa uwanja wa ndege Shinyanga kwa sababu mfadhili wa mradi huo, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) alikuwa ameingia mkataba na TAA tarehe 30 Juni, 2017 ila baadaye akataka kujitoa baada ya jukumu la kujenga uwanja kuhamishiwa TANROADS;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Serikali irejeshe kikamilifu jukumu la ujenzi, ukarabati na usimamizi wa viwanja vyote vya ndege hapa nchini kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) kabla ya mwaka huu wa fedha kukamilika ili kuokoa fedha za umma zinazopotea kwa muingiliano uliopo wa taasisi mbalimbali za Serikali (TAA, KADCO na TANROADS).

### 3.3.5 Kutoanza Ukarabati wa Kituo cha Umeme cha Hale Tangu kusainiwa Mkataba wa Mkopo Tarehe 11 Julai, 2013 Hivyo Kusababisha Hasara ya Shilingi 772,156,800

**KWA KUWA,** Taarifa ya ukaguzi wa Kituo cha kuzalisha umeme Hale pamoja na ziara ya Kamati vimebainisha kuwa tarehe 11 Julai, 2013 mkataba wa ukarabati wa kituo hicho uliingiwa ila hadi sasa haujaanza kutekelezwa;

**NA KWA KUWA,** Kutoanza kwa utekelezaji wa kituo hicho kumesababisha hasara kwa Serikali kwa kuchelewa kupatikana kwa mkandarasi, ongezeko la muda wa mkopo mara kwa mara, kuchelewa kwa malipo kwa mhandisi mshauri na hasara ya **Kroner 2,880,000** sawa na **Shilingi 772,156,800** kutokana na ubadilishaji wa fedha za kigeni (exchange loss);

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze mradi huo mapema iwezekanavyo kabla ya kufikia ukomo wa mkataba wa fedha za mkopo na msaada ili kuokoa fedha za umma.

### 3.3.6 Mapungufu Katika Usimamizi wa Mikataba na Ongezeko la Gharama za Miradi

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG kuhusu utekelezaji wa miradi mbali mbali, uchambuzi wa kamati pamoja ziara za ukaguzi wa miradi zilizofanywa na Kamati zimebaini uwepo wa usimamizi mbovu wa mikataba, pamoja na kutofanyika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo;

**NA KWA KUWA,** Kukosekana kwa usimamizi wa mikataba pamoja na mapungufu katika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa kiasi kikubwa kumesababisha miradi mingi kutokuwa na thamani ya fedha iliyotarajiwa, kutokamilika

kwa wakati uliopangwa, miradi kutekelezwa chini ya kiwango na ongezeko la gharama za utekelezaji wa miradi hiyo;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; -

a) Serikali ihakikishe upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unafanyika ipasavyo kabla ya utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo; na
b) Serikali iwe na utaratibu wa kuchukua hatua stahiki na kwa wakati kwa watendaji wote na wasimamizi wa miradi iliyobainika kuwa na dosari kutokana na kutokuwa na matumizi bora ya fedha za umma pamoja na kutowasimamia wakandarasi ipasavyo.

### 3.3.7 Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Kaguzi za Kiufundi, Kaguzi za Kina na Kaguzi za Ufanisi

**KWA KUWA,** Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekamilisha kaguzi tisa (9) za kiufundi, kiufanisi na ukaguzi wa kina katika Sekta muhimu ambapo amebainisha mapungufu kadhaa ya kufanyia kazi. Mapungufu hayo ni pamoja na kuchelewa kukamilika miradi kwa wakati, dosari katika ujenzi wa miradi na riba inayotokana na kuchelewa kulipa malipo ya wakandarasi kwa wakati;

**NA KWA KUWA,** Dosari zilizobainishwa zimepelekea Serikali kupata hasara kwa baadhi ya miradi, kuongezeka kwa gharama za baadhi ya miradi, kutopatikana kwa thamani ya fedha kwa baadhi ya miradi hali inayoweza pelekea matumizi yasiofaa ya fedha za umma;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali itekeleze ushauri na mapendekezo yote katika taarifa hizo tisa (9) kwa ukamilifu. Aidha, katika kipindi cha kila robo mwaka, Sekta husika zilizokaguliwa ziwasilishe kwa CAG taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ambapo itafanyiwa

uhakiki na kisha kuwasilishwa Bungeni kupitia kwa Kamati kwa ajili ya ufuatiliaji, tathmini na muendelezo.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini hivyo kuliongoza Bunge letu kwa umakini na weledi mkubwa. Siku zote uongozi wako umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti kwa Kamati kila mara.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa ufanisi na weledi mkubwa. Tumefanya kazi wote kwa nusu ya uhai wa kwanza wa Bunge letu la kumi na mbili (12) kwa ushirikiano mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Japheti Ngailonga Hasunga, Mb – **M/ Mwenyekiti**
3. Mhe. Dr. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mb
4. Mhe. Eng. Isack Aloyce Kamwele, Mb
5. Mhe. Simon Songe Lusengekile, Mb
6. Mhe. Anton Albert Mwantona, Mb
7. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
8. Mhe. Juma Othman Hija, Mb
9. Mhe. Idarus Faina Ravia, Mb
10. Mhe. Deus Clement Sangu, Mb
11. Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb
12. Mhe. Aida Joseph Khenani, Mb
13. Mhe. Aysharose Ndogoli Matembe, Mb
14. Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
15. Mhe. Aleksia Asia Kamguna, Mb
16. Mhe. Jakcline Kainja Andrea, Mb

17. Mhe. Daudi Protas Venant, Mb
18. Mhe. Zubeida Khamis Shaibu, Mb
19. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb
20. Mhe. Bakar Hamad Bakar, Mb
21. Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb
22. Mhe. Emmanuel Lekishon Shangai, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa ushauri wake kwa Kamati. Natoa shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati kupitia kwa Mkurugenzi wa Idara Ndugu Athuman Hussein, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, *ndc*, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Sostenes Maseke, Ndugu Amina Salumu Namtema na Ndugu Joseph Munishi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) na kwa namna ya kipekee kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ndugu Charles Kichere na Maafisa wake wote. Aidha naishukuru Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen), Msajili wa Hazina (TR) na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali (DGAM) na Maafisa wao wote kwa ushirikiano waliotoa katika kuratibu shughuli za Kamati.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**HESABU ZA SERIKALI (PAC)**
07 Februari, 2023

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa namuita Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kwa mwaka 2022 katika kushughulikia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa kuu iliyowekwa mezani, ningependa kuwaelekeza Waheshimiwa Wabunge Kipengele Namba 1.2 ukurasa wa kwanza kinahusu muundo wa taarifa. Kipengele namba 1.3 ukurasa wa pili kinahusu msingi wa shughuli za Kamati na kipengele namba 1.4 ukurasa wa tatu kinahusu nyaraka zilizotumika. Kipengele namba 1.5 ukurasa wa nne kinahusu mbinu na utekelezaji wa kazi, wakati kipengele nambari 1.6 ukurasa wa nne kinahusu changamoto tulizokabiliananazo, hususan ufinyu wa muda. B

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu bajeti na hoja ya ukaguzi kukaa muda mrefu tangu hesabu za Serikali zilipofungwa ni kwa mughtasari tu, naomba taarifa nzima ya kamati inukuliwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge, kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati, mwaka 2022 katika sehemu ya pili; shughuli kubwa iliyotekelezwa na kamati kwa mwaka huo ilikuwa ni

kuchambua taarifa ya CAG ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 na kuwahoji baadhi ya maafisa masuuli waliohusika na hoja hizo. Taarifa ya CAG ndiyo inayounda msingi wa majukumu ya Kamati kila mwaka, kwa mujibu wa Kauni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa taarifa ya CAG ulionesha kuwa kuna hoja za ukaguzi za aina mbili; yaani hoja ya ukaguzi wa kawaida wa kila mwaka na hoja za ukaguzi maalum *(Special Audit Quarries)*.

Mheshimiwa Naibu Spika,Kuhusiana na hoja za ukaguzi wa kawaida Kamati iliandaa maoni na mapendekezo 11 yaliyowasilishwa Bungeni tarehe 4 Novemba, 2022. Mapendekezo hayo yalijielekeza katika maeneo yaliyobainishwa katika kipengele namba 2.22 cha taarifa ya Kamati ukurasa wa nane.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kukumbusha kwamba, Bunge bado halijapatiwa majibu ya Serikali kuhusiana na hoja zilizowasilishwa tarehe 4 Novemba, 2022. *LAAC* itapenda kupata majibu ya hoja hizi mapema kabla ya taarifa ya CAG ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 haijawasilishwa Bungeni ili iweze kutathmini mwelekeo wa kazi zake na kujipanga ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia mwezi Novemba, 2022 hadi Februari, 2023 Kamati imechambua hoja za ukaguzi maalum na kuandaa mapendekezo sita ambayo yatawasilishwa hapa Bungeni leo tarehe 7 Februari, 2023 katika sehemu ya tatu ya taarifa ya Kamati katika ukurasa wa 22 hadi 29 wa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya CAG na mahojiano na maafisa masuuli kuhusiana na hoja za ukaguzi maalum kwa Manispaa za Ubungo,

Kigamboni, Ilemela na Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa yanaonesha kwamba bado kuna changamoto katika nidhamu ya ukusanyaji na utumiaji wa mapato ya Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, uvujaji wa mapato katika mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato. Kimsingi kuna uvujaji mkubwa wa mapato ya Serikali katika mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato wa *Local Government Revenue Collection Information System (LGRCIS)* endapo mfumo huo utakuwa bado unaendelea kutumika katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Uvujaji huu unasababishwa na baadhi ya watumishi wa Serikali wasio waaminifu wanaohusika moja kwa moja na uingizaji wa miamala katika mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushahidi uliopo una uhusiano wa mfumo uliokuwepo awali *(LGRCIS)* ambao kwa sasa ni tausi. Kamati ina maoni kwamba, kinachofanyika ni wizi kwa sababu ya mazingira ambamo mrekebishaji au marekebisho ya miamala hufanyika. Kuna maeneo ambamo miamala hufutwa kabisa au baadhi ya tarakimu kurekebishwa bila idhini ya maafisa masuuli au bila kuwepo kwa nyaraka za uthibitisho wa uhalali wa marekebisho hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mifano michache ya kusindikiza hoja hii kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo pamefanyika vitendo kadhaa vyenye kutia shaka katika mfumo wa kukusanyia mapato. Kwa mfano: -

i. Taarifa ya wadaiwa katika mfumo iliyofanyiwa ghiliba kiasi cha kushindwa kuonesha mapato halisi ya

Halmashauri kwa kuingiza kiasi cha shilingi 6 *trillion,* 500.6 ambacho badaye kilifutwa kwa maelezo kwamba, kilikosewa. Hata hivyo Manispaa haikutoa maelezo ya kiasi halisi kilichotakiwa kuandikwa kilikuwa ni kipi.

ii. Mnamo tarehe 16 Juni, 2019 muamala wa shilingi milioni 471.4 ulirekebishwa katika mfumo na kuwa shilingi 450 bila ya idhini ya afisa masuuli. Marekebisho haya yanaleta upungufu wa kiasi cha shilingi 21.4 milioni ambazo Kamati ina maoni kuwa zimechukuliwa na watumishi waliohusika na marekebisho hayo.

iii. Miamala ya kiasi cha shilingi 156.9 milioni ilirekebishwa kwenye mfumo wa *LGRCIS* bila ya kuwa na nyaraka za kuthibitisha uhalali wa marekebisho hayo. Tarehe 4/9/2019 kiliingizwa kiasi cha shilingi 689.3 milioni katika akaunti ya manispaa na kutolewa siku hiyohiyo kama fedha taslimu kwa maelezo kuwa Benki ya *CRDB* ilikosea na kuandika namba ya simu ya mteja. Kamati ilitaka kujua kiasi halisi ambacho kilitakiwa kuandikwa, lakini haikupata maelezo ndiyo maana kamati ina maoni kuwa huenda palikuwa na vitendo vya ubadhirifu na utakatishaji fedha hizi. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo ya fedha, yaani 2018/2019 na 2021 watumishi wasiostahili wa Manispaa ya Kigamboni walifanya marekebisho ya miamala ya mapato ya jumla ya shilingi 10.8 bilioni bila idhini ya maafisa masuuli. Aidha, maelezo ya Halmashauri hayakuweka bayana sababu ya kufanyika kwa marekebisho hayo ndio maana kamati inaona kwamba, nyuma ya marekebisho haya huenda kuna nia ovu dhidi ya mapato ya Serikali. Ni wakati muafaka sasa kwa wahusika waweze kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi maalum uliofanyika katika Manispaa ya Ilemela ulijielekeza katika vipindi vitatu vya miaka ya fedha, yaani 2018/2019, 2020 na 2021. Mnamo tarehe 30 Septemba, 2021 CAG alitoa taarifa yenye matokeo ya ukaguzi maalum kwa Manispaa ya Ilemela. Baada ya zaidi ya mwaka mmoja kupita, yaani tarehe 18 Januari, 2023 Manispaa ilianza kushughulikia hoja za ukaguzi zilizomo kwenye taarifa hiyo, ambapo imeweza kujibu hoja tano kati ya hoja 30. Baadhi ya hoja za ukaguzi zilizobainika katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela zipo katika kipengele cha 2.31 (C) cha Taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ubadhirifu wa fedha za umma kutokana na matumizi ya fedha kabla ya kuzipeleka benki, yaani fedha mbichi; katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo 2018/2019, 2020 na 2021 Manispaa ya Ubungo ilitumia fedha mbichi kiasi cha shilingi 196.3 milioni, Manispaa ya Kigamboni ilitumia shilingi 47 milioni, Manispaa ya Ilemela ilitumia shilingi 627.8 milioni na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilitumia shilingi milioni saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha halmashauri mbalimbali kutumia fedha kabla ya kuzipeleka benki, yaani fedha mbichi, kinaathari nyingi hasi. Kwanza kinatoa mwanya wa ubadhirifu kwa wakusanyaji wasio waaminifu kuzitumia fedha zinazokusanywa bila uwazi. Pili, kitendo hiki kinawakosesha wakaguzi na wadau wengine wa taarifa za mapato halisi na matumizi endapo miamala itasuluhishwa kwa njia ya mifumo ya kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kukosekana kwa mapato stahiki ya Manispaa ya Ubungo kutokana na utata katika umiliki wa uendeshaji nyumba za upangishaji za *Oysterbay Villa*. Katika Manispaa ya Ubungo kuna nyumba zilizojengwa kati ya mwekezaji mwenza, yani Bakilsimadzik na

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Manispaa ya Ubungo imekuwa sehemu nya uwekezaji huo na kupewa uendeshaji wa nyumba saba baada ya Manispaa ya Kinondoni kugawanywa na kuwa Manispaa mbili, yaani Ubungo na Kinondoni. Hata hivyo, Manispaa ya Ubungo hainufaiki ipasavyo na mradi huu kutokana na sababu ya mgogoro wa umiliki na uendeshaji wa mradi baina ya washiriki, yaani Bwana Bakilsimadzik na Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni pamoja na Ubungo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kushughulikia suala hili kwa kueleza bayana umiliki na uendeshaji wa mradi huo ukoje na changamoto zilizopo zishughulikiwe ili mradi uweze kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na upotevu wa mapato stahiki ya halmashauri mbalimbali nchini kutokana na uvamizi wa ardhi ya wazi; uchambuzi wa nyaraka mbalimbali unaonesha kuwa pamefanyika uvamizi mkubwa wa umilikishaji wa maeneo ya wazi katika Manispaa ya Ubungo. Kwa mfano, maeneo 13 yamevamiwa na yanatumika kwa makazi na biashara, maeneo 97 yanatumika kwa makazi, maeneo 52 yanatumika kwa shughuli za biashara, maeneo nane ni ofisi mbalimbali, wakati maeneo 37 hayajaendelezwa. Aidha katika maeneo ya wazi na maeneo ya vizimba vya maji *(water points)* maeneo 53 yana hati za umiliki, maeneo 63 yana *offer* wakati maeneo 57 hayana kabisa nyaraka zozote za umiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uvamizi wa maeneo ya wazi umevuruga sana ramani halisi za mipango miji katika miji mbalimbali nchini. Hali hii imeleta athari kubwa katika utoaji wa huduma mbalimbali kama vile udhibiti wa majanga ya moto, lakini pia uvamizi huu unazikosesha Mamlaka za Serikali za Mitaa ada ya pango kutoka katika maeneo hayo. Hivyo

kuchangia udhaifu wa makusanyo ya mapato ya ndani ya Mamlaka hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Kutozingatiwa kwa Masharti ya Sheria ya Manunuzi ya Umma; kwa ujumla upo upotevu mkubwa wa fedha za umma nchini kutokana na kutozingatiwa kwa masharti yaliyowekwa katika sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya umma nchini. Miradi iliyotekelezwa chini ya utaratibu wa *force account* imeathiriwa sana na ukiukaji huu. Miongoni mwa taasisi zilizobainika kuwa na tatizo hili ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa kama mfano ambayo iliyobainika kuwa na changamoto zifuatazo:-

(a) Iliipatia Kampuni ya Kukusanya mapato ya *Lexspancer International Limited* kazi ya kukusanya ushuru wa mazao ya misitu bila ya kuwa na Mkataba na ikailipa kamisheni ya kiasi cha Shilingi 31.8 milioni;

(b) Katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Halmashauri ilinunua vifaa vyenye thamani ya shilingi milioni 29.4 zaidi ya idadi iliyokuwa inatakiwa. Vifaa hivyo vikabaki tu kusubiria matumizi yatakayojitokeza;

(c) Katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Halmashauri iliitunuku Kampuni ya *Sao Hill* zabuni ya kusambaza mbao baada ya kumkataa Mzabuni mwenye bei ya chini *M/s Pelano Resources Limited* bila sababu za msingi. *Sao Hill* aliposhindwa kukamilisha kazi, Halmashauri ilirudi tena kwa Kampuni ya *Pelano Resources Limited*. Kutokana na kuitunuku zabuni Kampuni isiyostahili, Halmashauri ilipata hasara ya Shilingi 15.9 milioni.

(d) Katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Halmashauri ilinununua vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi

345.3 milioni na kuvitumia katika ujenzi huo kabla ya vifaa vyenyewe kukaguliwa na Kamati ya Mapokezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ina mashaka kwamba huenda vifaa hivyo havikununuliwa au havikutumika kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kujielekeza katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa kuu katika ukurasa wa 22 hadi wa 29 ili kutoa Maoni na Mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati; baada ya maelezo kuhusu maeneo mbalimbali yenye changamoto ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Nchini, Kamati ina maoni ya jumla kwamba bado kuna changamoto ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Nchini. Changamoto hizi ni bayana katika eneo la ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mifumo ya kielektroniki, manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii inatukumbusha sisi sote, Serikali, Mabaraza ya Madiwani, Asasi za Kiraia, Vyombo vya Habari na umma kwa ujumla kuona kwamba usimamizi wa nidhamu ya mapato na matumizi ya fedha za umma nchini ni jukumu letu sote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia, hali hii inatukumbusha sisi sote, Serikali, Mabaraza ya Madiwani, Asasi za Kiraia, Vyombo vya Habari na umma kwa ujumla kuona kwamba usimamizi wa nidhamu ya mapato na matumizi ya fedha za umma nchini ni jukumu letu sote. Tunapaswa kushirikiana kuhakikisha kuwa mipango na fedha za mlipa kodi vinaleta tija katika maisha halisi ya Watanzania kwa kuhimiza uwazi na uwajibikaji Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati ina mapendekezo sita (6) yafuatayo:-

(i) Kuhusu Uvujaji wa mapato katika Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato wa *LGRCIS*.

Kwa kuwa nia ya serikali kuwa na utaratibu wa kukusanya mapato kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ni kuimarisha ukusanyaji kwa gharama nafuu za usimamizi;

Na kwa kuwa nia hiyo njema inaharibiwa na baadhi ya watumishi kwa kufanya ujanja kwenye mifumo hiyo kwa nia ya kujipatia manufaa binafsi ya kifedha kama ilivyoonekana katika ukaguzi maalum wa Manispaa za Ubungo, Kigamboni na Ilemela kwa miaka ya fedha ya 2018/2019, 2019/2020 na 2020/2021;

Kwa hiyo basi Bunge linaazimia kwamba:

(a) Serikali itumie uzoefu uliopatikana kutokana na udhaifu wa Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato wa *LGRCIS* kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato katika mfumo mpya wa *TAUSI.* Aidha, kabla ya mwaka wa fedha 2023/2024 kuanza Mfumo wa *TAUSI* uwe umesimikwa na kutumika katika Halmashauri zote nchini; *(Makofi)*

(b) Serikali ihakikishe kuwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa njia za kielektroniki inafanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara *(regular systems audit*) ili kujiridhisha juu ya ufanisi wake. Aidha, taarifa za ukaguzi huo ziwe zinawasilishwa kila mwaka kwenye Kamati husika za Bunge kwa ajili ya mapendekezo na usimamizi zaidi; na

(c) Kabla ya mwaka wa fedha 2023/2024 kuanza, Serikali iwe imechukua hatua stahiki kwa watumishi wa umma waliohusika na marekebisho ya miamala iliyoelezwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii katika Manispaa zilizotajwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Ubadhirifu wa Fedha za Umma kutokana na Matumizi ya Fedha kabla ya kuzipeleka Benki (Fedha Mbichi):

Kwa kuwa utaratibu wa Serikali kwamba mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali yasitumike kugharamia shughuli zozote kabla ya kupelekwa benki una nia njema ya kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma nchini;

Na kwa kuwa imebainika kwamba baadhi ya Halmashauri zinaendelea kutumia fedha kabla ya kuzipeleka benki, hivyo kuathiri dhana nzima ya uwazi katika mapato ya Serikali;

Kwa hiyo basi, Bunge linaitaka Serikali:-

(a) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa utaratibu huu wenye faida nyingi za kiudhibiti na tija katika matumizi ya fedha za umma nchini; na

(b) Kuwawajibisha kwa mujibu wa sheria Watumishi wa umma watakaobainika katika hoja za ukaguzi kwamba wamekiuka utaratibu huu ikiwemo wale waliofanya hivyo katika halmashauri tulizozitaja na katika miaka ya fedha ya 2010…

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti muda wako umekwisha nenda kwenye hitimisho. Taarifa yote iko kwenye *Hansard*. *(Makofi)*

**MHE. STANSLAUS S. MABULA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo naomba taarifa yangu yote iingie kwenye hitimisho. Sasa naomba nimalizie na maneno ya shukurani.

Mheshimiwa Naibu Spika,Kamati inaishukuru Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wako kwa kutuwezesha kutekeleza maju…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda ukurasa wa 31 nenda hitimisho na hoja.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA- MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho; mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kwenye taarifa hii yamejengwa katika msingi wa hoja za ukaguzi wa *CAG*. Mapendekezo haya yanakusudia kuimarisha nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na kuimarisha matumizi bora ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuyaafiki maoni na mapendekezo yaliyomo katika Taarifa ya mwaka ya kazi iliyotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC) KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2022 HADI JANUARI, 2023 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) mwaka 2022 katika kushughulikia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021[11].

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii upo katika Sehemu Kuu Tatu zifuatazo[12]:

(a) Sehemu ya kwanza ni ya utangulizi ambayo inatoa maelezo ya jumla kuhusu kuhusu muundo wa taarifa, msingi wa kazi za Kamati, nyaraka zilizorejewa na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;

(b) Sehemu ya pili inaelezea kazi zilizofanyika na hoja mahsusi zilizojitokeza. Sehemu hii inaweka msingi wa maoni na mapendekezo ya Kamati katika Sehemu ya Tatu;

---

[1] Kanuni ya 136(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

[12] Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020

(c) Sehemu ya Tatu inabainisha maoni na mapendekezo kutokana na shughuli zilizotekelezwa. Aidha, Sehemu hii inajumuisha pia Hitimisho na Hoja ya Kamati.

### 1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** LAAC ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Bunge zilizoundwa chini ya Ibara ya 96 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Shughuli za Kamati hii zipo pia kwa mujibu wa Katiba chini ya Ibara ya 96(2). Aidha, shughuli za LAAC zinafafanuliwa katika Fasili ya 15 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, LAAC ina wajibu wa kusaidia utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge kwa kusimamia nidhamu ya mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara. Jukumu hili hutekelezwa kwa kutegemea Hoja za Ukaguzi zinazotolewa ukaguzi unaofanywa na CAG kila mwaka[13].

### 1.4 Nyaraka zinazotumika

(a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;

(b) Kanuni za Kudumu za Bunge;

(c) Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(d) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008;

(e) Sheria ya Fedha ya Umma (Finance Act) ya kila mwaka;

---

[13] Fasili ya 16 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020

(f) Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali (The Appropriation Act) ya kila mwaka;

(g) Sheria ya Fedha za Umma, Sura 2001;

(h) Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290;

(i) Sheria ya Ukaguzi wa Umma, 2008;

(j) Sheria ya Ununuzi wa Umma, 2002; na

(k) Sheria zingine za nchi.

**Mheshimiwa Spika**, nyaraka hizi ni muhimu sana katika kuweka misingi ya maoni na mapendekzo ya Kamati kwa namna yenye kuzingatia maudhui ya hoja ya ukaguzi na utawala wa sheria kwa ujumla wake.

### 1.5 Njia zilizotumika kutekeleza majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, shughuli za Kamati hutekelezwa kwa njia mbalimbali. Miongoni mwa njia hizo ni vikao vya uchambuzi wa taarifa ya CAG na vikao vya mahojiano, ziara za ukaguzi wa ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na mashauriano na Wadau mbalimbali. Pamoja na kuwepo kwa njia hizi mbalimbali, njia kuu iliyotumika katika kushughulikia taarifa ya hesabu zilizoishia tarehe 30 Juni, 2021 ilikuwa ni vikao vilivyokuwa vikifanyika mjini Dodoma.

### 1.6 Changamoto zilizoikabili Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri 185 zilizokaguliwa na CAG kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 Kamati iliweza kuhojiana na Halmashauri 42 tu sawa na 23% ya Halmashauri zote. Lakini pia, katika Halmashauri 34 zilizofanyiwa ukaguzi maalum na kwa maelekezo ya CAG,

Kamati ilihoji Halmashauri 4 tu sawa na 12% ya Halmashauri zote. Changamoto kubwa ikiwa ni ufinyu wa muda na bajeti ya utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Changamoto nyingine ni muda mrefu ambao hoja za ukaguzi zinakaa tangu Taarifa ya CAG inapokuwa imewasilishwa Bungeni na kipindi ambacho Mapendekezo ya Kamati yanasomwa Bungeni. Kimsingi, pana muda mrefu sana katika kuandaa hesabu za Serikali, kuziwasilisha Bungeni na kuzijadili kisha kuzitolea mapendekezo. Ubadhirifu unakuwa ulishatendeka muda mrefu uliopita kiasi cha kuweza kuathiri hatua za udhibiti.

**Hivyo, Kamati inaunga mkono maelekezo yako yaliyopelekea PAC na LAAC kuwasilisha Taarifa zao mwezi Novemba katika mwaka 2022.**

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA KATI YA FEBRUARI 2022 NA JANUARI, 2023

### 2.1 Maelezo ya Jumla

Sehemu hii inakusudia kulieleza Bunge shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa mwaka 2022 katika kushughulikia Taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021. Aidha, sehemu hii ya taarifa inakidhi matakwa ya Kanuni ya 136 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020. Kanuni hii inaitaka kila Kamati ya Kudumu ya Bunge kuwasilisha Bungeni Taarifa ya shughuli ilizotekeleza ili ijadiliwe Bungeni kabla ya Mkutano wa Bunge wa Bajeti.

Taarifa ya CAG inayorejewa hapo juu ilikuwa na hoja za aina kuu mbili. Yaani; hoja za ukaguzi wa kawaida wa kila mwaka uliofanyika katika Halmashauri zote 185 zilizopo Tanzania Bara

na hoja za Ukaguzi Maalum uliofanyika katika Halmashauri 34 za mfano kwa maelekezo ya CAG.

## 2.2 Shughuli Zilizotekelezwa

### 2.2.1 Mafunzo

Kamati ilishiriki mafunzo chini ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuhusu aina za Kaguzi zinazofanywa na CAG na namna ya kuendesha mahojiano na Maafisa Masuuli. Katika hatua nyingine Kamati ilipata mafunzo kutoka kwa Wakala wa Manunuzi Serikalini (GPSA) kuhusu ushiriki wa Wakala huo katika mchakato wa Manunuzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini na changamoto zilizopo.
Mafunzo haya yameleta tija sana katika utekelezaji wa shughuli za Kamati hususani katika uchambuzi wa hoja za ukaguzi, uendeshaji wa mahojiano na uandaaji wa maoni na mapendekezo.

**Maoni ya Kamati ni kwamba mafunzo kuhusiana na majukumu ya Kamati za Kudumu za Bunge ni muhimu sana ili Kamati hizo ziweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kutoa ushauri unaotekelezeka Serikalini.**

### 2.2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya CAG kuhusiana na Hoja za Ukaguzi wa Kawaida wa Kila Mwaka.

Katika eneo hili, LAAC ilichambua Taarifa ya CAG kwa kuangalia hoja za ukaguzi zilizopo katika Halmashauri zote 185. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda ilihoji sampuli ya jumla ya Halmashauri 40 sawa na 26% ya Halmashauri zote zilizofanyiwa ukaguzi wa kawaida kwa mwaka huo.

Zoezi hili lilianza kutekelezwa Mwezi Julai 2022 na kukamilishwa tarehe 04 Novemba, 2022 ambapo maoni na

mapendekezo ya Kamati yakiwa na Hoja 11 zifuatazo yaliwasilishwa Bungeni:

(a) Uendeshaji na ustahimilivu wa Mfuko wa Mikopo kwa Vikundi vya Akina Mama, Wanawake na Watu wenye Ulemavu;

(b) Mwenendo wa upatikanaji wa ruzuku ya maendeleo katika Halmashauri;

(c) Hali ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(d) Hali ya Utekelezaji wa Mikataba katika Manunuzi ya Bidhaa na Huduma mbalimbali katika Halmashauri;

(e) Upatikanaji wa stahili za Watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini;

(f) Hali halisi katika Ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini;

(g) Matumizi yasiyofaa ya fedha katika Akaunti za Amana katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini;

(h) Upotevu wa Mapato katika mifumo ya kielektroniki katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini;

(i) Namna mwenendo wa baadhi ya Taasisi za Umma nchini unavyoathiri ufanisi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kutekeleza majukumu yake;

(j) Hali halisi ya uteketezaji wa dawa za binadamu inavyo athiri mapato na matumizi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini; na

(k) Mapungufu katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

**Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kukumbusha kwamba Serikali bado haijaleta Bungeni au kwenye Kamati majibu yake kuhususiana na Maazimio haya. LAAC itapenda kupata majibu ya hoja hizi mapema kabla ya Taarifa ya CAG ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 haijawasilishwa Bungeni ili iweze kutathmini mwelekeo wa kazi zake na kujipanga ipasavyo.**

### 2.2.3 Uchambuzi wa Taarifa ya CAG kuhusiana na Hoja za Ukaguzi Maalum.

Taarifa ya CAG ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 ilikuwa na hoja za ukaguzi maalum ambao CAG kwa utashi wake aliamua kujiridhisha kwa kina juu ya mwenendo wa ukusanyaji na utumiaji wa fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 34 za Tanzania Bara katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo (2018/19- 2020/21).

Kati ya mamlaka 34 zilizofanyiwa ukaguzi huo maalum, Kamati ilihoji Maafisa Masuuli wa Mamlaka 4 sawa na 12%. Mamlaka hizo ni Manispaa ya Ubungo, Kigamboni, Ilemela na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Vigezo vilivyotumika kupata sampuli ya Halmashauri za kuhoji vinajumuisha aina ya hati ya ukaguzi, muda uliopo kwa Kamati kuweza kutekeleza majukumu yake kwa wakati na uzito wa hoja ya ukaguzi katika halmashauri husika.

### 2.3 Hoja Mahsusi kutokana na Ukaguzi Maalum

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa za Ukaguzi Maalum uliofanyika katika Manispaa za Ubungo, Kigamboni, Ilemela na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Matokeo yanaonesha kwamba bado kuna changamoto

katika nidhamu ya ukusanyaji na utumiaji wa mapato ya Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

**Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zinapaswa kutafutiwa ufumbuzi wa haraka ili kila senti ya Serikali ilete tija katika kuwahudumia Wananchi. Miongoni mwa suluhu ni Serikali hususani katika ngazi za Sekretarieti za mikoa kujipanga kikamilifu kwa ajili ya kufanya usimamizi madhubuti na ufuatiliaji wa kina katika shughuli zinazotekelezwa na mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo chini yao. Kwa sasa inaonekana kuna ulegevu wa Sekretarieti za Mikoa katika kuzisimamia Halmashauri. Ulegevu huu hautavumiliwa hata kidogo na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.**

**2.3.1 Uvujaji wa mapato katika Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato.**

**Mheshimiwa Spika**, kimsingi kuna uvujaji mkubwa wa mapato ya Serikali katika mfumo wa kielektroniki wa kukusanya mapato wa *Local Government Revenue Collection Information System* (LGRCIS) endapo Mfumo huo utakuwa bado unaendelea kutumika katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Uvujaji huu unasababishwa na baadhi ya Watumishi wa Serikali wasio waaminifu wanaohusika moja kwa moja na uingizaji wa miamala katika Mfumo huo. Ushahidi uliopo unahusiana na Mfumo uliokuwepo awali wa LGRCIS ambao kwa sasa ni TAUSI.

**Kamati ina maoni kwamba kinachofanyika ni wizi kwa sababu ya mazingira ambamo marekebisho ya miamala hufanyika. Kuna maeneo ambamo miamala hufutwa kabisa au baadhi ya tarakimu hurekebishwa bila idhini ya Maafisa**

**Masuuli au bila ya kuwepo kwa nyaraka za uthibitisho wa uhalali wa marekebisho hayo.**

Mifano ya Halmashauri zilizobainika katika Hoja hii ni:

**(a) Manispaa ya Ubungo**

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo pamefanyika vitendo kadhaa vyenye kutia shaka katika Mfumo wa kukusanyia mapato. Kwa mfano:

(i) Taarifa ya wadaiwa katika Mfumo ilifanyiwa ghiliba kiasi cha kushindwa kuonesha mapato halisi ya Halmashauri kwa kuingiza kiasi cha Shilingi **500,666,683,784,266,000,000,000/=** ambacho badae kilifutwa kwa maelezo kwamba kilikosewa. Hata hivyo, Manispaa haikutoa maelezo ya kiasi halisi kilichotakiwa kuandikwa kilikuwa ni kipi;

(ii) Mnamo tarehe 16 Juni, 2019 muamala wa **Tsh. 471,410,886** ulirekebishwa katika mfumo na kuwa **TSh. 450, 029, 376** bila ya idhini ya Afisa Masuuli. Marekebisho haya yanaleta upungufu wa kiasi cha **Tsh. 21,381,510/=** ambazo Kamati ina maoni kuwa zimechukuliwa na Watumishi waliohusika na marekebisho;

(iii) Miamala ya kiasi cha **Shilingi 156.9 milioni** ilirekebishwa kwenye Mfumo wa LGRCIS bila ya kuwa na nyaraka za kuthibitisha uhalali wa marekebisho hayo;

(iv) Tarehe 4. 9. 2019 kiliingizwa kiasi cha **Shilingi 689, 260,490** katika akaunti ya Manispaa na kutolewa siku hiyohiyo kama fedha taslimu kwa maelezo kuwa benki (CRDB Bank) ilikosea kwa kuandika namba ya simu ya mteja. Kamati ilitaka kujua kiasi halisi ambacho kilitakiwa

kuandikwa lakini haikupata maelezo. Ndiyo maana Kamati ina maoni kuwa huenda palikuwa na vitendo vya utakatishaji wa fedha.

**(b) Manispaa ya Kigamboni**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo ya fedha yaani 2018/2019- 2020/21 watumishi wasio stahili wa Manispaa ya Kigamboni walifanya marekebisho ya miamala ya mapato ya jumla ya **Tsh. 10,857,780,242** bila ya idhini ya Afisa Masuuli.

Aidha, maelezo ya Halmashauri hayakuweka bayana sababu za kufanyika kwa marekebisho hayo. Ndiyo maana Kamati inaona kwamba nyuma ya marekebisho haya huenda kuna nia ovu dhidi ya mapato ya Serikali. Jambo hili linahitaji uchunguzi zaidi ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria.

**(c) Manispaa ya Ilemela**

Ukaguzi Maalum katika manispaa ya Ilemela ulijielekeza katika vipindi vitatu vya miaka ya fedha (2018/19- 2020/21). Mnamo tarehe 30 Septemba, 2021 CAG alitoa taarifa yenye matokeo ya Ukaguzi Maalum kwa Manispaa ya Ilemela. Baada ya zaidi ya mwaka mmoja kupita, yaani; tarehe 18 Januari, 2023 Manispaa ilianza kushughulikia hoja za ukaguzi zilizomo kwenye Taarifa hiyo ambapo imeweza kujibu Hoja 5 kati ya hoja 30.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya hoja za ukaguzi zilizobainika katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ni hizi zifuatazo na bado hazijajibiwa. Serikali lazima ichukue hatua za haraka dhidi ya Watumishi wote waliohusika:

(i) Ankara zenye thamani ya **Tsh. 8.7 bilioni** zilirekebishwa kwenye Mfumo wa Mapato bila kufuata taratibu;

(ii) Kiasi cha **Tsh. 1.4 bilioni** kilipelekwa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kujenga Jengo la Wasafiri katika Uwanja wa Ndege wa Mwanza bila ya kuwa na Memoranda ya Makubaliano juu ya namna ambavyo Manispaa ingenufaika na uwekezaji huo;

(iii) Jumla ya stakabadhi 822 za mapato hazionekani katika daftari la fedha la mfumo wa ukusanyaji wa mapato;

(iv) Jumla ya **Shilingi 627.8 milioni** hazikupelekwa benki mpaka sasa;

(v) Hakuna ushahidi wa malipo ya kiasi cha **Tsh. 356.4 milioni** kwamba zililipwa kwa Mhandisi Mshauri Elekezi katika usimamizi wa mradi wa Stendi ya Mabasi na Maegesho ya Malori;

(vi) Manispaa ilimlipa Mkandarasi aliyejenga Stendi ya Mabasi na Maegesho ya Malori kiasi cha **Tsh. 237.6 milioni** ikiwa ni Zaidi ya fedha anazodai;

(vii) Manispaa ilimlipa Mkandarasi (TBA) kiasi cha **Tsh. 138.7 milioni** kwa kazi ambazo hajafanya;

(viii) Watumishi waliohama na wengine kustaafu wakawa bado wanaingia kwenye Mfumo wa Mapato kiasi cha kutishia usalama wa mfumo wa Serikali katika ukusanyaji wa mapato;

(ix) Katika hesabu za mwisho kwa Mwaka wa fedha 2019/20 Manispaa ili ripoti zaidi madeni ya Wazabuni na Wakandarasi kwa kiasi cha **Tsh. 200 milioni**;

(x) Kiasi cha Tsh. 15.6 milioni kililipwa kwa Mkandarasi *Ejae Investment Group* kwa kutumia Risiti ya kughushi hivyo kuikosesha Serikali Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kiasi cha **Tsh. 2.8 milioni**;

(xi) Manispaa haikuweza kutoa nyaraka za kumthibitishia CAG kuhusu Kampuni zipatazo 270 zinazofanya biashara katika maeneo mbalimbali ya Manispaa bila kulipa ushuru wa huduma (service levy) kwa muda mrefu sasa; na

(xii) Hadi tarehe 23 Januari, 2023, ambapo LAAC ilijadili Taarifa za Manispaa ya Ilemela, Mfumo wa TAUSI ulikuwa bado haujasimikwa.

**Maoni ya Kamati ni kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inapaswa kufuatiliwa kwa karibu kuhusiana na mwenendo wake katika kukusanya na kutumia mapato yake. Ofisi ya Rais- TAMISEMI inatakiwa kuisimamia kikamilifu Manispaa hii na kuchukua hatua kali dhidi ya watumishi ambao utendaji wao ulisababisha kuwepo kwa hoja hizo**.

### 2.3.2 Ubadhirifu wa Fedha za Umma kutokana na Matumizi ya Fedha kabla ya kuzipeleka Benki (Fedha Mbichi)

Utaratibu wa Serikali katika masuala ya mapato na matumizi unaelekeza kwamba makusanyo ya fedha za umma yasigharamie shughuli zozote kabla ya kupelekwa benki. Utaratibu huu upo kwa mujibu wa Sheria. Lengo kubwa ni kuwezesha usuluhishi bora wa hesabu za mapato na matumizi ya Serikali.

Kitendo cha Halmshauri mbalimbali nchini kutumia fedha kabla ya kuzipeleka benki (fedha mbichi) kina athari nyingi hasi. Kwanza kinatoa mwanya wa ubadhirifu kwa Wakusanyaji wasio waaminifu kuzitumia fedha

zinazokusanywa bila uwazi. Pili, kitendo hiki kinawakosesha wakaguzi taarifa za mapato halisi na matumizi endapo miamala itasuluhishwa kwa njia ya mifumo ya kielektroniki.

Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo 2018/19 – 2020/21 Manispaa ya Ubungo ilitumia fedha mbichi kiasi cha **Tsh. 196.3 milioni**, Manispaa ya Kigamboni ilitumia **Tsh.47 milioni**, Manispaa ya Ilemela **Tsh.627.8 milioni** na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ilitumia **Tsh. 7milion**.

### 2.3.3 Kukosekana kwa mapato stahiki ya Manispaa ya Ubungo kutokana na utata katika Umiliki na Uendeshaji wa Nyumba za kupangisha za Oysterbay Villa

Katika Manispaa ya Ubungo kuna nyumba zilizojengwa kati ya mwekezaji mwenza Bakir Samardrzic na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Manispaa ya Ubungo imekuwa sehemu ya uwekezaji huo kwa kupewa uendeshaji wa nyumba saba (7) baada ya manispaa ya Kinondoni kugawanywa na kuwa Manispaa mbili yaani Ubungo na Kinondoni.

Hata hivyo, Manispaa ya Ubungo hainufaiki ipasavyo na mradi huu kutokana na sababu ya mgogoro wa umiliki na uendeshaji wa mradi baina ya washirika (Bw. Bakir Samardrzic na Halmashauri za Manispaa ya Kinondoni na Ubungo).

**Mheshimiwa Spika, Kamati inaona ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kushughulikia suala hili kwa kueleza bayana umiliki na uendeshaji wa mradi huo ukoje na changamoto zilizopo zishughulikiwe ili Mradi uweze kuleta tija iliyokusudiwa.**

**2.3.4 Upotevu wa Mapato stahiki ya Halmashauri mbalimbali nchini kutokana na Uvamizi wa Ardhi ya Maeneo ya Wazi.**

Ramani ya Mipango Miji ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 1974 mathalani Mchoro Namba 1/73/174 SINZA, 1/529/369 DAR ES SALAAM AREA 18 KINONDONI na 1/530/369 DAR ES SALAAM AREA 19 MANZESE inaonesha kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo ina maeneo ya wazi 51 na maeneo 211 tengefu kwa ajili ya vizimba vya maji.

Uchambuzi wa nyaraka mbalimbali unaonesha kuwa pamefanyika uvamizi mkubwa na umilikishaji wa maeneo ya wazi katika Manispaa ya Ubungo. Kwa mfano; maeneo 13 yamevamiwa na yanatumika kwa makazi na biashara, 97 yanatumika kwa makazi, 52 yanatumika kwa shughuli za biashara, 8 ni ofisi mbalimbali wakati maeneo 37 hayajaendelezwa.

Aidha, katika maeneo ya wazi na maeneo ya vizimba vya maji (water points), maeneo 53 yana hati za umiliki, maeneo 63 yana *offer* wakati maeneo 57 hayana nyaraka zozote za umiliki.

**Mheshimiwa Spika, uvamizi wa maeneo ya Wazi umevuruga sana ramani halisi za mipango miji katika miji mbalimbali nchini. Hali hii imeleta athari kubwa katika utoaji wa huduma mbalimbali kama vile udhibiti wa majanga ya moto. Lakini pia uvamizi huu unazikosesha Mamlaka za Serikali za Mitaa ada ya pango kutoka katika maeneo hayo hivyo kuchangia udhaifu wa makusanyo ya mapato ya ndani ya Mamlaka hizo.**

### 2.3.5 Kutozingatiwa kwa Masharti ya Sheria ya Manunuzi ya Umma

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, upo upotevu mkubwa wa fedha za umma nchini kutokana na kuto kuzingatiwa kwa masharti yaliyowekwa katika sheria, kanuni na taratibu za manunuzi ya umma nchini. Miradi iliyotekelezwa chini ya utaratibu wa *force account*imeathiriwa sana na ukiukaji huu. Miongoni mwa taasisi zilizobainika kuwa na tatizo hili ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ambayo iliyobainika kuwa na changamoto zifuatazo:

(a) Iliipatia Kampuni ya Kukusanya mapato ya *Lexspacer International Ltd* kazi ya kukusanya ushuru wa mazao ya misitu bila ya kuwa na Mkataba na ikailipa kamisheni ya kiasi cha **Shilingi 31.8 milioni**;

(b) Katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya Halmashauri ilinunua vifaa vyenye thamani ya **shilingi 29.4 milioni** zaidi ya idadi iliyokuwa inatakiwa. Vifaa hivyo vikabaki tu kusubiria matumizi yatakayojitokeza;

(c) Katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya, Halmashauri iliitunuku Kampuni ya *Sao Hill* zabuni ya kusambaza mbao baada ya kumkataa Mzabuni mwenye bei ya chini *M/s Pelano Resources Ltd* bila sababu za msingi. *Sao Hill* aliposhindwa kukamilisha kazi, Halmashauri ilirudi tena kwa Kampuni ya *Pelano Resources Ltd*. Kutokana na kuitunuku Zabuni Kampuni isiyostahili, Halmashauri ilipata hasara ya **Shilingi 15.9 milioni**.

(d) Katika ujenzi wa hospitali ya Wilaya, Halmashauri ilinununua vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya **shilingi 345.3 milioni** na kuvitumia katika ujenzi huo kabla ya vifaa vyenyewe kukaguliwa na Kamati ya Mapokezi.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo kuhusu maeneo mbalimbali yenye changamoto ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini, Kamati ina maoni ya jumla kwamba bado kuna changamoto ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Changamoto hizi ni bayana katika eneo la ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mifumo ya kielektroniki, manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hali hii inatukumbusha sisi sote, Serikali, Mabaraza ya Madiwani, Asasi za Kiraia, Vyombo vya Habari na umma kwa ujumla kuona kwamba usimamizi wa nidhamu ya mapato na matumizi ya fedha za umma nchini ni jukumu letu sote. Tunapaswa kushirikiana kuhakikisha kuwa mipango na fedha za mlipa kodi vinaleta tija katika maisha halisi ya Watanzania kwa kuhimiza uwazi na uwajibikaji Serikalini.

Kutokana na hali hiyo, Kamati ina mapendekezo Sita (6) yafuatayo:

### 3.1 Kuhusu Uvujaji wa mapato katika Mfumo wa Kielektroniki wa Kukusanya Mapato wa LGRCIS.

**KWAKUWA,** nia ya Serikali kuwa na utaratibu wa kukusanya mapato kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ni kuimarisha ukusanyaji kwa gharama nafuu za usimamizi,

**NA KWAKUWA,** nia hiyo njema inaharibiwa na baadhi ya Watumishi kwa kufanya ujanja kwenye Mifumo hiyo kwa nia ya kujipatia manufaa binafsi ya kifedha kama ilivyoonekana katika Ukaguzi Maalumu wa Manispaa za Ubungo,

Kigamboni na ilemela kwa miaka ya fedha ya 2018/19, 2019/20 na 2020/21;

**KWA HIYO BASI,** Bunge lina azimia kwamba:

(a) Serikali itumie uzoefu uliopatikana kutokana na udhaifu wa Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato wa LGRCIS, kudhibiti mianya ya uvujaji wa mapato katika mfumo mpya wa TAUSI. Aidha, kabla ya mwaka wa fedha 2023/24 kuanza Mfumo wa TAUSI uwe umesimikwa na kutumika katika Halmashauri zote nchini;

(b) Serikali ihakikishe kuwa mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa njia za kielektroniki inafanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara (regular systems audit) ili kujiridhisha juu ya ufanisi wake. Aidha, taarifa za ukaguzi huo ziwe zinawasilishwa kila mwaka kwenye Kamati husika za Bunge kwa ajili ya mapendekezo na usimamizi zaidi; na kwamba

(c) Kabla ya mwaka wa fedha 2023/24 kuanza, Serikali iwe imechukua hatua stahiki kwa watumishi wa umma waliohusika na marekebisho ya miamala iliyoelezwa katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii katika Manispaa za Ubungo, Ilemela na Kigamboni.

**3.2 Kuhusu Ubadhirifu wa Fedha za Umma kutokana na Matumizi ya Fedha kabla ya kuzipeleka Benki (Fedha Mbichi).**

**KWAKUWA**, utaratibu wa Serikali kwamba mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali yasitumike kugharamia shughuli zozote kabla ya kupelekwa benki una nia njema ya kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma nchini,

**NA KWAKUWA**, imebainika kwamba baadhi ya Halmashauri zinaendelea kutumia fedha kabla ya kuzipeleka benki hivyo kuathiri dhana nzima ya uwazi katika mapato ya Serikali,

**KWAHIYO BASI,** Bunge linaitaka Serikali:

(a) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa utaratibu huu wenye faida nyingi za kiudhibiti na tija katika matumizi ya fedha za umma nchini; na

(b) Kuwa wajibisha kwa mujibu wa Sheria Watumishi wa umma watakaobainika katika hoja za ukaguzi kwamba wamekiuka utaratibu huu ikiwemo wale waliofanya hivyo katika Halmashauri za Manispaa za Ubungo, Ilemala na Kigamboni katika miaka ya fedha ya 2018/19, 2019/20 na 2020/21 kama ilivyobainika katika Ukaguzi Maalum wa CAG.

**3.3 Kuhusu kukosekana kwa mapato stahiki ya Manispaa ya Ubungo kutokana na utata katika Umiliki na Uendeshaji wa Nyumba za kupangisha za Oysterbay Villa.**

**KWAKUWA**, masuala ya ushirikiano katika uwekezaji wa mitaji ya maendeleo upo kwa mujibu wa Sera ya Taifa na Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP) kwa nia ya kuharakisha maendeleo na upatikanaji wa huduma katika sekta mbalimbali,

**NA KWAKUWA**, katika baadhi ya maeneo ubia huu unaonekana kutoleta tija iliyokusudiwa mathalani katika umiliki na uendeshaji wa mradi wa nyumba za kupangisha za *Oysterbay Villa* katika Manispaa ya Ubungo Jijini Dar es Salaam Jijini,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaitaka Serikali kushughulikia changamoto zilizopo katika umiliki na uendeshaji wa Mradi

wa *Oysterbay Villa* ili washirika waweze kunufaika ipasavyo na mradi huo na kwamba taarifa ya Serikali kuhusiana na namna ilivyoshughulikia suala hili iwasilishwe Bungeni ndani ya Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge hili.

**3.4 Kuhusu Upotevu wa Mapato ya Halmashauri mbalimbali nchini kutokana na Uvamizi wa Ardhi ya Maeneo ya Wazi.**

**KWAKUWA**, maeneo ya wazi katika Halmashauri mbalimbali nchini ni mahsusi kulingana na ramani za mipango miji yao,

**NA KWAKUWA**, kupitia maeneo hayo Halmashauri zinaweza kunufaika kutokana na ada ya pango,

**NA KWAKUWA** maeneo yaliyo mengi yamevamiwa na kutumika kwa shughuli binafsi ikiwemo makazi na ofisi,

**KWAHIYO BASI**, Bunge lina azimia kwamba kabla ya Mwaka wa Fedha 2023/24 kuanza Serikali:

(a) Iwe imefanya tathmini maalum ya maeneo ya wazi na namna yanavyotumika katika halmashauri zote nchini kwa nia ya kuyalinda maeneo hayo na kujiepusha dhidi ya migogoro inayoweza kujitokeza kutokana na uvamizi wa maeneo hayo; na

(b) Iwe imetoa Mwongozo wa namna Hati za Umiliki wa Ardhi zilizotolewa kwa Wavamizi mbalimbali wa Maeneo ya Wazi hususani katika Manispaa ya Ubungo zinavyoweza kushughulikiwa baada ya kuisha muda wake.

Pendekezo hili ni muhimu ili Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa upande mmoja na Wavamizi kwa upande mwingine wajue hatma yao. Kwa sasa Manispaa ya Ubungo haipo tayari kutoa vibali vya

kuhuisha Hati hizo kwa sababu maeneo yanayokaliwa ni ya wazi kwa mujibu wa Ramani Kuu ya Mipango Miji ya Jiji la Dar es Salaam.

**3.5 Kuhusu upotevu wa fedha za umma kutokana na kutozingatiwa kwa masharti ya sheria ya Manunuzi.**

**KWAKUWA** masharti ya Sheria ya Manunuzi ya Umma (2004) ni kwa ajili ya uwazi, uwajibikaji na tija katika matumizi ya fedha za umma,

**NA KWAKUWA** Halmashauri mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa (katika ujenzi wa hospitali ya Wilaya) ilikiuka masharti hayo kisha kuisababishia Serikali hasara;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaitaka Serikali na taasisi zake kuzingatia masharti ya Sheria, Kanuni na taratibu za manunuzi ya umma katika kutekeleza miradi ya maendeleo nchini. Aidha, Watumishi wote wanaobainika kuhusika na ukiukwaji huu wanatakiwa kuchukuliwa hatua stahiki mara moja.

**3.6 Kuhusu Utaratibu wa kufunga, kukagua, kuwasilisha na kujadili taarifa za Hesabu za Serikali.**

**KWAKUWA**, utaratibu na muda mrefu wa kisheria uliopo sasa katika kufunga, kukagua, kuwasilisha na kujadili taarifa za hesabu za Serikali uliwekwa katika Sheria mbalimbali za nchi kama vile Sheria ya Fedha za Umma (2001) na Sheria ya Ukaguzi wa Umma (2008) kabla ya mifumo ya kielektroniki ya mapato na matumizi kuanza kutumika nchini,

**NA KWAKUWA**, muda huo ulivyo mrefu unazifanya hoja za ukaguzi kujadiliwa na Kamati za Bunge baada ya ubadhirifu kuwa umetendeka muda mrefu uliopita,

**KWAHIYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kupitia upya masharti ya vifungu vya Sheria zinazohusika katika muda wa kufunga na kuanza kukagua hesabu za Serikali na muda wa kuziwasilisha Bungeni taarifa za hesabu zilizokaguliwa ili uweze kurekebishwa kwa kuzingatia taratibu za utungaji wa sheria za nchi.

**Mheshimiwa Spika**, pendekezo hili linakusudia kuweka mazingira yatakayo wezesha hoja za ukaguzi kujadiliwa kwa wakati Bungeni na kupunguza ubadhirifu katika fedha za umma kwani mapendekezo ya hatua stahiki yatakuwa yanatolewa kwa wakati Bungeni kuliko yanavyotolewa sasa.

3.7 **SHUKRANI**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inakushukuru Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wako kwa kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Tuna mpongeza Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa Mwihambi (*ndc*) kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati. Pongezi hizi zimfikie pia Mkurugenzi wa Kamati za Bunge Bw. Athuman Hussen, Mkurugenzi Msaidizi katika Sehemu ya Fedha na Uchumi Ndg. Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati ya LAAC Ndg. Dickson M. Bisile akisaidiana na Bi. Jesca T. Sanga na Ndg. Paul Chima.

Tunaishukuru Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi chini ya Ndg. CPA Charles Kichere CAG kwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Tunaipongeza Ofisi ya Rais TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kila wakati tulipohitaji ufafanuzi wa hoja mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa naomba kuwashukuru Wajumbe wa LAAC kwa uvumilivu, ushirikiano na uchapa kazi, na ninaomba kuwatambua kwa majina yao kama ifutavyo:-

1. Mhe. Halima J. Mdee, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Stanslaus S. Mabula, Mb - Makam Mwenyekiti
3. Agnes E. Hokororo, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Ally M. Twaha, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Benaya L. Kapinga, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Conchesta L. Rwamlaza, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Elibariki E. Kingu, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Jeremiah A. Mrimi, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Jesca J. Msambatavangu, Mb- Mjumbe
10. Mhe. John M. Sallu, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Joseph Z. Kamonga, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Joseph A. Tadayo, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Francis K. Ndulane, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Issa A. Mchungahela, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Khadija H. Aboud, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Maimuna S. Mtanda, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Maimuna A. Pathan, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Masache N. Kasaka, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Ng'wasi D. Kamani, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Rehema J. Migila, Mb - Mjumbe

### 3.8 HITIMISHO NA HOJA

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati katika Taarifa hii yamejengwa katika msingi wa Hoja za Ukaguzi wa CAG. Mapendekezo haya yanakusudia kuimarisha nidhamu ya ukusanyaji wa mapato na kuimarisha matumizi bora ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, naomba sasa Bunge lipokee, lijadili na kuyaafiki Maoni na Mapendekezo yaliyomo katika Taarifa ya mwaka ya kazi zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa mwaka 2022.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa hoja.

……………………………….
Stanslaus S. Mabula, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA**

07 Februari, 2023

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na hoja imeungwa mkono. Ahsante kwa taarifa nzuri. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye kuchangia na tunaanza na Mheshimiwa Jacqueline Kainja Andrea, ajiandae Mheshimiwa Ng'wasi, ajiandae na Mheshimiwa Vuma.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia taarifa hii ya *CAG* katika Kamati ya Hesabu za Serikali *PAC*. Moja kwa moja niweze kuchangia kuhusu ukaguzi wa kiufundi katika ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *CAG* inaonesha kwamba hakukuwa na mawasiliano mazuri kati ya Wizara ya TAMISEMI pamoja na ya Afya, ina maana pesa zimeenda Wizara ya TAMISEMI kwenda kujenga yale majengo kwa ajili ya hospitali za rufaa lakini hawajawashirikisha wataalam ambao wako Wizara ya Afya ili waweze kuwapa michoro na

ramani nzuri ambazo wanaona kwamba zinafaa na zina sifa za kuwa hospitali. Matokeo yake taarifa hii ya *CAG* inatuonesha kwamba yale majengo hayana sifa ya kuwa hospitali kwa maana kwamba pesa za umma hazijaenda kuwa na tija, kwa sababu tayari moja kwa moja yale majengo inavyoonekana wataalam watashindwa kuyatumia kwa sababu michoro ile na ramani ile haijaenda sawa pamoja na Wizara ya Afya wanavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika eneo hilo hilo, pesa zilizoenda kwa mfano katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mara ambayo imekwenda kujengwa ni pesa zaidi ya bilioni tano, lakini sasa majengo yale kwa taarifa ya *CAG* na sisi kama Wanakamati tumeona, *beam* za majengo tayari zimepinda, lakini vile vile mabati yamepinda, nyufa tayari zimeshatokea. Sasa unaanza kujiuliza, kama pesa imeenda bilioni tano na zaidi kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na tayari umepeleka mkandarasi pale, walitumia vigezo gani mpaka yule mkandarasi anajenga vitu ambavyo havieleweke yaani hata kwa mwonekano, hata nyumba ya mwananchi hawezi kujenga *beams* zimepinda, mabati yamekaa shaghala baghala, kuta tayari zina nyufa. Hizi ni pesa za wananchi ambao ni walipakodi, wananchi wanyonge, Serikali tunakaa hapa tunapitisha bajeti, Wizara inachukua pesa, inaenda *site* kutuletea matokeo ambayo yanasikitisha na yanatia uchungu kwa matumizi mabovu ya pesa za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihamie katika suala hilo hilo katika kipengele cha ukiukwaji wa sheria za manunuzi. Kwa mfano, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya ambayo imejengwa *Consultant* hakuleta *performance security bond.* Sasa kama *Consultant* hajapeleka *performance security bond,* maana yake ni kwamba yule *consultant* asipoweza kufanya ile kazi, wewe Serikali unaweza ukambana kwa kupitia kitu gani? Utarudisha vipi zile pesa? Tayari tutakuwa

tumeshapoteza hizo pesa na kama wamekiuka kifungu cha Sheria 58(1) cha Sheria ya Manunuzi ina maana wale watu hawako *serious* na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba watu hawa wanaofanya *business as usual* katika pesa za wananchi kutuletea hasara, kutupigisha *mark time* hapa, kila siku tutakaa hapa tunapitisha pesa, watu waende *site,* matokeo yanayokuja, *CAG* anakuja na mambo ambayo hayaeleweki, mwisho wa siku wanaoumia ni wananchi. Kwa haya yaliyofanyika katika Hospitali hizi za Rufaa za Kanda ambazo *CAG* ameweza kukagua na kuona kwamba ufanisi wa majengo haya haukidhi vigezo, basi sasa wale Wakandarasi au watu ambao wamechukua mkataba huu wa kutujengea zile gharama ziwe juu yao. Majengo yale yabomolewe, wajenge kwa gharama zao wao wenyewe, sio tena kesho na keshokutwa tukae hapa tuambiwe tunapitisha bajeti ya ukarabati wa majengo ambayo tayari tulishapitisha, tunategemea kazi nzuri ije mikononi mwetu, inakuja kazi ambayo haina viwango. Kwa hiyo gharama iwe juu yao na sio juu ya wananchi wanyonge, wanalipa kodi, biashara zenyewe ni ngumu, watu wanahangaika kutafuta ada za watoto wao, kodi zinakatwa kila kukicha, kodi nazo ni nyingi, leo tena tuna kazi ya kujenga hospitali kila kukicha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuishia hapo kwa sababu ya muda. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kamani, jiandae na Mheshimiwa Vuma.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia katika ripoti za Kamati hizi tatu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu wa leo utajikita katika wizi, upotevu, ubadhirifu na ufujaji wa fedha katika halmashauri zetu. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na katika moja ya majukumu ya Kamati yangu ni pamoja na kuangalia namna fedha zinavyotumika kuendesha miradi mbalimbali na kuleta maendeleo kwa wananchi katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mengi ambayo yamesomwa kwenye ripoti yetu naomba tu ni-*highlight* machache. Kuna suala zima la kubadili miamala katika mfumo bila kufuata utaratibu na katika halmashauri ya Ubungo tuna hasara ya Shilingi Milioni 21.3; Kigamboni, Bilioni 10.8; Ilemela, Bilioni 8.7. Katika matumizi ya fedha mbichi; Ubungo tuna Milioni 196.3, Kigamboni Milioni 47, Ilemela milioni 627, lakini hii ni bila kuzungumzia fedha ambazo zimelipwa kwa mkandarasi bila kuwa ametoa ushahidi Milioni 356, fedha ambazo zimelipwa kwa kazi ambayo haijafanyika Ilemela Milioni 138 na Fedha ambayo imelipwa zaidi ya kiwango kilichokuwa kinadaiwa Milioni 237.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimeyataja haya? Nimeyataja ili Bunge lako Tukufu na wananchi wajue viwango vya fedha tunazozungumzia. Katika hizi halmashauri tatu tu ripoti yetu inaonesha ni zaidi ya Bilioni 20 zinaoneshwa kwenye ripoti ya *CAG* zina mashaka na hazijaeleweka namna ya matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoshangaza zaidi ni kwamba, watumishi wanaohusika katika wizi, ubadhirifu au uzembe huu wanafanyiwa yafuatayo:-

(i) Wanapewa barua za onyo;

(ii) Wanahamishwa kupeleka katika halmashauri zingine;

(iii) Wanaanza kufanyiwa uchunguzi na cha kushangaza zaidi baadhi ya watumishi bado wapo katika halmashauri wakati bado wanafanyiwa uchunguzi; na

(iv) Wengine wanapelekwa Polisi au TAKUKURU na hawa ni wachache, lakini bado haitoi *justification* kuwapeleka watumishi hawa Polisi au TAKUKURU kwa ajili ya uchunguzi kwa sababu ripoti ya *CAG* ina uzito wa kuweza kutumika kama ushahidi mahakamani. Kwa hiyo, maana yake hawa watu walitakiwa wafikishwe mahakamani na hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, inakuaje leo hii Mheshimiwa Rais anazunguka sehemu mbalimbali kutafuta fedha kuhakikisha wananchi wanaletewa maendeleo, fedha zinamwagwa kwenye halmashauri zetu ili watu tupate maendeleo. Fedha hizi tulitakiwa tuzione zina-*reflect* kwenye mzunguko wa fedha kwa wananchi, lakini hatulioni kwa sababu kuna uzembe, wizi na upotevu mkubwa unafanyika kwenye halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, humu Wabunge wengi sana kwenye simu zao wana *soft cope* za *CV* zimejaa watu wanaomba watafutiwe ajira, wana *hard copy* mafaili yamejaa wanaomba watafutiwe ajira. Hizi ajira zinatoka wapi kama fedha ambazo zinapelekwa kwenye halmashauri zetu kwenye jamii zetu zitumike kuleta maendeleo, kuzalisha ajira, kufanya uwekezaji zinaibiwa na zinaingia kwenye mifuko ya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Taarifa.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii darasa moja fedha zimeenda kwenye halmashauri zetu Milioni 20 kwa darasa moja, darasa la vioo la...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa subiri kuna taarifa.

**MHE. NICODEMUS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda nimpe taarifa tu dada yangu mchango wake ni mzuri sana kwa kusisitiza kwa kweli Serikali, hawa waliothibitishwa na *CAG* ni majangili, ni majambazi wanatakiwa wakamatwe mara moja haraka, tena wakaishi mahabusu huko. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamani, taarifa hiyo.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii huko mitaani vijana wanakosa hata shilingi laki mbili ya kuanza kujiajiri kuanzisha kitu kidogo tu, lakini kuna watu kwenye halmashauri zetu wamejilipa pesa. Pesa ambazo hazina idadi wamejilipa na ikithibitika kwamba wameiba wanaambiwa warudishe taratibu kwa muda ambao haueleweki ni muda gani. Hii naiona kama ni mikopo ambayo mtu anaamua kujipa isiyo na riba, isiyo na muda siku akiamua kumaliza kulipa anajilipa. Hii sio haki na haikubaliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia sisi kama Wabunge, Madiwani na Mheshimiwa Rais hatutakubali mwaka 2025 tusulubiwe na wananchi kwa sababu hatujaweza kutatua changamoto zao, lakini fedha zilikuja na baadhi ya watu wali-*mismanage* fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hapana, hapana, hapana, hatutakubali. Ninachoomba ushauri wangu, Serikali

iangalie namna, ituletee mabadiliko ya Sheria katika Bunge hili na Wabunge najua ni wazalendo tutapitisha mabadiliko hayo, tuangalie upya mfumo wa uwajibikaji katika utumishi wa umma. Hatuwezi kuwa watu wanafanya makosa kama haya, viwango vikubwa vya fedha kama hivi tunaishia kuwapa onyo au kuwahamisha hapana. Kuna vijana wengi sana mtaani ambao wangeweza kufanya kazi hizi, ni wazalendo basi tuwaondoe watu hawa tuwape wale vijana kazi wafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupe mfano mdogo, leo hii tuna *project* ya vijana chini ya Wizara ya Kilimo, *building a better tomorrow* imepewa bilioni tatu tu kwa hatua ya mwanzo ya kuandaa hekari laki na sitini kutengeneza miundombinu kwa ajili ya kuwaweka vijana waanze kufanya kazi. Kama Shilingi Bilioni tatu inaweza kufanya kazi kwenye mikoa mitatu tu hizi Bilioni 20 tungepeka Tanzania nzima tungefanya nini kwa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wananchi wa kawaida kwenye Sheria zetu, *The Penal Code, Section* ya 265, mwananchi wa kawaida akikutwa na kosa la wizi *regardless* ya kiwango hata kama ni kuku, anapewa adhabu ya mpaka miaka saba kufungwa, lakini hawa watu wanaoiba kutumia *numbers,* wanaiba kutumia mifumo yetu, mabilioni ya fedha, tunawapa onyo na kuwahamisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haikubaliki. Naomba sheria ije tuifanyie marekebisho na kama inashindikana, kusiwe na *double standard;* basi na wananchi wanaoiba nao tuishie kuwapa onyo au waishie tu kuwashauri ili nao wawe sawa na sisi. Vinginevyo nasema fedha ya umma lazima itumike kuleta maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Vuma, halafu Mheshimiwa Geoffrey Mwambe na Mheshimiwa Francis Ndulane, wajiandae.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii nami niweze kuchangia kuhusu taarifa za Kamati ambazo ziko mbele yetu. Awali ya yote napenda kuishukuru Serikali kupitia Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Kilimo. Kama taarifa yetu ya *PIC* ilivyojieleza, tulipata nafasi ya kuwaita kwa ajili ya kufuatilia maazimio ambayo tuliyaweka hapa ya Serikali kulipa deni kwenye Sekta Ndogo ya Bodi ya Pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, waliweka wazi kwamba wanakamilisha uhakiki na wakasema mpaka kufikia mwezi wa tatu uhakiki utakuwa umekamilika na wataingiza kwenye mwaka wa bajeti unaokuja kwa ajili ya kulipa. Nawapongeza, lakini niseme tu Serikali ijipange ihakikishe kweli kwenye bajeti ijayo inaingiza deni hili la sekta ndogo ya pamba. Kwa nini? Kwa sababu sekta ndogo ya pamba imedorora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu ilipotokea ile patashika ya mwaka 2019, baada ya Soko la Pamba Duniani kucheza, na hatimaye watu wakaingiza mitaji yao kwa *promise* ya Serikali kwamba itaweza kutoa ruzuku, ukweli ni kwamba Serikali iliposhindwa kutoa ruzuku upatikanaji wa pembejeo umekuwa ni shida. Kwa sababu kuna deni la zaidi ya Shilingi bilioni 80 la pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wanunuzi wenyewe wamesinyaa kuendelea na shughuli hiyo, kwa sababu yako madeni makubwa ambayo ni zaidi ya Shilingi bilioni 100 Serikali inapaswa kulipa ili kuhakikisha kwamba sekta ndogo ya pamba inaendelea kustawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye taasisi yetu, Shirika la *TANAPA*. Jambo la kwanza, Hifadhi ya *TANAPA* labda kwa uelewa tu, awali ilikuwa na hifadhi 16 ambazo zina kilomita za mraba zaidi ya 57,000. Zikaongezeka mwaka 2019 kama sikosei, zikaongezeka hifadhi sita ambazo zina kilomita za mraba 47,000. Ikafanya jumla ya hifadhi zote zikawa 22 ambazo zina kilomita za mraba zaidi ya 100,004.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni ongezeko zaidi ya asilimia 45. Cha kushangaza sasa, badala ya Serikali kuwa inaongeza fedha za maendeleo na matumizi ya kawaida, imekuwa inazipunguza kila mwaka. Cha ajabu hicho! Ukiangalia kwa mfano, kuanzia mwaka 2019 zilipoongezeka hifadhi sita mwaka 2019 Serikali ilitenga shilingi bilioni 70 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwenye Shirika la *TANAPA*. Mwaka uliofuata wakapunguza shilingi milioni 500, yaani ikawa ni shilingi bilioni 69.5. Mwaka uliofuata wakapunguza zaidi wakatenga shilingi 64,500,000,000/=. Mwaka huu tulionao wamepunguza zaidi, wametenga shilingi bilioni 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unafikiria, ni kitu gani hiki? Yaani umeongeza ukubwa wa kazi kwa *TANAPA* kutoka hifadhi 16 mpaka 22 ongezeko la zaidi ya asilimia 45, badala uwaongezee fedha, wewe unapunguza. Mimi sijui tunafanya kitu kitu hapa! Ni kituko ambacho hakivumiliki. Wamekuja kwenye Kamati wanalialia pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima Serikali ichukue hatua. *TANAPA* tuna kila sababu ya kuiongezea fedha. Kwanza, ni taasisi za kimkakati. Hawa wanasimamia zaidi ya asilimia 11 ya eneo la nchi yetu. Bwawa la Mwalimu Nyerere liko chini yao pia. Kuna Askari zaidi ya 120 ambao wanalinda pale Bwawa la Mwalimu Nyerere. Wanaimarisha ulinzi na usalama. Hawa hawana nyumba za kulala, hawana usafiri wa uhakika. Bwawa ambalo lina matrilioni ya Shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, *TANAPA* tunajua imeajiri Watanzania wengi sana; tunajua *TANAPA* ni chanzo cha mapato kwa Serikali; tunajua *TANAPA* kupitia hifadhi zake na shughuli zake ni chanzo kikubwa cha fedha za kigeni; pia *TANAPA* inalinda urithi wetu na utambulisho wetu kupitia mbuga zetu mbalimbali na vivutio vya kiutalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba tuna kila sababu ya kuongezea fedha shirika hili. Kama tunaihitaji *TANAPA* kwa maana ya hifadhi zake ziendelee kuwepo, urithi wetu uendelee kuwepo, utambulisjho wetu uendelee kuwepo, tuendelee kupata mapato, ajira za Tanzania, tuendelee kusimamia kikamilifu hii asilimia 11 ya nchi yetu, lazima tuwaongezee fedha *TANAPA* ili waendelee kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TANAPA* mahitaji yao; tuliwahoji siku ile walivyokuja kwenye Kamati. Wao wanaomba fedha za maendeleo shilingi bilioni 120 kwa ajili ya vifaa vya maendeleo. Wanaamini wakipata fedha hizi watafanya miradi mikubwa ambayo itaboresha sana mazingira ya hifadhini na hatimaye kuongeza watalii kwa kiasi kikubwa sana. Hata hivyo, wanahitaji zaidi ya shilingi bilioni 220 kwa sababu tumewaongezea eneo la kufanya kazi zaidi ya asilimia 45. Wanahitaji shilingi bilioni 222 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashindwa kuelewa, yaani Serikali kupitia Mheshimiwa Rais, amefanya kazi nzuri sana ya ku-*promote* utalii wa nchi hii kupitia *Royal Tour* na watalii wameongezeka kweli kweli, wanatiririka kweli kweli! Tume-*overcome* hata ile *challenge* ya *Covid,* imeisha na watalii wanazidi kuja kutokana na *initiative* ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya kupitia *Royal Tour.* Sasa Watendaji wa Serikali wanashindwa vipi kuhakikisha kwamba wanaweka mazingira

mazuri ili hao watalii wakija wakutane na mazingira ya kisasa zaidi ambayo ni rafiki, wazidi kuja Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Wabunge wote, naomba sana tuweze kuungana kuibana Serikali kwa kuishauri iongeze fedha kwa ajili ya *TANAPA* ili *TANAPA* wawe na uwezo wa kusimamia na kuendesha hifadhi zake vizuri kwa ajili ya maslahi mapana ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana *TANROADS* kwa kazi nzuri sana ambayo wanayoifanya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa mchango mzuri, muda wako umekwisha.

**MHE. VUMA A. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Geoffrey Mwambe, halafu Mheshimiwa Ndulane na Mheshimiwa Dkt. Kikoyo wajiandae.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza napenda kuunga mkono hoja za Wenyeviti wa Kamati zote tatu ambao wamewasilisha hapa Bungeni siku ya leo. Hata hivyo, naomba nichangie kwenye baadhi ya maeneo nikiwa kama Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali *PAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba jukumu tulilonalo kama Bunge ni usimamizi wa Shughuli za Serikali ikiwa ni pamoja na kushauri pale ambapo panawezekana. Kwa hiyo, naomba niwe na maeneo ya kushauri kutokana na *observations* ambazo nitazifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujikita zaidi kwenye taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali kutokana na ufinyu wa muda ili angalau niwe na mchango fulani wa kutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwenye nchi yetu na bahati nzuri Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamezungumza hapa, kwamba tuna kiu kubwa ya maendeleo kwenye nchi yetu. Pia, tuna changamoto kubwa sana ya ajira kwa vijana. Vijana tunao wengi na tuliahidi kwenye ilani CCM kwamba tutatengeneza ajira zisizopungua milioni nane kufikia mwaka 2025. Hata hivyo, tumejiainisha kupitia Ilani ya CCM kwamba tutaenda kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya yote ambayo tumeyafikiria na tumeyapanga yatawezekana tu kama maeneo mawili makubwa ndani ya Serikali tutaweza kuyafanyia kazi. Kwanza ni kutengeneza mapato ya kutosha. Kuhakikisha kwamba tunakuwa na mapato ya kutosha kwa Serikali yetu kuweza kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ni la msingi pia ni kudhibiti matumizi yasiyo sahihi na kuchukua hatua kali kwa wote ambao wametumia vibaya fedha za Serikali. Sasa nataka niguse maeneo machache tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kuhusiana na miradi ya maji ambayo imekaguliwa. Mwenyekiti wa Kamati amezungumza hapo kwamba kuna matatizo makubwa ambayo tumeyaona ndani ya miradi ya maji. Hii ipo kwenye eneo pana la utambuzi wa mradi, *designing* ya mradi na utekelezaji wake. Inaonekana kama hatuna *National Water Supply Master Plan.* Ni kama tunabahatisha tu kulingana na vyanzo vidogo vidogo ambavyo tunavipata kwenye maeneo

ili tu-*address* tatizo kwenye maeneo kule. Matokeo yake tunajikuta tunatumia fedha nyingi za Serikali kufanya miradi midogo midogo ambayo siyo endelevu, na hata mingine inapelekea kuwa chanzo cha uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba tuwe na *Master Plan* ya Kitaifa, tuainishe vyanzo vikubwa, vichache, na tupeleke fedha kwa ajili ya kwenda kuibua miradi ile mikubwa na kusambaza maji kwenye maeneo yote kupitia miradi mikubwa kuliko miradi hii midogo midogo ambayo tunatumia pesa nyingi ambayo siyo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, tuna Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini pale chini tuna Kijiji cha Mlalo, *Lower* Rufiji, maji yanapoelekea Baharini kutoka kwenye Bwawa, ni maji ambayo tayari yameshatumika kwenye Bwawa. *Designing* ambayo inafikiriwa kufanyika sasa hivi ni kutoa maji pale, kupeleka Kibiti, Ikwiriri, Mkuranga Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tulifikiri kwamba ilitakiwa ifanyike *comprehensive designing* ili kuwe na *Northern Circuit* au *Northern Zone* na *Southern Zone* ili maji yale ya Bwawa la Mwalimu Nyerere pia yaweze kuelekezwa kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara, ili kuhakikisha kwamba tunatatua kabisa tatizo la ukosefu wa maji Lindi na Mtwara, kwa sababu tu tunacho chanzo cha uhakika wa maji kwa upande wa Rufiji. Kwa hiyo, tukifanya hivyo itatusaidia sana kupunguza gharama na pia kuwa na vyanzo vya uhakika vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile miradi mingi imetekelezwa ikiwa na *variations* nyingi. Tunalazimika kulipa fedha nyingi kutokana na usimamizi mbovu na uwajibikaji mdogo wa watumishi wa umma kusimamia hii miradi. Hii

tumekuwa tukiizungumza sana na kwa kweli labda tujaribu kufikiria kama Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maswali yetu ambayo tulikuwa tunawahoji hata Maafisa Masuhuli, tulikuwa tunawauliza, hii *business as usual, comfort zone* ambayo watumishi wa umma wanayo na kinachoitwa *security* kwa watumishi wa umma kwamba huwezi kufukuzwa kazi kirahisi ndani ya Serikali, tuendelee nayo au twende kwenye ajira za mikataba ambayo ni *performance based?* Kwamba ukisababisha hasara kwa Serikali, unaondoka. Kuliko ilivyo sasa wako kwenye *comfort zone,* kumfukuza mtumishi ni kazi ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuliangalia eneo la uingizaji wa mapato. Kwenye kuingiza mapato, tuliangalia eneo la utalii, bahati nzuri Mheshimiwa Vuma amezungumza hapa, ingawa tutatofautiana naye kidogo kwa jinsi ambavyo tulikuwa tumeona sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya mahojiano na watu wa utalii wakiongozwa na Afisa Masuhuli wa Wizara ile, tulibaini kwamba hawana mkakati wa wazi wa kukuza utalii kwenye eneo letu. Pia kuna ushirikishwaji mdogo au uratibu mdogo ndani ya Serikali na sekta ya utalii na sekta nyinginezo ambazo shughuli zao kwa namna moja au nyingine zinaathiri shughuli za utalii. Kwa hiyo, tulikuja kuona kwamba hata wakiomba bajeti, unawapa kwa ajili ya kazi ipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Tanzania ni ya pili baada ya Brazili kwa kuwa vivutio vingi vya utalii; kuanzia utamaduni *(culture)*, mpaka vivutio vyenyewe vya kwenye mbuga. Tuna kila kitu; ukienda kwenye *beach tourism,* kwenye kila kitu, lakini idadi kubwa ya watalii ambayo

tumewahi kuipata ni watu milioni moja laki tano sijui na ishirini na mbili elfu sijui na ngapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni idadi ndogo mno ukilinganisha nchi kama ya Ufaransa ambayo imeweza kuingiza watu milioni 89.4 kwa mwaka; ukienda Hispania imeweza kuingiza watu milioni 83.7 kwa mwaka; ukienda Marekani milioni 79.3 kwa mwaka ambao hawana kabisa vivutio kama tulivyo navyo sisi, lakini wameweza kuvutia watu mamilioni kwa mamilioni. Sisi tumevutia watu milioni 1.5, tena hao milioni 1.5 kuna *double counting* humo ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna *conference tourism*. Kuna watu wanakuja tu kwenye mikutano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, wanahesabika kwamba ni watalii. Wanakuja kwa ajili ya mikutano ya *SADC,* wanahesabika kama ni watalii. Sasa hivi *JKCI* tunatibu watu. Watu wanatoka Malawi wanakuja kutibiwa pale *JKCI* Muhimbili, nao tunawahesabu kwamba ni watalii. Ni watalii wangapi wametokana na mipango hasa ya Wizara ya Utalii na *implementation* yake katika eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni maeneo ambayo tungeweza kuingiza fedha za umma ambazo siyo za kikodi *(non-tax revenue)*. Ni *public asset* ambayo tunayo na hatuitumii. Kwa kweli tunasikitika kwamba tunavyo vyanzo kabisa vya kuweza kuingiza fedha, lakini hatuvitumii kuingiza fedha. Hii inapelekea *pressure* kubwa kwa Waziri wa Fedha, inabidi ahangaike kutafuta mikopo. Mikopo ya sasa hivi, *concession loans* zinapungua na *non-concession* zinaongezeka, ambapo baadaye tutakuja kutengeneza *burden* kubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tuna vyanzo vya uhakika vya kuongeza fedha ambazo ni *non-tax revenue*

ambazo ni za kwetu. Mungu ametujalia hivi vyanzo vya kutuingizia kipato kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda kusisitiza kwamba sisi kama Bunge tuitake Serikali kuangalia upya mifumo ya usimamizi wa shughuli za Serikali ikiwemo watumishi wa umma. Watumishi wa umma hawawajibiki ipaswavyo. Tumelipa *variations* nyingi kwenye miradi ni kwa sababu tu kuna mtumishi mmoja au wawili hawakusaini *GN* mapema, basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi ule wa *Terminal Three*, wakati tunaangalia Viwanja vya Ndege, tumemlipa *BAM* ile *construction company ya Netherland* faini ya Dola milioni 20 baada ya ku-*negotiate*. Walimtoza Dola milioni 50, ambayo ni sawa sawa na Shilingi bilioni 54 kwa sababu tu ya uzembe wa mtu mmoja au wawili walioko pale *TRA* na hazina kupitisha *GN*. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri. Ahsante sana.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane, jiandae Mheshimiwa Kikoyo.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika mjadala huu wa leo. Kwanza napenda nimpongeze *CAG* kwa kufanya kazi nzuri ya kukagua Halmashauri zetu katika ukaguzi maalum ambao ulifanyika mwezi Mei hadi Julai,

mwaka 2021. Kwa hakika *CAG* ametufungua macho. Kama tafsiri halisi ilivyo, lile ni jicho letu sisi Wabunge na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla. Kwa hiyo, ameifanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama walivyotangulia kuzungumza wazungumzaji wenzangu waliochangia hii taarifa ya *LAAC*. Kwa ujumla kuna madudu mengi sana yameonekana katika ule ukaguzi maalum uliofanyika mwaka 2021, lakini hatua hazijachukuliwa. Ukienda pale katika Halmashauri hizo nne ambazo zilifanyiwa ukaguzi maalum; Halmashauri ya Ubungo, Kigamboni, Ilemela pamoja na Iringa *DC,* kuna karibu Shilingi bilioni tisa ambazo zimevuja kutokana na miamala kufutwa kinyume cha utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ukienda kwenye suala la ubadhirifu wa fedha za umma kutokana na matumizi ya fedha kabla ya kuzipeleka benki, yaani fedha mbichi, kuna shilingi milioni 858, Halmashauri nne tu.Kwa hiyo, kuna shida katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilicho kibaya zaidi, pale katika Halmashauri ya Ilemela ule mfumo sijui ukoje! Kwa sababu imefikia hatua watumishi waliohama wamekuwa na wale ambao wamestaafu wamekuwa na *access* ya kuingia kwenye mifumo. Pia hii inaonesha namna gani mifumo yetu haiko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu nilikuwa naiomba Wizara yetu ya TAMISEMI inapokuja na mfumo mpya wa TAUSI, baada ya kuachana na ule wa *LGRCIS,* izingatie suala la *security* ya hii mifumo. Inaonesha mifumo yetu haiko madhubuti kwenye *security*. Tusije tukarudia makosa. Haya makosa yaliyojitokeza yawe fundisho kwetu ili tunapotengeneza ile *database* ya Mfumo wa TAUSI, basi iwe madhubuti makini katika ku-*trace* makosa mbalimbali

ambayo yatafanyika ikiwemo haya ya watu ambao wamehama au kustaafu kuweza kuingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo ningeomba wizara ya TAMISEMI ifanye kazi kwa karibu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningeiomba TAMISEMI ifanye kazi kwa karibu sana na hizo Halmashauri zetu, kuna wakati niliwahi kusema kwamba *CAG a*napofanya ukaguzi ni kama vile mvuvi ambaye anakuwa anavua kwa njia yile ya kokoro. Kwa hiyo, ndani ya zile hoja zinapotengenezwa unakuta kuna mapendekezo yanahitaji utekelezaji wa Wizara ya TAMISEMI nyingine Sekretariati za Mikoa, nyingine Halmashauri zenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hakuna muunganiko mzuri wa kujibu hizi hoja tutaendelea kupigwa kila siku na mwisho wa siku hizi hoja zitabaki zinaelea hazijibiki. Kwa hiyo, ninaiomba TAMISEMI kwanza ichukue hatua dhidi ya wale wote waliohusika na hizi changamoto, kwa sababu imeonekana tangu mwaka juzi ukaguzi ulivyofanyika na hizi taarifa zikawasilishwa Wizara ya TAMISEMI na kule kwenye Halmashauri zetu mwezi Septemba hatua madhubuti hazijachukuliwa kuwadhibiti hawa Watumishi ambao wamefanya huu ubadhirifu. Hii inaonesha kwamba ni kwa namna gani TAMISEMI imetengeneza *gap* kati yake na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba TAMISEMI tumieni nafasi yenu kwa sababu hizi hoja ni mtambuka, zingine zinahitaji utekelezaji wa moja kwa moja na TAMISEMI, kama haya masuala ya kinidhamu chukueni hatua na mchukue hatua haraka. Mna-*premises* nyingi hapa Dodoma, mnaweza mkaziita zile Halmashauri husika, mkakaa nazo mkajadili kwa pamoja ili hoja ambayo inahusika na TAMISEMI utekelezaji wake unatakiwa utekelezwe na TAMISEMI kama uchukuaji wa

hatua zile za kinidhamu, basi chukueni hatua haraka ili kudhibiti vitendo hivi vya ubadhirifu wa fedha za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalia kila siku mapato ya Halmashauri ni madogo lakini udhibiti ukifanyika basi mapato yataongezeka. *Securit*y zikiongezeka kwenye mifumo yetu tutajikuta tayari mapato yetu yanaweza kulindwa na kuweza kutumika kwa ajili ya shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika. vilevile kumekuwa na changamoto kubwa kwenye manunuzi, imefika mahali kule kwa mfano kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, hospitali inajengwa vifaa vinapokelewa, vinaonekena vimezidi hata idadi ya vile vifaa vilivyokuwa vinatakiwa. Sasa hii inatokeaje? Ni ukosefu wa kuzingatia Kanuni na Sheria ya Manunuzi. Kwa hiyo, ninaiomba TAMISEMI pamoja na Sekretariati zichukue majukumu yake ya kuzilea hizi Halmashauri pia kuchukua hatua pale inapoonekana kwamba kuna shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa nyingi inakwenda kwenye manunuzi, matumizi ya fedha za Serikali sehemu kubwa inakwenda kwenye eneo la manunuzi, ndiyo maana nafikiri huyu *CAG* amezingatia sana hayo maeneo hayo muhimu, kwa hiyo niombe Serikali isimamie vizuri hizi Halmashauri ili hatua zichukuliwe kwenye maeneo yote ambayo yanaonekana taratibu hazifuatwi lakini kuna ukiukwaji mkubwa wa taratibu za mapato na mambo mengine ambayo yanafanyika kule kwenye Halmashauri ili kuondoa haya madudu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, jiandae Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Jeremiah Amsabi.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PIC* ambayo iko chini ya Msajili wa Hazina. Msajili wa Hazina anayo Mashirika zaidi ya 230 ambayo Serikali yetu imewekeza mtaji wa zaidi ya trilioni 67.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa taasisi hizo yapo makampuni ambayo Serikali yetu ina hisa chache mojawapo ni kampuni ya *TANICA* ambayo iko Mkoani Kagera. Namshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa aliyoifanya kuhakikisha kwamba anaboresha zao la kahawa Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi ambazo Waziri wetu Mkuu alizifanya Kagera ningeomba ziende sambamba na kuboresha Kiwanda cha *TANICA* Mkoani Kagera. Nashukuru sana Kiwanda cha *TANICA* kagera ambacho Serikali yetu inamiliki hisa asilimia Saba, *TANICA* kilijengwa mwaka 1963 kwa hiyo teknolojia iliyojenga kiwanda hicho nyakati hizi, hiyo teknolojia haipo imepitwa na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema tunaboresha kilimo lazima twende sambamba na kujenga viwanda ambavyo vitaongeza thamani ya mazao ya mkulima. Mkoa wa Kagera unazalisha zaidi ya tani 34,000 za kahawa lakini kiwanda hiki ambacho Serikali ina hisa asilimia Saba kinaweza kikaongeza thamani asilimia mbili tu ya kahawa inayozalishwa Mkoani Kagera. Ndiyo maana kila mwaka Serikali inatumia nguvu sana kuweza kupambana na magendo ya kahawa kwa sababu wakulima hawana soko la uhakika la kuuza kahawa yao. Kama Serikali ingeongeza mtaji kwenye kiwanda suala la kukimbizana na kahawa au magendo ya kahawa Mkoani Kagera ingebaki historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *TANICA* ambacho Serikali ina hisa chache, kina mtaji wa bilioni kumi lakini *share* ambazo zimelipiwa ni bilioni moja na milioni mia nne tu, zaidi ya bilioni 8.6 hazijalipwa. Nakumbuka mwaka jana tulikuwa na Kamati Teule chini ya Viwanda na Biashara, ambayo ilifanya tathmini ya hiki kiwanda na ikatoa mapendekezo kwamba Serikali kutokana na umuhimu wa hicho kiwanda cha *TANICA* Mkoani Kagera ilipe lile deni la shilingi bilioni 8.6 ili Serikali iweze kumiliki hisa nyingi zaidi kwenye hicho kiwanda na iweze kukipatia mtaji kusudi kiweze kuongeza thamani mazao ya kahawa Mkoani Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwenye hili pamoja na viwanda vingine ambavyo vinaendeshwa chini ya mtaji wake, maana yake vinazalisha chini ya viwango, Serikali itafute pesa iviongezee mtaji ili viweze kuzalisha kwa kiwango kinachotakiwa. Kwa kusema hivyo, tutakuwa tumewasaidia wakulima wetu ambao wanazalisha kwa wingi na wakati mwingine tunakosa masoko kwa sababu hatuna viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao tunayozalisha nchini, kufanya hivyo tutakosa pesa ya nje ambayo tunahitaji sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema kuongeza mitaji kwenye viwanda, tumesikia kwenye Kamati ambazo zimesoma ripoti za leo, pesa ambayo inaibiwa kama tutaweza kuithibiti tunaweza ikatusaidia kuongeza mitaji kwenye viwanda ambavyo vinahitaji hizi pesa nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili haya Mashirika ambayo yako chini ya Msajili wa Hazina yanaendeshwa chini ya sheria na utaratibu ambao tumeuweka sisi wenyewe. Lakini cha kushangaza Sheria ya Msajili wa Hazina ni sheria ambayo ilitungwa mwaka 1959, nchi hii kabla haijapata uhuru, lakini bado tunatumia sheria kongwe ya namna hiyo kuendesha uchumi, kuendesha mashirika 237, yenye mtaji wa trilioni 67 kwa kutumia sheria kongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia utajiri ambao tunao kwenye haya mashirika ambayo tumesema trilioni 67, kama tungekuwa na sheria ya kisasa ambayo inampa nguvu na uwezo Msajili wa Hazina, tungekuwa na utajiri zaidi ya hapo labda zaidi ya mara mbili.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana niliongelea hili kwamba Sheria ya Msajili wa Hazina imepitwa na wakati, ni muda muafaka sasa tuifute na tutunge sheria mpya ambayo inalingana na uchumi wa sasa lakini ambayo itampa nguvu na mamlaka Msajili wa Hazina ili aweze kuchukua hatua pale ambapo inahitajika kuhakikisha kwamba Watendaji wa Mashirika haya ambayo ni ya umma pale ambapo anawapa vigezo *KPI* wanashindwa kuvitekeleza, pale ambapo mashirika hayana bodi lakini Msajili yupo amebaki tu kama Mshauri, ni muda muafaka sasa kumpatia nguvu, kumpatia meno ili aweze kuyawajibisha mashirika haya ambayo yanasababisha hasara, ambayo hayazalishi, na ambayo yanafanya chini ya viwango lakini kwa sasa kwa sheria tuliyonayo hayo mamlaka hana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia mashirika haya ambayo yanazalisha mali ni mfumo wa kampuni na mengine Mashirika ya Umma, mengi Serikali imewekeza lakini ukiangalia tija tunayoipata ni ndogo mno, kwa maana hiyo naomba nishauri Sheria ya Msajili wa Hazina iletwe Bungeni ifanyiwe kazi na kwa ushauri wangu ifutwe na tutunge sheria mpya na ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Deus Clement na Mheshimiwa Jeremiah Amsabi ajiandae.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa fursa hii na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye taarifa zilizowasilishwa hapa. Kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono hoja kwa Kamati zote tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nitaanza kwanza ku-*recall* katika Bunge la Bajeti ndani ya Bunge hili, tulipisha fedha nyingi zilizoenda kwenye Wizara ya kilimo ambayo inaenda takribani Bilioni 954. Kati ya fedha hizo asilimia 35 inaenda kwenye sekta ya umwagiliaji, tunatamani na Wabunge tunaamini kwamba fedha hizo zilizopitishwa zinaenda kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitarudi nyuma mwaka 2018/2019 *CAG* alifanya ukaguzi kwenye miradi Tisa ya umwagiliaji, ambayo ilifanyika chini ya Wizara ya Kilimo, Wizara ya Kilimo ilikuwa inasimamia miradi miwili na miradi Saba ilikuwa chini ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Alikutana na mambo mengi ya ajabu na hii itupe fundisho kwamba tunapoenda kutekeleza miradi ya umwagiliaji tuliopewa pesa Bilioni zaidi ya 300 tupate somo kwa miradi hii ambayo imefanyika na imepelekea Taifa hili hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na miradi ile miwili ule wa Msolwa pamoja na Kingali iliyofanyika chini ya Wizara ya Kilimo. Ile miradi ilikuwa na mambo mengi ya ajabu. Kwanza Msanifu aliyepewa kusanifu alipewa kazi hajaona *site,* ni mtu aliyepewa kazi akiwa ofisini, mradi wa shilingi milioni 835 na baadae akaleta ripoti, ripoti ile alipowaletea wataalam Wizarani hawakufanya uhakiki, moja kwa moja wakaingia *field* na baadae akawaletea yeye binafsi kwa kufanya kazi ile v*ariation* ya karibia asilimia 58. Kwa hiyo, kutoksa milioni 835 alienda kulipwa zaidi ya bilioni moja na milioni mia tatu. Kwa hiyo, ikawa *variation* ya asilimi 56 na hiyo ni kinyume na Sheria ya Manunuzi iko-*very clear*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Manunuzi ili uweze kufanya v*ariation* ni *plus fifteen or minus fifteen* kwa maana *fifteen percent* kama unaongeza na kama unapunguza ni *fifteen percent*. Nje ya hapo *scope* hiyo haipo rudia upya tangaza tenda upya maana yake ni kitu kizima. Kwa hiyo, watu hawa wakafanya maksudi wakaingiza Serikali hasara kubwa!

Mheshimiwa Naibu Spika, hawakuishia hapo huyu mtaalam mwelekezi hakufanyiwa *due diligence,* katika *application* yake aliambatanisha *CV* za wataalam lakini kumbe wale wataalam ilikuwa ni gelesha, walioenda kufanya kazi *actual field* hawakuwa wale walio-*submit* zile *CV*. Kwa hiyo ilikuwa ni kuwa-*fix* wale watu wa *evaluation* wamu-*award tender* wakishamu-*award* wanaoenda ku-*perform* ile *contract* kwenye *field* ni watu wengine ambao ni makanjanja, haya mambo yamefanyika kwenye miradi ya umwagiliaji ambayo pesa ile pia ilikuwa ni mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikopo inakopwa kuja kufanya kazi za maendeleo, kuna watu wajanja wanajiita wataalam wako huko Wizarani. Juzi nimekuona Mheshimiwa Bashe uko huko Ruvuma tayari wameshaanza kukuchezea, tayari Mkandarasi mwaka huu fedha hizi ameenda kufanya madudu Ruvuma na ume-*terminate contract!* Hiyo ni *postmortem* hatutakiwi kufanya *postmortem,* kuanzia *stage* ya kwanza tunapoanza *initial procurement proceedings* lazima tuhakikishe kwamba kuna *compliance (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutaenda kwa staili hii ya kufanya *postmortem* ya ku-*terminate contract* tutaliingiza Taifa hili hasara kubwa sana. Huyu mtu hajafanyiwa *due diligence* na *average* ya mikataba yote imechukua muda mrefu sana zaidi ya siku 450 amezidisha kwenye ku-*implement* huu mradi, leo hii tumepitisha kwenye Bunge hili tuna miezi 18,

sitarajii baada ya miezi 18 tuje tuanze kufanya *the same postmortem* ndani ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, huku ndiyo tunaona Watanzania wote kwenye kilimo kwenye umwagiliaji hawakuishia hapo wameendelea miradi mingine mitatu waka-*award contract* walivyo-*award contact* Tume hii ya Taifa ya umwagiliaji baadae wakasaini mkataba na Wakandarasi hawa watatu, walivyosaini mtakaba kesho yake wasema hatuna fedha tuna-*terminate* hizi *contract*. Sasa kuna *litigation issue, legal status* ya mambo haya iko wapi? Mtapelekwa Mahakamani kama Wizara! Kama mlijua hamna fedha nani aliwatuma mkatangaze tenda na Sheria ya Manunuzi iko *very clear (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hautakiwa ku-*initiate procurement proceedings* kama hamna *availability of budget, full stop*. Sasa mlienda sijui wapi. Baada ya muda mfupi wakatangaza tena upya, kuna *Tender Board* zinakaa hapo ni *cost* za walipakodi tena Wizara maskini kama Wizara ya Kilimo ya watu ambao ni wanyonge, mnakaa *Tender Board* mna-*award* mnasaini mikataba na mikataba kwa sababu ni mikubwa ni ya Mabilioni inaenda mpaka kwa *AG*. *AG* naye kule anaenda kufanya *vetting* inarudi mnakuja pale kwamba sisi tume tume-*cancel* kesho tunatangaza upya tenda! Taifa hili linachezewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawakuishia hapo, baada ya ku-*award* wameendelea na michezo hiyo wakawa-*award* tena Wakandarasi wengine mikataba mitatu iko hapa, walivyowa-*award* wale watu hawaku-*perform* wakashindwa, Tume ikasema kwamba basi jamani, safi ninyi ni Watanzania meshindwa tupeni, wakaenda kufanya kwa *force account* wakatumia tena fedha zilezile za Tume ya Umwagiliaji ku-*implement* miradi ile ile kwa *force account* wakati kuna Mkandarasi walimpa. Hatujawahi kusikia kwamba

Mkandarasi alipelekwa Mahakamani kwa ajili ya *liquidated damages,* hatujawahi kuona kwamba kuna hatua zozote kali zimechukuliwa, *business as usual,* maisha yanaendelea tumepewa Bilioni 300, na nampa *alert* Mheshimiwa Bashe hatutaki tena baadae story kama hizi. *(Makofi)*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mzuri anaoendelea nao kuzungumza mzungumzaji, nilitaka nimpe tu taarifa kwamba changamoto unayoiona sasa hiyo kwenye Tume ya Umwagiliaji Fungu 05, tayari kwenye fedha za *ECF* nilizokuwa nazizungumza wamepewa bilioni 215, sasa changamoto ikija hiyo sasa sijui kama tutaendelea kupewa zile Awamu Sita zilizobakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hiyo tu taarifa niliyokuwa nampa *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deus.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa. Leo sina mambo mengi nilikuwa mime-*focus* tu kwenye Tume ya Umwagiliaji na rafiki yangu Mheshimiwa Bashe Waziri wa Kilimo, umenipa mradi mkubwa nashukuru lakini jambo hili tusimame pamoja tukaisimamie hii Tume ya Umwagiliaji. Nakuamini sana, nakuomba sana pesa zote wanachezea huku tunapiga kelele sawa, mmefanya *reshuffle* mmemuweka *MD* mpya na nini. Tunaomba muende mpaka chini, wataalam Maafisa Manunuzi wadogo mnawaacha ………*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deus ahsante muda wako umekwisha, sasa namuita Mheshimiwa Jeremiah Amsabi na Mheshimiwa Dkt. Pallangyo ajiandae.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote naunga mkono hoja ya Kamati zote tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kwa kutafuta fedha na kupeleka fedha nyingi sana za maendeleo katika Halmashauri zetu. Kwa kweli hii ni kazi kubwa sana amefanya na kushirikiana na Serikali. Bado tunaona wako baadhi ya watumishi katika Halmashauri zetu ambao wanaturudisha nyuma kutokana na utendaji wao wenye madhaifu makubwa pamoja na vitendo vinavyotia shaka katika matumizi ya fedha hizi zinazoenda katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitolea mfano, pesa ambayo ilipelekwa katika ujenzi wa Vituo vya Afya karibu nchi nzima Shilingi Milioni 500, sasa hivi ukizunguka katika vituo vingi hivi havijakamilika. Vingi vimebaki tu majengo yako hapo, pia ukiangalia pembeni unakuta baadhi ya majengo utaona kuna vifaa vya ujenzi ambavyo vilikuwa vimenunuliwa vimebaki na hatua hiyo imeshapitwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii sasa inaleta mashaka, wanachi wengi wanafika mahali wanaitilia mashaka Serikali yetu na wanafikia mahali ambapo hawaiamini Serikali yetu. Sasa baadhi madhaifu ambayo yanaonekana katika kazi hizi kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja; halmashauri nyingi zimeingia katika ujenzi wa majengo haya pasipokuwepo na *quantity surveyors*. Kwa hiyo, unaona *BOQ* nyingi ambazo zinaandaliwa, hazijaandaliwa na *quantinty surveyors*. Sasa mwisho wa siku jengo linafikia mahali halikamiliki ukiuliza wanasema hatukuwa na *quantity surveyors*. Sasa je, ni kwanini Serikali isitumie *quantinty surveyors* ili kuwa na uhakika wa gharama ya kujenga jengo hilo, badala yake tuanjenga na tunafikia mahali ambapo tunakwama na jengo halijakamilika, tunasema pesa hakuna?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunajenga tunafikia mahali vifaa vinabaki ambavyo havihitajiki tena na haviwezi vikatumika tena na ili hali tunasema kwamba hatukuwa na *quantity surveyors*? Inaigharimu shilingi ngapi hata kuweza ku–*outsource quantinty surveyor* ili tuweze kufanya kazi kwa uhakika?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia imeonekana kuwa watu wetu wengi wa manunuzi, kwa maana ya wale maafisa wa manunuzi, hawana *knowledge* ya kutosha katika *supply chain management*. Hivyo nitoe mapendekezo machache kwa ajili ya kuiomba Serikali iyafanyie kazi mapema ili tuondokane na changamoto hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja; tunaomba sasa majengo yote yanayojengwa katika halmashauri zetu tusiingie kujenga majengo haya pasipo kuwepo na *BOQ* ambayo imeandaliwa na *quantinty surveyors*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; hawa wataalam ambao wamesomea manunuzi, kila siku zinapoenda mtu anahitaji kuendelea ku-*upgrade* knowledge yake. Tunaomba hawa watumishi katika halmashauri ambao wanahusika na manunuzi wapatiwe *knowledge ya supply chain management*. Huwezi kukutana na habari ya *material* kubaki

katika *sites* kama tutatumia watu wenye *knowledge* ambayo ni *up to date*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini majengo yale ambayo yalijengwa katika halmashauri zetu na pesa zikaonekana hazitoshi yakiwemo majengo ya sekondari na majengo ya vituo vya afya, tunaiomba Serikali, kwa maana ya TAMISEMI, itenge pesa ili kukamilisha majengo yale kwa sababu sasa ni aibu kubwa sana katika maeneo yetu. Wananchi wanalaumu, wananchi wanalalamika na majengo yale yamekaa ilhali pesa nyingi ya Serikali imeenda pale na hakuna kinachoendelea. Naomba sana watu wa TAMISEMI watukumbuke pia katika kazi hii kule Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Dokta Pallangyo, jiandae Mheshimiwa Venant Protas.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kwenye hoja ambayo ipo mezani.

Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PIC*, Kamati ambayo ni mtambuka, kwa hiyo moja kwa moja niseme kwamba naunga mkono hoja zote tatu za *PIC*, *PAC* na *LAAC*. Pia, nichukue nafasi hii kupongeza sana Wenyeviti wetu kwa jinsi ambavyo wamewasilisha taarifa hizi; na kwa sababu ya ufinyu wa muda na mimi nitazungumza kwa kifupi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TANAPA*; kuna mwenzetu ameshalizungumzia lakini nongezee. Mwaka 2020 tulipitisha sheria hapa, Sheria ya Fedha Namba Nane ambayo ilipelekea makusanyo yote yanayokusanywa na mashirika haya ya uhifadhi kukusanywa na mamlaka ya

mapato. Pamoja na nia njema ya Serikali kuhakikisha kwamba haya mashirika hayaathiriki na athari za UVIKO – 19 ambayo ilisababisha kukawa na upungufu wa watalii nchini lakini hatua ile imefanya mashirika haya ambayo yanafanya kazi kwenye mazingira magumu ya porini kushindwa kutekeleza majukumu yake sawa sawa, hasa kwenye miundombinu ambayo kwa sababu ya hali ya mazingira huwa inaharibika haribika hasa kwenye barabara na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunashauri kwamba ili kutatua tatizo hilo Serikali iangalie namna ya kuwaruhusu wa-*retain*, kuwe na *retention* yale makusanyo wabaki nayo moja kwa moja bila ya kungojea kwenda kuomba fedha Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Dar es Salaam iliyopo chini ya Mamlaka ya Bandari ndilo lango kuu la uchumi wa *landlock countries* za DRC, Rwanda, Burundi, Uganda, Malawi, Zambia, Zimbabwe na Sudan ya Kusuni. Wingi wa shehena ambazo zinapitia pale bandarani zinafanya bandari hii inaelemewa. Sasa hivi Bandari ya Dar es Salaam inafanya upanuzi lakini bado upanuzi ule hautakidhi uzito wa kuelemewa na shehena ambazo zinapitia pale. Kuna mradi wa ujenzi wa Bandari Kavu Kwala ambao sahivi umefikia *percent* 98 kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashauri Serikali iharakishe na ihakikishe kwamba mradi ule unamalizika haraka kwa sababu bandari ile itakapoanza kufanya kazi itapunguza mzigo wa shehena pale bandarini kwa *percent* 30; lakini pia kuna mpango wa kujenga Bandari mpya ya Mbegani Bagamoyo ambayo sana sana itatumika kwa ajili ya kushushia makontena. Bandari ile nayo ni muhimu sana, hivyo mradi ule utekelezwe haraka ili kunusuru Bandari ya Dar es Salaam na kuifanya itekeleze majukumu yake kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya ufinyu wa muda, hayo ndiyo niliyokuwa nataka kusema. Niseme naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Venant.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe miongoni mwa wachangiaji katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja hapa leo kujadili ripoti tatu mbazo zote zinahusu usimamizi wa fedha za walipa kodi. Sisi kama Bunge anayetusaidia kwenda kwenye ukaguzi kwenye taasisi zetu na mashirika na halmashauri zetu zote nchini ni *CAG* ambaye kwa mujibu wa Katiba tumempa mamlaka hiyo kama Bunge, lakini na sisi Bunge tuna haki ya kuhoji na kuisimamia Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesimama hapa kama Wabunge kwa Kanuni mbalimbali za Bunge na sisi hapa tupo kwa niaba ya wananchi wa Tanzania nzima, kwa hiyo tunapoleta maoni yetu hapa si maoni ya sisi kama Wabunge tulipo huku ndani, ni maoni ya wananchi waliotutuma kuja kuwawakilisha. Kwa hiyo, tunaposema ubadhilifu wa fedha zinazotokea katika Serikali, mambo hayaendi sawa katika Serikali, si kama sisi Wabunge ndio tunayasema ni wananchi wanasema mambo hayaendi sawa. kwa hiyo tunaomba tueleweke kwa namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti zote za *CAG* kila mwaka tunapokuja hapa, hata hizi ripoti za Kamati za Fedha, hatuwezi kwenda hata siku moja tukasema Serikali hakuna sehemu ambapo tumepoteza au tumepata hasara. Kila siku tunapata hasara na hasara kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika mchango wangu nataka tuishauri Serikali; tuna miradi mikubwa ambayo Serikali inatafuta fedha, tuna Mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere ambao tunaweka matrilioni ya fedha, tuna mradi mkubwa wa *SGR*. Kama tusipoweka mipango madhubuti ya usimamizi wa fedha hata hizi fedha tutakuja tutakaguliwa tena tutaambiwa zimepigwa na bado Watanzania wataendelea kuumia. Katika ripoti ya *CAG* ambayo leo tumekuja kuijadili hapa, kuna changamoto kubwa ya riba ambazo tunalipa kwa wakandarasi; na hii yote inasababishwa na uzembe wa watumishi wetu katika Wizara na taasisi mbali mbali. Sasa wewe unakuta mkandarasi una mcheleweshea malipo mpaka siku 205, halafu tunakwenda kulipa the *deference* ya riba ya zaidi ya bilioni 11 halafu bado watu tunakuja hapa, mnasema kama hatuwezi tujadili masuala ya uganga wa kienyeji, tukae kimya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niwaombe Waheshimiwa Wabunge kama tusipojisimamia sisi wenyewe kuna siku hapa mtakuja mtukanwe na bado mtapiga makofi. Kwa hiyo, mimi niwaombe tunapokwenda kuishauri Serikali si kwa nia mbaya ni kuisaidia Serikali iweze kufanya kazi. Sasa waganga wa kienyeji tupo, sasa tunawapa mkeka. Wizara ya Fedha, hizi *variations* zote ambazo tunazisema; wakandarasi kulipwa kwa kuchelewa, tunakwenda kulipa fedha nyingi, zote zinasababishwa na Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *TAA* tu, nilikuwa napitia hapa ripoti ya *CAG*, kuna mkandarasi ambaye alipewa kutengeneza mitambo na mfumo katika Uwanja wa Julius Kambarage Nyerere. Alicheleweshewa malipo zaidi ya siku 216 tukalipa zaidi ya bilioni 13, tukijadili hapa tena unaambiwa kazi yetu kujadili waganga wa kienyeji. Bilioni 11 imekwenda lakini waliochelewesha ni Watumishi wa Wizara ya Fedha, *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini palikuwa na ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, mkandarasi amecheleweshewa malipo tukalipa bilioni 2.5, Wizara ya Fedha, lakini vile vile palikuwa na ucheleweshaji wa msamaha wa kodi ambapo kontena 223 zilikaa bandarini pale tukalipa tena mkandarasi *delay* ya kucheleweshewa msamaha wa kodi, zaidi ya bilioni 11. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujawahi kusema shilingi 10,000 shilingi 100,000 kila siku tunazungumzia mabilioni. Ni lini tutashuka kutoka kwenye bilioni kuja kwenye mamilioni, tuje kwenye maelfu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna miradi mikubwa ambayo tunaenda nayo, Mama yetu anajitahidi kuhakikisha miradi iliyoachwa inaendelea na inakamilika na imaleta tija. Kwa stahili hii miradi, tumekadiria Bwawa la Mwalimu Nyerere liishe kwa trilioni 6.5 ngapi huko litaisha kwa trilioni 8. Kama tusipodhibiti mapema kuzuia waganga wa kienyeji kudhibiti hizi fedha; kama mradi wa *SGR* tumehakikisha tutumie trilioni kumi na ngapi sasa zitaisha kwa zaidi ya trilioni 40. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niiombe Serikali, tunapokuja humu kuishauri Serikali watusikilize, ndiyo kazi yetu. Wananchi walijipanga mstari kwachagua wabunge kwa niaba yao kwenda kuwasemea. Sasa wanatozwa tozo wanavumilia. Hizo tozo ambazo wanajibana na familia zao leo tena zinakuja kuibiwa huku, eti sisi tuwe tumekaa. Sasa tuna maana gani ya kukaa kama Bunge? Basi ijulikane kuna mihimili miwili, Mahakama na Serikali, kazi iendelee, sie tukalime, Wizara imeongezewa bajeti ya kilimo, tukaongeze mashamba, uzalishaji watu wa mjini waje wapate…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango mzuri. Tutamalizia na Mheshimiwa Anatropia. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ya kuchangia machache kati ya yaliokuwa mengi yaliojiri kwenye Kamati yetu. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*. Tumetoa taarifa yetu, hayo ni baadhi ya mengi tuliyoyaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kuseme bado kuna changamoto kubwa ya *value for money* kwenye taasisi mbali mbali ambazo zinapewa fedha na Serikali. Taasisi nyingi au matumizi ya fedha yamekuwa si sahihi kwa sababu ya namna ambavyo haya mafungu, fedha zinavyotoka ina maana fedha kama haitoki kwa wakati, wakati mwingine inachelewesha kazi na hivyo Serikali kulipa riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia maeneo mawili, suala la kwanza ni mifuko ya uwekezaji ya wananchi kiuchumi lakini suala la pili, nitaongelea miradi ya maji, usanifu wa miradi ya maji; na hizi ni taarifa ambazo zipo kwenye Ripoti ya *CAG*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kuhusu mifuko ya uwekezaji wa wananchi kiuchumi. Katika taarifa ambayo ipo kwenye kishikwambi chetu, Mdhibiti ameonyesha ni kwa kiwango gani fedha zimetumika ndivyo sivyo; na kama hiyo haitoshi imetumika kwa watu wasiokuwa walengwa. Imesema *out of 99 bilion* ambazo zilitolewa ni zaidi ya bilioni 50.4 zilipigwa kwa maana ziliishia kwenye mikono ambayo haikuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kulikuwa na mifuko mitatu, mfano, mfuko wa pembejeo ambao ulitengewa bilioni 28, bilioni 20 zilipigwa ina maana kilichoweza kutumika ni bilioni nane tu ambapo ni sawa na zaidi ya asilimia 72

zilitumika ndivyo sivyo. Mfuko wa Kilimo Kwanza ambao ulitengewa bilioni 34, bilioni 28 zilipigwa au kutumika ndivyo sivyo, sawa na asilimia 80. Katika Mfuko wa *Self-microfinance out of* 34 ni bilioni 3.7 ambazo zilitumika ndivyo sivyo sawa na asilimia saba ya kile kiwango cha fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninasema haya, na kwa nini naongelea hizi fedha, ni kwa sababu hizi fedha zimetengwa kwa ajili ya kusaidia wale wafanyabiashara wadogo wadogo, wale watu ambao hawana *access* na maeneo ya benki. Takwimu zinaonyesha ni asilimia 28 ya…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaomba utulivu *please*, tunaomba utulivu.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nasema zaidi ya ailimia 28 ya Watanzania hawawezi ku-*access* fedha za benki, hawawezi ku - *access* mikopo. Kwa hiyo, hiyo mifuko ililenga asilimia 28 ya lile kundi la kundi la Watanzania ambalo haliwezi ku-*access fund,* kwa maana ya vikundi vidogo vidogo na watu ambao wana maisha ya chini. Kwa takwimu zetu leo ina maana ni zaidi ya watu milioni 17; na ukilinganisha na nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki, Kenya ni watu asilimia 18 ambao hawawezi ku–*access* fund, Uganda asilimia 14 na Rwanda asilimia 11. Kwahiyo, unaona kwamba Tanzania tuna asilimia kubwa ya wananchi hawawezi ku-*access fund;* na Serikali kwa maksudi ilianzisha mifuko na kuweka fedha ili ziweze kuwasaidia hawa watu kujikwamua.

Mhesimiwa Naibu Spika, nini kilichotokea? Kitu cha kwanza kilichotokea, wale ambao walipaswa kusimamia mifuko badala ya fedha hizo kupelekwa kwa wale

wajasiriamali na watu wanaohitaji fedha; katika tathmini au katika *study* walioifanya mwaka 2016 na 2017 zaidi ya *80 percent* ya zile fedha zilikuwa zimewekezwa benki au zimekopesha benki badala ya wajasiriamali wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si hiyo tu wamesema kwa tathmini ya 2017 mpaka 2021 zaidi ya asilimia 72 fedha zilienda ambako hazikupaswa kwenda. Kwa maana ya wajasiriamali, wale watu wadogo wadogo wakulima akina mama hawakuweza ku-*access fund*. Kwa hiyo tunaweza kuwa humu ndani tunapiga kelele tunaangalia tutawakwamua vipi wananchi kumbe kuna watu wamepewa mamlaka, watu wanakusanya fedha au watu wamekuwa *custodian* wa hzio fedha lakini wanazipeleka maeneo yasiyofaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nakumbuka kipindi fulani nikiwa Halmashauri ya Ilala vilikuwa vinatengenezwa vikundi vya mfukoni watu wanaenda wanakusanya fedha wanapiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na wameeleza na *CAG* ameeleza ni kwa nini hizo fedha zimepotea. Kwanza, watu walikuwa wanapewa fedha bila kufuata hata vigezo; pili, kulikuwepo na eneo la kuweka dhamana watu walikuwa wanapewa fedha bila hata ya kuweka dhamana, tatu; watu walikua wanakopa fedha bila hata kwenda kufanyia maksudi makubwa waliyoombewa fedha. Ambacho unaweza ukasema kwa kifupi ni kuona kwamba ni *conspiracy*. Watu waliopaswa kusimamia fedha walishirikiana na baadhi ya watu wakaweza kupoteza hizo hela. Inasikitisha sana, lakini si hiyo tu, walianzisha mifuko mingi; na Kamati yetu imekuja na pendekezo kwamba hiyo mifuko zaidi ya 52 waliyoanzisha kwa kazi ile ile; ningepata muda ningewasomea hii mifuko; mifuko hiyo inatoa mikopo kwa

makundi yale yale na mwisho ya mwisho hizo fedha zikapotea. Ndiyo maana tumekuja na pendekezo kwamba mifuko iwe *consolidated,* iwe michache na iweze kuwa *manage*. Hayo ni machache *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika miradi ya maji, fedha nyingi zinapotea kwa sababu ya miradi ya maji ambayo Mdhibiti na Mkaguzi ameonesha katika ripoti yake ya ufanisi kwamba tatizo kubwa ni kutokuwa na *masterplan.* Ina maana usanifu wa kina haufanyiki licha ya kwamba sheria…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzumnguzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili tayari. Sasa mnabisha? Au unataka kwenda kwa mganga wa kienyeji? *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa tuna wananfunzi wetu mahiri sana 80 na walimu watano wa Shule ya Msingi Kikombo, Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa jioni tutaanza na Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mhesimiwa Hamad Bakar.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

*(Saa 07:00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma Kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022 na**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Tulishamtangaza Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, ajiandae Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema. Pia nikushukuru wewe kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze moja kwa moja kwa kusema kwamba Maafisa Maduhuli kwa maana ya Wakurugenzi wanalo jukumu kubwa sana la kuhakikisha kwamba kila senti inayopitia katika mikono yao kwa maana ya halmashauri iko katika mikono salama. Jukumu hili ni la kisheria na linawataka wao kuhakikisha kwamba wanafanya kila kinachowezekana kuhakikisha kwamba fedha ya Mtanzania au kwa maana ya fedha ya wananchi inalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu gani? Mimi kama Mjumbe katika Kamati ya *LAAC*, tumekuwa tukihojiana na halmashauri mbalimbali. Katika halmashauri 34, tuliweza kuhojiana na Kamati nne ambazo zilifanyiwa ukaguzi maalum kwa maana ya *special audit*. Tulivyohojiana na Kamati hizi, tulikuta kwamba kuna upotevu wa fedha nyingi sana ya Serikali. Kwa mfano, katika halmashauri nne,

mojawapo ikiwa ya Dar es Salaam kwa maana ya Ubungo, Kigamboni, Ilemela pamoja na Iringa. Halmashauri hizi kwa pamoja zilipoteza takriban shilingi bilioni 9.055 kama ifuatavyo:-

(a) Halmashauri ya Ubungo ilipoteza takribani shilingi bilioni 4.9;

(b) Halmashauri ya Kigamboni ilipoteza shilingi bilioni 1.1;

(c) Halmashauri ya Ilemela ilipoteza shilingi bilioni 2.9; na

(d) Halmashauri ya Iringa ilipoteza takribani shilingi milioni 124.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla ndiyo kama hiyo *amount* niliyoisema hapo. Fedha hizi zimekuwa zikipotea vipi kwa namna moja au nyingine, kunakuwa na njama zinazofanyika kuhakikisha hizi fedha zinapotea. Njia mojawapo ni ya kurekebisha au kubadilisha miamala pamoja na tarakimu za ankara. Njia nyingine ni ya kufuta ankara pamoja na miamala hiyo na njia nyingine pia ni ya kuweka miamala ambayo haistahili maana yake miamala ambayo siyo sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ni nini? Kwa kufuta miamala hiyo lakini pia na kurekebisha tarakimu za miamala pamoja na ankara kunakusudia wao kupata kiasi kidogo kwenye ripoti, kwamba ionekane kuna fedha ndogo kwenye ripoti lakini wakiwa wana fedha nyingi mkononi, hivyo kuwafanya waweze kutumia fedha hii kwa makusudio ambayo hayakukusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine kwenye hilo, ni kwamba ile ya kuweka miamala isiyostahiki, lengo ni kufanya *financial statement* kwa maana ya ripoti iwe *impaired,* yaani

ionekane kwamba haina sifa ya kuweza kutumika wakati ikihitajika, kama mtu anashtakiwa. Kwa hiyo hayo yote tunaona kwamba ni makusudio ovu ambayo yanatokana na watendaji ambao siyo waaminifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hilo, kuna jambo lingine ambalo limeashiria pia upotevu mkubwa wa fedha. Zile pale zilikuwa tayari zishapotea lakini hizi ni kiashirio cha upoteaji. Kwa mfano, ukienda moja kwa moja kwenye halmashauri ambazo nimezitaja, kwa Halmashauri ya Ubungo kwa mfano. Kumekuwa na ubadilishaji wa miamala yenye thamani ya takribani shilingi milioni 156. Halikadhalika kumeripotiwa madeni hewa kwa maana ya madeni ya uongo ya takribani shilingi milioni 976. Vilev vile kumeripotiwa pia madeni yasiyokuwa na viambatanisho au madeni yasiyokuwa na *justification* takribani ya shilingi bilioni 1.076.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mweka Hazina wa Halmashauri ya Ubungo kwa wakati huo, jina tunamhifadhi yeye alimdanganya *Auditor* kwa kusema kwamba amekusanya takriban shilingi bilioni 33.4, lakini kiuhalisia baada ya kufanya *reconciliation* ikaonekana kwamba ameweka benki kiasi cha shilingi bilioni 31.4 pekee, hivyo ni kwamba kuna kiasi cha takribani shilingi bilioni mbili ambacho kilikuwa hakieleweki, kimepotea. Inawezekana kwamba kweli alikusanya lakini fedha hii ikawa imetumika isivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika ripoti hiyo hiyo kwenye Halmashauri ya Ubungo ambapo iliripotiwa kiasi cha takribani shilingi milioni 829 ambayo mdaiwa wa halmashauri alikwenda akailipa benki moja kwa moja. Kitu cha kushangaza fedha hii ilitolewa siku hiyo hiyo kwa mfumo wa *cash,* kwa maana ya fedha taslimu. Sasa hapo unaweza ukaona jinsi gani mambo hayo yanavyokwenda.  Kuliripotiwa pia kiasi cha mapato ambacho kilikuwa ni takribani shilingi

milioni 623. Fedha hii ilikuwa ni mapato ya halmashauri lakini haikuripotiwa, yaani ilikuwa imeripotiwa pungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na suala lingine la *adjustment* imefanyika, kwa maana ya marekebisho ya miamala. Kwenye Halmashauri ya Kigamboni kulikuwa na marekebisho ya takribani shilingi bilioni 10.8. Kwenye Halmashauri ya Ilemela kulikuwa na marekebisho yanayofanana na hayo ya takribani shilingi bilioni 8.7. Kulikuwa na fedha ambayo imeripotiwa ambayo yenyewe ilikuwa imefutwa kwenye *POS* kwa maana ya *system* za ukusanyaji takribani shilingi milioni 554. Halikadhalika kulikuwa na fedha pia imeripotiwa kwamba fedha hiyo haikupelekwa benki, takribani shilingi milioni 627. Kwa ushahidi huu unaweza ukaona ni kwa jinsi gani fedha za Serikali zinavyopotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, nini kifanyike? Kwa hali ya sasa hivi jinsi ilivyo inaonekana kabisa utaratibu unaofanyika kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa maana ya *Auditor,* jinsi anavyoripoti haioneshi kama kutakuwa na dalili ya tatizo hili kwisha. Kwa sababu gani? Yeye anavyokwenda kukagua anaenda moja kwa moja kukagua halmashauri, akishakagua yeye anaripoti kwa Bunge kwa maana ya Kamati ya *LAAC* na Kamati zingine. Akisharipoti pale, anatoa *copy* kwa Serikali akiiambia Serikali mambo ambayo amekutana nayo lakini kwa kuishauri marekebisho yafanyike wapi na wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, akisharipoti huku *LAAC,* sisi kama wasimamizi wa Serikali tunafanya majadiliano kama hivi na mwisho wa siku hatuna maamuzi ya kufanya ya kumchukulia mtu hatua. Yaani tumekuwa hatuna meno. Kinachofanyika sasa, sisi tunaishauri tena Serikali, tunawaambia kwamba fanyeni marekebisho, chukueni hapa, fanyeni hapa. Jambo ambalo ni kama vile mtoto

aliyekosea, jirani amekosewa halafu anamwambia mwenye mtoto amuadhibu mtoto wake kwa kosa alilolifanya. Sidhani kama kitu kama hicho kinaweza kikafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hali hiyo, tatizo ni nini? Nashauri kama tatizo ni sheria, naiomba Serikali kufanya jitihada ya kuileta hiyo sheria hapa kusudi tufanye mchakato wa kuirekebisha, kusudi Bunge liwe lina maamuzi sahihi ya kuweza kumwajibisha mtu yeyote yule au chombo chochote kile ambacho kimekutwa na ubadhirifu wa fedha za umma, la sivyo tutakuwa tukiongea hapa kwa mtindo huu na ndivyo ilivyo miaka nenda, rudi tunakuwa tukisema hapa fedha zinapotea, fedha zinapotea, hakuna *action* yoyote inayochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, unasema kwamba TAKUKURU waende kufanya uchunguzi, wanaenda kufanya uchunguzi vipi wakati tayari uchunguzi ulishafanyika. Kwa mfano, uchunguzi uliofanyika wa *special audit*. Ule ni uchunguzi sahihi ambao una ushahidi wa kuweza kumpeleka mtu mahakamani. Inakuwaje uchunguzi unaostahili kumpeleka mtu…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mchungahela kwa mchango mzuri.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Namwita Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, wajiandae Mheshimiwa Jesca na Mheshimiwa Zuwena Athumani Bushiri.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia kwenye hoja hizi za Kamati zetu tatu ambazo ni Kamati ya

*PIC*, *PAC* pamoja *LAAC*. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa zawadi yake hii ya uzima na wa afya njema na kuweza kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu jioni hii kuweza kuchangia machache ambayo tumeyaona kwenye Kamati yetu ya *PAC*.

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea kuitumikia nchi yetu. Kwa kweli tunampongeza sana na tunamwambia aendelee kupiga kazi na sisi tuko nyuma yake, tunamuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mchango wangu leo nitaelekeza kwenye Kamati ya *PAC* na moja kwa moja nitazungumzia mambo matatu. Jambo la kwanza nitaangalia dosari katika usimamizi na ufuatiliaji wa mikataba. Moja ya miongoni mwa eneo ambalo Kamati yetu ya *PAC* imetumia muda mrefu kuchambua na kuangalia kwa kina ni eneo la namna gani mikataba yetu tunayoingia kwenye taasisi mbalimbali inavyoweza kusimamiwa na inavyoweza kufuatiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dosari nyingi sana kwenye eneo hili na naiomba sana Serikali iangalie upya kwa namna ambavyo tunaweza kusimamia kwa sasa kwa kweli bado tuna changamoto kubwa sana kwenye usimamizi wa mikataba yetu na kwenye ufuatiliaji wa mikataba yetu, jambo ambalo linapelekea hasara kubwa kwa Serikali lakini pia upotevu wa fedha nyingi lakini na ucheleweshwaji wa miradi mbalimbali ambayo inatekelezwa kupitia maeneo mbalimbali au sekta mbalimbali ambazo zinatekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni tumepata taarifa kwamba Serikali tutaenda kutekeleza miradi kupitia *EPC+F* pamoja na *PPP*. Sasa kama hatukuwa makini sana kwenye

suala la usimamizi wa mikataba, kiukweli tutaenda kuisababishia Serikali yetu hasara kubwa sana na mabilioni ya fedha yatapotea kupitia mifumo hii ambayo tunakwenda kutekeleza miradi kupitia mifumo mipya hiyo ambayo nimeitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia tu mfano wa fedha ambazo zimepotea. Kwa mfano, ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza ambapo ilitakiwa ilipwe shilingi milioni 134, imelipwa shilingi milioni 154. Hii ni kwa sababu tu ya usimamizi mbovu na ufuatiliaji mbovu wa mikataba yetu. Ukiangalia pia ujenzi wa Hospitali ya Mkoa wa Mtwara, hali iko hivyo hivyo zimelipwa shilingi milioni 200 zaidi. Kwa hiyo hii ni mifano tu kuona kwamba mikataba yetu namna tunavyoweza kusimamia na namna ambavyo tunaweza kuifuatilia, kwa kweli tuna dosari kubwa na tuna udhaifu mkubwa sana Serikalini kwenye jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili niangalie kwenye mwingiliano wa majukumu ya kiutendaji kwenye taasisi zetu, mamlaka mbalimbali na mashirika mbalimbali ambayo yapo Serikalini. Kwenye Kamati yetu sisi hatukatai taasisi kushirikiana, lakini tunakubaliana na jambo hili endapo ushirikiano huo utaenda kuongeza ufanisi, ubora na utaenda kupunguza gharama za utekelezaji wa miradi hiyo ambayo wanaenda kushirikiana. Kwa hali ilivyo sasa, hatuoni kwamba kuna umuhimu kwa baadhi ya mashirika au kwa baadhi ya taasisi kuweza kushirikiana. Kwa sababu kwa mfano tu *TAA (Tanzania Airport Authority)* pamoja na *TANROADS* wanashirikiana kwenye ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea kwamba ushirikiano wao utupe ufanisi mkubwa kwenye utekelezaji wa majukumu ambayo wamepeana, utupe ubora kwenye kazi hizo ambazo wanazifanya na gharama pia ziwe chini kwenye

mambo haya ambayo wanashirikiana, lakini hali ni tofauti sana. Kwa mfano, kuna hasara ya zaidi ya shilingi milioni 236 ambayo Uwanja wa Ndege wa Dodoma, *TAA* walienda kuondoa taa uwanjani pale ambazo zilikuwa zinatumia nishati ya jua na wakaweka nishati ya umeme, taa nyingine ambazo taa hizo ziliwekwa na *TANROADS*. Kwa kweli ni hasara kubwa za Serikali, zaidi ya shilingi milioni 236 zimepotea kwa sababu tu ya ushirikiano dhaifu uliopo baina ya taasisi hizi mbili, *TAA* pamoja na *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo hizo taasisi mbili zimesababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa Mradi wa Uwanja wa Ndege wa Shinyanga, kwa sababu mkataba na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya uliingia baina yake pamoja na *TAA*, lakini mkataba huo ukataka kupewa *TANROADS* jambo ambalo ilicheleweshа sana utekelezaji wa mradi huu. Tunaiomba sana Serikali, kwenye ripoti yetu sisi tumeshauri kwamba majukumu yote ambayo yanahusika na ujenzi wa viwanja vya ndege yarudishwe kwa taasisi ambayo inahusika na viwanja vya ndege ambayo ni *TAA*. Kwa hiyo naiomba sana Serikali izingatie mapendekezo haya, izingatie ushauri huu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo nataka nichangie, ni namna Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inavyoweza ku-*operate* hapa katika nchi yetu. Tunayo Mifuko mingi ambayo hapa imetajwa kwamba kuna Mifuko zaidi ya 52, lakini tunaona ufanisi na utendaji wake bado ni mdogo. Tunaona kwamba *control* na usimamizi wa Mifuko hii ni jambo linalopelekewa na sababu ya kutosomana kwa mifumo hii na hivyo mtu anaweza akakopeshwa kwenye Mfuko mmoja na mtu huyo huyo akaenda akakopa kwenye mfuko mwingine bila ya kujulikana kwa sababu mifumo hii haisomani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mtu mmoja anaweza akakopeshwa na zaidi ya Mifuko miwili au mitatu, kitu ambacho kinapelekea mikopo chechefu mikubwa ambayo tumeiona. Mfano wa mikopo chechefu hiyo ni Mfuko wa Pembejeo za Kilimo, zaidi ya shilingi bilioni 20.1 zimepotea kwenye mifuko…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Hamad Bakar.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Jesca, halafu Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara wajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie. Kwanza nichukue nafasi hii kupongeza sana Ofisi ya *CAG* kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha kwamba Bunge hili linakwenda siyo kama kipofu, bali tunakwenda huku tukiwa tunaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo ambayo nataka niongee kutoka kwenye ripoti ya *CAG,* nami ni Mjumbe wa Kamati. Kwanza kabisa, yapo mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wameshaongea. Cha kwanza nilichotaka kuongea ambacho *CAG* amekiongea na kinaonesha wasiwasi, nami binafsi pia nikapata wasiwasi, kwanza ni kuhusiana na fedha za ruzuku ya maendeleo ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* anasema pesa za maendeleo zinazopelekwa kwenye Halmashauri zetu baadhi yake zinaonekana zimepelekwa bila kupitishwa au kupatiwa idhini kutoka kwenye Bunge hili. Wasiwasi wangu unaanzia

hapo. Zipo zaidi ya Halmashauri 19 ambazo zimepelekewa fedha zaidi ya shilingi bilioni 47 bila idhini ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi yetu kubwa hapa kama Wabunge ni pamoja na kuisimamia Serikali na kupitisha hizi bajeti za Serikali. Sasa nashindwa kuelewa, ni kwa nini fedha hizi shilingi bilioni 47 zipelekwe katika Halmashauri, hata kama nia ni njema, ndiyo zipelekwe katika hizi Halmashauri bila Bunge kujua au kuidhinisha matumizi yake kwenye hizi Halmashauri?

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu unakuja, pale ninapojiuliza, wenzetu Serikali wana mpango gani na Bunge? Je, wanataka kutunyang'anya ajira zetu? Kwa sababu sisi kazi yetu ndiyo hiyo, tuje hapa tupitishe bajeti, tuwahoji na kadhalika. Sasa unapokwenda moja kwa moja unapeleka fedha hizi bila kunipa mimi, una nia gani? Kwamba unanifuta kazi yangu, au una mpango gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine, fedha zimepelekwa kwenye miradi ya maendeleo zikiwa pungufu. Hapa naipongeza Serikali. Zaidi ya Halmashauri 163 zimepelekewa shilingi bilioni 500 kama ruzuku ya miradi ya maendeleo, lakini wamejitahidi kwa sababu upelekaji wa miaka mitano mfululizo ni wastani wa asilimia 46; lakini kwa mwaka 2020/2021 wamepeleka asilimia 62 kwenye ruzuku ya miradi ya maendeleo. Hapo tunawapongeza na tunaona nia njema ya Serikali, lakini bado kuna upungufu wa asilimia 38 zaidi ya shilingi bilioni 300 ambazo hazijapelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaiomba Serikali iangalie namna, kwa sababu tunapopeleka fedha hizi kwenye miradi ya maendeleo ndivyo tunavyokwenda kuchakachua uchumi kule chini kwa watu wetu. Halmashauri tatu zenyewe zimepelekewa fedha kama ambavyo jinsi

tulikuwa tume-*plan* bila kuwa na mambo yoyote meusi ndani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili; ili tuendelee tunahitaji watu; lakini tunahitaji watu tu, tunahitaji watu walioongezewa thamani. Hatuwezi kuendelea kama tuna watu ambao hawana thamani kubwa. Taarifa ya *CAG* inaonesha bado yako madai kwa watumishi wa umma wa nchi hii. Wanatudai mishahara shilingi bilioni 63. Yapo madeni ya malimbikizo ya posho, likizo kwa watumishi milioni karibu 96,650,000,000. Hawa ndio rasilimali watu tunaotegemea kwamba wafanye kazi kubwa kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hatutaweka uwekezaji kwa watu hawa, ina maana utendaji wao ndio maana unakuwa ni duni. Watu hawa ndio tunaopelekea mabilioni ya fedha kwenye miradi ya maendeleo, halafu hujampa fedha yake ya nauli anapokwenda likizo, ndio maana unakuta sasa wana-*temper* na mifumo, wanafanya mambo meusi meusi ili angalau waweze kufidia ule upungufu na makali wanayopata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumeelezwa hapa, Manispaa moja tu ya Ilemela kwenye mitando tayari wame-*temper* na shilingi bilioni karibu nane, zimefutwa vocha za karibu 822 kwenye mfumo bila utaratibu unaoeleweka. Tumeelezwa hapa, Ubungo wameingiza *figure* kwenye mfumo ambao Mwenyekiti wangu wa Kamati amesema tu kwamba ni shilingi milioni 500 ambayo haieleweki yaani. Ukiwauliza, wanakwambia ilikuwa ni namba ya simu. Unashindwa kuelewa, namba ya simu gani inaanza na kodi ya 500? Ni ujanjaujanja na ubadhirifu ili kuhakikisha kwamba wanakuja ku-*temper* na fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoangalia, na kuwaangalia watumishi wa umma, hatuwezi kufanya mambo

makubwa yakaenda sawa sawa na maendeleo kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna malalamiko ya kikokotoo kwenye nchi hii…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, …

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa mchango wake, lakini nadhani Bunge hili pia linapaswa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu baada ya *CAG* kuwa ametoa taarifa hiyo na hasa kwenye malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishajipambanua kwamba anahitaji rasilimali watu iweze kupatiwa haki na stahiki iweze kutekeleza wajibu sawa sawa; mpaka tarehe 31 Januari, Serikali ya Awamu ya Sita imeshalipa malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa umma 116,792. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haikuishia hapo. Katika hayo malimbikizo ya mishahara imekwishakutumia fedha za Kitanzania shilingi bilioni 199.365. Kwa hiyo, tunampongeza *CAG* kwa kazi nzuri, lakini hapo hapo pia tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuona jambo hilo na kulipa stahiki za watumishi wa umma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba unilindie muda wangu, lakini nashukuru kwa taarifa hiyo ya Serikali na naipokea. Hata hivyo tunayojadili hapa ni ile iliyoishia Juni, 2021. Kama wamekwenda hatua hiyo, tunawapongeza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwaombe, suala lingine linaloleta malalamiko, pamoja na mambo mengi tuliyoambiwa kuhusiana na kikokotoo, lakini kikokotoo kile ndani ya watumishi wa umma kinasumbua. Tunaomba Serikali ione namna ambavyo itakaa na watumishi wa umma na kuona wanafanya kazi kwa moyo bila kuwa na malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kukaa hata na Jeshi la Polisi tu, wakielezea hali yao ya utendaji wa kazi wanakwambia sisi hatuna hata muda wa kupumzika kusema tutatafuta hela ya ziada kwa ajili ya kuweka kibanda. Tunategemea tukilipwa mafao yetu ndiyo tuweke kibanda. Leo ukiniambia unanipa kidogo halafu unanilipa kidogo kidogo unakuwa hunisaidii. Tunaomba Serikali ikakae ili kuendelea kupunguza malalamiko haya kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nataka kuongea, upo ubadhirifu wa mikataba ambayo Halmashauri zetu zinaingia, na uwekezaji ambao Halmashauri zetu zinaingia. CAG ameelezea. Yapo mambo ambayo Halmashauri zinafanya bila upembuzi yakinifu, kwenda kuwekeza miradi ya ujenzi wa mastendi na masoko. Unakuta kwa sababu tu Halmashauri hii imejenga soko, na wengine wanataka wakajenge soko na wangine wanataka wakajenge stendi na wengine wakaige kitega uchumi hiki, lakini bila kuangalia mazingira yao yanaendana na hicho

kitega uchumi wanachotaka? Ndiyo maana yapo majengo mengi sana yamejengwa kwa gharama kubwa lakini hayatumiki ipasavyo kwa sababu Halmashauri zetu hazifanyi upembuzi yakinifu wa kujua mradi ule kama unaweza ukawa sahihi kwa mazingira yao na kama watu wao wanauhitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali iwasimamie. Hizi Halmashauri, Wizara husika, isimamie. Ile ya kwamba tunakwenda kujifunza mahali fulani, Waheshimiwa wanasafiri wanakwenda kujifunza mahali, anachukua tu ile utaratibu wa kujenga *Machinga Complex* ya Dar es Salaam anataka labda ajenge Iringa, wakati ni tofauti kabisa. Yaani Machinga wa Iringa ni tofauti kabisa na Machinga wa Dar es Salaam, na hawawezi kuendana katika biashara zao wanazozifanya. Kwa hiyo, hii imeipotezea Serikali mapato hela nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia zipo taasisi nyingine…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, nakuongezea sekunde 10.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taasisi nyingine ambazo nazo zinasababisha Halmashauri zetu kupata hasara. Taasisi kama TEMESA ni za Serikali, lakini nazo zimekuwa funza kwenye Halmashauri zetu. Kwanza, ukitaka kupeleka gari TEMESA watakuandikia vifaa vya bei kubwa kuliko hata kwa Mangi, unakwenda unatengeneza kwa gharama kubwa, wanakufungia kifaa kimekufa, yaani hawaeleweki. Kwa nini tutumie TEMESA kama tunajua kabisa hii inatuletea tatizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna *NHIF,* kila wakati kwenye hela za vituo vyetu vya afya wanatafuta visingizio vidogo vidogo, kwamba hawa wameshindwa kujaza fomu…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, ajiandae Mheshimiwa Waitara.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nichangie taarifa ya mwaka 2020/2022. Kwanza napongeza Kamati zote tatu kwa mawasilisho yake mazuri. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PIC,* nitachangia yale ambayo tumeyaongelea katika Kamati yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia katika maeneo matatu. La kwanza ni changamoto ya mitaji katika taasisi; ya pili, ni *TANAPA* na ya tatu ni mali ghafi katika viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na changamoto za mitaji. Tunalo Shirika la *TEMESA*. Shirika hili linafanya kazi ya kutengeneza magai ya Serikali yaliyo mengi pamoja na kampuni. Serikali imewekeza mtaji na linajiendesha mpaka sasa hivi shirika hili linasuasua, limekuwa na madeni makubwa ambapo Serikali hii ambayo imewekeza, imeikopa taasisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka dakika hii TEMESA inadai shilingi milioni 45.39. Haiingii akilini kwamba sasa hivi kule ambako tunategemea tupeleke magari yetu TEMESA wao wanafika mahali hata vipuri vya kutengenezea magari yetu hawana. Wanashindwa hata kutoa gawio katika Mfuko

wa Serikali kuu kwa kuwa hawana fedha za kuendeshea taasisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa Kamati tunaishauri Serikali ihakikishe kwamba inalipa madeni yote ya TEMESA na kuhakikisha kwamba inatengeneza utaratibu mzuri ambao utakuwa ni utaratibu wa *prepaid* yaani tengeneza, lipa, ili kuhakikisha kwamba madeni mengine hayazalishwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchangia *TEMESA,* nakuja katika Shirika la Hifadhi, *TANAPA*. Wabunge wengi wamesimama kuongolea suala la *TANAPA*. Mwanzo *TANAPA* ilikuwa ina hifadhi 16, mpaka sasa hivi ina hifadhi 22, lakini kwa bajeti ile ile ambayo ilikuwa inaendeshea ikiwa na hifadhi 16.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kwa sasa ongezeko la hifadhi sita halitatosheleza bajeti ya kuendeshea shirika hilo. Ikumbukwe kwamba kuna changamoto mbalimbali ambazo barabara zetu zinazoingia katika hifadhi siyo rafiki, hivyo zinahitaji kufanyiwa ukarabati ili kuleta tija hasa watalii wetu wanapokuja kutembelea wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna changamoto nyingine ambayo ni maji. Serikali inabidi ijipange katika kujenga mabwawa ili kuepusha ule utamaduni ambao naweza nikauita utamaduni wa wanyama kutoka katika hifadhi na kuja katika makazi ya watu na baadaye kuleta athari ya watu kufariki na kuharibiwa mali zao. Kamati imechambua kwa kina, inaishauri Serikali ihakikishe kwamba inaongeza fedha za kutosha katika shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije katika viwanda vyenye changamoto ya mitaji. Nichangie kuhusu Kiwanda cha Ngozi

cha Kimataifa cha Kilimanjaro kilichopo Manispaa ya Moshi Kata ya Karanga. Tulienda kutembelea kiwanda hicho, tulifika tukaona jinsi walivyo na vitu vizuri, na bahati nzuri pia walishakuja kutembelea Bunge wakaleta bidhaa zao tukaziona. Cha kusikitisha ni kwamba kiwanda hicho hakina malighafi za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Halmashauri zetu, Watanzania tunachinja sana ng'ombe na mbuzi. Ni vizuri Serikali ikajipanga sasa kupitia Halmashauri zetu, sekta ya mifugo wakahakikisha kwamba ngozi zile ambazo zinachinjwa zinahifadhiwa vizuri ili hatimaye ziweze kuja kuuzwa katika viwanda vyetu ili viweze kufanya kazi na vilete tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Nilishamwita Mheshimiwa Waitara atafuatiwa na Mheshimiwa Katani na Mheshimiwa Simon Songe ajiandae.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wakati ukaguzi wa *CAG* unafanyika mpaka tarehe 30 Juni, 2020/2021 tulikuwa na Halmashauri za mamlaka 185, lakini mpaka tarehe hiyo walikuwa wameshakagua Mamlaka ya Serikali za Mitaa 42 sawa na asilimia 23. Pia walifanya ikaguzi maalum kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 34. Kamati ya *LAAC* ilikutana na kuwahoji mamlaka nne, hiyo taarifa yote ambayo imezungumzwa hapa. Sambamba na hilo ni kwamba kulikuwa na shida ya muda na bajeti vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Waheshimiwa Wabunge waone huu ukosefu wa muda na bajeti, madhara yake ni nini? Nikijaribu kuangalia, ukiacha mengine ambayo yametajwa hapa kule Ilemela, inawezekanaje watu ambao

walikuwa ni watumishi, bado wanaingia kwenye mfumo wa Serikali na wanabadilisha ankara ambazo ni mabilioni kwa mabilioni kwamba hao watu kweli hawajulikani?

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekanaje kwamba kuna stakabdhi 822, yaani hazionekani! Halafu kuna makampuni 270 wanafanya biashara katika Halmashauri ya Ilemela halafu hawalipi kodi. Pia ukiangalia kwa mfano fedha ambazo ile asilimia 10 ambayo inapelekwa, mamlaka 155 fedha haijarejeshwa shilingi bilioni 47.01. Pia mamlaka 83 hawajapeleka fedha katika makundi yale matatu; vijana, wanawake na watu wenye ulemavu shilingi bilioni 6.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika ukaguzi maalum uliofanyika, katika mamlaka 37 shilingi bilioni 19.72 hazikupelekwa benki. Hawajaishia hapo, kwenye mashine za *POS* katika ukaguzi wa *CAG* yenye ukurasa 308 wanasema kuna shilingi bilioni 18 zilipotea au hazikwenda benki, hawajui ziko wapi. Pia wanatuambia, kuna vyanzo ambavyo ni muhimu hawakukusanya kodi au ushuru wenye jumla ya shilingi bilioni 14.3. Vilevile kuna maeneo ya *levy* haikukusanywa ambayo ni shilingi bilioni 6.03.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye afya wanatuambia, kwenye mamlaka 46 za Serikali za Mitaa, dawa zili-*expire* ambazo zilikuwa na gharama ya shilingi bilioni 3.49. Pia wanatuambia kwenye ukaguzi, nimefupisha tu, kwamba kuna fedha ambazo kuna madai mbalimbali ya mishahara na taasisi, amesema Mheshimiwa Waziri, lakini hapa walikuwa wanadai jumla ya shilingi bilioni 160 hazijalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia fedha ambazo zilipaswa kwenda *Social Security Funds* hazikupelekwa. Katika mamlaka 42 ni shilingi bilioni 183.09. Kuna miradi ya maendeleo ya wananchi ilicheleweshwa katika mamlaka 128 yenye jumla ya shilingi bilioni 195.65. Vilevile mamlaka 21,

Shilingi bilioni 41.51 Wilaya ya Buhigwe iliachwa iliachwa. Sasa yako mengi ya kutaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, walipanga kupeleka vitabu Million 6.3 vilienda vitabu Milioni 1.4 yenye gharama ya Bilioni 5.18. Nachosema ni kwamba ukiangalia kazi ambayo Mheshimiwa Rais Mama Samia anayofanya na kutafuta fedha katika vyanzo mbalimbali, ukasoma ripoti ya *CAG* yenye kurasa 308, ukaangalia upotevu wa fedha zilizopotea, jambo hili Waheshimiwa Wabunge halipaswi kunyamaziwa. Jambo hili ni lazima Mheshimiwa Rais, achukue hatua, Serikali ichukue hatua na Bunge lazima liwe na meno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hata taarifa yenyewe imekuja hapa tunapewa Dakika Tano, unaambiwa ingiza kwenye *Hansard* hili jambo tulipaswa tujadili siku tatu, kila Kamati na siku zake na tufanye maazimio na Serikali ipewe muda ije itupe majibu. Hatuwezi kuwaambia wananchi wachangie maendeleo wakati kapu limetoba, tenga haliwezi kujaa, kuna matundu kibao. Waheshimiwa Wabunge tumekutana kwenye Bunge hili kwa ajili ya Watanzania maskini, wanatusikiliza lazima tuwe sauti kwa wasiokuwa na sauti, tufanye maamuzi sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili lazima kabla ya Bajeti ijao Serikali ije na mpango mkakati vinginevyo ukaguzi wa *CAG* ni kupoteza fedha. Fedha hizi ni nyingi kwelikweli lazima zisimamiwe. Nilikuwa nasoma ripoti naangalia kule Nyamungo ambapo wananchi wangu hawana maji, hawana barabara, watoto wanakaa chini, nikajiuliza tungeweza kuchimba visima vingapi katika Halmashauri yetu? Tungenunua magreda mangapi katika hizi fedha? Tungetengeneza madawati mangapi watoto wasome? Walimu wangejengewa nyumba ngapi? Hili Waheshimiwa Wabunge ni jambo ambalo ni muhimu, lazima tuchukue hatua na Serikali hapa lazima iwajibike.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa walioiba fedha washughulikiwe, tuambiwe kwanini hawapo jela? Wako wapi na wanafanya nini? Nani anawalinda, anawalinda kwa faida ya nani, kwanini wasiwajibishwe? Kama watu wameiba fedha hawajahukumiwa utamkamata nani? Haya ni mambo ya kupendeleana, Bunge msikubali kufanya hivyo, lazima tuwawajibishe watu. Serikali isilete maneno maneno hapa watu wawajibishwe, hawa ni wezi sawa na vibaka wengine mtaani, wawajibishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie ripoti hii iko mtaani, ripoti hii wananchi wanasoma, wanaelewa, wanataka kuwaona Wabunge wao wa Chama Cha Mapinduzi kwa asilimia kubwa mnachukua hatua gani? Tuanze kuchukua hatua sasa kabla ya sisi kwenda kuwajibishwa na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Katani, jiandae Mheshimiwa Simon Songe.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi. Nataka nianze kuchangia ripoti iliyotolewa hapa na Ndugu zetu wa *PAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu wa pamba wa mwaka 2019/2020 Serikali kama kawaida yake ilifanya yale ambayo yalifanywa kwenye msimu wa korosho mwaka 2019/2020. Bodi ya Pamba imekwenda kutengeneza deni la zaidi ya shilingi bilioni 102.5. Bodi ya Pamba kwa maelekezo ya Serikali ya kwamba wanunuzi wanunue tu pamba Serikali itawafidia, wanunuzi tu peke yake wanadai zaidi ya shilingi bilioni 21,

lakini wazabuni wetu wa pembejeo, wazalendo, Watanzania wa ndani wanadai zaidi ya shilingi bilioni 80 na ilitamkwa la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka hapa kwenye korosho mlivyofanya maamuzi hivyo hivyo kwamba Serikali iende ikanunue korosho kule, madeni kwenye Serikali hii bado ni makubwa. Leo *PAC* wamesema hapa na walitoa mapendekezo ambayo mpaka leo watu hawa hawajalipwa. Nini kinataka kutokea? *Projection* yako Mheshimiwa Bashe Waziri wa Kilimo ya kwamba mwaka 2025 unakwenda kuzalisha pamba tani Milioni Moja, Mheshimiwa Katani nipo hapa! Ukizalisha hata tani Laki Saba mimi na Ubunge wangu nikakae Tandahimba kule. Ukizalisha tani Laki Saba nikakae Tandahimba kule nilime korosho. Hakuna *projection* ya hovyo namna hii! Wazabuni hamjawalipa fedha, benki ambako mnasema kwamba *agricultural input* mnakopesha *single digit* ya asilimia tisa, mnakopesha fedha kwa zaidi ya asilimia 14. Unasema unaenda kumsaidia mkulima! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnasimama watu hapa, mimi nashangaa mnasema mnawasemea wakulima, mnalalamika bei imepanda, bei imepanda, bei ya vyakula iliyopanda mbona mkulima wa korosho ameuza korosho shilingi 1,700 hakuna aliyemtetea hapa, sijasikia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima gani Wabunge wenzangu mnayemtetea, mnamtetea mlaji au mkulima? Hebu tujiangalie Wabunge wa Vijijini hapa. Nani anamtetea mkulima? Yupi anamtetea mkulima? Tunauza mazao bei ya chini kule ya mashambani, wanaoleta mchele Mjini hao ni wafanyabiashara tu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamtetea mlaji hapa...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa Kaka yangu Mheshimiwa Katani hapa kuwa ni kweli kwamba mkulima anatakiwa kulindwa, lakini sasa alindwe ahakikishe anauzwa kwa bei ambayo anapata faida. Nikupe tu taarifa kwamba kule kijijini kwetu Nyabiromo - Tarime debe la mahindi ni shilingi 10,000 ambalo halijakobolewa wala kusagwa, huku au ukienda mtaani au ukiuliza hapa Dodoma ni kati ya shilingi 22,000 mpaka Shilingi 28,000. Sasa huyo mkulima wa kule umemtetea vipi? Debe la mahindi ina maana kwenye kusafirisha tu ndiyo shilingi 15,000 *difference*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa yake inaongezea nyama kwamba kweli mkulima kule hakuna anayemtetea, ndicho anachokisema na anathibitisha kile ninachokisema, nakushukuru sana na naipokea taarifa kwamba wakulima wa nchi hakuna wanaowatetea kwa kauli ya Mbunge pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe kwanza Wizara ya Fedha mpo hapa, hapa mnaposema *single digit* kwenye bidhaa hizi za kilimo, pembejeo na vitu vingine muende mkasimamie. Waziri wa Kilimo Bashe uende ukasimamie, hayo maporojo yako utakuwa na *vision* kubwa na utakuwa na *mission* kubwa kwa *trend* tunayokwenda nayo huwezi kufanikiwa nakuambia kaka yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hapa mwaka 2025 ukipata tani laki saba za pamba mimi Katani nabaki Tandahimba na Ubunge wangu nauacha huko huko, nakuhakikishia leo hapa, kwa *trend* hii tunayokwenda nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninyi Wabunge wenzangu mmewahi kulima kweli au ninyi mnadhani *garden* mzoweka nyumbani kwenu ndiyo kilimo kile? Umeweka maua kidogo na nini, mnadhani ndiyo kilimo kile? Rudini mashambani sisi tunakotoka wakulima mkajaribu kulima, mtamtetea mkulima kwa uchungu kuliko haya tunayoyafanya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Bashe hii itakwenda kukutafuna, *mission* na *vision* zako ziko vizuri sana, lakini kama hutakuwa na mkakati thabiti kwa sababu fedha huna, hapo unakaa unajitetea hela zinakuja, zinakuja ziko wapi? Wakulima watalalamika hawa! Ziko wapi? Ziko wapi zinakokuja, ziko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnatudanganya watu wazima hapa mfumo, mfumo, miezi Sita hakuna cha mfumo hakuna cha nini! Hela hatuna, semeni! Mfumo! Mnatudanganya mfumo. Waziri hapa anafanya kazi kubwa, maminara mpaka Kilimanjaro huko, mfumo upi? Mkatudanganya mfumo! Tuambieni ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuambieni ukweli, tunataka tumsaidie Mama, kila anayesimama anaona kazi inayofanywa na Mheshimiwa Rais, lakini ninyi wasaidizi wake, fanyeni tathmini ya kina. Mimi nawaambia, fanyeni tathmini ya kina tunakwenda wapi! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo unapaswa umwambie mtu mdogo sana, Mheshimiwa Mwigulu Kaka yangu na rafiki yangu, umetutukana Wabunge sana. Mimi

nakuambia! umetutukana Wabunge sana, unapaswa ukae, utafakari, hapa hakuna anayeweza kujadili waganga wa kienyeji hapa, hamna, hamna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya tunayojadili ni maisha ya Watanzania na tumeletwa Bungeni tuwasaidie Watanzania, hata wananchi wa Iramba kule wanataka uwasaidie Watanzania wa Taifa hili. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Kuhusu Utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Kuhusu Utaratibu.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika ....

**NAIBU SPIKA:** Kanuni?

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 71 na kama utaruhusu nisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maslahi ya muda ninaomba Mbunge anapochangia, Kanuni yetu inazuia kusema jambo la uwongo. Sasa Mheshimiwa Mbunge anapo-*generalize* kwamba mimi nimewatukana Wabunge, hiyo ni *allegation* kubwa sana ambayo Bunge lako haliruhusu na mimi nisingeweza kutukana Wabunge na Kiti kikiwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa heshima zote ningemuomba Mbunge anapochangia pamoja na hoja kubwa aliyokuwa anaijenga, aepuka *generalization* kama ambavyo amejaribu ku-*twist* ili kuweza kuweka uhalali wa hoja anayoiweka.

**NAIBU SPIKA:** Haya Kanuni zetu zinasema kabisa kuwa Kiti kitaamua kuhusu Utaratibu au kuhusu Mwongozo kujibu hapo hapo au baadae. Kwa hivyo, baadae tutakaa na wahusika wa Sekretarieti ya Bunge kutazama maneno ya Mheshimiwa Mbunge anayoyasema. Mheshimiwa Mbunge endelea. *(Makofi)*

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nakuambia jambo la wakulima, nikasema Wabunge wote hapa kwenye nyumba zetu tumeweka *gardens,* wasiwasi wangu tunadhani ndiyo ukulima wenyewe *garden*s zile. Umewaka *palm* nyumbani kwako, umeweka sijui maua ya *rose,* sijui umeweka vitu gani! Tujaribu hata hekari mbili, mbili kila Mbunge na tuweke azimio hapa na kila Mbunge awe na heka mbili kule anakotoka muone adha ya wakulima wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niwaombe sana Wabunge wenzangu, tuweke azimio hapa kila Mbunge awe na heka mbili, maana hapa wengi tunakaa na tunazungumza hapa, tunakaa Mijini tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima ambaye Dada yangu Mheshimiwa Matiko alikuwa anamsema, anazungumza kile nilichokuwa nakisema cha kuwa anapata bei ndogo na hakuna anayemsemea. Korosho hapa nimesema hapa mwaka huu, *average* ya korosho tuliyouza bei ya juu haizidi shilingi 2,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kuangalia gharama tunazozitumia na bei anayopewa mkulima, hakuna siku tumekaa mkulima amepata bei ndogo, Bunge likakaa hapa kujadili wakulima kwa nini wanapata bei ndogo. Leo walaji sisi tunaokuja kununua mchele pale Majengo Sokoni, wananunua mchele Dar es Salaam ndiyo tunakaa leo, bei imepanda, bei imepanda! Tunapotaka kumsaidia mkulima

tumsemee mkulima hata pale anapouza bei ndogo ndiyo tutaonekana wazalendo wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kaka yangu Bashe nikukumbushe tena kwenye kilimo na hili nishauri sana, ile *export levy* tuliyoipitisha uje na mabadiliko hapa, yote irudi kwenye tasnia ya korosho, yote. Utapona, utapona! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana mmeagiza pembejeo zenye zaidi ya thamani ya Shilingi Bilioni 98, lakini kukusanya fedha zenu zote hata ukichukua na *export levy* zote, ukasema ulipe wazabuni, una deni la Shilingi Bilioni 10, piga hesabu zako utaona, piga hesabu zako utaona!*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimerudia tena....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katani ahsante muda wako umekwisha. Sasa namwita Mheshimiwa Songe, jiandae Mheshimiwa Shabiby na Mheshimiwa Angella Kairuki ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie taarifa hizi za Kamati Tatu, nizipongeze sana Kamati kwa kazi kubwa ambazo zimefanya kutuletea taarifa ambayo inaenda kutufungua macho nini kinafanyika kwenye Kamati hizi Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa masikitiko makubwa sana katika taasisi zetu hizi mbili *TANROADS* pamoja na *TAA* katika muingiliano wa mamalaka ya utendaji wa kazi, kuna tatizo kubwa ambalo 2016 Mwezi Agosti ujenzi na upanuzi wa viwanja vya ndege ulihamishwa kutoka *TAA* kwenda *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona matatizo makubwa viwanja wana-delay kufanya kazi lakini bado haitoshi wanaingiliana katika maamuzi. Nikupe mifano michache, mpaka sasahivi tunavyozungumza Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga, Tabora, Sumbawanga hakijajengwa kwa sababu ya muingiliano wa majukumu kati ya *TAA* pamoja na *TANROADS* nini kilifanyika hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfadhili aliyekuwa anatuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa viwanja hivi alifanya *due-diligence* pamoja na *TAA* mwaka 2017 lakini baadae alivyotaka kuleta fedha akagundua kwamba tayari Mamlaka ya Ujenzi wa Viwanja Vya Ndege umehama kutoka *TAA* kwenda *TANROADS* akakataa kuleta fedha na ujenzi haukuendelea, nini kilifanyika hapa? Wamekaa zaidi ya miezi 30 hamna kilichoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais ameendelea na mazungumzo, mwaka jana Mwezi Februari, wameleta Dola za Kimarekani Million 12 kwa ajili ya Ujenzi wa Viwanja hivi, kwa masikitiko makubwa kwa sababu ya mwingiliano huu mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea na fedha zipo kwa Serikali yetu, ni masikitiko makubwa sana fedha hizi ni za mkopo walipa kodi watakuja kurudisha mkopo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo mpaka sasa hamna kinachoendelea itafika sehemu tutalipa riba ya kutokutumia fedha ambazo zimekopeswa. Mpaka sasa hivi Mkandarasi aliyefanya *quotations* 2017 ameambiwa afanye *implementations* ya mradi naye amekataa amesema hawezi kwa sababu vitu vimepanda bei hawezi kufanya sasa hivi naye ameongeza bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wako ofisini wamekaa, watu wanajadili ofisini zaidi ya miezi 11 wako ofisini wameshindwa kutoa maamuzi kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Shinyanga, Tabora na Sumbawanga. Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa sana katika Nchi yetu, lakini Watendaji wa Wizara wanamuangusha Rais kwa kutofanya maamuzi kwa wakati. Leo tuna Dola za Kimarekani Million 12 *TANROADS* hazijafanya kazi ni kwa sababu ya mwingiliano wa majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaomba sasa kama inawezekana tuamue kwa pamoja Wabunge turudishe Mamlaka ya Ujenzi wa Viwanja Ndege tutoe *TANROADS* tupeleke *TAA* ili kazi iweze kufanyika la sivyo tutakuwa tunazungumza viwanja havipanuliwi, hakuna kinachoweza kufanyika lakini mwingiliano huu utaona umetupa hasara ya Million 236 Kiwanja cha Ndege cha Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana walipanua wakaweka taa za *solar* kwa ajili ya kutua hizi ndege kubwa, lakini leo *TAA* zile taa ziliwekwa na *TANROADS* leo *TAA* wamekataa kwamba zile taa hazifai tena kwa sababu Mji wa Dodoma umepanuka sasa hawatatumia tena taa za *solar* wanaitaji taa za umeme Million 236 za walipa kodi zimepotea na sasa haiwezekani. Kwa nini? Kwasababu wanakati wanaweka hizi taa za *solar* hawakuwa na mawasiliano na kati ya *TAA* na *TANROADS* na fedha Million 236 za walipa kodi zimepotea kwa sababu ya Watendaji ambao hawana mawasiliano, hawawezi kufanya kazi zao kwa ajili ya kumsadia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima leo tuwe na maamuzi ili tuweze kuisaidia Serikali, hawa wote ambao wanasababisha hasara kwa Taifa hawa wote ambao wanasababisha hasara kwa nchi yetu wachukuliwe hatua ili

iwe mifano kwa watu wengine kwa ajili ya kunusuru Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nataka nichangie. Limechangiwa kidogo suala la riba katika miradi yetu. Leo nilikuwa natafakari hivi inawezekanaje Afisa Masuuli yeye anajisikiaje moyo wake anasaini vocha ya kupitisha malipo ya nyongeza ya kutokulipa kwa wakati kwa sababu amechelewa! Unapitisha *voucher* ya Milioni 100, unapitisha *voucher* ya Bilioni Moja unaenda kulipa kwa sababu wewe mwenyewe ulichelewa kumlipa Mkandarasi, haiwezekani leo Wabunge tuamue! Ni kwanini kila siku tunapiga kelele kwa sababu ya ucheleweshaji wa malipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwezekana Bunge hili liamue sasa Wizara ya Fedha ituletee taarifa ya kutupatia sababu kwa nini wanachelewa kulipa Malipo kwa Wakandarasi na kuleta riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano Daraja la Busisi wamechelewa siku 30 wamelipa riba ya milioni 58. *TAA* Bilioni 11 lakini Kiwanja cha Ndege cha Mwanza bilioni mbili. Sasa inawezekanaje Afisa Masuuli unasaini *Vocha* ya kulipa kwa sababu wewe mwenyewe ulichelewa na wewe uko ofisini haiwezekani! Ni lazima tutafakari tuisaidie nchi, ni lazima tutafakari tumsaidie Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa, hawa Watendaji hawamsaidii. Leo Bunge tuamue ili tumsaidie Mheshimiwa Rais na wananchi wanamfurahia lakini kuna watu wanamuangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naiba Spika, nizungumze kidogo kwa ajili ya mifuko hii ya wakopeshaji ya wajasiliamali wadogo wadogo. Tumeletewa taarifa kwenye Kamati tuna Mifuko 52 na ilikaguliwa Mifuko 13, lakini nimekuja kugundua katika mikopo waliyotoa bilioni 90 kati ya hiyo bilioni 90, bilioni 50 ni mikopo chechefu haiwezi kukusanyika, inawezekanaje?

Haiwezekani watu wanakopeshwa na mwisho wa siku hawarejeshi! Tumegundua kwa sababu, gani? Ni kwa sababu, wanakopeshwa watu ambao hawana sifa, inafika sehemu wanashindwa kurejesha mikopo ile. Sasa haiwezekani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini eneo la pili kwenye hii mifuko; wamekopesha zaidi ya asilimia 72 kwa benki za biashara, jambo ambalo si lengo la mifuko hii. Lengo kubwa la mifuko hii ni kukopesha wajasiriamali wadogowadogo, lakini tumekuja kugundua zaidi ya asilimia 70 zinakopeshwa benki ambayo si lengo la mifuko hii, tunayo ya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mifuko hii imetengenezwa ili iawasaidie wajasiriamali wadogowadogo kule vijijini, lakini hawapati mikopo kwa sababu wanaokopeshwa si wale wanufaika; na ndiyo maana sasa tunakuwa na mikopo chechefu kwa sababu watu wameacha malengo na makusudi ya ile mikopo wameenda kwenye malengo ambayo hawakupanga kuyafanya. Ukiona hivi maana yake hatukujiandaa katika hili eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunayo mifuko mingi, 52, wote wanafanya kazi moja; na kwa sababu hawawasiliani, hamna sehemu wanaonana; leo Mheshimiwa Songe anakopa mfuko A, kesho akifulia kidogo anaenda kukopa B, keshokutwa akifulia kidogo anaenda kukopa C, mwisho wa siku anashindwa kurejesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaishauri Serikali, ifike mahali mifuko hii sasa iunganishwe iwe michache, badala ya 52 iwe hata minne ili iweze kuwasaidia wananchi wetu. Hata ikiwa inawezekana basi iweze kusomana ili kama umekopa sehemu A basi usipewe mkopo sehemu B, kwa sababu, hatimaye utashindwa kurejesha mikopo hii, ili iweze kuwasaidia wananchi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili linatakiwa lichukuliwe hatua za haraka ili tuinusuru nchi yetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Songe, kengele ya pili. Mheshimiwa Shabiby. *(Makofi)*

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante…

**NAIBU SPIKA:** Jiandae Mheshimiwa Kairuki, jiandae Mheshimiwa Mwigulu, jiandae Mheshimiwa Prof. Makame na Mheshimiwa Bashe.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi na mimi kuwa mmoja wa wachangiaji katika hizi Kamati zetu tatu. Mimi leo nitachangia sehemu mbili tu; sehemu za kilimo na sehemu ya mifugo kwa sababu hizi zote, hawa maafisa ugani, nani wako kwenye TAMINSEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tu niseme, nataka niwaambie ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge. Tunazungumza sana habari ya mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei kwa sasahivi ni lazima uwepo; na kwa nini upo? Ni kwa sababu miaka hii miwili, mitatu ya nyuma kwanza kidogo palikuwa na shida ya mvua na vilevile vyakula vilikuwa bei ya chini. Kwa hiyo mkulima hakuweza kupata pesa ya kulima eka nyingi anavyohitaji. Mkulima atalima eka nyingi anazohitaji, akiwa na eka 100 ili alime zote lazima alichokivuna kiendane sambamba, ili auze, kiendane sambamba na eka anazoweza kulima mwakani. Akipata kidogo badala ya kulima 100 zile alizonazo atalima 20. Kwa

hiyo *automatically* mazao yatakuwa machache na bei itakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mkulima akipata bei kubwa, kama ya mwaka huu, na mnaona wenyewe, kwa mfano Jimboni kwangu Gairo na majimbo mengine yote, wamelima takriban mashamba yote, hata mkipita njiani mnaona watu wamelima mashamba yote. Kwa hiyo, mavuno yatakuwa mengi na bei *automatically* itashuka. Lakini hapa habari ya kusema kwamba kuna mfumuko wa bei, lima na wewe, kama alivyosema Mheshimiwa Katani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani ukalalamikia mfumuko wa bei, nasikiasikia hata huko nje. Unasikia maharage yamepanda bei, yule pale Mheshimiwa Mwijage amelima shamba la maharage, safari hii amepata maharage ndiyo maana anachekacheka tu, kapata hela nzuri, miaka yote anapata hasara. Kwa hiyo, lazima tusichanganye mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima, kama alivyosema Mheshimiwa Katani, mkulima tumuache auze anavyotaka yeye kwa sababu yeye ndiye amelima, tusimpangie. Na Serikali nayo tusiilaumu sana kwa sababu Serikali nayo hailimi, ila tumshauri tu Mheshimiwa Waziri atoe chakula kama alichosema kwenye Halmashauri na aangalie watu wa kuwapa. Apeleke tu pale sokoni, asimpe dalali kwa sababu dalali naye ataminya baadaye naye atauza bei kubwa. Kwa hiyo wangalie namna ya kutoa kile chakula ili kishuke bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama kweli tuumize watu asilimia 70 wakulima wa nchi hii kwa sababu tu ya kutetea watu asilimia 30, halafu hawa asilimia 70 tunaowaumiza ni kwa ajili ya jasho lao, haiwezekani kitu kama hiki. Na mimi

ninataka kama kuna Mbunge yeyote anataka mkulima hapa ashushe bei ya mahindi hebu tusimame hapa, Wabunge wangapi wanataka wakulima washushe wasimame hapa tuwaone hapa? Muone hapa kama mtapata kura hata mbili majimboni huko. Ndio ukweli huo, tusiingilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi ninamshangaa Mheshimiwa Bashe ana maneno mengi tu, aah ngoja, mimi hapa, wakulima, wambie ukweli kwamba hatuwezi tukaingilia masuala ya mkulima, muacheni mkulima auze anavyotaka. Na ninawahakikishia kwa mwaka huu kwa bei hii mtaona kuanzia mwezi wa saba, wa sita, vyakula vitashuka mpaka mtashangaa. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili. Hawa wafugaji nao sasa wamekuwa wanasumbuliwa yani, wamekuwa sasa kama hawaishi kwenye maeneo ya nchi yao. Mimi nilishangaa nilijua labda Waziri wa Mifugo atakuja na mpango wa kupima maeneo ya ufugaji akazanie huko, yeye anakazania heleni. Maana ng'ombe nao sasahivi wamekuwa masharobaro, wanatakiwa wavae heleni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu hizo heleni zimejaribiwa pale, nimeona Pandambili, zimejaribiwa Katavi. Mimi napenda sana kufanya *research;* nimezichukua, hata sasahivi nina heleni nne pale, lakini ukizi-*track;* nimewapa mpaka watu wa *IT;* hazioneshi ng'ombe kama yuko Dodoma. Maana ukichukua heleni si ni lazima ng'ombe aonekane yuko Dodoma? Hazioneshi.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilikuwa nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, yaani wanaokazania heleni wanataka ziishe ndani ya mwaka mmoja, wakati vitambulisho vya taifa vinatakiwa viishe miaka 11 havijaisha. Yaani vitambulisho vya taifa havijaisha ila heleni ziishe. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shabiby.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, naikubali taarifa. Imekaa vizuri. Haiwezekani kitu kama hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nina wasiwasi, jamani, huyu Mama yetu, Mheshimiwa Rais, mambo kama haya hajui; lakini ninataka niseme ana kazi ya ziada upigaji an chi hii uko waziwazi. Sisi wengine tunajua na bahati nzuri tunawajua mpaka hao wenye hizo tenda, tunawafahamu. Kama kweli kule Katavi walikofanyia majaribio watuambie ng'ombe wangapi waliokufa? Ng'ombe wangapi ambao waliwaona wamechepuka wameingia labda kwenye hifadhi au kwenye nini, kama wanayo hiyo taarifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii wazungu ulaya wanatumia, lakini wanajua kila kitu. Hapa Kenya hawatumii, Uganda hawatumii, *South Sudan* hawatumii, eeh, hapa tunataka sisi tunaanzisha vitu ambavyo havina mfano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ng'ombe mlianza na chapa, chapa imekuja imeshindikana. Mmekuja kengele, kengele imekuja imeshindakana. Sasa mmekuja na heleni, heleni ikishindikana mtataka wavae shanga za kiuno; eeh! ndiyo maana yake hiyo. Ikitoka hapo mtataka wavae vikuku vya miguu; maana yake sasa tunawavisha ng'ombe hawa.

Mimi nasema, kwa suala kama hili msiichafue hii Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutoweka mipango. Kama mipango ni mizuri mna harakanayo ya nini? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu Mheshimiwa fanyeni uchunguzi…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Sekunde 30.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Naibu Spika, fanyeni uchunguzi. Yule mwenye tenda hiyo wale wanaotaka kuzigawa ndio wanakaa na hawa watu wa Wizara ya Mifugo wanaongea, waklimaliza kuongea ndipo wanaenda kuwashauri wale wafugaji. Haya ni mateso makubwa sana, mimi sikubaliani kabisa na hii heleni. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kairuki, ajiandae Mheshimiwa Mwigulu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nishukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kujibu au kuchangia hoja hizi zilizoko mezani, na hasa hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa au *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hoja ya kwanza, kuhusiana na kutokupeleka taarifa ya utekelezaji wa maazimio ambayo yalitolewa tarehe 04 Novemba, mwaka jana; nipende tu kusema kwamba, tayari tulishapeleka na tumewasilisha Ofisi ya Bunge na tunaamini itaweza kuwasilishwa kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa mujibu wa taratibu. Kwa hiyo, kwenye hilo tulishawasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, kumekuwa na hoja, na hususan changamoto ya nidhamu katika ukusanyaji na utumiaji wa mapato ya Serikali katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwenye hili nikubali, ni kweli changamoto hii ipo. Tumekuwa tukiendelea kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba tunafuatilia, lakini vilevile kuhakikisha kwamba fedha hizi zote zilizoko katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, zilizokusanywa, zinatumika kama ambavyo inatakiwa kwa mujibu wa kanuni na sheria zetu za matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kuimarisha udhibiti tumeendelea kuboresha pia ofisi za wakuu wa mikoa na hasa kupitia sekretarieti za mikoa yetu kwa kupitia na kuuangalia upya muundo wa sekretarieti zetu za mikoa. Kwenye eneo hili tumeendelea kuhakikisha kwamba, tunaanzisha *section* ya usimamizi, ufuatiliaji na ukaguzi ambayo pamoja na mambo mengine watakuwa pia na jukumu la kuweza kusimamia, kufuatilia, lakini pia kukagua shughuli mbalimbali ambazo zinatekelezwa katika mikoa, lakini pia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizoko chini ya mikoa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa wakuu wa *sections* katika mikoa 22 tayari wameshapatikana, lakini vilevile tunaendelea na taratibu za kujaza wakuu wa *sections* katika mikoa minne katika sekretarieti za mikoa, ili kuhakikisha kwamba zinakuwa zimekamilika na wanatimiza majukumu yao ipasavyo. Si hilo tu, tumeendelea pia kuongeza fedha za matumizi mengineyo katika sekretarieti za mikoa kutoka bilioni 57.44 hadi kufikia bilioni 79.09. Lengo ni kuhakikisha kwamba tunaziwezesha sekretarieti za mikoa na wataalam wetu katika *sections* hizo kuhakikisha kwamba wanaweza kutekeleza majukumu yao ipasavyo likiwemo jukumu kubwa na la msingi la ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli mbalimbali za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja ya kaguzi mbalimbali ambazo zimefanyika kupitia kwa Mkaguzi wetu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali. Ameweza kufanya kaguzi nyingi na nitagusia tu chache kama ambavyo na wenyewe kwenye Kamati wamegusia, hasa kuhusiana na ile kaguzi maalum ya Manispaa ya Ilemela, Manispaa ya Ubungo, Kigamboni, Iringa, na nikipata muda nitaweza kugusia au kujibia chache: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kusema kwamba baadhi ya maeneo kweli tunakubaliananayo na tunaendelea kuchukua hatua kwa kujibia hoja hizo za ukaguzi. Nipende tu kukuhakikishia Mheshimiwa Naibu Spika na Bunge lako, kwamba tayari kama Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, tumeshaanza kuchukua hatua mbalimbali, lakini vilevile tumeiweka Manispaa ya Ilemela kwenye uangalizi wa karibu sana. Tunaendelea kuziangalia Manispaa na Halmashauri mbalimbali ikiwemo Bunda, Ilemela, Kigamboni, vilevile Halmashauri mbalimbali za Mkoa wa Tanga, Mkoa wa Morogoro pamoja na nyinginezo vilevile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna hoja kwamba, hatua hazichukuliwi. Watu wamekuwa wakiishia tu kuhamishwa. Nipende kukuhakikishia kwamba tunaendelea na hatua mbalimbali za kinidhamu, lakini vilevile za kijinai. Kwa yale ambayo yanatakiwa kuchukuliwa hatua mbalimbali za kiutumishi tayari tumeshatoa maelekezo katika sekretarieti zetu za mikoa kupitia makatibu tawala wa mikoa kuweza kuchukua hatua. Vilevile tayari kupitia kwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU hatua mbalimbali pia zimeendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumepata mrejesho kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU. Takribani watumishi nna wazabuni 672 wameshafanyiwa uchunguzi,

lakini vilevile watumishi na wazabuni 46 kati ya hao uchunguzi wao tayari umeshakamilika kutokana na kutothibitika kwa tuhuma dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile watumishi na wazabuni 53 majalada yao yako katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka, kwa sababu ndio utaratibu, kwa ajili ya kuwaombea kibali cha kuweza kuwafikisha Mahakamani kwa ajili ya mshitaka ya jinai. Pia tayari watumishi na wazabuni 51 mashauri yao yako Mahakamani tunavyoendelea hivi sasa, lakini vilevile yako mashauri yanayowahusisha…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, muda wako umekwisha na tuta…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru na nipende kusema naunga mkono hoja na yote yaliyopendekezwa hapa tutayatekeleza na kuhakikisha kwamba hatua stahiki zinachukuliwa. Hatutamfumbia macho yeyote atakayetumia fedha kwa kukiuka taratibu. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, jiandae Mheshimiwa Makame Mbarawa, jiandae Mheshimiwa Hussein Bashe, tutamalizia na Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja zetu zilizoko mezani. Awali ya yote nikiri kwamba tumepokea maeneo ambayo yanahusu ushauri, tutayafanyia kazi ili kuweza kuboresha kama Waheshimiwa Wabunge walivyoshauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja zilizojitokeza nifafanue hoja mbili/tatu. Hoja ya kwanza, limejitokeza jambo la Taarifa ya *CAG.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sana kwenye hili pia tukazingatia taratibu zinazotumika. Utaratibu unaotumika ambao tulijiwekea wenyewe kwenye sheria ni kwamba baada ya *CAG* kufanya ukaguzi wake, cha kwanza anachotoa ni hii taarifa yake, na baada ya hapo kutakuwepo na utaratibu wa Serikali kujibu. Lakini kwa taratibu zilivyo akishatoa taarifa ile Waziri wa Fedha anaipeleka Bungeni. Sasa zikishapita taratibu hizo itachambuliwa, ikiwa kwenye hatua za kwanza inapokuwa imekamilika kunakuwepo na hoja za ukaguzi na baada ya uchambuzi kutakuwepo na wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa hoja za kiukaguzi kuna vitu vingine vinakuwa vya kiuhasibu. Hata hapa tu sasa hivi ukituuliza tutoe risiti mara moja kwa watu wengi namna hii, tutoe risiti mara moja ya mafuta ya kujia hapa, hauwezi ukapata risiti hizo kwa mara moja. Kwa hiyo, aliyekagua mara ya kwanza anaweza akaona risiti aliyotumia Mheshimiwa Dotto haipo. Huu hautakuwa wizi mpaka pale ambapo itajulikana kwamba Mheshimiwa Dotto hakwenda Dodoma lakini mafuta yake yametoka. Kwa hiyo, kunakuwepo na hoja za ukaguzi ambazo Serikali itafanya *reconciliation,* ikishafanya *reconciliation* hatua inayofuata tunabainisha yale ambayo yanahusu *criminality,* yale ambayo ni ya wizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na utakumbuka kauli ya Mheshimiwa Rais; mara ya kwanza tu alipokuwa anapokea Ripoti ya *CAG,* alimwambia *CAG* usipepese macho, usifanye kuficha. Kauli ya aina hiyo ni mwongozo mkubwa ambao Waheshimiwa Wabunge hampaswi kutilia shaka utayari wa

Serikali kuchukulia hatua masuala yanayohusu rasilimali za nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, sisi tumepokea taarifa ya *CAG* kama Serikali na hatua zinazofuata itafuata taratibu hizo za kiutawala bora kama inavyotaka, kukagua wapi pana hoja ya kiuhasibu na wapi pana upotevu. Pale ambapo pana upotevu hatua stahiki zitachukuliwa, wale waliohusika watafika kwenye mkono wa sheria na watawajibika kwa makosa ambayo wameyafanya.

Kwa hiyo, kwenu ninyi Waheshimiwa Wabunge tumepokea maelekezo yenu na Serikali itachukua hatua kwa yote yale ambayo yanahitaji hatua za kisheria kuchukuliwa; na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ameongelea kwa upande wa TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, na si tu taarifa ya *CAG,* makosa yote yanayohusisha ukosefu wa maadili kazini yamekuwa yakichukuliwa hatua hata kabla ya Taarifa ya *CAG* kutolewa. Kuna watu wanafukuzwa kazi, kuna watu wanapelekwa mahakamani, kuna watu wako TAKUKURU, kuna watu wameshahukumiwa. Tuna kesi za kutosha, na ndiyo maana tukienda kwenye utawala bora tunakuwa kwenye *rank* za nchi ambazo zinafanya vizuri, ni kwa sababu tunafuata utaratibu wa utawala bora. Utaratibu wa utawala bora una gharama yake, gharama yake ni ufuate taratibu na wakati ule ule wakithibitika wanachukuliwa hatua. Kwa wale Wanasheria watasema kwamba ni namna gani ambavyo kwao kisheria ni kosa kubwa sana kumwonea ambaye hana hatia kuliko hata kuswaga wale ambao wana hatia ukaunganisha na wale wasio na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la mwisho lilikuwa linahusu suala la mfumo, Mheshimiwa Mbunge ame-*generalize* sana, anasema muda wote mnatudanganya,

mnasema mifumo, mifumo, mifumo. Ndiyo haya ninayoyasema tuongee kama viongozi, panapokuwepo na tatizo tuliseme lile tatizo tu tusi-*over generalize,* unavyo-*over generalize* hivi tunaipaka matope nchi yetu, pia tunamvunja moyo Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge hawa wanatoka majimboni, katika kipindi ambacho fedha zimemiminika mikoani kuliko kipindi chochote ni wakati huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizokwenda *TARURA* ni nyingi kuliko kipindi chochote tangu *TARURA* ianzishwe, namba hazidanganyi, ndivyo ilivyo. Ukienda kwenye Elimu hakuna mwaka tumewahi kujenga madarasa mengi kwa mpigo kuliko hii miaka miwili iliyopita, hizo ni fedha zinakwenda kwenye halmashauri zetu. Sio hivyo tu, ukienda kwenye elimu bure ambako na kwenyewe wanapokea watoto wetu, hakuna mwezi umepita kwamba fedha hazikwenda. Kwa hiyo, ikitokea mfumo umeleta hitilafu *either* kwenye mwezi, *either* kwenye halmashauri, *either* katika baadhi ya maeneo...

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri taarifa.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba anavyosema Waziri wa Fedha hakuna wakati kama sasa fedha nyingi zimetengwa kwenda kwenye halmashauri. Shida kubwa iliyokuwepo kuanzia mwezi Oktoba mpaka Januari pamoja na uwepo wa hizo fedha nyingi, lakini fedha zilikuwa hazitoki. Kwa hiyo hazitoki kwa nini? Mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani zipo nyingi na kwa kweli tunamshukuru kwa kutenga fedha hizo nyingi, lakini zilikuwa hazifanyi nini? Hazitoki, ndio shida iliyokuwepo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, taarifa hiyo.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge ameongea Kibunge ili na Watanzania waweze kuelewa nampongeza sana Mheshimiwa Kanyasu. Hilo likoje? Liko hivi unapokuwa na utekelezaji wa miradi mingi kwa wakati mmoja. Zimeiva *certificate* mathalani imeiva Busisi ina *deadline*, imeiva Bwawa la Mwalimu Nyerere ina *deadline*, imeiva ya reli *lot* mbili, tatu, nne, kwa utaratibu wowote ule imeangukia pamoja na mishahara, imeangukia pamoja na Deni la Taifa. Utaratibu wa malipo unaanza na *first charge,* baada ya hapo unaenda kwenye vyombo, baada ya hapo unaenda kwenye mikataba ambayo ukichelewa ina riba, baada ya hapo tunaendelea kutiririka na zingine, hivyo ndivyo tunavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye kipindi ambacho hutekelezi miradi mingi ni kawaida kwamba kila unachokipeleka kitakuwa kinatoka tu. Kwa mfano, sisi tu hapa tukiambiwa tutoke kwa mara moja hapa, siku zingine tunavyotoka kwa utaratibu huu mlango ni mkubwa, lakini tukiambiwa tutoke kwa mara moja hapa hatutaweza kutoka kwa wote kwa mara moja. Sio kwamba humu ndani kutakuwa hakuna watu, tupo wengi wa kutosha, lakini hatuwezi tukatoka mara moja mlango ule pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, fikirieni Mheshimiwa Rais wakati anaingia Bwawa la Mwalimu Nyerere lilikuwa kama asilimia 34, 35 au 37 Wizara ya Kisekta inaweza ikaniweka sawa, lakini ndani ya miaka miwili tumeshapiga tunaitafuta asilimia 90; hebu waniambie mtiririko

wa *certificates* ukoje, kuna wakati *certificate* zinaingia kwa mara moja. Kwa mfano mwezi ule uliopita aliotolea mfano hapa, *certificate* ya bwawa peke yake ilikuwa dola milioni 137, dola milioni 137 kwa mradi mmoja weka Busisi, weka reli, *lot* moja unakuta dola milioni 49 au 50 ukiziweka zote ni dola milioni 150 haya weka ya elimu bila malipo kuanzia chekechea mpaka *form six*. Ukishachanganya haya yote kuanzia tarehe 20 mpaka tarehe 24 au 25 kuna mishahara, baada ya hapo kuna deni la Taifa, ndugu yangu ni lazima tu mtiririko wa malipo lazima uwe na namna ya kuwa na utaratibu kwenye miradi ile mingine midogo tofauti na utaratibu ulivyokuwa mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utaratibu huo, ushahidi ndio huo sasa, hakuna mradi wowote ambao umekosa malipo, yaani hakuna mradi ambao umekwama mikubwa kwa midogo. Kwa hiyo, ule utaratibu wa mtiririko kama alivyosema Mheshimiwa Kanyasu nadhani ni vizuri kuelewa majira ya utekelezaji wa miradi na kuweza kwenda sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lile lingine alilosema Mheshimiwa Mbunge kama fedha zipo toeni. Narudia tena utaratibu wa utoaji wa fedha tunautoa kwa *certificate* na huu utaratibu umewekwa na Bunge, hatugawanyi fedha kufuatana na bajeti kwamba kwa sababu huyu ana bajeti ya kiwango hiki tunampatia akae nazo, hapana. Tunatoa kufuatana na *certificate,* tunatoa kufuatana na utekelezaji wa mradi, kazi zilizofanyika. Fedha ambazo tunazitoa ifikapo muda ni mishahara, ukifika muda wa mishahara tunatoa, lakini utekelezaji wa mradi, kama mradi wa ni trilioni 20, hatutoi trilioni 20 hizo zote zisubirie utekelezaji wake, tunatoa kufuatana na *certificate,* kwamba wametekeleza hapa, pameshakaguliwa na pameonekana panafaa kulipwa, ndio tunalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na miradi hii yote kama ambavyo nimekuwa nikisema na huu ni ukweli...

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Hakuna nchi inatekeleza miradi mikubwa mingi kwa wakati mmoja kama Tanzania, kwa Afrika Mashariki na *SADC,* hakuna mradi ambao umelala kwa sababu tumeshindwa kuulipia hivyo hivyo na kwa miradi mingine…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu kuna taarifa.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kinachozungumzwa na Mheshimiwa Kanyasu labda pengine hakukipata vizuri. Ni kwamba kule kwenye halmashauri zetu tunakuwa na pesa na zimeshaingia kwenye vitabu vyetu, sasa *certificate* inaletwa, lakini pesa haitoki kwenye mfumo, ndio hilo tu labda angetusaidia kufafanua, haviingiliani kabisa taarifa za Nzega Vijijini haziwezi kuingiliana na miradi mikubwa ya kimkakati kama Daraja la Kigongo - Busisi haviwezi kuingiliana, hiyo ni *project* tofauti na Nzega ni *project* tofauti. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mMtoa ruhusa wa malipo yoyote ni Mlipaji Mkuu wa Serikali, kama hilo litaingilia katika kipindi ambacho ni cha malipo ya mishahara *definitely* itasubiri, kitakachokuwa kimesubirisha ndio hicho kule mfumo utakuwa *down* kwa sababu mlipaji mkuu haja *authorize*, *first charge* lazima…*(Kicheko)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima *first charge* itoke kwanza ndio utaratibu ulivyo. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante muda wako umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu. Wajiandae Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Simbachawene.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja zenu zinajibiwa na Serikali. Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu, hoja zenu zinajibiwa na Serikali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hii.

Kwanza nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wote wa Kamati zote tatu kwa taarifa zao. Niseme tu kwamba mapendekezo yote yanayohusu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tumeyapokea na tunaahidi kwamba tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ufafanuzi kwa maeneo mawili ama matatu kulingana na muda na naomba nianze na eneo la kurejesha majukumu ya ukarabati, ujenzi na kazi zote za viwanja vya ndege kutoka Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* kwenda Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge, *CAG*, Kamati ya Miundo Mbinu lakini pia na Kamati ya *PAC*. Niwajulishe Waheshimiwa Wabunge kwamba tayari kazi hiyo imeshaanza na niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge kwamba shughuli za *TAA* kwenda *TANROADS* zilikuwa ni *presidential decree* na hii ilikuwa ni baada ya kuona shughuli nyingi wakati ziko chini ya *TAA* zilikuwa haziendi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tayari wataalam wameshatoa mapendekezo ya namna ya kuhamisha majukumu kutoka *TANROADS* kwenda *TAA* kwa hatua kwa sababu ziko kazi ambazo tayari zinaendelea na hatuwezi leo tukaziondoa ghafla. Kitakachoweza kutokea kama tutakifanya hicho, ndio kama walivyosema baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna viwanja vilisimama kwa sababu wakati *TAA* inatekeleza hiyo miradi ama imeshaingia mikataba tukafanya mabadiliko. Kwa hiyo tutahakikisha hilo halifanyiki na wataalam wameshatoa mapendekezo yao, hatua za kuanza kuchukua, hatua baada ya hatua na tunategemea kwamba zile fedha ama zile kazi ambazo zitafanyika kwa fedha hasa ya Tanzania kwa maana haina wahisani, miradi yote tutakayoanza kutekeleza itaanza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengine watakuwa mashahidi kwamba hata sasa hivi tumeanza, pale ambapo kunakuwa na kazi wote wanakuwepo kwa ajili ya kuanza taratibu ya kuwajengea uwezo na uzoefu. Hilo kwa upande wa Serikali halina tatizo, tumeshalifanyia kazi na tunaamini kadri tunavyokwenda shughuli zote zitahamia *TAA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu bado vile viwanja vyote tulivyovijenga kama Msalato, Songea vimejengwa na

hawa *TANROADS* na wataalam kwa hiyo tunategemea baada ya hapo pia kutakuwa na kuhamisha wataalam ambao wamepata uzoefu kutoka *TANROADS* kwenda kule *TAA* ili kuwajengea uzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo kuna Mbunge amelichangia kwa nguvu kuhusu *TEMESA*. Tunatambua hii taasisi ni muhimu sana kwa sababu ndio inayoshughulikia magari ya Serikali ya Viongozi lakini pia na vivuko. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali inapitia hii Taasisi na majukumu yake ili iweze kufanya kazi vizuri zaidi. Kwa hiyo, tumelipokea Kamati ilishauri, lakini pia Wabunge wameshauri na wameendelea kushauri na sisi tunasema tumeshaona kwamba, kuna haja kubwa ya kuangalia muundo wake, majukumu yake na utendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ilikuwa ni taarifa na mapendekezo ya kiufundi na ufanisi. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara tunaangalia na kuweka mifumo imara sasa hivi ya jinsi ya kuangalia upungufu unaojitokeza wa kiufundi na hasa ya kiuhandisi yanayosababisha baadhi ya kazi zetu kufanyika chini ya kiwango. Niwahakikshie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tumeliona hilo, tumelichukua, lakini tumeshaanza kuweka mifumo ambayo itahakikisha kwamba tunazuia hilo lisitokee na pale ambapo linatokea, hatua kubwa sana zinachukuliwa za kisheria na kinidhamu kwa wale ambao watakuwa wamesababisha kufanyika kwa kazi za kiufundi chini ya kiwango kama ambavyo ripoti imesema na tarifa ya *PAC* imesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala mengine ambayo yameongelewa hasa ya ulipaji wa *certificate*, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameelezea vizuri, kwa hiyo hilo naomba nisilieleze tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, jiandae Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Nitachangia katika maeneo makubwa mawili; la kwanza Taarifa ya *CAG* imeongelea eneo la umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli *findings* za *CAG* kwenye Miradi ya *ERPP* na hata iliyokuwa miradi ya *DADPUS* ni sahihi na ripoti hii ya *CAG* ndio imekuwa msingi mkuu wa sisi kufanya mabadiliko katika Tume ya Umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya *ERPP* ambayo Mheshimiwa Deus ameitaja ni miradi ambayo ilikuwa *funded* na *World Bank* na mfumo ule wa *funding* ulikuwa unaamua wenyewe namna ya kuwapata hadi Wakandarasi, hili ni jambo la kwanza. Wizara tumefanya mabadiliko sasa hivi ni sisi ndio tuna-*design* namna gani *external funding* ziende kwenye miradi ya umwagiliaji na hatutatekeleza mradi wowote wa umwagiliaji ambao hauna *visibility study* wala *detail design*. Hili ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili miradi hii ya *DADPs* na *ERPP* kwa mfumo ulivyokuwa Tume ilikuwa makao makuu na sote tunafahamu katika Bunge hili. Nimekuwa Mbunge toka 2015, tumepitisha bajeti mbalimbali za Wizara ya Kilimo,

tulikuwa hatutengi fedha za usimamizi wa umwagiliaji na sisi ndio tulikuwa tunapitisha fedha. Meneja wa Umwagiliaji wa Mkoa kwa mwaka anatengewa milioni mbili, tunatarajia muujiza. Sote tukiri hatukuweka *concentration* kwenye *irrigation as a country for a very long time*. Kwa hiyo tuchukue yale matokeo ya nyuma kama *lesson* wakati tunafanya *reform*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Serikali inafanya nini? Sasa hivi tunaajiri Mainjinia 350, kila Wilaya tutapeleka Injinia wa umwagiliaji na Mheshimiwa Rais mwezi Machi atazindua magari ya Tume ya Umwagiliaji kwa ajili ya kupeleka katika kila wilaya ili tuweze kusimamia miradi ya umwagiliaji na fedha tunazopeleka katika eneo la umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nataka niseme na Mheshimiwa Katani ametoka na hapa tumekuwa tunajadili. Je, bei inayoonekana sokoni anaipata mkulima ama haipati mkulima? Tumefanya *survey* kama Wizara na tuko tayari ku *submit* ripoti mbele ya Bunge hili. Mkulima wa mpunga msimu wa 2020/2021 na msimu wa 2021/2022 bei aliyoipata shambani ni mara mbili kuliko bei aliyoipata msimu wa 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili lazima watu tuelewe, msimu wa 2021/2022 sote sisi tunafahamu tumeishi na wakulima. Mkulima aliyeenda shambani kulima heka moja ya mahindi, alitumia shilingi 300,000 kwa ajili ya mbolea ya kupandia, alitumia shilingi 240,000 kwa ajili ya mbolea ya kukuzia, alitumia shilingi 60,000 kununua mbegu, alitumia shilingi 60,000 kulimia, alitumia wastani wa shilingi 40,000 kupandia na kupiga halo. *Cost of production* ilikuwa ni shilingi 720,000, tuna *expect* kitu gani kwamba auze, sisi Serikali *NFRA* tumenunua mahindi kwa wastani wa shilingi 700 na shilingi 800, haya tunayoyauza kwa shilingi 700 na shilingi 800 tuna-*subsidize as a government*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli, wote tunafahamu kwenye *commodity trading*. Naomba hili nilisema kwa heshima kabisa, mkulima anayelima Nzega au anayelima Mbarali hutarajii ndio afikishe zao Soko la Dar es Salam lazima kuna *intermediary*. Ni jukumu letu kuviwezesha Vyama vya Ushirika viwe *central aggregating* na ndio hatua ambayo Serikali inachukua, ndicho tunachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaambie ukweli, *there is no way* tutaondoa *intermediaries*. Tunachotakiwa kuangalia kama bei ya mlaji imeongezeka kwa asilimia mia kwa mkulima aliyeko shambani ka-*benefit* kwa asilimia ngapi kutoka kwenye ile asilimia mia, hili ndio la msingi. Sasa hivi Mheshimiwa Esther katolea mfano Tarime, Serikali imefanya nini? Tumevi-*unlock* Vyama vyote vya Kahawa, Pamba, Tumbaku vyote. Tumevipa *mandate* mbili ku *aggregate cereals* na ku-*aggregate* mazao yao ya biashara yanayoitwa, kwa sababu *the biggest business* itakuwa chakula. *There is no way* tutakimbia kwenye huu ukweli. Ni lazima sisi kama Serikali na sisi kama Wabunge, tum-*protect* mkulima, lakini hatuwezi kum-*protect* mkulima bila kufanya *proper investment* kwenye *infrastructure*. Serikali imetoa fedha mwaka huu, inajenga maghala 70, tuna-*revive* masoko ya Tarime, tuna-*revive* soko la Ngara, tuna-*revive* soko la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Nimekuongezea sekunde 40 endelea Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kusema hivi, hakuna njia tutamwondoa mfanyabiashara kwa mazao, hakuna.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Hakuna taarifa sasa hivi. Endelea Mheshimiwa Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, namalizie tu. Hakuna njia tutamwondoa mfanyabiashara kwenye mazao. Vile vile hakuna njia tutakwepa *forces* za *demand and supply* kwenye soko. Bungeni hapa tuliilazimisha Serikali kwenye Korosho, tumeenda kuwatia hasara wakulima. Bungeni hapa tuliilazimisha Serikali ku-*intervene* kwenye pamba, tukatoa *One thousand and two hundreds* ambayo haiko sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tuna-*struggle* na matatizo ya pamba, *it was this Parliament* iliyoifikisha Serikali kununua pamba kwa shilingi 1,200 ambayo haiko sokoni. Aliyepata hasara ni mkulima. *We will never allow this. Never government intervention* ku-*disturb* soko. Tutapunguza gharama za ununuzi, tutapunguza gharama za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo *best practice,* tutaongeza tija, tutaendelea kupunguza gharama za *production* ili mkulima azalishe kwa gharama ndogo, auze anakotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene, malizia kwa upande wa Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kupongeza Kamati hizi tatu kwa kazi kubwa sana na nzuri ambayo wamefanya. Kusema ukweli wamefanya Bunge hili leo lichangamke kwa sababu ya kazi kubwa ambayo imefanywa na Kamati hizi tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *LAAC* wamekuja na Maazimio sita, *PIC* imekuja na maazimio 11, na *PAC* imekuja na maazimio saba. Serikali tumeyachukua maazimio yote *positively* na kusema kweli ni kazi ya Serikali kwenda kuyafanyia kazi. Napenda nikuhakikishie kwamba tumeyasikia, na pia tumesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii iliyofanyika leo inatokana na ripoti ya *CAG* ya mwaka 2019/2020. Huu udhaifu mliousema hapa, ni ya 2019/2020. Sasa taarifa ambayo sisi tunaamini imeandaliwa na *CAG* na ikapokelewa na Mheshimiwa Rais, na ikaletwa humu Bungeni, na mmeifanyia Kazi mkaitendea haki, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wakati anapokea taarifa hii, alisema maneno yafuatayo: "Kumekuwepo na mifumo mingi Serikalini, mifumo ambayo haisomani, na kila mmoja ukitengeneza mfumo unauruhusu uchotaji wa fedha." Pia akaendelea kusema, "kuna usimamizi usiokuwa na weledi Serikalini unaosababisha wizi." Mwisho wa kunukuu. Akaagiza *CAG, PCCB* na *DPP* wachukue hatua bila kuogopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwa taarifa hii na michango hii na mapendekezo ya Maazimio haya ya Kamati, Mheshimiwa Rais naamini atayapokea kwa mikono miwili na atahakikisha kwamba haya yote yanaenda kusimamiwa na kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa niaba ya Serikali kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, na hasa Bunge hili ambalo kimsingi ni Bunge la CCM. Kama Bunge la CCM linaikosoa Serikali yake katika chombo muhimu, maana

yake Bunge hili linaaminika na wananchi. Kwa hiyo, michango yenu Waheshimiwa Wabunge na maazimio haya, ni kazi ya Serikali kufanyia kazi. Tumeyapokea na naomba kuwahakikishia kwamba tunakwenda kuyafanyia kazi na tutarudisha hapa taarifa wakati kama huu mwaka unaokuja na mtaona mabadiliko makubwa sana Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo hapa yamezungumzwa ni aibu. *Accounting Officer* huyo huyo anachelewa kulipa, mradi unakuwa *penalized,* halafu yeye mwenyewe anasaini malipo ya kumlipa tena Mkandarasi huyo huyo. Haiwezi kuwa sawa sawa. Ni lazima tuseme, na tuje tueleze ndani ya Bunge hili, nani alichelewesha? Nani amechukuliwa hatua? Hatua zionekane kweli zikichukuliwa, siyo zisemwe tu zimechukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lazima tuweke mfumo wa sasa ambao utaruhusu kwamba yule anayekosea Serikalini anaadhibiwa; na yule anayefanya vizuri, anapongezwa na kusifiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nataka niwahakikishie tumewasikia, nami na wenzangu tunaunga mkono hoja hizi za Kamati na Serikali iko tayari kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kwa maelezo mazuri sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya *PIC,* dakika kumi.

**MHE. JERRY W. SILAA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa kuja kuhitimisha hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza sana wachangiaji wote waliochangia hoja zote tatu mezani. Tumetambua wachangiaji 24 ambao waamechangia kwenye maeneo mbalimbali ya hoja hizi tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ni mtambuka. Katika wachangiaji waliochangia zipo taaisi zimetajwa ambazo zinasimamiwa na Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Viwanja vya ndege *(TAA),* Mamlaka ya barabara kwa maana ya *TANROADS, TANAPA, TAMESA,* Mfuko wa Bima ya Afya *(NHIF),* Kiwanda cha Ngozi Kilimanjaro *(KLICL),* Mamlaka ya Bandari *(TPA),* Mamlaka ya Mapato *(TRA)* na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya wachangiaji wamezungumzia suala la uhamishaji wa Mamlaka ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege toka *TANROAD* kwenda *TAA*. Naomba nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba katika kikao chake cha tarehe 4 Novemba, 2022, katika Mkutano wake wa Tisa, Bunge lilikuwa na Azimio mbalo lilitokana na Mapendekezo ya Kamati yetu Na. 9, kwamba Serikali ihamishie Mamlaka ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege kutoka *TANROAD* Kwenda *TAA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuthibitishie, kama alivyosema Naibu Waziri wa Ujenzi, tayari Serikali imeanza mchakato wa kuhamishia na wameleta utekelezaji wa azimio hili kwenye kamati na utekelezaji wake unaridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kwa kifupi maeneo Matano. Eneo la kwanza ni Mfuko Maalum wa Uwekezaji *(Investment Fund)*. Kamati imeleta pendekezo la kuiomba Serikali ianzishe mfuko huu ili kusaidia mashirika na

taasisi yenye kuhitaji fedha za uwekezaji kuweza kupata fedha kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya, ipo Bodi ya Mazao Mchanganyiko *(CPB)* chini ya Wizara ya Kilimo. Bodi hii ikiwezeshwa fedha za kutosha ina uwezo wa kununua mazao, kwa maana ya mazao ya nafaka na inaweza ikasaidia huko mbele ya safari hata hili tatizo ambalo Waheshimiwa Wabunge leo wamesema la mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaamini kama Bunge lako litapitisha azimio hili, basi *Investment Fund* hii itasaidia siyo tu taasisi za kiuwekezaji za biashara, bali hata taasisi kama *CBP* ambayo inaweza ikasaidia kwenye mifumuko ya bei ya chakula nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni eneo la Mifumo ya TEHAMA. Namshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene, amemnukuu Mheshimiwa Rais katika kikao chake cha tarehe 28 Machi, 2021 akipokea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hata hivyo, pale alipoishia kunukuu, yapo maneno ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anasema, "kama mifumo imewashinda, basi ombeni misaada kwa wataalamu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la mifumo limesemwa hapa na Wabunge wengi, na maelezo yake ukitoa majibu yake hapa, hakuna anayeelewa. Ipo mifumo mingi ambayo haieleweki. Leo wafanyabiashara ikifika muda wanaweka *return* zao *TRA,* mfumo uko *down.* Yaani mtu anataka kulipa kodi, anaambiwa mfumo uko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumezungumzia Mamlaka ya Bandari *(TPA)*. Pale *TRA* wana mfumo wao wa *TANCIS* wa kulipa *custom duty;* huku bandarini nao wana mfumo wao wa *cargo system.* Ukishalipa kodi, uende bandarini na wakati

mwingine kodi mfumo uko chini. Ukienda bandarini wanaku-*charge storage*. Kule bandarini nako, ingawa wanaweza kuingia kwenye *TANCIS* na kwenyewe kuna matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Mheshimiwa Rais anasema, siyo lazima kila jambo ujidai wewe Masoud Mwamba unaliweza. Kama limewashinda, tafuteni wataalamu waliobobea kwenye maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi tukizungumzia mifumo, tunatoa mifano. Sisi wote hapa tuna simu za mikononi, na wote hapa tukifanya miamala ya simu za mikononi, hakuna siku muamala unazidiwa, hakuna siku unatuma pesa ambayo hauna; hakuna siku unadhulumu muamala unaenda kushughulikia mahali unaambiwa jambo limeshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mifumo ya kitaalamu ikijengwa vizuri; ndiyo maana Kamati inashauri Bunge kwamba uanzishwe mfumo wa *single integrated information management system and network* ambao utajumuisha mambo yote haya. Ukisikia mtu ana *NIDA* basi itambulike maeneo yote. Sio mtu wa Halmashauri hii anakopa, halafu anaenda Halmashauri nyingine; au unasikia kuna *POS* Halmashauri, mtu anaingiza anachokitaka yeye. Leo kuna Halmashauri fedha hazionekani, nyingine zinakusanywa haziendi Benki halafu unaambiwa huo ni mfumo. Hakuna mfumo wenye tabia kama hizo. Hicho ni kitu kingine, labda kitafutiwe jina lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali na Mheshimiwa Simbachawene kwa kauli hiyo aliyoisema ya Mheshimiwa Rais. Tunaiomba Serikali iende ikawe *serious* kwenye mifumo ili Watanzania hawa, watu wanaotumia bandari yetu waweze ku-*clear* mlzigo yao wakiwa Congo. Unaweza ku-*trace* mzigo kuanzia *Congo* mpaka unafika

bandari ya Dar es Salaam, lakini ukifika pale ni nenda rudi, mfumo uko chini, baadaye unachelewa kulipa kodi, ukilipa kodi, unakuwa *charged* kwenye *storage,* mwisho wa siku bandari inakosa wateja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ni la utalii. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana kwenye eneo hili. Filamu yake ya *Royal Tour* imeongeza watalii kwa kiasi kikubwa. Leo Ngorongoro mpaka kufikia Desemba wamekusanya zaidi ya shilingi bilioni 98. Leo *TANAPA* mpaka kufikia Januari 23, wamekuja kwenye Kamati wamekusanya shilingi bilioni 233. Tunategemea hawa kufikia mwezi Juni mwaka huu 2023 watakuwa wamevunja rekodi ya ukusanyaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nenda huko Ngorongoro, pita hiyo barabara, ukienda likizo Serengeti kupumzika na mkeo, zile rasta utakazopiga njia nzima mpaka ufike hotelini, hata hiyo sababu yenyewe ya kwenda kufanya na mkeo inaweza ikakushinda kwenye kufanya huko. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ngorongoro waliomba Shilingi bilioni 160 tu kujenga barabara inayoendana na mazingira, na walipata kibali *UNESCO,* mpaka leo hawajapewa fedha hizo. *TANAPA* walikuwa na hifadhi 16 zenye jumla ya Kilomita za mraba 57,000, wameongezewa hifadhi sita zenye jumla ya Kilomita za mraba 47,000, karibia mara mbili ya eneo lao. Fedha za maendeleo ni hizo hizo, fedha za matumizi ya kawaida ni hizo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea hivyo, alisema mchangiaji mmoja hapa, fedha za utalii ni *Non-Tax Revenue.* Ni pesa ambazo tunazipata kwa kile ambacho Mwenyezi Mungu alitujalia kama Rasilimali zetu. Tukiwekeza vizuri *TANAPA,* Ngorongoro na *TAWA,* tutapata mapato makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watalii 1,500,000 tunaozungumzia ni wale tu wenye kiu ya kwenda kuona *The Eighth Wonder of the World, Serengeti.* Akifika pale, zile rasta atakazopiga saa ya kwenda na kurudi, harudi tena. Kwa hiyo, tunaomba sana Bunge lako Tukufu lipitishe azimio na *TANAPA* itengewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ule utaratibu wa kukusanya fedha kupitia *TRA* siyo mbaya, lakini utengenezwe utaratibu mzuri wa *Revenue Disbursement Automated System* wa kurejesha fedha kwa wakati. Wanakusanya fedha nyingi, wanaomba pesa za maendeleo, mtu akae Hazina apeleke kwa muda anaotaka yeye. Kuhusu mifumo ameleezea vizuri sana kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwamba wakati mwingine inakuwa na *first track* na mambo mengine mengi ya miradi mikubwa ambayo yanafanya fedha zisiende kwa wakati. Kwa hiyo, tunaliomba sana Bunge lako liazimie fedha ziende kwa wakati. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, ni deni la Pamba. Tunaishukuru Serikali imeonesha jitihada kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tano na la mwisho, ni sheria ambazo zimepitwa na wakati, alisema Mheshimiwa Dkt. Kikoyo kuhusu Sheria ya *TR,* Sheria ya *TBS,* Sheria ya *TRA* ya *Stamp Duty,* tunaiomba Serikali iharakishe mchakato ilete sheria hizi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba kutoa hoja.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja hiyo, imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Uweklezaji wa Mitaji ya Umma *(PIC)* kuhusu shughuli za kamati kwa mwaka 2022.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma yaliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana. Hii sasa ni taarifa rasmi. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)*. *(Makofi)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuhitimisha hoja yetu ya *PAC*. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia hoja ya Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* pamoja na kutambua maelezo ya Serikali kuhusu hoja mbalimbali za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia ni saba na maeneo waliyowekea msisitizo na Wajumbe ni kama ifuatavyo:-

(a) Kukosekana kwa thamani ya fedha *(value for money)* katika baadhi ya miradi ya maendeleo;

(b) Upotevu wa fedha za umma zinazolipwa katika riba kwa wakandarasi;

(c) Ukiukwaji wa Sheria ya manunuzi na kanuni zake na kanuni zake katika utekelezaji wa baadhi ya miradi;

(d) Kuongezeka kwa gharama za utekelezaji katika baadhi ya miradi, (*variations)*.

(e) Kutofanyika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kabla ya kutekeleza kwa baadhi ya miradi;

(f) Kukosekana kwa *master plan* katika utekelezaji wa miradi ya maji nchini na dosari katika usimamizi wa mikataba;

(g) Uwepo wa mwingiliano wa majukumu baina ya taasisi ya Serikali kama vile *TAA* na *TANROADS*.

(h) Mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi kutofikia malengo ya uwanzishwaji wake kutokana na fedha kupelekwa kwa watu ambao sio walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kutekeleza kikamilifu mapendekezo yote ya *CAG* na Kamati. Aidha, katika kipindi cha kila robo mwaka sekta husika zilizokaguliwa ziwasilishe kwa *CAG* taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi ambapo itafanyiwa uhakiki na kisha kuwasilishwa Bungeni kupitia kwenye Kamati kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya mwendelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yetu sisi Kamati kwamba Serikali itatimiza wajibu wake ili kuongeza uwajibikaji katika fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijahitimisha hoja yangu. Nieleze kutoridhika na majibu ya Waziri wa Fedha aliyoyatoa. Kwa kweli mifano aliyoitoa inanipa wasiwasi na nafikiri inaipa wasiwasi na Bunge hili kwamba Serikali itakuwa tayari kusimamia fedha za umma inavyotakiwa. Hakuna *justification;* upeleke fedha nyingi kwenye miradi ambayo

huwezi kui-*monitor* na ambayo huwezi kujua kwamba *certificate* hii inatakiwa ilipwe kipindi hiki, kwa hiyo, lazima ilipwe kwa wakati. Uko tayari fedha za mikopo upeleke fedha nyingi na riba ziwe kubwa kuliko hata mradi wenyewe. Hiyo, nafikiri Bunge halitakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa fedha. Tunaomba aende akasimamie kikamilifu ulipaji wa hizi *certificate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kusema fedha zimepelekwa nyingi, na mifano ya kwamba tutajazana wote tukiambiwa tutoke kwenye mlango huo, hakuna fedha ya Serikali inaweza kutolewa kwa *emergence* namna hiyo, kwamba iende tu, halafu isiangaliwe itatumikaje; halafu izuie kwamba zile *certificate* ambazo zimefikia wakati wake zisilipwe kwa wakati maana kuna hela nyingi bado zinashughulikiwa huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa mawazo hayo, nina wasi wasi sana kwamba hata hizi fedha ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anazozileta, kama mtazamo ndiyo huo, hatuna imani kwamba kweli fedha hizo zitatutumika kwa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, licha tu ya kulipa riba kubwa ambayo mkiangalia ni mabilioni ya fedha, matrilioni ya fedha, bado miradi ile haitekelezwi kwa wakati. Sasa kama haitekelezwi kwa wakati tunafanya nini? Ina maana fedha ya mlipa kodi, fedha ya mkulima huyu tulikuwa tunamsemea hapa, ambapo hata kule kwetu kwenye Jimbo la Same Mashariki, Tangawizi iliyokuwa inauzwa kilo shilingi 1,000, au shilingi 2,000, sasa hivi inauzwa kilo shilingi 400 kutokana na changamoto mbalimbali. Sasa uniambie kwamba walipa kodi hao wanaohangaika, wananchi fedha zinaletwa za mikopo nyingi, halafu uambiwe kwa vile zimepelekwa nyingi lazima ucheleshwaji utatokea! Hakuna kitu kama hicho!

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hela ni nyingi lazima iwe na mpangilio, ina maana gani ukakope hela nyingi ambayo hakutakuwa na uwajibikaji? naomba nitahadharishe hilo, nimshukuru sana Mheshimiwa Simbachawene kwa maelezo yake ambayo yametia moyo kidogo, kwamba kwa kweli Serikali itasimamia hayo yote, na tunasema kwamba kunapokuwa na *exit meetings* za *CAG* hatuwezi kukaa tena hapa tukaambiwa longolongo zile kwamba hapa ilikuwa hivi hapa ilikuwa hivi, hapa siyo mahali pa ku-*justify* uzembe ni mahali pa kuwajibisha watendaji wazembe.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, Mheshimiwa Simbachawene nimefurahishwa na majibu yako ya kuonesha ukomavu na kuonesha kwamba kweli utasimamia Serikali ipasavyo kuhakikisha kwamba inatumia fedha za umma vizuri *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge hili likubali maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yetu hii ya *PAC* yawe maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu shughuli za Kamati za mwaka 2022 wanaoafiki waseme ndiyo.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wasioafiki waseme siyo. Wote mmesema ndiyo ahsanteni sana. Hii sasa inakuwa ni Taarifa Rasmi ya Bunge. Sasa namuita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninakushukuru na ninaseme ahsante kwa fursa hii, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuisikiliza taarifa ya mwaka ya Kamati na ninatambua michango ya Wabunge mmoja mmoja kwenye hoja za Kamati na kwa kuwataja wachache ni kama ifuatavyo; Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Francis K. Ndulane, Mheshimiwa Jeremiah M. Amsabi, Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela, Mheshimiwa Jesca J. Msambatavangu; na Mheshimiwa Mwita M. Waitara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wameonesha namna ubadhilifu wa fedha za umma unavyofanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, wameonyesha kuwepo kwa upotevu wa fedha za umma katika mifumo ya kielektroniki ya mapato, manunuzi, mikataba na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati zinapokuwa zimepokea taarifa ya Mkaguzi ya *CAG* maana yake ni kwamba taarifa hii imepitia hatua nyingi sana ikiwemo kuzipa fursa Halmashauri ya kujibu hoja ambazo zimejitokeza wakati wa ukaguzi. Hoja wanapewa zaidi ya siku 21 wakati mwingine ili waweze kuzitolea majibu, inaposhindikana kabisa majibu yake hakuna bado wanapata nafasi na *CAG* anapokwenda anakuwa na vikao mbalimbali, kikao cha kwanza, anachofanya wakati anaingia lakini kunakuwa na kikao cha

pili ambacho sasa kina mpa nafasi ya kuendelea na kazi yake, hata anapomaliza ndani ya siku 30 alizopewa bado atafanya *exit meeting* ambayo ataeleza kwenye eneo husika nini alichokutana nacho na atawaachia nafasi ya kujibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachojitokeza Halmashauri nyingi hazitoi majibu kwa wakati na hazitoi vielelezo vya maswali magumu waliyoulizwa na Mkaguzi. Lakini bado wanapata nafasi ya kuja mbele ya Bunge lako kwa maana ya Kamati ili waweze kuelezea na Bunge lako linatumia nafasi hiyo kuhoji likimhoji pande zote mbili kwa maana ya CAG lakini linawahoji pia watu waliokaguliwa, bado taarifa na majibu ya hoja zlilizotolewa hayapatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana taarifa zinazoingia hapa ndani kwenye bunge lako tunaamini ni taarifa zilizotenda haki kwa pande zote mbili na ni imani yetu kwamba Wakurugenzi na Watendaji Maafisa Masuuli wakifanya wajibu wao sawasawa inawezekana kabisa hoja hizi zikapungua sana na hizi sintofahamu, hii ni kweli au siyo kweli ikawa imeonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge wamehimiza Serikali kuchukua hatua madhubuti dhidi ya ubadhirifu huo. Aidha Waheshimiwa Wabunge wameshauri Serikali kuzingatia utaalam katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Michango hii imeimarisha zaidi mapendekezo ya Kamati katika taarifa yake ya mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninahitimisha kwa kauli kwamba ubadhirifu katika mapato na matumizi ya fedha za umma ni jambo lisilostahili kufumbiwa macho, hivyo nalishawishi Bunge lako tukufu liunge mkono mapendekezo ya Kamati kuwa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivi tutasaidia sana iko mifano mingi kwa mfano, unakutana na hoja ya ukaguzi ambayo Mkaguzi amekuta Halmashauri Mtumishi aliyepaswa kulipa kwa mfano analipa Shilingi Laki Nne badala ya kulipa Shilingi Laki Nne anasema akaingiza namba ya simu ambayo tarakimu zake uki-*count* kwenye hela inakuwa, kwa mfano anaingiza namba 068… *and so on*, ambayo ukichukua 068 unatoa sifuri unazungumzia Milioni Mia Sita. Sasa cha kujiuliza kama yalikuwa ni makosa fedha hii imeingia kwenye *account* ya benki, baada ya masaa machache yaliyofuata fedha ile ile ya namba imeenda kutolewa benki kama *cash money* na kwenda sehemu ambayo haijulikani. Hizi ni moja ya changamoto ambazo ukweli zinaonyesha kabisa yako maeneo ambayo bado yanatakiwa kufanyiwa kazi, huu inawezekana ni utaalam mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri ya kuchukua hatua na kuendelea kufuatilia lakini tuna imani inawezekana mfumo wa TAUSI ukafanyiwa marekebisho zaidi na kutumia fursa na changamoto zilizojitokeza ili kudhibiti changamoto hizi za upotevu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Ofisi ya CAG kwa kuwa jicho makini la Bunge katika hali kama hii, tuna imani Serikali itazidi kuiwezesha kifedha ofisi ya CAG ili kuwa na muda wa utekelezaji wa wigo mpana wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine tena nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge na naomba kutoa hoja.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kwamba Bunge sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa – *LAAC,* kuhusu shughuli za Kamati za mwaka 2022 wanaoafiki waseme ndiyo.

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Maazimio ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa yaliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haya sasa ni Maazimio rasmi ya Bunge, yamehama kutoka kwenye Kamati na sasa ni Maazimio rasmi ya Bunge kwenda Serikalini. Ninaiomba Serikali mambo muhimu sana yamezungumzwa, Serikali mmejibu vizuri, nendeni mkafanyie kazi hoja za Wabunge kwa mujibu wa Katiba inavyosema.

Suala la mifumo *CAG* amezungumza sana lakini mpaka leo marekebisho bado, kuna mvutano wa maksudi unaofanywa huko kwenu, kila mtu anajivutia upande wake ambayo hii siyo jambo jema kwa Taifa, mnajiweka katika mazingira magumu kuja kujibu upotevu wa pesa ambao *solution* zake ni kuweka mfumo mmoja tu hii ni *file payment system* ya Serikali na hakuna mtu yoyote anayeweza kuchezea mfumo huu. Mtakuta baada ya mfumo huu kuwekwa mtajikuta mapato ya Serikali yanaongezeka kwa asilimia zaidi ya asilimia 25. Kwa hiyo, niwaombe sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nichukue nafasi hii kumpongeza *CAG* kwa kweli ndiyo jicho la Taifa na ni jicho la Bunge, amefanyakazi nzuri sana nampongeza sana. Nawapongeza Wabunge na Kamati kwa kazi nzuri ambazo mmeziwasilisha Bungeni na kutimiza wajibu wenu kwa mujibu wa viapo vyenu vya Kibunge na Katiba ya Taifa letu.

Waheshimiwa Wabunge, Serikali leo imejibu vizuri tunaomba muendelee kujibu vizuri, lakini myafanyie kazi haya mapungufu yaliyooneshwa na Kamati hizi Tatu leo na Kamati zingine zote ambazo zimeshatoa taarifa zao na ambazo zitatoa taarifa zao mpaka siku ya mwisho wa Kikao cha Bunge hili.

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 1.08 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 8 Februari, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*